

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 20 Desemba, 2013**

*(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilisha Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM):**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa Mwaka 2011/2012 [*The Annual Report of Tanzania Revenue Authority (TRA) for the Year 2011/2012*].

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM)]

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ulaguzi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 [*The Annual Report and Audited Financial Statement of Vote 45 – National Audit Office for the Financial Year ended 30<sup>th</sup> June, 2012*].

### **MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka, 2013.

### **MHE. REBECCA M. MNGODO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Mwaka, 2013.

### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 159

#### **Kutumia Maji ya Chemchem Jimboni Tabora Kaskazini**

**MHE. ISMAIL A. RAGE (K.n.y. MHE. SHAFFIN A. SUMAR)** aliuliza:-

Katika Kata za Magiri, Ishilimulwa na maeneo mengine ya Jimbo la Tabora Kaskazini, kunapatikana maji ya chemchem:-

Je, kwa nini Serikali isiyatambue maeneo hayo na kupima hayo maji kama yanafaa kwa matumizi ya binadamu na kisha kuboresha huduma hiyo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini, kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Magiri na kijiji cha Ishihimulwa katika Kata ya Bukumbi, kuna chemchem tatu (3) zilizo hai, kati ya hizo mbili ziko katika Kata ya Magiri na moja katika kijiji cha Ishihimulwa Kata ya Bukumbi katika Jimbo la Tabora Kaskazini. Aidha, Jimbo zima la Tabora Kaskazini lina jumla ya chemchemi kumi na tatu (13).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa fedha 2010/2011 Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ilitenga na kuidhinishwa shilingi 4,000,000,000/= ambazo zilitumika kufanya utafiti na kupima ubora wa maji katika chemchem ya kijiji cha Isikizya na kubaini kuwa maji haya yanafaa kwa matumizi ya Binadamu.

Chanzo hiki cha maji kimeboreshwa na kinatoa huduma katika Ofisi za Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui na kwa wananchi wa maeneo ya jirani. Mradi huu uligharimu jumla ya shilingi 200,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2011/2012 zinazohusisha uboreshaji wa chemchem sita (6) pamoja na ujenzi wa miundombinu mingine ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 kiasi cha shilingi 9,000,000/= kutoka Bajeti ya matumizi ya kawaida ya Halmashauri zilitengwa na kutumika kupima ubora wa maji pamoja na wingi wa maji (*Yield*) yake katika chemchem 12 pamoja na vyanzo vingine vya maji katika Jimbo la Tabora Kaskazini na kubaini pia kuwa maji haya yanafaa kwa matumizi ya binadamu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (TAMISEMI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa maeneo hayo katika kutoa huduma ya maji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, ilitenga na kuidhinisha shilingi 100,000,000/= ambazo zilitumika kuimarisha chemchemi ya Isikizya, Ndono, Lende na Goweko ambapo jumla ya wakazi 1,500 wananaufaika na huduma ya maji kutoka katika miradi hii.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, anaweza kulifahamisha Bunge hili Tukufu na wananchi wa Tabora ule mradi kabambe wa kutoa maji kutoka *Lake Victoria* mkakati wake umefikia wapi?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kufanya upembuzi, usanifu wa mradi huo wa kutoa maji kutoka bomba la *Lake Victoria* mpaka Shinyanga na kupitia Nzega hadi Tabora inaendelea.

Hatua ya kwanza ya kutathmini kama inawezekana kufanya hivyo imekamilika na gharama za kutekeleza mradi huo zinajulikana sasa na Serikali inahangaikia kupata fedha ili mradi huo utangazwe na uanzwe kujengwa.

Na. 160

### **Ushiriki wa Vijana Kwenye "Big Brother Africa"**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

- (a) Je, Serikali inahusikaje katika ushiriki wa Vijana wa Tanzania kwenye mashindano ya "*Big Brother Africa*"?
- (b) Je, kuna faida gani kwa Taifa kutokana na ushiriki wa vijana kwenye mashindano hayo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haihusiki moja kwa moja na ushiriki wa vijana katika mashindano ya mchezo wa "Big Brother Africa" bali inatambua uwepo wa mashindano ya "Big Brother Africa" yanayoendeshwa na Kampuni ya "Multichoice" ya Afrika ya Kusini yenye tawi lake hapa nchini.

Kama walivyo vijana wengine wanaoshiriki Mashindano haya kutoka nchi mbalimbali za Afrika, vijana kutoka Tanzania hujaza fomu za ushiriki kuititia kwenye mitandao kama vijana wengine kwa utashi wao binafsi. Mchakato wote wa ushiriki wa vijana wanaoomba hufanywa na Multichoice Africa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanaoshiriki mbali na kuzitangaza nchi wanazotoka, hutangaza vivutio vilivyo katika nchi zao ikiwa ni pamoja na kutangaza vivutio vya utalii na maliasili. Hivyo Vijana wa Tanzania wanaoshiriki Mashindano haya; wameitangaza Tanzania na maliasili zake katika ramani ya Dunia. Kwa wale waliofanikiwa kuingia katika hatua za ushindi wamepata zawadi za fedha taslimu ambazo zimewasaidia kuboresha maisha yao.

Aidha Mashindano hayo huwezesha vijana kufahamiana, kuvumiliana, kujifunza na kujenga urafiki mionganoni mwao licha ya kuwa na tamaduni zinazotofautiana.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuuliza maswali mawili mengine ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu lake Mheshimiwa Waziri amesema Serikali haihusiki moja kwa moja, lakini anaonesha ni namna gani Serikali inavyohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali ya Uganda imepitisha sheria inayokataza vipindi, uandishi na mavazi yenye kuchochea ngono na tayari Rais Museveni amesaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali ya Tanzania inawaachia vijana hawa kushiriki mashindano ambayo yanaonekana au mwonekano wake mkubwa ni kushadidia vitendo nya ngono na ufuska?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Hivi Mheshimiwa anasema kwamba washiriki wale wanatangaza vivutio nya utalii, ilihali Watanzania wote ni mashahidi kwamba vitendo vinavyoonekana pale ni nya kuchochea ngono, ukahaba na ufuska.

Je, Serikali inatumia vigezo gani pale inapotumia Jeshi la Polisi kuwakamata dada poa na kaka shughuli ilihali ikiwaachia vijana wa Tanzania wakipeperusha bendera ya Watanzania kwenye mashindano ambayo maadili yake makubwa ni kushadidia ngono, ufuska na ufisadi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yangu ya awali yameonyesha ni namna gani ambavyo Serikali haihusiki. Lakini Serikali inatambua vijana wale wanaoshiriki kwa maana vijana hawa hujaza fomu zile kupitia katika mitandao na mashindano haya yanasmamiwa na *Multichoice Africa* ambaeo wana tawi lao hapa Tanzania.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO]

Nimeeleza zile faida za msingi ambazo Mtanzania yoyote anayechaguliwa afike pale awe anajua Kiingereza awe na umri usiopungua miaka 18 lakini kueleza wenzake vivutio vya utalii vilivyopo hapa. Pamoja na kasoro zote zinazoonekana wapo Watanzania karibu 3 nao walitolewa kwa sababu ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge nakubaliana naye. Tunaweza tukapima faida na hasara lakini chang amoto zinazojitokeza, Serikali itazifanya kazi na itatoa taarifa juu ya kuendelea kwa vijana wetu kushiriki ama la. (*Makofî*)

Pili, nakubaliana naye kwamba wapo washiriki wa nchi mbalimbali wameweza kufedhehesha nchi zao kwa kushiriki ngono katika mashindano haya. Naomba tu kutumia nafasi hii kusema kwamba kama nilivyo sema kwenye majibu yangu ya msingi tumeyapokea tunaya fanyia kazi na tutatoa tamko. (*Makofî*)

Na. 161

### **Kuboresha Hospitali ya Muhimbili**

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. RITA L. MLAKI**  
aliuliza:-

Hospitali ya Muhimbili ndio hospitali kubwa ya Rufaa Dar es Salaam na nchi nzima na wagonjwa wengi mpaka wanakosa mahali pa kulala na kulazwa chini:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha hospitali hiyo ili angalau ipatikane nafasi ya kulala wagonjwa na vitanda?

(b) Je, ni uwiano gani wa Daktari kwa kuona wagonjwa kwa siku ili kuhakikisha kuwa kuna Madaktari wa kutosha?

(c) Je, Serikali inatenga fedha kiasi gani kwa mwaka kwa ajili ya kuhudumia hospitali hiyo kwa matumizi mbalimbali kama dawa, chakula na magari?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

### **WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kujenga jengo la kutolea huduma kwa wagonjwa wanaotaka huduma binafsi ambalo litakuwa na vitanda 200. Jengo hili litaongeza upatikanaji wa nafasi za kulaza wagonjwa wengine.

Aidha, kuanza kutumika kwa jengo la Kituo cha Matibabu na Mafunzo ya Magonjwa ya Moyo ambacho kina vitanda 100 kutaongeza upatikanaji wa nafasi ya kulaza wagonjwa wengine.

Vilevile, Hospitali ya Taifa Muhimbili inaendelea kuzisaidia Hospitali za Rufaa ngazi ya Mkoa za Manispaa tatu za Jiji la Dar es Salaam na vituo vingine ili kuboresha huduma katika vituo hivyo. Hatua hii itapunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa katika Hospitali ya Taifa na hivyo kupunguza msongamano usio wa lazima katika Hospitali hiyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwiano wa Daktari na wagonjwa ni kwamba Shirika la Afya Duniani (*WHO*) limeweka kiwango cha Daktari mmoja kuhudumia wagonjwa 600 (kutoka kiwango cha Daktari mmoja kuhudumia wagonjwa 5,000 hapo awali).

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

Hii ina maana kuwa ili kufikia kiwango kilichowekwa na WHO hapa nchini kunatakiwa kuwepo na Madaktari 75,000 ili kuhudumia watu 45,000,000 waliopo. Kwa sasa hapa nchini kuna Madaktari 2,250 na Madaktari Wasaidizi 2,500. Kwa hiyo idadi ya Madaktari inaweza kuchukuliwa kuwa 4,750. Hii inafanya uwiano wa Daktari na Wagonjwa kuwa Daktari mmoja kuhudumia wagonjwa 10,000.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imetengewa kiasi cha shilingi 8,018,147,862/= . Kati ya hizo Shs. 2,345,621,730 zikiwa kwa ajili ya Maendeleo na shs. 5,672,526,132/= kwa Matumizi Mengineyo (kwa ajili ya kununua dawa, vifaa, vifaa tiba, chakula, magari na kadhalika). Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha hakitoshelezi mahitaji ya hospitali hiyo kwa sasa. Hii ni kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na maelezo ya mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza.

Katika majibu yake yanayojitosheleza lakini kwa mfano katika mkoa wa Mwanza mbali na Hospitali ya Bugando tunayo hospitali ndogo pale ya Sekoutoure ambayo ina matatizo mengi sana haina vitanda vya kutosha haina waganga wa kutosha na majengo pia.

Je, Serikali ina utaratibu gani sasa wa kuiboresha ile Hospitali ya Sekoutoure badala ya kuegemea upande mmoja Hospitali ya Bugando peke yake?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Serikali kuboresha huduma za afya katika ngazi zote kuanzia zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa hadi Hospitali za Rufaa za Kanda. Ndio maana kila mwaka tunajaribu kuweka Bajeti.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

Wizara yangu kwa sasa ina shughulikia zaidi Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Mikoa na Wilaya pamoja na vituo vya chini vinawekwa katika Bajeti ya Halmashauri na mikoa husika. Tutaendelea kuhakikisha kwamba fedha zinazowekwa katika Bajeti zinaongezwa kadri uwezo unavyoweza kupatikana.

Lakini vilevile tumeamua kwa makusudi kuweka vyanzo vipyta katika hospitali hizi ikiwemo fedha zinazopatikana kutoka kwenye Bima ya Afya. Nawasihi wahusika wazitumie vizuri ili kuboresha huduma za afya katika maeneo mbalimbali nchini mwetu.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kasulu ndio Muhimbili yetu sisi watu wa Kasulu na hospitali hiyo haina Daktari wa Wilaya tangu Dr. Erick Bakusa ahamishiwe Wilaya ya Mufindi Hospitali hiyo haina Daktari wa Wilaya. Sasa ni lini hospitali hiyo itapatiwa Daktari?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna Wilaya kadhaa kwa sasa hazina Madaktari wa Wilaya kwa maana ya (*District Medical Officers*). Wako wengi ambao bado wanakaimu na kuna maeneo mengine ambapo hawapo kabisa.

Suala hili tunalitambua pale Wizara ya Afya na tayari tumeshatengeza orodha ya kukamilisha idadi ya Waganga Wakuu wa Mikoa yaani (*RMO's*) tumeikamilisha na tumeshaipeleka Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ili wawze kutangaza kwanza Waganga Wakuu wa Mikoa yote katika kipindi hicho hicho sasa hivi tunashughulikia orodha ya Waganga Wakuu wa Wilaya zote nchi nzima ili hatimaye kusiwe kuna mtu yoyote ambaye ana Kaimu tukamilishe jambo hili. Nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili litakamilika hivi karibuni.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwaiposa jiandae Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

**MHE. EUGINE E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kupata nafasi. Kwa kuwa hospitali ya Muhimbili kujaa kwa wagonjwa katika hospitali ya Muhimbili kuna sababu nyingi lakini sababu moja wapo ikiwepo pia kwamba hospitali nyingi za Wilaya zimekuwa hazina vifaa nya kutosha lakini pia hakuna madaktari mabingwa wa kutosha suala ambalo linapelekea sasa wananchi wengi kupelekwa kwa wingi katika hospitali hii ya Rufaa.

Je, ni nini sasa mpango wa Serikali au sera ya Serikali ya kuboresha hizi hospitali za Wilaya lakini pia kuanzisha hospitali nyingine za Wilaya ambazo zimeshainisha kama hospitali ya Kivule ambayo kwa miaka mingi Serikali ina mpango wa kujenga ili kuweza kupunguza songamano la wagonjwa katika hospitali hizi kubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwaiposa, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kwamba moja ya sababu zinazofanya Muhimbili kuwa na msongamano mkubwa, ni wananchi kutotumia vyema hospitali za Wilaya za Manispaa ya Dar-es-salaam. Ndio maana katika jibu langu la msingi nilisema kwamba madaktari wa Muhimbili kuna utaratibu sasa ikiwemo wale wa Moi wa mifupa kwenda kwenye hospitali za Wilaya kutoa huduma ili kupunguza watu wanaokwenda Muhimbili moja kwa moja.

Lakini vilevile upo utaratibu wa kuziboresha hospitali za Manispaa ya Dar-es-salaam na ndio maana kuna Miradi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

kadhaa sasa hivi inaendelea ya Ujenzi wa hospitali hizi ili kupunguza msongamano Muhimbili. Isitoshe karibu hospitali zote za Manispaa sasa hivi zinao madaktati bingwa sema hawatoshelezi kwasababu nchi inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi katika Sekta ya afya lakini tutaendelea kuwapatia vifaa, tutaendelea kujenga na kukarabati hospitali hizo na kupunguza kwa kuanzisha hospitali mpya. Mfano mzuri ni ile hospitali ya *CCBRT* ambayo ni ya wazazi.

Hii ni ili wananchi wenyewe matatizo madogo ambayo hayaitaji kwenda Mmuimbili wasiwe wanakwenda. Kwa mfano utaratibu tu wa kujifungua tu kwa kawaida watu wengi wanakwenda Muhimbili jambo ambalo halipaswi kuwa hiyo. Kwa hiyo tutaendelea kuboresha hospitali hizi za Manispaa ili kupunguza msongamano huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi natambua juhudini nzuri za Serikali za kuanzisha hizi hospitali za Rufaa ambazo zipo Mikoani, hii ni pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Iringa ambayo ina hudumia maeneo mbalimbali na wananchi wengi kwa ujumla.

Lakini kwa kutambua hospitali hizi zinazidiwa hazina Wataalamu hazina vifaa Manispaa yetu ya Iringa imejaribu kupanua huduma za afya na vituo vya afya mbalimbali ni pamoja na Hospitali ya Manispaa ambayo binafsi nilishiriki kutoa vitanda, magodoro na kadhalika, kwa ajili ya kuifanya ianze kazi. Lakini tumekuwa na changamoto ya madawa ambayo mara nydingi zile pesa zinazotoka Serikalini zinashindwa kutekeleza kwa wakati wake.

Je, Waziri unasemaje kuhusu hili, ili kupunguza msongamano huu katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Iringa ambayo kimsingi wanajitahidi lakini vifaa havipo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

**WAZIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msigwa kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze kwa juhudhi zake za kujitolea kusaidia Hospitali ya Manispaa. Lakini niseme tu kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba Hospitali hizi zote za ngazi zote zina mgao maalum wa dawa na vifaa tiba kutoka Bohari ya dawa (*MSD*).

Lakini tunatambua kwamba mgao huo kutokana na mfinyu wa Bajeti hautoshelezi mahitaji. Ndio maana tukaweka taratibu maalum za kupata fedha za ziada.

Mfuko wa Bima wa Afya watu wakitibiwa Hospitali zile zinalipwa. Wako wananchi ambao hawana Mfuko wa Bima ya Afya lakini wanalipa moja kwa moja kutoka Mifukoni mwao tunategemea kwamba fedha hizo zitumike kupunguza matatizo ya uhaba wa fedha katika Hospitali hizo.

Kwa hivyo napenda kurudia wito wangu kwamba *MSD* itaendelea kuongeza fedha kwa ajili ya kuwapatia mahitaji ya dawa na vifaa tiba. Lakini na fedha zinazopatikana moja kwa moja kwa vyanzo vingine katika Hospitali zitumike vyema ili kupunguza uhaba wa vifaa na dawa katika Hospitali zetu. (*Makofj*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, sasa na tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mbassa, katika Wizara hiyo hiyo.

Na. 162

**Kuongeza Wanafunzi na Ruzuku kwa  
Vyuo Binafsi vya Afya**

**MHE. DKT. ANTONY GERVAS MBASSA** aliuliza :-

Vyuo vingi vinavyotoa taaluma ya Sekta ya Afya hususani Maafisa Tabibu na Wauguzi vinamilikiwa na Madhehebu ya Dini.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wakufunzi katika vyuo hivi ili kuwe na ufanisi wa utoaji wa taaluma hiyo inayohitajika sana hapa nchini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa huu ni muda muafaka wa kutoa ruzuku kwa Vyuo hivi ili kuimarisha uendeshaji wake?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inathamini mchango unaotolewa na vyuo vya binafsi na vyuo vya Mashiriki ya Dini katika kuonge za rasilimali watu katika sekta ya afya. Wizara yangu inao upungufu wawakufunzi katika vyuo vya afya inavyovimiliki.

Awali wakati watumishi wote wa umma katika sekta ya afya walipokuwa chini ya ajira ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ulikuwepo utaratibu wakuwashikiza (*secondment*) baadhi ya walimu katika vyuo vya mafunzo binafsi hususani ya Mashariki ya Dini.

Hata hivyo, kutokana na utaratibu uliopo wa Mamalaka za ajira za Watumishi wa Umma kuwa katika ngazi za Halmashari /Manispaa na mikoa tunashauri wamiliki wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

vyuo binafsi vya afya kuwasiliana na mamalaka za ajira katika sehemu zao ili kupata wakufunzi ambao watashikizwa kufundisha katika vyuo hivyo.

Baadhi ya vyuo binafsi vimetumia njia hii kupata wakufunzi. Mfano Chuo cha Wauguzi cha *KIUMA* wilayani Tunduru, kimepata wakufunzi kufundisha chuoni hapo ambapo ni waajiriwa wa Halmashauri ya Tunduru.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa na utaratibu wa kutoa ruzuku kwa vyuo binafsi na Mashirika ya Dini kwa kiasi cha shilingi 40,000/= kwa kila mwanafunzi, kwa mwaka pale fedha zinapokuwa zimepatikana, katika mwaka husika wa fedha.

**MWENYEKITI:** Dkt. Anthony G. Mbassa.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Waziri amekiri wazi kwamba kuna upungufu mkubwa wa Wauguzi au Wakufunzi katika vyuo hivi. Utaratibu anaosema kwamba kuitia Mamlaka za ajira katika Halmashauri, Manispaa nako kuna tatizo la Watumishi vilevile.

(a) Je, haoni kwamba sasa ni wakati mzuri wa kurudisha utaratibu uliokuwepo wa *Secondment* ili kusudi walimu hawa waende kwenye vyuo hivi waweze kutoa wahitimu ambao wana ubora?

(b) Kwa kuwa amekiri kwamba Serikali inatoa ruzuku kiasi cha elfu arubaini kwa kila mwanafunzi katika vyuo hivi vya Mashirika ya dini na vya umma?

Je, Serikali ipo tayari kutuletea mchanganuo wa ruzuku hizo katika vyuo hivyo, maana ukienda kule wanalamika kwamba hawapati rukuzu? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, kama ifuatavyo:-

(a) Napokea ushauri wake kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kurudisha utaratibu wa zamani ambapo hao wakufunzi pamoja na madaktari walikuwa *seconded* katika Hospitali za binafsi au vyuo vya binafsi na Masharika ya dini. Hili tutalifanyia kazi kwa sababu tunajua changamoto zilizopo katika ngazi za Halmashauri.

(b) Tulete mchanganua unaonyesha fedha zinazopelekwa katika vyuo hivi, hili tunalipokea na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaleta mchanganuo huo kwa taarifa yake.

### **TANGAZO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nina tangazo muhimu. Naomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa Bunge kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi leo, siku ya Ijumaa tarehe 20 Desemba, 2013 saa tatu na nusu asubuhi katika Ukumbi wa Spika.

Wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria. Kama kuna Mjumbe wa Kamati ya Uongozi naomba aelekee ukumbi wa Spika sasa hivi. Tunaendelea. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Said Mkumba.

Na. 163

### **Biashara ya Tumbaku kwa Dola**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA** aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya Wakulima wa Tumbaku nchini juu ya kuendesha biashara ya Tumbaku kwa Dola na wakati wa kubadili fedha kutoka Dola kwenda fedha za Kitanzania. Wakulima wamekuwa hawabadilishiwi kulingana na kiwango kilichopo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SAID JUMA NKUMBA]

(a) Je, kwa nini biashara ya ndani ya Tumbaku isifanyike kwa Shilingi ya Tanzania?

(b) Je, Serikali iko tayari kuchunguza kwa nini Wakulima hawataki biashara ya Tumbaku kwa Dola na Viongozi wanaitaka kwa nguvu biashara hii ya Dola kwa zao la tumbaku?

### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Saidi Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a0, na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Biashara ya ndani ya tumbaku hufanyika kwa dola ya kimarekeani baada ya makubaliano yawadau Halmashauri ya tumbaku (*Tobacco Council*). Sababu za msingi za maamuzi hayo ni kutokana kwamba biashara ya pembejeo kwenye zao la tumbaku hufanyika kwa kwa dola.

Hivyo, basi ili kupunguza uwezzekano wa kuwakanganya wakulima hasa kwa kuzingatia ukweli kuwa thamani ya shilingi imekuwa ikibadilika mara kwa mara kulingana na Dola ya Kimarekeani wadau walikubaliana kutumia dola katika biashara ya tumabku nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na thamani ya shilingi ya Tanzania kushuka na kupanda dhidi ya dola ya Kimarekani, mkulima anapolipa deni lake la pembejeo kwa dola huondokana na uezekano wakupata hasara inayotokana na mabadiliko hayo. Aidha, kwa utaratibu huo mkulima ana uwezo wa kulinganisha faida au hasara itokanayo na biashara yake kwa kuzingatia mnyororo wote wa uzalishaji hadi mauzo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli pia kama alivyooleza Mheshimiwa Nkumba kwamba utaratibu huu umeonyesha usumbufu kwa wadau wengine.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mfano tafsiri potofu za thamani halisi za biashara hiyo, ambayo haiwanufaishi wakulima kutokana na udanganyifu unaofanywa na wasimamizi wa biashara hizo, hususan viongozi wa Ushirika, Mawakala na Taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeelekeza Bodi ya Tumbaku kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa tumbaku hususan wakulima kufanya uchunguzi zaidi juu ya Mfumo huu wa matumizi ya dola kwenye biashara ya tumbaku ili kuona ni kwa namna gani mkulima ananuifaika au kupunjika kutokana na biahara ya tumbaku kufanyika kwa dola.

Aidha, baada ya kuainisha changamoto zinazotokana na mfumo huu wa matumizi ya dola, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa tumbaku nchini itatoa mapendelekezo ya namma bora ya kukabiliana na changamoto hizo kwa manufaa ya wadau wote wa tumbaku hususan wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendelekezo hayo yatawasilishwa kwa wadau wote ili yakiridhiwa yatengenezewa utaratibu wa utekelezaji kwa manufaa ya wakulima wa tumbaku nchini. (*Makofii*)

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwakuwa utaratibu huu Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba hauna manufaa kwa wakulima na unaleta usumbu na wizi kwa wakulima wa tumbaku nchini na Serikali pamoja na yote haya bado mnaendelea kufanya utafiti kwenye wizi.

Je, Serikali mnataka alalamike nani ndio msikie kwa sababu wakulima wote hawautaki mfumo wa dola unaowaibia fedha zao?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SAID JUMA NKUMBA]

(b) Kwa kuwa mfumo huu wa dola hauna mamslahi kwa wakulima na kwakuwa wakati wa kuuza na kuwakopesha Pembejeo wakulima, dola inakuwa juu. Lakini wakati wa kulipa dola inakuwa chini na hivyo kwa wakulima wanapunjwa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa Serikali itakuwa tayari sasa kuturuhusu Wabunge wote tunaotoka katika maeneo ya tumbaku twende tukawahamasishe wakulima wanaolima tumbaku sasa waachane na zao hili linalowanyonya kila wakati ili walime mazao mengine.

Je, Serikali itakuwa tayari kuturuhusu kufanya hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu maswali ya myongeza ya Mheshimiwa Saidi Juma Mkumba kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusema kwamba mfumo huu hauna manufaa, nilichosema ni kwamba mfumo huu inapotokea kwamba dola inayumba mara nyingi anayeathirika kwa kiasi kikubwa ni Mkulima kwa sababu ufahamu wake wa *movement za exchange rate* ni ndogo.

Lakini pia hawa Mawakala na hata viongozi wao wa Vyama vyta Ushirika wakati mwingine wanatumika katika kupata manufaa ambayo yana wahujumu Wakulima wenzao. (*Makof*)

Kwa hiyo, tulichosema kama nilivyosema mwanzoni kuwa *structure* yake hii Serikali imeiagiza Bodi ya tumbaku iende ikafanya *review* ya Mfumo huu mzima kwa kuwashirikisha Wakulima wenye, badala ya watu wachache pale juu wanaosimamia Mfumo huu. Ili kabla ya msimu ujao wa tumbaku tuje na mapendekezo ambayo yatakuja ku-*review* Mfumo huu na kuangalia namna ambavyo Wakulima wananzaika nao kwa kiasi kikubwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lingine naomba nikiri kama nilivyosema kwamba kama biashara hii inafanya kama bereau de change ukiuza unakosa, ukinunua unakosa tumesema hivi kwamba tutafanya review lakini namwomba Mheshimiwa Said Mkumba kwasababu na ye ye pia ni sehemu ya Wadau hawa twende tukakae katika Mfumo huu wa kufanya tathmini tusiwhamasishe Wakulima kuondokana na zao hili ambalo kwa sasa hivi ndio linalochangia mapato makubwa zaidi kuliko zao lolote la Kilimo nchini. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Bodii Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuwa malalamiko haya kama alivyosema Mheshimiwa Mkumba kwa Wakulima kuhusiana na Mfumo huu wa dola. Sisi kule Namtumbo mwaka huu kwa kupitia Wakulima wenye na uongozi wa Wilaya, Kamati ya Pembejeo tulitangaza tenda kwa ajili ya kupata *supplier* kwa hela kitanzania na ameshusha bei ya Mfuko kutoka iliyokuwa laki moja mpaka elfu 74 kwa hela ya Kitanzania na tumeomba benki watukopeshe kwa hela za Kitanzania.

Je, Serikali itakuwa tayari kusimamia benki hizi zitukopeshe kwa fedha za Kitanzania ili tuweze kuwafaidisha Wakulima hao ambao wamekuwa wakilalamikia mtindo huu wa dola?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nijibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Nimefanya mukutano na Wakuu wa Mikoa na Mabenki yanayokopesha Wafanyabiashara na Wakulima wa Tumbaku. Tumekubaliana wanafanya mapitio na wamekubaliana tayari na hivi sasa nimemwahidi Mheshimiwa Kawawa kwamba nitampa taarifa ya makubaliano ya jinsi Mfumo mzima kwa msimu huu utakavyosimamiwa na ambavyo wamekubaliana kwamba kwa kweli tutajitahidi Wakulima wasinyonywe kwa ajili ya kutozwa matuzo ambayo siyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti lakini pia niongezee kwa kusema kwamba Mfumo mzima wa tumbaku katika msimu uliopita taarifa za awali zimeonyesha upotevu wa takribani shilingi bilioni kumi na sita. Hivi sasa tunavyozungumza nimemwomba CAG ameeanza kukagua Mfumo mzima wa Tumbaku na wale watakaopatikana wamesababisha hasara hizi na kwa vile Sheria ya Ushirika tayari imesainla na Mheshimiwa Rais. Watakumbwa na dhahama ile ambayo tumeipitisha kwamba si tu watashitakiwa, hata ile adhabu kubwa tuliyoiweka kwamba watafilisiwa itatumika.

Kwa hiyo, yote hayo tunatarajia baada ya CAG kukagua yatachukuliwa hatua. Kwa hiyo, hakuna haja ya Wakulima kuanza kuogopa tena kulima tumbaku na kuandamana, Serikali ina chukua hatua. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Tunandelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Asumpter Mshama.

Na. 164

**Kuelekeza Nguvu Katika Kilimo cha Mpunga  
Mahindi na Alizeti – Wilaya ya Miseni**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA** aliuliza:-

Wilaya ya Miseni ni moja ya maeneo yenye rutuba, na mabonde ya kulima Mpunga, Mahindi na hata Alizeti ikiwemo Kata ya Kilimilile ambapo utafiti ulifanyika na kuonekana kuna udongo unaofaa kilimo cha Alizeti:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

Je, Serikali ina mpango gani wa kuelekeza nguvu katika kilimo cha mazao hayo, ikiwemo kutafuta wataalam, vifaa na hata wawekezaji katika kilimo ili kuongeza pato la wananchi wa eneo hilo na taifa kwa ujumla?

### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Utafiti uliofanywa na kituo cha Utafiti cha Maruku mwaka 2008/2009 ulibaini kuwa zao la alizeti hususan mbegu aina ya RECORD inastawi vizuri katika Wilaya ya Misenyi katika maeneo ya kata ya Kyaka ambapo Mashambadarasa (*FFS*) matatu (3) yalitumika kuhamasisha kilimo cha Alizeti. Aidha, katika msimu 2013/2014 jumlaya ekari 8 zimetengwa kwa ajili ya mashamba darasa ya kilimo cha alizeti katika vijiji vya Kenyana na Kilimele ambayo yatatumika kutoa mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha alizeti kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Kupitiwa utekelezaji wa Mradi wa DASIP Wilayani Misenyi hadi kufikia mwezi Julai, 2013 jumla ya mashamba darasa (*FFS*) sabini na saba (77) ya kilimo bora cha mahindi yameanzishwa ambapo wakulima zaidi ya 1,862 wamenufaika kwa kufundishwa kanuni za kilimo bora pamoja na vikundi 72 vya wakulima kupatiwa mafunzo ya kuendesha kilimo cha biashara (*farming as a business*) katika zao la mahindi.

Aidha, katika msimu wa 2012/2013 Serikali ilitoa jumla ya vocha 3,000 za pembejeo za ruzuku kwa ajili ya mbegu bora za mpunga, mbolea ya kupandia na ya kukuzia kwa madhumuni ya kuinua Kilimo cha mpunga wilayani Misenyi.

Mheshimiwa Spika, serikali kupitia utekelezaji wa Mpango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPS*) imewezesha upatikanaji wa zana bora za kilimo, matrekta

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Madogo (*Power Tiller*) Saba (7) Na Matrekta Makubwa 16 pamoja na kuongeza wataalam wa kilimo kutoka 12 mwaka 2007/2008 hadi 46 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza mnyororo wa thamani (*Value Addition*) Serikali kwa kushirikiana na taasisi ya *EU-North-South Transborder Project* itanunua mashine ya kukamulia mafuta ya alizeti na hivyo kuwaongeza kipato wakulima.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2011/2012 kupitia mradi wa *DASIP* maghala matatu (3) ya kuhifadhi nafaka yamejengwa, mashine tisa (9) za kusaga nafaka na mashine mbili (2) za kupukuchua mahindi zimesambazwa kwa wananchi wa Misenyi. Jitihada zote hizi zitachangia katika kuongeza pato la wananchi wa Misenyi na Taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kunipatia nafasi nitoe maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mikakakti iliyopo kwa ajli ya kuendeleza Kilimo hasa cha Alizeti katika Wilaya yetu ya Misemi. Kwa kuwa amesema matrektra kumi na sita (16), haya matrekta ni watu binafsi waliyapata kwa njia zao na wala si kwa kusaidiwa hata na Halmashauri na matokeo yake ni kwamba ni binafsi. Haya saba (7) tunashukuru lakini tunalo jambo moja la kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yetu tulijikusanya tukawa na milioni 100 na tukachukua *profoma invoice* kutoka JKT kwa ajili ya kupata matrekta. Tulipofika matrekta yalikuwa hakuna na ukizingatia tunayo hekta 99,726 za kilimo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA]

Je, serikali inasemaje kutusaidia kupata matrekta hayo ili tuweze kuendeleza kilimo hicho? (*Makof*)

Swali lingine. Kwa kuwa sasa hivi Nkenge wana Nkenge wamejikita katika kilimo cha miwa na kinaonekana kinaleta mapato vizuri.

Je, Serikali iko tayari kuachana na kutupa ruzuku ya mpunga ambayo imefeli mwaka jana, watu wengi hawakuchukua na kutupatia ruzuku katika mbolea ya miwa hasa ya kupandia ambayo ni kani na *urea* kwa ajili ya kukuzia? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana muda wetu umekwenda.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niseme hili la kwamba walikwenda na milioni 100 ni jambo zuri Halmashauri tunahamasisha kwenda wao wenyege kukopa. Milioni 100 zingewapatia trekta kama mbili hivi na ekari 99 elfu bado ni trekta chake.

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba tunahamasisha aandae wazalishaji wake kwa njia ya vikundi ili waweze kupata matrekta hata 20, 30 katika awamu ya pili ya trekta zitakazotoka SUMA ambazo ni kama trekta 3,500. Kwa hiyo, hapo Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba na namwahidi kwamba Wizara yetu itakuwa tayari kulisukuma jambo hili kwa sababu wananchi wa Misenyi wanaonyesha ari kubwa katika kuzalisha mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili, mbadala wa miwa na mpunga. Mimi nadhani ni maamuzi ya Halmashauri kulingana na mapato ambayo wakulima wanapata. Lakini sisi kwa upande wa Wizara ya Kilimo tuko tayari Mheshimiwa Mwenyekiti kupadilisha ruzuku kama wao watakavyoona wanataka kulima miwa badala ya mpunga na ina uchumi nzuri zaidi kwao tuko tayari kufanya nao kazi kwa karibu. (*Makof*)

### **Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Pamoja na nia njema ya Serikali ya kumsaidia Mkulima kuondokana na maisha duni kuitia mpango wa Kilimo Kwanza:-

(a) Je, Serikali itahakikisha kwamba pembejeo zinawafikia walengwa kwa wakati muafaka?

(b) Je, Serikali iko tayari kuondoa kodi ya zuio (2% *withholding tax*) ambayo imekuwa kero kwa wakulima na kuawaachia ushuru wa mazao tu?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa madhubuti wa kuhakikisha kuwa mazao ya wakulima hususan mahindi yananunuliwa kwa wakati bila kukopwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** aliibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa pembejeo nchini kwa utaratibu wa ruzuku na soko kwa muda mrefu umekuwa na changamoto za aina mbalimbali ambazo zimepelekea kupungua kwa matumizi ya pembejeo.

Katika kushughulikia changamoto hizo katika upatikanaji wa pembejeo nchini Serikali itaongeza udhibiti na usimamizi wa mfumo wa ruzuku pamoja na kuweka mfumo mpya wa usambazaji wa pembejeo unaotumika katika msimu huu wa kilimo 2013/2014 ambapo katika baadhi ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

wakulima kuititia vyama vyaya ushirika watapata mikopo ya muda mfupi na yenye riba nafuu kwa ajili ya kununulia pembejeo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya zuio ya asilimia 2 kwa thamani ya bidhaa inayouzwa kwa maana ya 2% *withholding tax* hutozwa kwa mfanya biashara ambaye hana namba ya usajili *Tax Identification Number (TIN)*.

Kwa kutambua kuwa wakulima wengi wadogo huuza mazao yao kukidhi mahitaji yao muhimu na mazingira yao hayawawezi kurasimisha mauzo hayo na kujisajili kama walipa kodi na hivyo kupata *TIN*, Serikali kuititia mamlaka *TRA* imeondoa kodi kwa wakulima ambao hawana *TIN* wakati wa kuza mazao yao.

Hata hivyo, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kilimo nchini ili wakulima wawe wachangiaji wakubwa katika pato la Taifa kuititia utaratibu wa kodi na ongezeko la uzalishaji.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa mazao ya wakulima hususan mahindi yananunuliwa kwa wakati na bila kukopwa. Serikali itahakikisha ushiriki wa wadau wengi katika biashara ya mazao ili kutoa ushindani na hivyo kuongeza bei ya wakulima. Hata hivyo, imekuwepo changamoto kwa baadhi ya wafanya biashara kuwalipa wakulima bei ndogo ikilinganishwa na gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukubaliana na changamoto hiyo, Serikali itaimarisha uwezo wa wakala wa (*NFRA*) kwa kuongeza Bajeti ya ununuzi wa mazao. Ujenzi na ukarabati wa maghala ya kuhifadhi na Serikali ikishirikiana na Sekta Binafsi inatekeleza mkakati wa kuanzisha soko la bidhaa *commodity exchange market* kwa lengo la kuwapatia wakulima nafuu na soko la uhakika wa mazao hayo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti kuniruhusu nipate kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali kama ifuatavyo:-

Ni ukweli usiofichika kwamba mpaka sasa hivi ninavyoongea leo hii kuna baadhi ya wakulima ambao hawajalipwa pesa zao ambazo waliuza mazao tangu mwezi wa nane na pia ni ukweli usiopinga kwamba Halmashauri za Mkoa wa Rukwa ambazo zinategemea makusanyo kutoka *NFRA* na kwa bahati nzuri tuliweka katika Bajeti kuhakikisha kwamba pesa hiyo inatumika kujenga zahanati. Mpaka leo hii pesa hiyo hajjalipwa na *NFRA*. Naomba kauli ya Serikali pesa hizo zitalipwa lini?

Swali la pili. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri katika jibu lake kwamba utaratibu mwingine ungeweza kutumiza wa kusambaza pembejeo ambao ungewahakikishia wananchi wanapata pembejeo bila shida.

Je, ni sababu gani ambayo imesababisha Mkoa wa Rukwa kwa ujumla wake, utaratibu huu mpya haujaanza kutumika mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema kwamba kuna baadhi ya wakulima bado hawajalipwa pesa zao na Mheshimiwa Mwenyekiti hili ni jambo ambalo kwa hizi siku za karibuni limesikika sana hata kwenye vyombo vya habari. Madeni yote kwa ujumla yalikuwa ni bilioni 24.

Lakini bilioni 14 zilikuwa ni za wakulima wenyewe moja kwa moja. Sasa yale madeni ya wakulima moja kwa moja Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikail imeshalipa yote. Tatizo ni yale madeni kama bilioni 9.5 ambayo ni madeni yamepitia kwa Mawakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaongea na Wizara ya Fedha na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha Sada ametuhakikishia kwamba ataenda kulifanyia kazi Wizara yake

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

na sisi wengine ili tupunguze makosa. Kwa sababu haya madeni mengine ni madeni ya wakulima ambayo yamepitia kwa Mawakala ambao bado hawajalipwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo *figure* zake ni kama bilioni 9.5 tunakadiria kwamba katika muda mchache ujao Hazina watawezwesha kulipa pesa hizi. Mheshimiwa Mwenyekiti zile pesa za Halmashauri *NFRA* wanazijua wana hesabu yao. Wakipokea pesa hizo wanatarajiwa walipe kwenye Halmashauri.

Hili la mwisho Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba pembejeo. Ni kweli kwa utaratibu wa mwaka huu Hazina ilikuwa itoe pesa kama bilioni 18 ili pesa hizo ziwezekane kuli-*average* vikundi hivi viweze kukopa kupitia mabenki. Pesu hizo bado hazijapatikana. Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti tuna matarajio pia kwamba zitapatikana kwa wakati kwa sababu mambo ya kilimo yanakwenda kwa msimu.

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyikti kunipa nafasi. Kwa kuwa mapinduzi ya kilimo yanategemea sana matumizi ya sanyansi na teknolojia na kwa kuwa Mkoa wa Rukwa una hali ya hewa nzuri inayoruhusu kilimo, mafanikio mazuri katika kilimo na kwa kuwa Mkoa wa Rukwa ni moja ya Mikoa yenye matrekta machache sana.

Je, kuna mpango wowote wa Serikali kwa makusudi kuwezesha Mkoa wa Rukwa kupata matrekta ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane naye hakuna mapinduzi ya kilimo bila sayansi na teknolojia. Mkoa wa Rukwa ni katika mikoa mihimili ya kilimo cha Tanzania na tumesema hivi kwenye awamu inayofuata kwa maana ya *mechanization* Mkoa wa Rukwa na Mkuu wa Mkoa ambaye ni Mbunge mwenzetu anahamasisha sana matumizi ya matrekta tumeshazungumza naye.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Tunatarajia kwamba Mkoa wenyewe Mheshimiwa Mwenyekiti utafanya tihada ya makusudi ili awamu hii ya matrekta 3,500 Mkoa wa Rukwa upate matrekta mengi zaidi hasa kwa kuzingatia kwamba ni Mkoa ambao unazalisha asilimia kubwa sana ya chakula cha Tanzania.

**MHE. JITU V. SONI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Nilikuwa naomba niulize Serikali.

Je, ni lini itatekeleza ahadi na mpango ambao tulipitisha hapa kwenye *Finance Bill* ya kuondoa kodi na tozo mbalimbali katika pembejeo za kilimo na zana za kilimo na badala yake sasa imeongeza kwa maradufu katika maeneo mengine. Kwa mfano kwenye *fire*, ardhi, mizani, leseni za biashara. Jumla sasa hizo tozo na kodi mbalimbali imefikia 26.

Je, ni lini sasa Serikali itaangalia upya Sekta hii ili kilimo pia iweze kuwa cha kibiashara?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kodi za kwenye vifaa, zana za kilimo na pembejeo, Mheshimiwa Jitu Soni amekuwa akilisemea kwa karibu sana na kwa muda mrefu sana. Hili ni tafsiri, ni tatizo la tafsiri baina ya kodi hizi ziwe *applied* katika misingi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye mazungumzo na Hazina wataalam katika ngazi ya wataalam ili kubaini kwamba hivi vitu moja, mbili, tatu vimo katika kodi ile iliyotolewa. Bahati mbaya sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba wakati wataalam wanaendelea kujadiliana na wanachukua muda mrefu bado kodi hizi zinaendelea kutozwa.

Kwa hiyo, naomba nimwahidi tu Mheshimiwa Jitu Soni, Wabunge na wakulima wote wa Tanzania kwamba tutajaribu haraka iwezekanavyo kumaliza majadiliano haya ili tafsiri ya kodi kwenye zana zipi ipatikane haraka na iwe na manufaa kwa wakulima. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Katika swali la msingi imezungumzia habari ya kuchelewa kwa pembejeo. Suala hili ni tatizo kubwa sana hasa pia hata katika nikitolea mfano katika Mkoa wetu wa Geita. (*Makofi*)

Mara nyingi wananchi wanapata pembejeo kwa kuchelewa sana, msimu wa kilimo unaanza mwezi wa tisa. Lakini wanapata pembejeo mwezi wa kwanza. Kwa hiyo, ningependa kusikia kauli ya Serikali kwamba Serikali inasemaje kuhusu suala hili kuhakikisha kwamba pembejeo zinafika kwa wakati? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hili tatizo limekuwa linatokea mara kwa mara. Lakini kwa msimu huu tumejitahidi kujipanga kidogo na ndiyo maana hata mzunguko wa bajeti na mzunguko wa vikao vyta Bunge la bajeti kubwa lilibadilishwa ili pesa iwe inapatikana mapema na pembejeo zinapatikana zinakwenda mapema.

Hata hivyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakavyozungumza jioni wakati wa kuzungumzia masuala ya Kamati ni kweli kwamba pesa zimechelewa na mpaka dakika hii baadhi ya mbolea imekwenda kwa mali kauli, kwenda kwa wakulima ili waweze kuwahi msimu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalifahamu lakini ni tatizo la ufinyu wa Bajeti kwa mwaka huu lakini ni jambo ambalo limezingatiwa haswa kwenye mzunguko wa Bajeti na kuitisha pesa za Serikali.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri, pembejeo za kilimo zinazokwenda Mikoani sasa kwa msimu huu wa kilimo ni pamoa na mbolea. Lakini kumekuwa na tabia ya Mawakala kulazimisha wananchi kusaini vocha za mbolea wakati wao hawataki. Naomba nifahamu nini kauli ya Serikali juu ya Mawakala wale wanaowalazimisha wananchi kusaini zile vocha za mbolea na wao wanabaki na mbolea hizo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hawa Mawakala walikuwa wanafanya mchezo huo na ndiyo maana tukabadilisha kwamba Mawakala sasa wawajibike kwa yule msambazaji wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila unapopita kushoto na wenzako wanapita kulia. Tulichosema ni kwamba tunakuja na mabadiliko ya Sheria kwenye *Miscellaneous Amendments*, kwenye Sheria za mbolea, Sheria za pembejeo na kadhalika ili adhabu hizi ziwe kali zaidi. Kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti, yunapofanya hivi wewe unajitengenezea manufaa ya kwako binafsi lakini unatengeneza utajiri kwa kuwafanya wenzako wawe maskini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linakuja kwenye Sheria kwenye *Miscellaneous Amendments*, tutafanya mabadiliko ili Sheria ziwe kali zaidi ili Mawakala wawajibike, na kama wakishindwa watafute biashara nyingine ya kufanya.

Na. 166

### **Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI (K.n.y. JENISTA J. MHAGAMA) aliuliza:-**

Katika Bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi billion mbili (Tsh. Bilioni 2) kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya wanawake nchini:-

Je, ni akina mama wangapi Vijijiini wameshafaidika na fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA  
WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mbunge kuwa Wizara yangu katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2013/2014 imepokea kutoka Hazina kiasi cha shilingi milioni 515 kwa ajili ya kuwakopesha wanawake wajasiriamali.

Wizara imeshaanda utaratibu wa ugawaji wa fedha hizo ambapo Halmashauri zote mpya zitapatiwa shilingi milioni 7 na halmashauri ambazo zillshapatiwa fedha za mfuko hapo awali zitapatiwa shilingi milioni 12 baada ya kurejesha fedha walizopatiwa. Wizara yangu imeshawasiliana na Mikoa na Halmashauri husika juu ya kukamilisha taratibu za kujaza mikataba ili wapatiwe fedha za Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi idadi ya wanawake watakaofaidika na fedha za Mfuko wa Maendeleo ya wanawake kwa mwaka wa fedha 2013/2014 itajulikana baada ya Halmashauri kupatiwa fedha hizo. Wizara imeshaandaa utaratibu nzuri wa kufuatilia utendaji wa Mfuko katika Halmashauri nchini.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Waziri kwa majibu mazuri na kuishukuru sana Serikali na Bunge letu Tukufu kwa kurejesha huu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ambao ulikuwa umeondolewa kwa miaka mingi mfululizo. Naomba kuuliza maswali ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

La kwanza, ni vigezo gani vilivyotumika vyta kuchagua hizi Halmashauri katika hizi Halmashauri za zamani. Ni vigezo gani vilivyotumika?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AMINA N. MAKILAGI]

Je, ni Halmashauri ngapi zitapatiwa fedha hizi katika hii robo ya kwanza ya mwaka? (*Makofii*)

Lakini swalii la pili, ningependa pia kujua kwa kuwa mfuko huu wa shilingi billioni 2 hautoshi. Lakini vile vile kwa kuwa fedha zilizotengwa za milioni 500 pia bado ni chache. Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inaongeza mfuko huu lakini vile vile na kuhakikisha fedha zinakwenda zote kama zilivyopangwa ikiwa ni pamoa na kuelekeza Halmashauri zote hapa nchini kutenga asilimia 10 kwa ajili ya vijana na wanawake? Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Wizara tunapenda sana kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa kuhakikisha kwamba fedha za mfuko wa maendeleo ya wanawake zinatengwa. Yeye na Kamati yake tunawashukuru sana.

Kuhusu sasa vigezo viliviyotumika kwa zile Halmashauri za zamani Mheshimiwa Mwenyekiti nataka kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba tumetazama ni Halmashauri gani zimerejesha fedha, Halmashauri gani zinadaiwa.

Kwa hiyo, zile ambazo zimefanya vizuri ndiyo tumeziingiza katika awamu ya kwanza ya kupatiwa fedha za mfuko wa maendeleo ya wanawake kwa mwaka huu wa fedha. Na kwa hiyo, tuna Halmashauri mpaka dakika hii katika hizi shilingi milioni 515 tumeshachagua Halmashauri 16 ambazo zitapata fedha na nyingine tutazipatia kadri tutakavyopata fedha.

Lakini swalii lake la pili ni vipi basi billioni 2 zitaweza kutengwa na pia ni vipi Halmashauri zitachangia. Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwathibitishie wanawake wa Tanzania hasa wanawake wa Chama cha Mapinduzi kuititia dada Amina kwamba hii ni ahadi yetu tumeahidi katika Ilani ya Uchaguzi naamini kwamba tutaweza kupata fedha Hazina ili wanawake wengi waweze kukopeshwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO]

Kwa sababu tunaamini nguvu ya kumkopeshwa mwanamke kiuchumi ina matokeo makubwa sana na ya haraka sana katika maendeleo ya wanawake. Sasa swali la pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vipi sasa Halmashauri zitaweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati tutakaoutumia ni kuzitangaza zile Halmashauri ambazo zinafanya vizuri na kuzitangaza zile Halmashauri ambazo hazifanyi vizuri. Katika *ma-pegion hole* yenu mtaona kwamba tumeweka karatasi ya kuonyesha Halmashauri gani, mapato yake ya ndani ni kiasi gani na inatakiwa kutenga kiasi gani cha fedha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kuititia Mabaraza ya Madiwani kuhakikisha kwamba tunatenga asilimia 5 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Mwongozo uliotolewa na Wizara kuhusu Halmashauri kutenga fedha za hiyo Mifuko ya Vijana na Wanawake mwongozo ule umepitwa na wakati na niliwahi kuuliza hapa Bungeni ni lini mtabadilisha ule mwongozo. Lakini mpaka leo mwongozo haujabadilishwa. Tunataka kupata kauli ya mwisho ya Serikali lini mtabadilisha huo mwongozo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchakato mzima wa kuboresha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa Mwaka huu wa fedha mojawapo ya eneo ambalo tunalifanya kazi ni kudurusu mwongozo kuboresha ni Halmashauri kutenga fedha za hiyo mifuko ya vijana na wanawake, mwongozo ule umepitwa na wakati. Niliwahi kuuliza hapa Bungeni ni lini mtabadilisha ule mwongozo, lakini mpaka leo mwongozo haujabadilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kupata Kauli ya mwisho ya Serikali ni lini mtabadilisha huo Mwongozo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Cecilia Pareoso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Katika mchakato mzima wa kuboresha Mfuko wa Mendeleo ya Wanawake kwa Mwaka huu wa Fedha, mojawapo ya eneo ambalo tunalifanya kazi ni kudurusu mwongozo kwa ajili ya uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Tayari Wizara yangu imeshakaa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ambayo ndio inatusimamia, katika kukubaliana na pia Kamati ya LAAC. Kwa hiyo, tayari mwongozo tunaufanya kazi. Tunaamini kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha tutakuwa tayari tumeu-review. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

Na. 167

### **Upatikanaji wa Nishati Mbadala ya Kupikia**

**MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MARTHA M. MLATA)** aliuliza:-

Miti mingi inakatwa kwa ajili ya kuni na mkaa vijijini. Ili kupunguza ukataji wa miti, nishati mbadala (kama umeme na *solar*) kwa ajili ya kupikia inahitajika:-

(a) Je, ni nani mwenye dhamana ya kusambaza *solar* vijijini na mahali pengine ambako kuni na mkaa hutumika kupikia?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu suala hilo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Martha Mlata, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ina jukumu la kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za usambazaji wa nishati ikiwemo *solar*.

Hata hivyo, mifumo midogomidogo ya *solar* inayotumika vijiji na maeneo mengine haina uwezo wa kutumika kupikia kwa sababu, umeme wake ni mdogo, lakini kwa mifumo milkubwa ambayo uwekezaji wake ni mkubwa pia, unaweza kutumika kwa kupikia. Aidha vyanzo mbadala vinavyoweza kusaidia kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti ni matumizi ya nishati mbadala kama vile majiko banifu, *bio-gas*, mabaki ya mimea na gesi ya mitungi (*Liquified Petroleum Gas*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nishati ya *solar* kwa vijiji na maeneo mengine nchini ni muhimu kwa matumizi mbalimbali kama vile kutoa mwanga majumbani na katika taasisi za afya na elimu. Katika vifaa vinavyotumia umeme mdogo kama kuchaji simu za mkononi na upozaji (*Refrigeration*) wa vifaa vya afya kwenye zahanati na majumbani pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, inawaasa wananchi watumie nishati mbadala zinazopendekezwa hapo juu katika kipindi hiki wakati Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa bomba la gesi na mara baada ya mradi huo kukamilika kutakuwepo na uwezekano mkubwa wa wananchi wengi kutumia gesi asilia kwa gharama nafuu kwa matumizi ya majumbani.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, taasisi za Serikali ndio waharibifu wakubwa wa mazingira na hasa Magereza na Shule za Sekondari, kwa kutumia kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia.

Je, Serikali iko tayari kuonesha mfano kwa taasisi zake kutotumia mkaa na kuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa, ukataji wa miti ni uharibifu mkubwa wa mazingira. Na kwa kuwa, sasa hivi Serikali inafanya utaratibu wa kuweka bomba la gesi kutoka Mtwara na kusambaza katika Mikoa mbalimbali.

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa elimu kwa wananchi wake ili kwamba, gesi itakapofika kwenye maeneo mbalimbali kwa wananchi, watumie bila kusita?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, taasisi nydingi vikiwemo vyuo, zikiwemo sekondari ambazo zinatumia kuni badala ya teknolojia hizi nilizosisema katika jibu langu la msingi zinaongeza kwa kiasi kikubwa ukataji miti.

Nichukue nafasi hii kuona kwamba, wito na maoni yanayotolewa na Mheshimiwa Mbunge hapa ni muhimu na sisi tutayazingatia kama Serikali, tuone ni namna gani tunaweza tukahamia kwenye teknolojia ya matumizi ya gesi na aina nydingine za nishati kwa sababu teknolojia hizi zipo. Aidha tumekuwa tukiziona teknolojia hizi kwenye maonesho mbalimbali yanayofanyika ya maendeleo ya sayansi na teknolojia hapa nchini. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. SIMBACHAWENE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili ni juu ya elimu huku tukiwa tunasubiri ujio wa gesi ambayo itakuwa nyingi. Nichukue nafasi hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba, *TPDC* wameanza kutoa elimu hiyo. Lakini naamini kasi kubwa inahitaji kuongezeka ili gesi itakapofika wananchi wengi hadi wa vijijini wawe wamejua matumizi ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi ambao sasa hata katika Kiwilaya unakuta wanatumia *LPG gas*. Lakini pia hata maeneo ya vijijini baadhi ya watumishi tumeona wanafanya hivyo; basi elimu hii tutaiendeleza kwa kasi kubwa.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua juhudni kubwa za Serikali sasa hivi za kusambaza umeme hata maeneo ya vijijini. Lakini kuna baadhi ya vijiji viko mbali kidogo na itakuwa kazi kufikiwa na umeme huu wa kawaida.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu, ili wananchi hasa jamii za kifugaji wawze kupata na wenye we nishati ambayo itapunguza uharibifu wa mazingira?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kamani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, sio rahisi hata katika utekelezaji wa miradi hii ya umeme ya awamu ya pili ya *REA* kwamba, tutaweza kufikia maeneo yote ya nchi hii. Lakini ni kweli pia kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema ni kwamba, lazima njia mbadala itumike katika kuhakikisha kwamba na wenzetu ambao hawatafikiwa sasa wanapata nishati nyingine.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. SIMBACHAWENE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajitahidi kuchukua maoni hayo ingawa tumeshaanza sasa na tumeweza kuweka programu mbalimbali ikiwemo ile programu ya *TEDAP* ambayo imefanyika katika Mikoa ya Sumbawanga Vijijini, Geita, Bunda na Iramba.

Lakini pia na Kanda ya Ziwa juu ya matumizi ya nishati mbadala kwa mwanga na kwa shughuli nyingine. Tutaendelea kufanya hivyo kwa maeneo hayo ambayo hayatakuwa yamefikiwa na umeme huu tunaotarajia kuusambaza wa *REA* awamu ya pili na miradi mingine.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza swali:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Nalbu Waziri, ningependa kumuuliza swali moja tu. Kwa kuwa, wananchi wengi wamehamasika sasa hivi kwa kutumia gesi ya *Liquidified Gas* kupikia katika majumba yao. Kwa vile siku chache zilizopita hii gesi imeongezeka tena bei, imewakatisha wananchi wengi tamaa ya kununua gesi.

Je, Serikali inasemaje kama itakuwa tayari kutoa ruzuku kwa ajili ya gesi ya matumizi ya majumbani, ili Watanzania walio wengi waweze kuinunua na kuitumia ili tupunguze matumizi ya mkaa? (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Dkt. Lucy Nkya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kasi ya matumizi na hasa kutohana na faida zake za matumizi ya *LPG* kwa maana ya gesi kama chanzo cha nishati, yamepokelewa vizuri sana na wananchi na ndio maana biashara hii ya mitungi ya gesi imekuwa kubwa. Matarajio yetu hapa ni kwambamatumizi haya ya gesi yakienda mpaka vijijini tutapunguza kwa kiasi kikubwa ukataji wa miti. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. SIMBACHAWENE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue maoni ya Mheshimiwa Mbunge na kwa sababu, suala hili ni suala mtambuka tuone wapi pamesababisha hiyo bei kupanda nap engine ni nini kifanyike. Kwa sababu, ni ukweli kabisa kwamba, kama gesi itauzwa kwa bei ambayo wananchi wote wanaiweza, tutapunguza sana uharibifu wa mazingira na hivyo kuleta faida pana zaidi kwa nchi yetu. (*Makofii*)

Na. 168

### **Hitaji la Umeme Katika Vijiji vya Wilaya ya Nzega**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliliza:-

Je, ni lini Wananchi wa Vijiji vya Lububo, Mwamala, Mwangoye, Sojo, Mogwa, Mbutu na Mambali katika Wilaya ya Nzega watapata huduma ya nishati ya umeme, illi waweze kuanzisha viwanda vidogo-vidogo na shughuli nyingine za kiuchumi za kuongeza thamani ya mazao yao ya kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Selemeni Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapeleka umeme katika vijiji vya Mwangoye, Wambali pamoja na vijiji vya jirani vya Ntubugo, Nangahe, Shimulwa, Kilabili, Polisi na *Market*, kupitia mpango kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili chini ya Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*). Mkandarasi wa kutekeleza miradi hii katika Mkoa wa Tabora amekwishapatikana, ambaye ni Kampuni ya *China Henan International Corporation Group Company Limited* wakishirikiana na Kampuni nyingine ya *China National Electric Wire and Cable* na tayari utekelezaji wa miradi umekwishaanza.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. SIMBACHAWENE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za mradi zitajumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa *Kilovolt* 33 yenye urefu wa kilometra 90.5, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa *Kilovolt* 0.4 yenye urefu wa kilometra 33.5, ufungaji wa *transformer* 8 na kuwaunganisha wateja wa awali wapatao 1,203. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 4.54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Mbutu na Mongwa tayari vimefanyiwa usanifu na taarifa zimewasilishwa kwa Wakala wa Nishati Vijiji kwa ajili ya Utekelezaji. Aidha, Vijiji vya Lububu, Mwamala na Sojo, vimewekwa kwenye awamu ya pili ya mradi kama nyongeza na vitakabidhiwa kwa mkandarasi husika, ambaye atafanya tathmini na kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya wananchi wa Bukene, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yenye matumaini na kwamba, sasa Vijiji vya Lububu, Mwamala, Mwangoye, Sojo, Mbutu, Mogwa na Mwambali, vimo katika Mpango wa Awamu ya Pili ya mpango kabambe wa *REA*. Aidha sasa Mkandarasi amepatikana na kazi imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuuliza tu ni lini mpango huu wa pili wa utekelezaji wa *REA* unatarajija kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selemani Zedi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru kwa kutupongeza. Lakini pili, mpango huu unatarajia kumalika mwakani, kwa maana ya mwaka 2014 wakati wowote kabla ya mwezi Oktoba, ingawa tunamatatarajio ya kama hakutakuwa na matatizo yoyote na kasi ya watendaji hawa ikawa nzuri, hawa wakandarasi, tunaweza tukafanya, sio kwa miradi yote, baadhi ikakamilika hata kabla ya wakati huo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hivi karibuni Serikali, ilizindua mtambo wa kufua umeme kule Mwanza, pale Nyakato, ambao tuliamini kwamba, ungefanya umeme ukawa wa uhakika Jiji la Mwanza pamoja na Mkoa mzima wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kwamba, umeme unakatika-katika sana Mwanza. Sasa ningependa kupata Kauli ya Serikali. Je, kuna mgao Jiji la Mwanza na Mkoa wa Mwanza au tatizo ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Wenje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kwa takribani siku mbili tatu hivi, umeme umekuwa ukikatika-katika sio maeneo ya Mwanza tu ni pamoja na Mbeya pia, Mheshimiwa Zambi aliniambia jana kwamba, pia kumekuwa kuna shida na hasa *line* inayokwenda mpaka kule Tunduma. Tatizo hili linachangiwa pia na miundombinu yetu, lakini tunajaribu kuona kwa nini *Gridi* inakuwa inashuka-shuka na kupanda. Kunaweza kukawa kuna shida ya kiufundi, lakini hadi sasa si mgao na hatujafika hapo na ikifika hatua hiyo, tutalitangazia Taifa.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa kuwa mradi wa usambazaji umeme awamu ya pili umeanza kwenye baadhi ya maeneo kwa wakandarasi kupatikana, lakini kwa miradi ya Mkoa wa Shinyanga hatuna taarifa zozote kwamba mradi umefikia hatua gani.

Je, Waziri anaweza akatuambia Mradi wa REA awamu ya pili kwa Mkoa wa Shinyanga utaanza kutekelezwa lini?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *REA* awamu ya pili Mheshimiwa Waziri alisema jana hapa kwamba, wakandarasi wote hadi ifikapo tarehe 30 Januari, 2014 watakuwa wameingia kazini.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi na mimi nipate kuuliza swali moja tu la nyongeza. Maeneo mengi ambayo tayari yameshapimwa alama zilizowekwa ni za muda tu, wamechomeka-chomeka miti hivi; kama wananchi wetu hawataona nguzo zinakwenda kupelekwa wana uwezekano kabisa wakapata hasira wakaanza kutupa zile mambo zilizochomekwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri, atuhakikishie hapa. Kule Chemba na kule Kondoa kwa Mama Zabein, ni lini kazi hiyo inaanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nkamia, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alama zimewekwa, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, sio tu alama zimewekwa kwa kutumia zile mambo, lakini tunatumia teknolojia ya kisasa zaidi ya *coordinates*. Kwa hiyo, zile alama ziliikuwa ni za msingi tu, lakini zile zimechukuliwa *coordinates* kwa hiyo, tunaangalia kwenye taaluma ya juu zaidi ambayo tunaangalia hata kwenye ma-websites. Kwa hiyo, usiwe na mashaka juu ya alama zile. Lakini juu ya Chemba lini kazi inaanza, Mkandarasi sasa hivi yuko kazini anaitwa *Demi Engineering*. Mheshimiwa Zabein Mhaji Mhita na Mheshimiwa Nkamia, msiwe na mashaka. (*Makofii*)

**Mradi wa Kupeleka Maji Kagongwa na Isaka**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Zipo ahadi nyingi za kupeleka maji katika Miji Midogo ya Kagongwa na Isaka, ikiwa ni pamoja na ahadi ya Rais ya mwaka 2008 na pia Kauli ya Serikali kuwa, mradi huo uunganishwe na ule wa kupeleka maji Tinde, Nzega, hadi Tabora, kitu ambacho kitachelewesha utekelezaji wa mradi wa awali:-

(a) Je, kwa nini Serikali, isitekeleze kwanza ahadi ya Rais ya mwaka 2008 ndipo ahadi nyingine zifuate?

(b) Je, ni lini hasa huu mradi wa Kagongwa na Isaka kutoka kahama utaanza?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kutatua tatizo la maji Isaka ambalo ni kubwa, kabla ya mradi wa Ziwa Viktoria kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa MaJi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rais, aliahidi kupeleka maji ya ziwa Viktoria kwenye mji wa Kagongwa, Isaka na Tinde kutoka mradi mkubwa wa Kahama – Shinyanga.

Ili kutekeleza ahadi hiyo, Serikali inaendelea na utaratibu wa kumpata Mtaalamu Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa mradi wa maji safi kutoka Ziwa Viktoria kwenda miji midogo ya Kagongwa, Isaka na Tinde.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Hivi sasa tathmini ya kiufundi (*Technical Valuation*) na kifedha (*Financial Valuation*) zimekamilika, Mtaalamu Mshauri ataanza kazi mara baada ya kusaini Mkataba mwezi Januari, 2014.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ujenzi wa mradi wa Kagongwa na Isaka itaanza baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuni. Ujenzi utaanza katika Mwaka wa Fedha 2014/2015.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua tatizo la maji katika mji wa Isaka kabla ya mradi wa Ziwa Viktoria kukamilika, Serikali katika kipindi cha mwaka 2008 - 2011 ilitumia kiasi cha shilingi milioni 130 kwa ajili ya ununuzi wa pampu na ukarabati wa miundombinu ya maji.

Aldha, Serikali kupitia Halmashauri ya Msalala kwa mwaka 2013/2014 imetoa shilingi milioni 59.3 kufanya ukarabati wa kisima kinachotoa huduma ya maji safi na kununua pampu mpya katika mji wa Isaka. Serikali pia kupitia KASHIWASA imeanza utekelezaji wa mradi wa vijiji 100, mradi huo utahusisha vijiji 17 vya Wilaya ya Msalala. (*Makofii*)

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kwa taarifa na jibu hili mradi huu wa maji kwenda Isaka, hautaanza sasa pengine unaweza ukaanza hata baada ya mwaka ujao. Na tatizo la maji Isaka ni bkubwa, pamoja na jitihada za kuweka pampu ambayo ameisema Waziri, bado tatizo lipo.

Je, Serikali, iko tayari kutusaidia kuwabana wenzetu wa Shirika la reli ambao wana kisima kwenye Kitongoji cha Shilabeli ambao wamekuwa wakiwakataza wananchi wasitumie maji ya kisima chao, ili waruhusu maji yale yaunganishwe na mtandao wa maji Isaka, ili watu wapate maji mengi zaidi?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. EZEKIEL M. MAIGE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, upande wa Kaskazini wa Jimbo la Msalala, Kata za Bugarama na Bulyanhulu zina matatizo makubwa sana ya maji na majirani wa Kata hizo ambao ni Mgodi wa Bulyanhulu...

### **MWENYEKITI** Swali?

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh, swali la pili; Mgodi wa Bulyanhulu wamekubali kufadhili mradi kwa nusu ya gharama ya mradi kutoka Ziwa Viktoria. Je, Serikali, iko tayari kuchangia nusu ya gharama itakayokuwa imebaki katika utekelezaji wa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ezekiel Maige kama ifuatavyo. Lakini nimshukuru kwa pongezi alizozitoa na mimi nampongeza sana yeze kwa jinsi anavyofatilia miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Nishauri kwamba kwakua hicho kisimia kinachosimamiwa na Shirika la reli kiko kwao pale Msalala basi wao wafanye maongezi na wakiona kwamba tunatakiwa kushiriki katika maongezi hayo tuko tayari kuyafanya maongezi ili tuone namna hicho kisima kinavyoweza kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwanza nitumie fulsa hii kuwashukuru sana wenzetu wa Mgodi wa Bulyankulu ambao wako tayari kutoa nusu ya gharama kwa ajili ya ujenzi wa miradi, katika Mji huo wa Isaka. Mimi niseme tu kwamba sisi Wizara tuko tayari kikubwa watuletee yale makubaliano na tuone namna gani ya kuweza tunaweza tukashirikiana kutekeleza huo mradi. Sisi Wizara na Halmashauri ya Msalala.

**MHE. SLVESTIRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona Mradi mkubwa wa maji kutoka Ruvu juu kipitia Kibaha kuelekea mpaka Kimara, wa bomba lenye kipenyo cha mita moja ulikuwa uanze toka mwanzoni mwa mwaka huu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SLVESTIRY F. KOKA]

Je, nini tatizo ambalo linazuia mradi huo mkubwa ambao utawapatia wananchi wa Kibaha maji bila tatizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba nimjibu Koka kama ifuatavyo. Ni kweli tuna mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ruvu juu kwenda Dar es Salaam, ambao umepangwa kuongeza kutoka lita milioni 82 mpaka lita milioni 96 na utekelezaji wake umeanza na mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya India kwa Dola milioni 78 sisi upande wetu tumeshafanya kazi zote za kutafuta mtalaamu, mshauri ameishapatikana, wakandarasi wa kuanza ujenzi amekwishapatikana na ilikuwa ianze mwezi wa Septemba, 2013 lakini kabla hatujaanza ujenzi lazima tupate kibali cha wenzetu wa India, ili tuweze kuendelea. Kwa hiyo, tunasubiri kibali wakati wowote kikitoka mradi huu utaanza kutekelezwa.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi mingi ambayo sasa hivi inasusua ya Benki ya Dunia, imekuwa ni tatizo kubwa katika maeneo mengi ya Nchi yetu na hasa ukizingatia hasa maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba kuiuliza Serikali kwa nini sasa hivi tusitafute fedha maalum (*special fund*) ili kuhakikisha kwamba miradi hii ambayo inasusua iweze kunasuliwa. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hii imechukua muda mrefu ilianza kutekelezwa mwaka 2007, mpaka ikaanza kujengwa rasmi mwaka 2012. Kutoka 2007 mpaka 2012 tatizo kubwa ilikuwa ni hivi vibali, *No Objection* ambavyo Mheshimia Waziri alianza kuvitoa mwaka mwezi Aprili, 2013 mwaka huu wakati wa Bajeti, miradi hii ndiyo imeanza kutekelezwa kwa kasi kubwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoonge tayari vijiji 193 miradi imekamirika na tayari miradi 854 inajengwa. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwamba miradi hii sasa inatekelezwa kuanzia 2012 inajengwa.

Lakini sasa kuhusu suala la kuongeza fedha, Wizara inafanya juhudhi mbalimbali za kutafuta fedha na hasa Mheshimiwa Waziri amekuwa akikutana na wafadhili mbalimbali na tutaendelea kufanya hivyo. Lakini sehemu ya pili ni hapa Bungeni, nimwombe Mheshimiwa Mtutura wakati wa Bajeti watupitishie maombi yetu wanaweza wakatuongeza ili tuweze kutekeleza miradi hii ya maji.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mradi wa maji ya Ziwa Victoria unaonekana utachukua muda mrefu sana mpaka ukamilishaji wake, Mheshimiwa Naibu Waziri je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu mkubwa wa kutafuta njia mbadala ili wananchi wa Kagongwa, Isaka na Tinde waweze kupata huduma ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo. Ni kweli utekelezaji wa mradi utachukua muda mrefu lakini suala la msingi ni kwamba tumekwisha anza, na Mheshimiwa Mbunge kama Serikali iliweza kupeleka maji Kahama na Shinyanga, sidhani kama itashindikana kupeleka miji hii Kagongwa, Isaka na Tinde kwa hiyo ni mchakato utakamilika na watu watapata maji. Lakini nini tunafanya sasa kwa Mji wa Kagongwa pale kuna mradi wa vijiji 10 na umetangazwa na unajengwa. Na pale Tinde pia tuna mradi wa vijiji 10 umetangazwa na unajengwa. Kwahiyoo kwa kipindi hiki, hii miradi ya vijiji 10 itapunguza tatizo la maji wakati tunasubiri huu mradi mkubwa.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Katika Wilaya ya Kilombero Mji wa Ifakara, takribani watu 100,000 na kuna shida ya maji, na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SUSAN L. A. KIWANGA]

Halmashauri ilishaomba kupatiwa hela za upembuzi katika chanzo cha Kiburugutu. Halmashauri ilishaleta ombi tangu wakati wa Bajeti iliyopita la shilingi Milioni 500 ili kuboresha ule upembuzi lakini mpaka leo Serikali haijajibu lolote. Je, wananchi wa Kilombero na Halmashauri nini kauli ya Serikali ya kuhusu kuboresha mradi huu wa kuburugutu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niamba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swalii la nyongeza kama ifuatavyo. Ni kweli haya maombi nayakumbuka na nimwombe Mheshimiwa Mbunge, nifatilia nione utekelezaji umefikia wapi lakini ni nahakika kwenye Bajeti hii tulionayo fedha zitakuwa zimetengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa maji pale Ifakara. (Makof)

Na. 170

### **Ujenzi wa Barabara ya Kibaoni - Mlowo Kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza mchakato wa ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Kasansa, Kasansa - Muze, Muze - Mtowisa – Illemba – Kaoze, Kaoze- Kilyamatundu na Kilyamatundu – Mlowo, kwa kiwango cha lami?

### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kibaoni- Kasansa- Muze, Muze - Mtowisa, Mtowisa- Illemba- Kaoze, Kaoze- Kilyamatundu na Kilyamatundu – Mlowo, yenye jumla ya (km 355) ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kuititia Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Barabara hii inaunganisha Mikoa ya Katavi, Rukwa na Mbeya.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kuimarisha mawasiliano ya barabara kwa kuanzia kujenga daraja la mto Mombasa. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imetenga Bajeti ya shilingi bilioni 2.294 kwa ajili ya kugharamia kazi ya usanifu na kuanza ujenzi wa daraja hilo. Mhandisi Mshauri *M/S ENV Consult (T) Ltd.* ameshaanza kazi ya usanifu wa kina wa daraja hili. Gharama za mkataba wa Mahandisi Mshauri huyo ni shilingi milioni 419,655. Aidha, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya kuifanya matengenezo mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika majira majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali haina mpango wa karibuni wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Serikali itaendelea kuifanya matengenezo barabara hii ili kuhakikisha kwamba inapitika majira yote. (*Makofî*)

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri na hasa kwakutambua umuhimu wa Daraja la mto Mombasa.

Pamoja na majibu hayo ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Barabara hiyo ilianzishwa enzi za Ukoloni, hii ni kutokana na umuhimu wake Kiuchumi. Bodi ya barabara ya Mkoa wa Rukwa ilipendekeza na kuomba barabara hiyo itengenezwe kwa kiwango cha lami, kupitia mfuko wa *MMCC TWO*.

Je, Serikali imeweka mkazo gani kuunga mkono mapendekezo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, *Consultant* aliyeefanya matengenezo ya barabara hiyo kwa mara ya kwanza kupitia Shirika la Danida, Madaraja na Kalvati yaliyotengenezwa ni chini ya kiwango hadi kusababisha *TANROADS* Mkoa wa Rukwa wa kuziba matundu mara kwa mara wakati mwingine Daraja linakuwa na vilaka zaidi ya vitatu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. IGNAS A. MALOCHA]

Je, Serikali haioni kuwa inahatarisha maisha ya wananchi wanaotumia barabara hiyo?

Je, ni lini Serikali itatenga pesa za kutosha ili kutengeneza madaraja upya?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malocha, Mbunge Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo.

Kwanza nimpongeze kwa namna anavyofuatilia matengenezo ya barabara hii. Miradi ya *MMCC TWO* tumepeleka mapendekezo lakini bado hatujainisha. Hii ni sababu tumepata *list* kubwa, kila Mkoa umeleta list kubwa.

Kwa hiyo, hatujainisha ni barabara zipo na kwa kiasi gani itatengenzwa. Kwa hiyo, hiyo taarifa tutakuja kuitoa baadaye tutakapofikia muafaka pamoja na wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalii lake la pili, kuhusu madaraja ambayo yalitengenezwa chini ya kiwango. Tunazo fedha za mfuko wa barabara ambazo huwa tunatumia pamoja na kutengeneza barabara tunashughulikia kutengeneza na kuimarisha madaraja ili kusudi barabara ile iweze kuwahudumia wananchi wakati wowote wa mwaka.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Awali ya yote naomba niishukuru Serikali kwa hatua iliyofikiwa ya kusaini mkataba pamoja na Wakandarasi wawili kuhusu barabara ya kutoka Mayamaya mpaka Bonga tarehe 2 Desemba, 2013. Pamoja na shukrani, naomba niulize. Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kujengwa kwa barabara kutoka Bicha kwenda Kondoaa Mjini (km. 5), kilomita tatu (km.3) zimeshajengwa.

Je, ni lini kilomita mbili (km.2) tu, zilizobaki zitajengwa kwa kiwango cha lami?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Mhita, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imeshajenga barabara inayotoka Bicha mpaka Kondoa. Pia barabara ya kutoka Babati mpaka Bonga na sasa hivi tumeshasaini mikataba miwili ya kujenga barabara *The Great North Road* kutoka Mayamaya, Mela, mpaka Bonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hiyo anayozungumza ni barabara ambayo iko chini Halmashauri ya Mji wa Kondoa. Kwa kuwa ni ahadi ya Rais namshauri kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kondoa aiweke kwenye mipango ya Serikali ili kusudi hizo km 2 anazozungumza Mheshimiwa Mbunge ziweze kujengwa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa swali la msingi naulizia bonde la Mto Rukwa na vijiji barabara inapopita ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. Maeneo ya Muze, mpaka huku kilyamatundu, Kaoze, nenda mpaka Mkoani Mbeya, pamoja na Wilaya ya Nkasi maeneo ya Kala na tarafa yote ya Wampembe.

Kwakuwa Serikali haina mpango wa kuweka lami muda mfupi Mheshimiwa Waziri ni *Engineerhamuwezi* mkaja na *chemical* nyngine *stabilization chemical Materials* kwa ajili ya kuimarisha barabara hizi pamoja na *drainage system* yake ili ziweze kukuza uchumi wa Taifa letu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa James Mbatia, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti wazo lake nila msingi kwamba tunaweza tukana na njia nyngine mbadala za kuimarisha hizi barabara za changarawe kuliko kuendelea tu kufkiria tu kujenga kwa kiwango cha lami. Swali la msingi lilikuwa linahusu katika kujenga kwa kiwango cha lami na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

mimi nimesema katika matengezo ya barabara sehemu kubwa tunatumia changarawe, lakini kuna maeneo mengine tunaona kama kuna umuhimu tunaweza tukachukua hilo wazo la Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, katika Bajeti iliyopita Waziri wa Ujenzi aliahidi kwamba barabara ile *daivation* yakutoka Uyole kwenda Mbalizi hadi kule Songwe ingewezwa kujenga nilitaka Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze barabara hiyo itaanza lini na matumizi yake yataanza lini.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swalil la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifuatilie niweze kuona ahadi hiyo imekaa vipi ili niweze kukupa jibu linalofaa lini itaanza kutekelezwa.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa majibu mazuri. Tunaendelea Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Arfi.

Na. 171

### **Ujenzi wa Barabara ya Mpanda Hadi Uvinza**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Mpanda hadi Uvinza itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziriwa Ujenzi, napenda kujibu swalil la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mpanda-Mishamo - Uvinza yenyeye urefu wa kilometa 194 ni sehemu ya barabara kuu inayoanzia Tunduma - Sumbawanga- Mpanda - Uvinza - Kigoma mpaka Nyakanazi Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuunganisha Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma kwa barabara ya lami, Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mpanda-Uvinza yenyeye urefu wa km. 194 kwa kiwango cha lami. Kazi ya upembuzi, yakinifu, usanifu wa kina na tathmini ya atahari kwa mazingira kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imetenga fedha kiasi cha Shilingi bilioni 4,539,210,000 kwa kuanza ujenzi wa barabara hii katika Mpanda hadi Mishamo yenyeye urefu wa kilometa 100 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea kutufuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali vyana ndani na nje ili kukamilisha ujenzi wa barabara hii.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nikushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, kwa majibu yako mazuri yenyeye kutia faraja kwa watu wa Mpanda, nilikuwa na mswali mawili ya nyongoeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Bajeti 2013/2014 kutenga bilioni 4.539 na ujenzi wa barabara hii kuanza nilikuwa nataka kujua ni mkandarasi gani amepewa barabara hii na itakamilika katika kipindi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naamini Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kwamba barabara hii haishii Nyakanazi tu, barabara hii inaanzia Kyaka mpakani mwa Uganda na Tanzania na inaishia Kaseshyia mpakani mwa Tanzania na Zambia. Ikiunganisha Nchi nne za Jumuia ya Afrika Mashariki, kwa maana ya Uganda, Tanzania, Rwanda, Burundi na Nchi za Kusini mwa Afrika.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. SAID A. ARFI]

Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuimarisha barabara hii ili kukuza biashara kati ya Nchi za Afrika Mashariki na Nchi za Kusini mwa Afrika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Arfi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa shukuruni ambazo umezitoa kwa Serikali na pili kuhusu Mkandarasi, kama nilivyo sema kwamba tumewe ka fedha za kuanza ujenzi. Sasa ujenzi unakua na mchakato wa hatua za manunu zili tuweze kupata Mkandarasi. Tutaanza kwanza kwa kutangaza Tenda, ndiyo tutajua mdandarasi na tutakupa jina baada ya hapo Mkandarasi akiweza kupatikana.

Katika swali lako la pili, maelezo yako ni sahihi kwamba tukijenga barabara hii tutakuwa tumeimarisha biashara katika Nchi za Jumuia Mashariki na ndiyo maana tunasema kwamba barabara yote hii sisi tutajenga na usanifu wa wa barabara nzima umeshafanyika sasa hivi Serikali inatafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ndani na nje ili tuweze kuimaliza barabara yote km.194 kwa kujenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha. Wageni waliokuwepo Bungeni asubuhi hii. Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanakwaya 40 kutoka Chuo cha Mipango cha Mendeleo Vijiji hapa Dodoma. Karibu sana Bungeni. Wageni wengine ni wanachama 45 kutoka chama cha Wafugaji Tanzania CCWT karibuni sana Dodoma. Wengine ni mwanafunzi kutoka shule ya *Home Boys* ya Tanga na anaitwa Danford Danford, karibuni sana.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni watano wa Mheshimiwa Mch. Israel Yohana Natse, ambaye ni mke wake Bi. Wilmina Surumbu akiambatana na mtoto wao, karibu sana Bungeni. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MWENYEKITI]

Mgeni wa Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge, ambaye ni Mheshimiwa Leonada Mayala, Diwani wa Kata ya Nyasubi - Kahama, karibu sana Bungeni. Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Machali, Mbunge, ambaye ni ndugu Eugen Male, kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu John. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, mnaomba kutangaziwa kwamba leo tarehe 20 Decemba, 2013 baada ya kuhairisha kikao cha Bunge jioni kutakuwa na tafrija ya Wabunge kuipongeza kumaliza Mkutano wa Kumi na Nne Salama na pia kuipongeza timu ya mpira wa mikono ya Bunge kwa ushindi walioupata huko Kampala kwa walioshiriki michezo ya Jumuiya ya Mabunge ya Nchi za Afrika Mashariki. Kutakuwa na burudani mbalimbali ikiwe na vichekesho vya *standup comedians* wote mnakaribishwa. (*Makof*)

Mwenyekiti wa Bunge Sports anaomba kuwatangazia Wabunge kuwa timu ya *Bunge Sports Club* iliyokuwa Uganda kwenye mashindano wa mpira wa miguu na *Netball* ya Mabunge ya Afrika Mashariki imerejea. Matokeo, *Netball* timu yetu ya Bunge imeshinda na kuwa mabingwa kwa mara ya pili mfululizo katika fainali waliwafunga Uganda 35 kwa 33. (*Makof*)

Mpira wa miguu timu ya Uganda mpira miguu ndiyo imekuwa bingwa wa mara ya tatu mfululizo baada ya kuifunga *EALA* kwa magoli matatu kwa bila. Taarifa kamili ya ushiriki itatolewa rasmi baadaye.

Tuzo kwa wachachezaji: Mheshimiwa Grace Kiwelu, amepata tuzo ya kuwa mchezaji bora wa mashindano. Hongera sana Mheshimiwa Grace Kiwelu, kwa kutuletea sifa Bunge na Tanzania. Mheshimiwa Halima Mdee amepata tuzo ya mlinzi bora. *Goal Defence* wa mashindano haya. Hali kadhalika na wewe hongera sana. Mheshimiwa Iddi Azzan amepata tuzo ya goli kipa bora wa mashindano hayo. Hongera sana Mheshimiwa Iddi Azzan. (*Makof*)

Mheshimiwa Rage, huu ni ushauri wa bure tu. Kwa vile mashindano haya yalikuwa Uganda na Iddi Azzan

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MWENYEKITI]

ameonekana bora na Okwi anatoka Uganda, ni bora umweke Iddi Azzan kesho ili aweze kupambana na mikakati ya Emmanuel Okwi. (*Makofii/Kicheko*)

Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii anaomba kuwatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo ljamua tarehe 20 Desemba, 2013 saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo kikao hicho kitafanyika katika ukumbi namba 227 iliyopo gorofa ya pili jengo la utawala.

Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o anaomba kuwatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 20 Desemba, 2013 saa saba mchana, kutakuwa na kikao cha Kamati kikao hicho kitafanyika katika ukumbi namba 219 lililopo jengo la utawala. Nawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge sasa namwita Mheshimiwa Naibu Spika aje kuendelea na kikao. (*Makofii*)

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia kitu*

**NAIBU SPIKA:** Miongozo yote nitaipokea baadaye, Katibu tuendelee.

### **HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili  
na Mazingira Pamoja na Mapendekezo na  
Maoni Yaliyomo Katika Taarifa Hiyo**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ratiba yetu leo iko *tight* sana, utaratibu tutakaoutumia kwa shughuli za leo hapa tutajadili Kamati moja moja badala ya kufanya zote kwa wakati mmoja kama tunavyofanya siku zilizopita. Kwa hiyo, tutashughulika na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwanza halafu jioni tutaendelea na Kamati inayofuata. Sasa moja kwa moja naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU SPIKA]

Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, karibu uwasilishé Kamati yako, yeye tumempatia muda wa saa moja ya kuwasilisha taarifa yake. (*Makofii*)

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 114, 115 toleo la 2007 naomba kuwasilisha taarifa ya kazi zilizofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kipindi cha mwaka 2013 ili iweze kujadiliwa na Bunge lako Tukufu na kutolewa maamuzi.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi chote cha mwaka 2013 mawazo na ushauri wao umewezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Aidha napenda kuwatambua Wabunge hao kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Abdulkarim Ismail Shah - Makamu Mwenyekiti, wakati wajumbe wengine ni Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri, Mheshimiwa Sylvester Muhoja Kasulumbayi, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Kika Saning'o Telele, Mheshimiwa Mwanahamisi Kassim Said, Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, Mheshimiwa Salim Abdallah Turkey na Mheshimiwa Abu Mohamed Jumaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira yameainishwa katika Kanuni za kudumu za Bunge Nyongeza ya 8 Kifungu Namba 7 na 9(1) Toleo la 2013 kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara za nchi, ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

(ii) Kushughulikia masuala ya sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji wa Wizara zilizo chini ya Kamati hii.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizi kwa mujibu wa ibara ya 65(3)(b) ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kazi za Kamati zilizopangwa kufanyika mwaka 2013, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa mwaka 2013 ilipanga kufanya kazi zifuatazo.

(i) Kufanya mikutano mbalimbali ya Kamati na watendaji wa Wizara husika ili kujadili na kutathmini shughuli za Kamati, shughuli za Wizara husika na kutoa mawazo ushauri pamoja na maelekezo.

(ii) Kufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini ili kujionea miradi ya maendeleo na utekelezaji wa maendeleo zilizochini ya Wizara husika.

(iii) Kupitia na kujadili taarifa za utendaji za ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

(iv) Kuchambua bajeti za Wizara husika na kuchambua Miswada ya Sheria Maazimio na mikataba iliyopendekezwa kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizotekelzwa na Kamati kwa mwaka 2013:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya uchunguzi. Mnamo mwezi Novemba, 2013 Kamati hii ilipewa kazi maalum ya uchunguzi kuhusu matatizo yaliyosababishwa na utekelezaji wa Operesheni Tokomeza iliyotekelizwa na Serikali kuanzia tarehe 4 Oktoba, 2013 na kusitishwa kwa muda tarehe 1 Novemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa taarifa hiyo imekamilika na imeambatishwa na itasomwa sambamba na taarifa hii. Kwa kuwa taarifa hii ni ndefu naomba iingie katika kumbukumbu za taarifa rasmi za Bunge ili nitumie muda huu kuzungumzia taarifa ya uchunguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu tathmini ya matatizo yaliyotokana na operesheni tokomeza. Utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Bunge likijadili hoja ya kuahirishwa shughuli za Bunge ili kujadili jambo muhimu la dharura kwa mujibu wa Kanuni ya 47 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge kuhusu Mgogoro kati ya Wafugaji na Wakulima, Hifadhi na Uwekezaji, Mheshimiwa Spika alitoa Uamuzi '*Speakers Ruling*' kuwa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ishughulikie kazi ya kutathmini na kuangalia jinsi Mpango wa Kupambana na Majangili ulivyopangwa na kutekelezwa na Serikali kuitia 'Operesheni Tokomeza'.

Kwa mujibu wa kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge za tarehe 1 Novemba 2013, wakati Bunge likihitimisha Hoja ya Kuairisha Shughuli za Bunge, Mheshimiwa Spika alitoa uamuzi ufuatao:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Nina nukuu;...Kamati ile ya kawaida ya Maliasili itaendelea na kazi yake ya kufanya tathmini ya kuangalia jinsi mpango ule wa Kupambana na Majangili ilivyopangwa na ndani yake itashughulikia kama kulikuwa na uzembe ama kuna watu wanahuksika katika kuondoa maisha ya watu kwa sababu za uzembe ...

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuundwa kwa Kamati Ndogo ya Uchunguzi, kufuatia uamuzi ulioutoa tarehe 1 Novemba, 2013 Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ilikutana Dodoma tarehe 9 Novemba, 2013 kwa lengo la kujadili utaratibu wa kutekeleza jukumu hilo. Katika kikao hicho Kamati iliazimia kuunda Kamati Ndogo kwa mujibu wa Kanuni ya 117(18) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013 ili iweze kushughulikia suala hilo kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hadidu za Rejea, Wajumbe wa Kamati na muda wa kazi Kamati Ndogo ya Ardhi, Maliasili na Mazingira iliyoundwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa agizo lako la tarehe 1 Novemba, 2013, ilipewa Hadidu za Rejea Nne (4) zifuatazo:-

- (i) Kutathmini na kuangalia jinsi Mipango ya Kupambana na Majangili ilivyopangwa;
- (ii) Kuangalia kasoro zilizojitokeza katika kutekeleza mpango huo;
- (iii) Kutathmini iwapo kulikuwa na uzembe katika kutekeleza Operesheni Tokomeza ambao ulisababisha watu wasio na hatia kupoteza maisha na mali zao; na
- (iv) Kuchunguza migogoro ya Ardhi inayohusu Wakulima, Wafugaji na Wawekezaji kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Lembeli sekunde mbili tu namwona Mheshimiwa Tundu Lissu, amesimama.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama tu ku-draw attention ya kiti kwamba hiki kinachosomwa hakipo kwenye hii ripoti. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Kamati hii ilikuwa na kazi ya kutoa taarifa ya kazi zao za kawaida za Kamati za mwaka mzima ambazo ndizo nakala yake mnazo. Lakini vilevile Kamati hii ilikuwa imepewa kazi maalum kama Kamati katika sehemu zake kama alivyoeleza hawa kazi zao za mwaka mzima walipewa kazi maalum ya kufuatilia suala zima ya ile operesheni na namna ilivyofanyika.

Kwa hiyo, leo hapa wamewasilisha kazi walizozifanya kama Kamati mwaka mzima na vilevile wanawasilisha taarifa ya kazi maalum waliyopewa kazi ambayo anaifanya hivi sasa ni sisi ofisi ya Bunge uchapaji umeleta matatizo kidogo lakini baada ya muda si mrefu mtapata wote nakala naomba tumruhusu Mwenyekiti aendelee samahani hatukutoa ufanuzi wa mambo haya. (*Makofii*)

Kwa hiyo, uchangiaji utaendelea kwa yote mawili kwa taarifa ya kawaida ya Kamati na hili ambalo liliikuwa ni jambo maalum ambalo ninyi Bunge mlipenda lifanyiwe kazi na ripoti yake ndiyo hii. Mheshimiwa Mwenyekiti endelea.

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba muda wangu ulindwe tafadhalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ya uchunguzi iliundwa na Wabunge Tisa (9) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah, Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mheshimiwa Kaika Sanin'go Telele, Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Haji Khatibu Kai, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, ambaye hata hivyo hakuweza kushiriki kutokana na udhuru aliokuwa nao.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti iliyohudumia Kamati Ndogo ya Uchunguzi iliundwa Ndugu Theonest K. Ruhilabake, Ndugu Gerald S. Magili, Ndugu Chacha T. Nyakega na Ndugu Stanslaus W. Kagisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati Ndogo ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilitakiwa kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha ripoti katika Mkutano wa Kumi na Nne (14) wa Bunge. Hivyo basi, baada ya uteuzi huo, Wajumbe wa Kamati Ndogo walipanga kuanza kazi tarehe 25 Novemba, 2013 na kuikamilisha ifikapo tarehe 15 Desemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Njia zilizotumika katika kukamilisha kazi, Kamati Ndogo ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilitekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na Hadidu za Rejea ilizopewa kwa kufanya rejea na kuzingatia yafuatayo:-

(a) Kusoma na kuchambua nyaraka zilizoandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuandaa na kutekeleza Operesheni Tokomeza nchini. Nyaraka hizo ni hizi zifuatazo:-

(i) Mpango Kazi wa Operesheni Tokomeza (*Concept Paper*).

(ii) Tathmini ya Utekelezaji wa Operesheni Tokomeza.

(iii) Sheria ya Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge (Na.3) 1988.

(iv) Sheria ya Wanyamapor (Na. 5) 2009.

(v) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013.

(b) Kufanya mahojiano na watu mbalimbali:-

(i) Waziri wa Maliasili na Utalii.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

- (ii) Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii.
- (iii) Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamaporini na wasaidizi wao.
- (iv) Mkurugenzi Msaidizi Kikosi wa Dhidi ya Ujangili.
- (v) Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.
- (vi) Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*).
- (vii) Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*NCAA*).
- (viii) Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Hifadhi za Misitu (*TFS*).
- (ix) Mahojiano na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge.

(c) Kuzuru maeneo yaliyoanishwa katika Taarifa ya Wizara kuhusiana na utekelezaji wa Operesheni Tokomeza na yale yenye migogoro kati ya Wakulima au Wafugaji na Wawekezaji katika maeneo ya hifadhi kwa lengo la kuhakiki (*verify*) masuala yaliyoainishwa kupitia uchambuzi uliofanywa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupokea na kuchambua nyaraka mbalimbali zilizohusu operesheni tokomeza. Hadidu Rejea ya kwanza iliitaka Kamati Ndogo ya Ardhi, Malisili na Mazingira, kufanya tathmini na kuangalia jinsi mipango ya kupambana na majangili ilivyopangwa. Ili kukamilisha jukumu hilo, Kamati ilifanya yafuatayo:-

(a) Kupitia na kuchambua Mpango Kazi wa Operesheni Tokomeza (*Concept Paper*) ulioandaliwa na Wizara.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

(b) Kupitia na kuchambua Tathmini ya Utekelezaji wa Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi Kuhusu Mpango Kazi wa Operesheni Tokomeza. Katika kuchambua Mpango Kazi wa Operesheni Tokomeza kwa lengo la kupata uelewa zaidi wa namna operesheni hiyo ilivyopangwa na kutekelezwa, Kamati ilibaini kuwa, mpango huo uliandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na ulikuwa na mambo yafuatayo:-

- (i) Ukubwa wa tatizo la ujangili.
- (ii) Aina za ujangili na sababu za ukuaji wake.
- (iii) Maeneo yaliyoathiriwa zaidi na ujangili.
- (iv) Malengo ya Operesheni Tokomeza.
- (v) Njia zilizotumika kutekeleza operesheni.
- (vi) Maeneo ya operesheni na gharama za utekelezaji.
  
- (vii) Tamko la Serikali kusitisha Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukubwa wa tatizo la ujangili. Kamati ilibaini kuwa, tatizo la ujangili ni kubwa na limekuwa likisababisha idadi ya Tembo au (Ndovu) iendelee kupungua nchini. Takwimu zinaonesha kuwa, idadi ya Ndovu imepungua kutoka 350,000 (miaka ya 1970) hadi kufikia 55,000 (mwaka 1989).

Juhudi za kukabiliana na hali hiyo kupitia Operesheni zilizowahi kutekelezwa huko nyuma zilisaidia kuongeza idadi ya Ndovu hadi 141,000 (mwaka 2006) ingawa ilishuka tena hadi kufikia 110,000 (mwaka 2009).

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Naibu Spika, Aina za ujangili na sababu za ukuaji, wake. Kwa mujibu wa Taarifa ya Serikali, vitendo vya ujangili vinavyofanyika nchini vimegawanyika katika makundi mawili yafuatayo:-

(i) Ujangili wa Kujikimu (*Subsistence Poaching*). Aina hii ya ujangili inahusisha watu wenyewe kipato kidogo na hulenga zaidi katika kujipatia kitoweo na fedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji mengine. Ujangili wa aina hii huathiri zaidi wanyama wanaoliwa na si Ndovu.

(ii) Ujangili wa Biashara (*Commercial Poaching*). Aina hii ya ujangili inahusisha zaidi watu wenyewe uwezo mkubwa wa kifedha na hulenga kupata nyara zenye thamani kubwa. Wanyama wanaoathiriwa zaidi na aina hii ya ujangili ni pamoa na Tembo, Faru, Simba na Chui.

Mheshimiwa Spika, taarifa ilibainisha kuwa, kuongezeka kwa masoko haramu katika nchi za Asia na Mashariki ya Kati ambayo yanatoa bei kubwa ya nyara hizo, imekuwa ni chachu ya kuimarika kwa mitandao inayojihusisha na ujangili (ndani na nje ya nchi) na hivyo kusababisha ongezeko kubwa la vitendo vya ujangili.

Mheshimiwa Spika, Maeneo yaliyoathiriwa zaidi na ujangili, Mpango Kazi wa Kupambana na Ujangili ulilenga kujikita katika maeneo yaliyoathiriwa zaidi na ujangili wa wanyamapori na misitu. Mpango huo ulioelezewa kuwa ni wa muda mrefu na kusimamiwa na kikosi kazi cha Taifa (*National Task Force*), umeanisha maeneo yafuatayo kuwa ndio yaliyoathirika zaidi:-

(i) Pori la Akiba *Selous*.

(ii) Hifadhi ya Taifa Serengeti, Pori la Akiba Maswa na Pori Tengefu la Loliondo.

(iii) Hifadhi ya Taifa Katavi na Mapori ya Akiba Rukwa na Lukwati.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

(iv) Hifadhi ya Taifa Mikumi.

(v) Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi za Taifa Tarangire na Ziwa Manyara.

(vi) Mapori ya Akiba Burigi, Biharamulo, Ibanda na Rumanyika.

(vii) Mapori ya Akiba Moyowosi, Kimisi, Ugalla na Hifadhi ya Misitu Luganzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Operesheni Tokomeza: Operesheni Tokomeza ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 4 Oktoba, 2013 ilikuwa na malengo yafuatayo:-

(i) Kuzuia vitendo vya ujangili ndani na nje ya Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu, Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro na Misitu ya Hifadhi na kufanya operesheni maeneo yote yaliyoathiriwa na ujangili.

(ii) Kuwatambua mapema majangili na kujua nyendo zao ndani na nje ya maeneo ya hifadhi.

(iii) Kuwakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria wafanyabiashara haramu wa nyara za Serikali na mazao ya misitu.

(iv) Kuvunja mitandao ya wafadhili, wanunuzi wadogo na wakubwa pamoja na mawakala wa biashara haramu ya nyara za Serikali na mazao ya misitu.

(v) Kufuatilia na kukamata mali za majangili zilizotokana na biashara haramu ya nyara za Serikali na mazao ya misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Njia zilizotumika kutekeleza Operesheni Tokomeza: Kamati ilibaini kuwa, Mpango Kazi wa Serikali kuhusiana na Operesheni Tokomeza, uliainisha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

kuwa operesheni hiyo itaendeshwa kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kufanya uchambuzi wa kina wa watuhumiwa wa mtandao wa ujangili wa nyara za Serikali na wavunaji na wasafirishaji haramu wa mazao ya misitu.

(ii) Kuwakamata watuhumiwa wote waliobainishwa kwenye taarifa za kiintelijensia.

(iii) Kupiga picha na kuchora ramani ya eneo la tukio kwa kila mtuhumiwa (*sketch map*).

(iv) Kuhoji na kuandika maelezo ya watuhumiwa wa ujangili wa nyara za Serikali na wavunaji na wasafirishaji haramu wa mazao ya misitu.

(v) Kukusanya na kuhifadhi vielelezo vyote vitakavyokamatwa kutoka kwa majangili kwa ajili ya kujenga ushahidi mahakamani.

(vi) Kuandika maelezo ya mashahidi na askari wakamataji kwa ajili ya kujenga ushahidi mahakamani.

(vii) Kuandaa mashitaka dhidi ya watuhumiwa na kuwapeleka mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maeneo ya Opereshini na Gharama za Utekelezaji. Mpango Kazi wa Operesheni Tokomeza ulianisha kuwepo awamu mbili za utekelezaji ambazoni; Mpango Kazi wa Muda Mfupi na Mpango Kazi wa Muda Mrefu.

Katika Mpango Kazi wa Muda mfupi itafanyika operesheni maalum katika maeneo yote ya ndani na nje ya hifadhi za wanyamapori na misitu nchi nzima. Maeneo hayo yaligawanywa katika kanda 12 za utekelezaji kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

- (i) *Selous*, Mikumi, Udzungwa, Lukwika/Lumesule na Liparamba;
- (ii) Burigi/Biharamuro, Ibanda/Rumanyika na Rubondo;
- (iii) Moyowosi, Ugalla na Lugazo;
- (iv) Serengeti, Loliondo, Maswa, Ikorongo na Kijeshi;
- (v) Kilimanjaro, Arusha, Mkomazi/Umba, Simanjiro na Longido;
- (vi) Tarangile, Manyara, Karatu/Ngorongoro, Swagaswaga na Mkungunero;
- (vii) Rungwa, Ruaha, Mpanda – Kipengele;
- (viii) Rukwa, Lukwati, Katavi, Lwafi, Piti na Wembere;
- (ix) Mahale na Gombe;
- (x) Saadani na kwenye maeneo yenye misitu ya mikoko;
- (xi) Pori Tengefu la Handeni, Kilindi na Mkinga; na
- (xii) Msitu wa Kazimzumbwi, Kisarawe, Rufiji na Mkuranga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilianishwa kuwa, awamu ya kwanza ya Mpango Kazi wa muda mfupi ingegeharimu jumla ya *Tshs. 3,968,168,667/=* ambazo zingechangwa na Taasisi za wanyamapori, kwa maana ya Idara ya Wanaymapori, Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamalaka ya Hifadhi Ngorongoro, na Wakala wa Misitu wa Serikali kwa kila moja jumla ya *Tshs. 992,042,167/=*.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Naibu Spika, Tamko la Serikali kusitisha Operesheni. Kufuatia michango na malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Said Nkumba Mbunge wa Sikonge, pamoja na maagizo ya Bunge kutaka Serikali itoe maelezo kuhusu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, Serikali ilitoa Tamko la kusitisha Operesheni Tokomeza tarehe 1 Novemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Taarifa ya awali ya Utekelezaji wa Operesheni Tokomeza. Taarifa hii ya awali kuhusiana na utekelezaji wa Operesheni Tokomeza ilikuwa na mambo yafuatayo:-

- (i) Washiriki wa operesheni;
- (ii) Awamu za operesheni;
- (iii) Mafanikio ya operesheni;
- (iv) Idadi ya watuhumiwa na kesi zilizofunguliwa; na
- (v) Changamoto za operesheni.

Mheshimiwa Spika, Washiriki wa Operesheni: Operesheni Tokomeza ilihusisha jumla ya washiriki 2,371 kutoka vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa mgawanyo ufuatao:-

- (i) Wanajeshi (885) kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania;
- (ii) Askari (480) kutoka Jeshi la Polisi;
- (iii) Askari (440) kutoka Kikosi Dhidi ya Ujangili (*KDU*);
- (iv) Askari Wanyamapori (383) kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*);

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

(v) Askari (99) kutoka Wakala wa Huduma za Misitu (TFS);

(vi) Askari Wanyamapor (51) kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA);

(vii) Waendesha Mashitaka (23); na

(viii) Mahakimu (10).

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu za Operesheni. Operesheni Tokomeza ilipangwa kutekelezwa katika awamu Nne (4) kama ifuatavyo:-

(i) Awamu ya kwanza ambayo ililenga kusaka Silaha za Kivita na Meno ya Tembo kutoka mlongoni mwa wanaojihusisha na vitendo vya ujangili.

(ii) Awamu ya pili ambayo ililenga kusaka silaha zisizomilikiwa kihalali na zile zinazomilikiwa kihalali lakini zinasadikiwa kutumika kwenye vitendo vya ujangili.

(iii) Awamu ya tatu , ambayo ililenga kutafuta yalipo Maghala ya Nyara, kusaka Wafadhili na Wanunuzi wa nyara hizo na kuwabaini watu wanaowakingia kifua, wahusika wa vitendo vya ujangili.

(iv) Awamu ya nne, ambayo ililenga kukamata Nyara nyingine mbali na Meno ya Tembo na kuhakikisha watu walio katika makundi yafuatayo wanakamatwa:-

- Wawindaji haramu;
- Wavunaji haramu wa mazao ya misitu;
- Watu wanaolisha Mifugo ndani ya hifadhi; na
- Watu waliojenga ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafanikio ya Operesheni Tokomeza na Idadi ya Watuhumiwa na kesi zilizofunguliwa. Tangu kuanza kutekelezwa kwa Operesheni Tokomeza (tarehe 4 Oktoba, 2013 hadi ilipositishwa (tarehe 1 Novemba, 2013) jumla ya kesi 687 zilifunguliwa zikiwahusisha watuhumiwa 1,030 katika maeneo yote kama ifuatavyo:-

(i) Kanda ya Kwanza kesi 105 zikiwahusisha watuhumiwa 105;

(ii) Kanda ya Pili kesi 370 ambazo zilihusisha watuhumiwa 375;

(iii) Kanda ya Tatu kesi 165 zilizohusisha watuhumiwa 498; na

(iv) Kanda ya Nne kesi 47 zilizohusisha watuhumiwa 52.

Mheshimiwa Spika, hadi wakati Operesheni Tokomeza inasitishwa tarehe 1 Novemba, 2013 kati ya Kesi 687 zilizokuwa zimefunguliwa ni 132 tu ndiyo zilikuwa zimetolewa maamuzi na 555 bado zilikuwa katika hatua ya kusikilizwa.

Kukamatwa kwa meno ya Tembo 211 yenyewe uzito wa kilo 522, meno ya Ngiri, Mikia ya wanyama mbalimbali 36, Ngozi za wanyama mbalimbali 21, Pembe za Swala 46, Mitego ya wanyama 134, ng'ombe 7,621 Baiskeli 58, Pikipiki 8 na Magari 9.

Kupungua kwa kasi ya mauaji ya Tembo kutoka wastani wa Tembo wawili (2) kwa siku hadi tembo wawili tu katika kipindi chote cha operesheni (siku 29).

Hadi kufikia tarehe 11 Novemba, 2013 jumla ya Bunduki za Kijeshi 18 zilikamatwa, Bunduki za kiraia 1579, Risasi 1964, Mbao vipande 27,913, Mkaa Magunia 1242, Magogo 858 na Misumeno 60. Vyote hivyo vilikamatwa katika Kanda ya Nne.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto za Operesheni Tokomeza na Vifo vivilvyotokea wakati wa Operesheni. Taarifa ya Serikali iliainisha vifo kama changamoto kubwa iliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Operesheni Tokomeza kutokana na maaskari 6 na watuhumiwa 13 kupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hujuma dhidi ya Operesheni. Taarifa ya Serikali ilifafanua kuwa, utekelezaji wa Operesheni Tokomeza ulikumbwa na vitendo nya hujuma kutoka kwa baadhi ya makundi ya jamii kama ifuatavyo:-

(i) Mamluki mionganini wa washiriki wa Operesheni. Mfano ni kukamatwa kwa Askari Polisi na Askari Wanyamapori wakisindikiza gari lenye Meno ya Tembo, na gari la Serikallikutumika kusafirisha Meno ya Tembo.

(ii) Vyombo nya Habari kutumika kuvuruga operesheni kwa kueneza propaganda zilizolenga kushawishi wananchi kupinga operesheni hiyo.

(iii) Baadhi ya wamiliki wa silaha kutuhumiwa kutoa silaha zao ili zitumike kwa ajili ya vitendo nya ujangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tuhuma dhidi ya Operesheni: taarifa ya Serikali ilifafanua kuwa, ingawa lengo la operesheni lilikuwa ni kupambana na vitendo nya ujangili dhidi ya raslimali za Taifa, utekelezaji wake ulikumbwa na tuhuma kadhaa zikiwemo zifuatazo:-

Mateso dhidi ya watuhumiwa yaliyosababisha maumivu, kupata ulemavu wa kudumu na hata wengine kupoteza maisha (Mfano ni Marehemu Emiliana Gasper Maro wa Gallapo - Babati Mkoa wa Manyara).

(i) Matumizi mabaya ya Silaha (Mfano; Mzee wa miaka 70 kuuawa kwa kupigwa risasi tatu (3).

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

(ii) Nyumba za wananchi kuchomwa moto (Mfano ni Kijiji cha Kabage Wilaya ya Mpanda – Katavi).

(iii) Mifugo kuuawa kikatili kwa kuchomwa moto na kupigwa risasi (Mfano; Ng'ombe 60 kuuawa kwa kupigwa risasi).

(iv) Kukosekana kwa mwongozo wa utoaji wa taarifa jambo liliosababisha viongozi husika wa Serikali kutopewa taarifa muhimu za utekelezaji wa Operesheni. (Mfano ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri wa Ulinzi na Wakuu wa Mikoa na Wilaya).

(v) Askari waliotuhumiwa kukiuka taratibu kukataa kutoa ushirikiano wa kutosha pale walipohitajika kufanya hivyo.

(vi) Kutoshirikishwa kwa viongozi wa Mamlaka za Utawala katika ngazi za Mikoa na Wilaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahojiano Bainya ya Kamati na Wizara Pamoja na Wabunge. Kamati ilifanya mahojiano na makundi yafuatayo:-

(i) Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi zake;

(ii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na

(iii) Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahojiano bainya ya Kamati na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi zake; ili kuhakikisha wajumbe wa Kamati wanapata uelewa wa kutosha kuhusiana na Operesheni Tokomeza, Kamati liagiza uongozi wa Wizara ya Maliasili na Utalii ukiongozwa na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Waziri Balozi Khamis Kagasheki, kufika mbele ya Kamati ili kueleza namna Operesheni Tokomeza ilivyoandalishiwa na kutekelezwa hadi iliposishwa kupitia tamko la Serikali lilitolewa Bungeni tarehe 1 Novemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na timu yake kwa siku tatu, tarehe 28 mpaka 29 Novemba, 2013 na tarehe 1 Desemba, 2013. Katika vikao hivyo, Waziri aliliezea Kamatijuu ya Mpango Kazi wa Operesheni Tokomeza, raslimali (watu na fedha) pamoja na tathmini iliyoafanyika kwa kipindi ambacho Operesheni Tokomeza ilitekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mahojiano na Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki na watendaji wake Kamati ilifahamishwa yafuatayo:-

Kwamba Operesheni Tokomeza ilikuwa ya kijeshi kama alivyonukuliwa katika Taarifa Rasmi za Bunge maana ya (*Hansard*) akisema: "...Operesheni ilikuwa ya kijeshi. Ilikuwa ya kijeshi kwa sababu ilitekelezwa kwa amri ya jeshi Namba 0001/13 iliyotolewa tarehe 28 Septemba, 2013 na kusainiwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi..."

Kwamba, kinadharia inaonekana kwamba, Waziri wa Maliasili na Utalii ndiye alikuwa Msemaji Mkuu, lakini kiuhalisia hakuwa msemaji mkuu wa Operesheni Tokomeza kama alivyonukuliwa katika Taarifa Rasmi za Bunge akisema; "...kinadharia inaweza ikasemekana kwamba mimi ndiye msemaji mkuu, lakini mimi sikuwa msemaji mkuu wa Operesheni Tokomeza ..." "

Utekelezaji wa Operesheni Tokomeza ulisimamiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Taarifa za mwenendo wa operesheni zilikuwa zinapelekwa moja kwa moja kwa Mkuu wa Majeshi na kwamba, hazikumfikia Waziri wa Maliasili na Utalii.

Operesheni Tokomeza iliingiliwa na Wanasiasa. Pamoja na Mpango kazi huo kuandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa namna ambayo haieleweki Waziri hakuona wala kuidhinisha rasimu ya mwisho ya Mpango Kazi wa Operesheni Tokomeza h. Hiyo iildhihirika mbele ya Kamati kutokana na Waziri kukiri kwamba hakuona wala kuuidhinisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Kamati Kuhusu Majibu ya Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Watendaji wa Wizara. Kwa kutumia tathmini ya awali ya nyaraka zillizowasillishwa pamoja na mahojiano na Waziri ilionekana kwamba, Operesheni Tokomeza iliandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake na kushirikisha vyombo vyta Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha Mpango wa Operesheni Tokomeza kuandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, hata hivyo utekelezaji wake ulisimamiwa na kuongozwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hatua ya jeshi kuchukua jukumu la kuongoza Operesheni Tokomeza, lilifanya viongozi wa Wizara kuijiengua katika jukumu la kuongoza (*Lead Agency*) na badala yake kuacha jukumu hilo kwa Jeshi pekee jambo lilitotafsiriwa kwamba, Operesheni Tokomeza ilikuwa ya kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mahojiano ilibainika kwamba, hakukuwa na utaratibu mzuri wa kupashana habari kuhusiana na mwenendo mzima wa Operesheni Tokomeza jambo lilitofanya baadhi ya wahusika kutotambua kikamilifu wajibu waokatika Operesheni hiyo. Mfano mzuri ni kwamba, licha ya kuelezwu kwenye Kanuni za Utendaji (*Operational Guidelines*) za Operesheni Tokomeza kwamba, Waziri wa Maliasili na Utalii ndiye atakuwa Msemaji Mkuu wa Operesheni Tokomeza, bado Mhe. Waziri hakutekeleza

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

jukumu hilo kwani alikwishatoa mapendekezo katika rasimu kwamba Msemaji Mkuu awe ni Mkurugenzi wa Wanyamapori. Aidha, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Watendaji wa juu wa Wizara walidaiwa kukwamisha utekelezaji wa maagizo ya Waziri wa Maliasili na Utalii kutokana na kuingilia mawasiliano aliyokuwa anayafanya na baadhi ya Watumishi. Kwa mfano ni majibzano kwa njia ya barua pepe kati ya Katibu Mkuu, Waziri na Mkurugenzi wa Wanyamapori na pia Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa Wanyamapori. Kwa mujibu wa majibzano hayo Waziri anaonekana kushangazwa na hatua ya Katibu Mkuukuhoho hatua ya yeye kumuita mmoja wa mtumishi wa Wizara ofisini kwake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa mfumo mzuri wa kupashana habari kwa pande husika kuhusu mwenendo mzima wa Operesheni Tokomeza, kulionekana kuathiri utaratibu mzima wa viongozi husika akiwemo Waziri wa Maliasili na Utalii, kupata taarifa zinazotakiwa kwa wakati. Hali hiyo ilichangia utekelezaji wa Operesheni Tokomeza kukumbwa na athari ambazo zingeweza kuepukika iwapo kungekuwa na mfumo mzuri wa mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mahojiano pia Kamati ilibaini kuwepo kwa hujuma kutoka kwa viongozi wa kisiasa na Serikali ambao kwa namna moja au nyingine walionekana kuhuishwa na Operesheni Tokomeza ama wao binafsi au ndugu zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa hujuma ambazo Kamati ilizibaini kupitia mahojiano na Waziri wa Maliasili na Utalii na Watendaji wake ni pamoja na:-

Baadhi ya watuhumiwa wenye mahusiano na viongozi wa kisiasa kutumia majina ya viongozi hao kuingilia utekelezaji wa Operesheni Tokomeza.

Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kutuhumiwa kujihusisha na vitendo vya ujangili na biashara haramu ya nyara za Serikali.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Baadhi ya Mawaziri kutoa kauli zenyе kuingilia utekelezaji wa Operesheni Tokomeza. (Mfano: kutoa maelekezo kwa wahusika wa Operesheni Tokomeza kwamba wasiguse viongozi wa kisiasa wa ngazi zote).

Baadhi ya viongozi wa vyombo vyaa Ulinzi na Usalama kushiriki kudhoofisha utekelezaji wa Operesheni Tokomeza kwa kusindikiza au kusaidia watuhumiwa wa ujangili kutoroka. (Mfano; viongozi wa Polisi wa Wilaya na Mikoa).

Mheshimiwa Naibu Spika, kubainika kwa hujuma hizo ni ishara tosha kwamba hata ndani ya Serikali yenye we hakukuwa na dhamira ya dhati kwa baadhi ya viongozi na watendaji katika kuhakikisha vita dhidi ya vitendo vyaa kijangili inapiganwa kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Nitarudia hapa. Kubainika kwa hujuma hizo ni ishara tosha kwamba hata ndani ya Serikali yenye we hakukuwa na dhamira ya dhati kwa viongozi na watendaji katika kuhakikisha vita dhidi ya vitendo vyaa kijangili inapiganwa kikamilifu. (*Makofi*)

Hali hiyo ilisababisha utekelezaji wa operesheni kukumbwa na athari nyingi kama vile; wananchi kupoteza maisha, mifugo kuuawa kwa kuchomwa moto, njaa, kiu au kupigwa risasi), upotevu wa mali, nyumba kuchomwa moto na vitendo vyaa ukatili dhidi ya wananchi ambavyo vilikiuka haki za kibinadamu. Hali hiyo imesababisha utekelezaji wa zoezi la Operesheni Tokomeza kutafsiriwa kwamba ulilenga wananchi wasio na hatia na kuacha wahusika wa ujangili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahojiano baina ya Kamati na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mnamo tarehe 30 Novemba, 2013 Kamati ilikutana na kufanya mahojiano na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili kubaini namna ilivyoshiriki katika Operesheni Tokomeza.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, alieleza kuwa, operesheni hii ilikuwa na lengo la kutimiza azma (*Commitment*) ya Serikali illyoitao Bungeni kwamba, inakusudia kufanya Operesheni ya kupambana na majangili. Wizara yake ilishiriki kwa kutoa Askari Polisi 504 pamoja na baadhi ya vyombo vyaa usafiri na kwamba vyombo vyaa Ulinzi na Usalama vyaa nchi vilikuwa vikikutana mara kwa mara kwa lengo la kuandaa mkakati wa namna ya kushirikiana katika kutekeleza mpango huo wa vita dhidi ya ujangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alikiri kuwa, licha ya lengo la operesheni kuwa zuri, kulijitokeza changamoto kadhaa zilizotokana na baadhi ya washiriki wa operesheni kwenda kinyume na malengo yaliyokusudiwa kama vile; ukatili dhidi ya mifugo na vitendo vyaa unyanyasajji wa wananchi kwa kuwatesa kiasi cha kuwasababishia ulemavu wa kudumu au vifo. Pia Mheshimiwa Waziri alikiri kwamba, kutokuwepo mfumo mzuri wa mawasiliano na Operesheni kuongozwa na jeshi, iliashiria kwamba taarifa za operesheni zilikuwa zinakwenda kwa Mkuu wa Majeshi - *CDF* moja kwa moja na hivyo kufanya pande zingine zinazohusika zisijue kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Kamati kuhusu Majibu ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Watendaji wake; Kamati ilibaini kuwepo kwamawasiliano hafifu kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara nyingine zilizoshiriki katika operesheni hii.

Pia, kukosekana kwa mfumo mzuri wa mawasiliano, kuliikosesha Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo iliandaan na kugharamia Operesheni Tokomeza, fursa ambazo zingeiwezesha kufanya tathmini kuhusu utekelezaji wa Operesheni hii.

Aidha, Kamati ilibaini kwamba, hatua ya kutoshirikisha Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ililenga kutovujisha siri dhidi ya watuhumiwa wa ujangili. Hatua hiyo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

ilisababisha usumbufu mkubwa kwa viongozi wa mamlaka za utawala za Wilaya na Mikoa kutokana na kulaumiwa na wananchi kwa kushindwa kuwasaidia pale walipokumbwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahojiano baina ya Kamati na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge; kwa kuwa suala hili liliibukia Bungeni baada ya wawakilishi wa wananchi kupaza sauti kuhusu athari zilizowakumba wapiga kura wao, Kamati iliona ni busara kuhoji baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii. Wabunge hao walitoa taarifa muhimu kuhusu vitendo vilivyofanyika katika maeneo yao wakati wa operesheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge walieleza kusikitishwa na namna ambavyo Operesheni Tokomeza ilikiuka malengo yaliyokusudiwa na badala yake ikanyanyasa wafugaji kwa kuangamiza mifugo yao na kuwaharibia mali zao kama vile; kuchoma moto nyumba, kupora fedha na vitu vingine. Mbunge mmoja alinukuliwa katika Taarifa Rasmi za Bunge akisema:- “*Badala ya Operesheni Tokomeza kusaka majangili, ikageuka kuwa Operesheni Tokomeza Ufugaji*” (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge walieleza Kamati kuwa, siyo jambo la kawaida kwa watu wanaoagizwa kufanya jambo fulani kwenda kinyume na maagizo. Wakashauri kuwa, wahusika wote waliotenda kinyume namaagizo wachukuliwe hatua stahiki ili kuepusha vitendo vya aina hiyo visijirudie katika operesheni zitakazofuata. Pia Waheshimiwa Wabunge walishauri kasoro zilizojiteza zirekebishwe na operesheni iweze kuendelea ili kutowapa mwanya majangili kujipanga upya.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Kamati Kuhusu Majibu ya Waheshimwia Wabunge; kimsingi Waheshimiwa Wabunge wanaunga mkono Operesheni Tokomeza ambayo ililenga kukomesha vitendo vya kijangili na kunusuru raslimali za nchi hasa wanyamaporí na misitu. Hata hivyo, walieleza

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]  
kusikitishwa na vitendo vilivyojitokeza wakati wa utekelezaji  
wa operesheni na walisema haviwezi kuvumilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata taarifa mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, mahojiano na viongozi na watendaji wa Wizara na kuzingatia taarifa zilizowasilishwa na Serikali, Kamati iliazimia kuzuru baadhi ya maeneo yaliyoathiriwa na Operesheni Tokomeza ili kufanya uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati Kuzuru Maeneo Yaliyoathirika Kwa Ajili ya Kuhakiki (*Verification/Outreach*). Kutokana na wingi wa maeneo pamoja na ufinyu wa muda, Kamati ilijigawa katika makundi matatu ili yaweze kutembelea baadhi ya maeneo yaliyoainishwa katika Taarifa ya Serikali ili kufanya tathmini (*verification*) kwa utaratibu ufuatao:-

Kundi la kwanza lilielekea Kanda ‘C’ iliyohusisha maeneo yaliyoathiriwana Operesheni Tokomeza katika Mikoa ya Shinyanga, Kagera, Tabora, Kigoma, Rukwa, Katavi na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi hili liliundwa na Wajumbe wafuatao:-

Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa Haji Khatibu Kai, na Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga.

Kundi la pili lilielekea Kanda ‘B’ iliyohusisha maeneo yaliyoathiriwa na Operesheni Tokomeza katika Mikoa ya Simiyu, Mara, Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi hili liliundwa na wajumbe wafuatao:-

Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu na Mheshimiwa Amina Andrew Clement.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Kundi la tatu lilielekeea Kanda ‘D’ iliyohusisha maeneo yaliyoathiriwa na Operesheni Tokomeza katika Mikoa ya Pwani, Morogoro, Iringa, Ruvuma na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi hili liliundwa na wajumbe wafuatao ambao ni Mheshimiwa Kaika Saning’o Telele, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, ambaye hata hivyo hakushiriki kutokana na dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoainishwa hapo juu lengo la Kamati kutawanyika Mikoani lilikuwa kutathmini athari zilizotokana na Operesheni Tokomeza ambayo iliendeshwa nchini kuanzia tarehe 4 Oktoba, 2013 hadi tarehe 1 Novemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutimiza jukumu hilo kikamilifu, Kamati iliongozwa na taarifa zifuatazo:-

- (i) Mpango Kazi wa Operesheni Maalum ya kupambana na Ujangili nchini;
- (ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Operesheni Tokomeza iliyotolewa na Serikali;
- (iii) Michango ya Waheshimiwa Wabunge kama ilivyonukuliwa katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*);
- (iv) Madai yaliyotolewa na Wabunge kuhusiana na athari zilizotokana na utekelezaji wa Operesheni Tokomeza;
- (v) Maelezo yaliyotolewa na Mashahidi ambao walihojwa na Kamati; na
- (vi) Vielelezo vilivyowasilishwa na Mashahidi waliofika mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makudi ya Kamati Yalivyotekeleza Majukumu yake. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilikutana na makundi yafuatayo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

- (i) Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya;
- (ii) Waheshimiwa Madiwani; na
- (iii) Waathirika wa Operesheni Tokomeza.

Mheshiwa Naibu Spika, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya; Kamati ilikukutana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya na kupokea taarifa iliyohusu hali ya Ulinzi na Usalama hususan wakati wa utekelezaji wa Operesheni Tokomeza.

Mheshimwa Naibu Spika, kwa sehemu kubwa taarifa za Ulinzi na Usalama za Wilaya zilisaidia kuanisha maeneo na matukio yaliyojiri wakati wa Operesheni Tokomeza na athari zillizojitokeza. Wajumbe wa Kamati wallitumia uchambuzi wa taarifa hizo kupata uelewa zaidi kuhusiana na utekelezaji wa Operesheni hiyo kabla ya kukutana na wananchi walioathirika ili kupata maelezo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Madiwani; katika baadhi ya Wilaya, Kamati ilikutana na baadhi ya Madiwani wakiwa ni wawakilishi wa wananchi katika ngazi ya halmashauri ili kupata maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa Operesheni Tokomeza kabla ya kukutanana waathirika wa Operesheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waathirika wa Operesheni Tokomeza; Kamati ilikutana na baadhi ya wananchi walioathirika na Operesheni Tokomeza na kupokea maelezo na malalamiko yao kuhusu namna walivyoathiriwa na uekelezaji wa Operesheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo baadhi ya waathirika walitoa ushahidi/vielelezo vya maandishi na picha ili kuthibitisha yale waliyokuwa wakiyaeleza mbele ya Kamati. Wengine walikwenda mbali kiasi cha kuonesha majerahana makovu waliyoyapata katika miili yao kutokana na mateso

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

waliyopata kwenye kambi maalum za mahojiano zilizoandaliwa na waendeshaji wa Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Spika, Kuzuru maeneo yaliyoathirika zaidi na Operesheni. Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya maeneo yaliyokumbwa na athari za operesheni Tokomeza kwa lengo la kushuhudia mabaki ya vielelezo ili kujiridhisha iwapo tuhuma za athari zilizotolewa kuhusu maeneo hayo zilikuwa za kweli.

Mheshimiwa Spika, yaliyobainika katika ziara za Kamati. Vikao na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa/Wilaya. Katika vikao na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa/Wilaya Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa Operesheni Tokomeza haukushirikisha viongozi wa maeneo hayo ya utawala.

Kulikuwa na manung'uniko kwamba licha ya Wakuu wa Wilaya na Mikoa kuwa wawakilishi wa Rais, waliachwa kando na Operesheni kuendeshwa katika maeneo wanayosimamia hadi malalamiko ya wananchi waliokamatwa yalipowafumbua macho kwamba walikuwa wanateswa na kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji na watekelezaji wa Operesheni.

Aidha, Kamati ilielezwa kwamba utekelezaji wa Operesheni Tokomeza ulisababisha hofu mionganoni mwa wananchi na viongozi na kusababisha baadhi yao kukimbia makazi. Mfano ni Mkuu wa Wilaya ya Ulanga alikiri kujihifadhi kwenye Hoteli moja nje ya Wilaya yake ambako alikutana na baadhi wananchi wake waliokimbia adha za Operesheni Tokomeza.

Viongozi hao walieleza kwamba, kimsingi hawapingi Operesheni Tokomeza Majangili kwaniililenga kunusuru raslimali za nchi hasa wanyamaporina misitu visitoweke kutokana nakushamiri kwa vitendo vya ujangili. Hata hivyo, walieleza kuwa hatua ya kutowashirikisha imelifanya zoezi hilo kuwa na kasoro nyingi pamoja na udhalilishaji hata kwa viongozi waliochaguliwa na wananchi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Spika, Vikao vya Kamati na Waathirika wa Operesheni Tokomeza. Kamati ilifanya mikutano mbalimbali katika baadhi ya maeneo ilikofanyika Operesheni Tokomeza kwa lengo la kuwasilikiliza waathirika na kubaini mambo yafuatayo:-

Watuhumiwa kupekuliwa, kudhalilishwa na baadhi kutojulikana walipo. Baadhi ya wananchi wakiwemo viongozi, Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji na Watumishi wa Serikali walikamatwa na kudhalilishwa mbele ya wananchi wanaowaongoza. Baadhi ya watuhumiwa waliokamatwa walikuwa hawajulikani walipo hadi Kamati ilipozuru maeneo hayo. Mfano; Vijana watatu wa Kijiji cha Osteti, Kata ya Chapakazi, Wilayani Kiteto, walituhumiwa kujihusisha na biashara ya Meno ya Tembo. Vijana hao ni Nyafuka Ng'onja, Ng'onja Kipana na Mswaya Karani.

Baadhi ya watuhumiwa waliokamatwa walidai kudhalilishwa mbele ya wanafamilia kwa kupewa adhabu wakiwa uchi na wanawake kushikwa sehemu za siri bila ridhaa yao. Mfano ni Ndugu Ali Nyenge (38) wa Kata ya Iputi, Wilaya ya Ulanga alidai kuvuliwa nguo, kumwagiwa maji yaliyochanganywa na chumvi na kuchapwa viboko huku mwanae wa kiume (11) akishuhudia. Pia alidai kulazimishwa kuchora picha ya Chatu kwa kutumia wembe kwenye paja lake.

Vilevile, Bi. Neema Moses wa Babati alidai kuvuliwa nguo na kulazimishwa afanye mapenzi na wakwe zake na pia kuingizwa chupa sehemu zake za siri. Aidha, baadhi ya akina mama walidai kubakwa na kulawitiwa. Mfano ni katika Kata ya Iputi, Wilaya ya Ulanga, mwanamke mmoja alidai kubakwa na Askari wawili (2) wa Operesheni Tokomeza Ujangili mida ya usiku. Vilevile, mama mmoja mkazi wa Kata ya Matongo Wilayani Bariadi, alibakwa na askari watatu (3) wa Operesheni Tokomeza Ujangili huku akiwa ameshikiwa mtutu wa bunduki.

Watuhumiwa waliokamatwa walifanyiwa upekuzi bila kuhusisha viongozi wa Serikali za maeneo husika na kutokuwepo kwa mashahidi na hati za upekuzi. Mfano ni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Ndugu Abdallah Pata na Bi. Flora Mwarabu wa Kata ya Iputi Wilayani Ulanga na Ndugu Elias Cosmas Kibuga wa Gallapo Babati, walipekuliwa bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, Ukatili na Udhililishaji katikaKambi za Mahojiano. Baadhi ya watuhumiwa waliopelekwa katika kambi za mahojiano walidai kuteswa kwa adhabu zinazokiuka haki za binadamu. Mfano; Diwani wa Kata ya Sakasaka wilaya ya Meatu Ndg. Peter Samwel, alidai kuadhibiwa akiwa mtupu kwa kupewa adhabu za kijeshi kama kuning'inizwa kichwa chini miguu juu, kupigwa kwa vyuma na kulazimishwa kufanya mapenzi na mti.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukatili uliopitiliza, baadhi ya kambi za mahojiano zilipewa majina kama vile Guantanamo.....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lembeli kidogo tu, Mheshimiwa Soni nilikuwa naona kwa hali ya uzito wa jambo hili liliopo na Wabunge wengine ni vizuri sana Mheshimiwa Waziri Mkuu akasikiliza hotuba hii moja kwa moja. Ninaomba tumpe nafasi.

Mheshimiwa James Lembeli, Endelea!

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda wangu uulinde.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukatili uliopitiliza, baadhi ya kambi za mahojiano zilipewa majina kama vile Guantanamo (Ruaha), Golgota (Ngorongoro), Duma na Andajega (Serengeti).

Mheshimiwa Naibu Spika, Upotevu wa mali za watuhumiwa na faini zisizoleweka. Ildaiwa kuwa wakati wa utekelezaji wa Operesheni TokomezaUjangili, baadhi ya watuhumiwa walipoteza mifugo, mali na fedha zao. Mfano;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]  
katika Wilaya ya Ulanga Kata ya Iputimwananchimmoja  
alidai kuporwa sanduku la VICOBA lenye shilingi laki saba  
na nusu (750,000/=) pamoja na simu ya mkononi na Askari  
wa Operesheni Tokomeza waliovamia nyumbani kwake.

Vilevile Ndugu Musa Masanja wa Sakasaka Wilaya ya  
Meatu, alidai kuporwa shilingi laki tatu 300,000/= pamoja na  
simu 2 za mkononi na Askari Askari wa Operesheni.

Mheshimiwa Spika, pia ilidaiwa kuwa mifugo ya  
watuhumiwa ilikamatwa na kuingizwa ndani ya maeneo ya  
hifadhina kufa kwa kupigwa risasi au kukosa maji na malisho  
kutokana na kuzuiliwa kwa muda mrefu. Baadhi ya mifugo  
ilitozwa faini bila stakabadhi au stakabadhi kuonesha  
viwango vidogo ikilinganishwa na fedha halisi iliyolipwa.

Mfano ni Ndugu Sosoma Shimula mwenye Ng'ombe  
1700 Wilayani Kasulu alidai kwamba alitakiwa kulipa faini ya  
shilingi Milioni thelathini (30,000,000/=, alipowasihi alipunguziwa  
hadi Milioni kumi na mbili (12,000,000/=) hata hivyo aliweza  
kulipa Milioni kumi (10,000,000/=).

Alionesa Kamati stakabadhi inayoonesha kuwa  
amelipa faini ya shilingi milioni moja tu (1,000,000/=).  
Stakabadhi hiyo ilijazwa sehemu ya tarakimu, lakini hakuna  
kilichoandikwa katika sehemu ya kiasi cha fedha kwa  
maneno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watuhumiwa kuteswa na  
kuumizwa. Baadhi ya watuhumiwa walidai kupigwa na  
kuumizwa na askari wa Operesheni na wengine kupata  
ulemavu wa kudumu.

Mfano katika Wilaya ya Itilima, Kijiji cha Mbogo Ndugu  
Sita Rumala, alidai kupigwa na kuvunjwa mkono alionesa  
wajumbe mkono uliokuwa umefungwa bandeji ngumu  
(P.O.P). Aidha, Diwani Peter Samwel Ndekija wa Kata ya  
Sakasaka, Wilaya ya Meatu, alidai kupigwa na kuumizwa  
vibaya mgongoni na alionesa kwa wajumbe wa Kamati  
makovu aliyoypata.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Vilevile, ilielezwa kuwa Ndugu Munanka Machumbe (24) ambayo ni bubu alipigwa risasi 3 zilizomjeruhi mapajani na kuharibu sehemu za siri wakati akijaribu kuwahoji Askari wa Operesheni kwa ishara sababu za kumtesa baba yake.

Aidha, katika tuko lingine Shekhe Mkuu wa Wilaya ya Ulanga Ali Mohamed (70) aishiye kijiji cha Iputi, alidai kurushwa kichura na kutandikwa bakora na Askari wa Operesheni Tokomeza. Pia, Ndugu Nyasongo Magoro Serengeti wa Kata ya Majimoto Wilaya ya Mulele alidhalilishwa mbele ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, Mifugo kuingizwa hifadhini na watuhumiwa kubambikwa kesi. Wakati wa Operesheni, mifugo mingi ilikuwa hifadhinilakini hata ile iliyokuwa nje ya hifadhi iliingizwa na askari wa hifadhi na wafugaji kutakiwa walipe faini ya shillingi Millioni tatu (3,000,000/=) hadi Sita (6,000,000/=) kwa idadi ya ng'ombe 30 hadi ng'ombe 100 na aliyeshindwa kulipa faini mifugo yake iliuawa au kupigwa mnada na mfugaji kafilisiwa.

Walioshindwa kulipa faini mifugo ilipigwa mnada na wafugaji hawakuruhusiwa kununua wala kukaribia eneo la mnada, na katika mnada mifugo iliuzwa kwa bei ya chini kuliko faini iliyo tozwa Mfano; shillingi elfu sitini (60,000/=) kwa kila ng'ombe wakati faini ni shillingi 180,000/=.

Ilidaiwa kwamba, Watuhumiwa kubambikwa kesi. Baadhi ya watuhumiwa walidai kubambikwa makosa ambayo hawahusiki nayo kama vile kumiliki silaha kinyume na sheria, kukutwa na bangi au nyara za Serikali. Mfano ni Bwana Elias Cosmas Kibuga wa Gallapo Babati alidai kubambikiwa kesi ya kumiliki bunduki kukutwa na mkia wa twiga kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Bibi Zuhura Ali wa Kilombero alidai kuteswa huku akilazimishwa kutoa silaha ambayo hakuwa nayo. Aidha, Bwana Melkzedek Abraham Sarakikya wa Itigi alidai kuteswa akilazimishwa atoe silaha.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Naibu Spika, Mateso navifo kwa Watuhumiwa. Baadhi ya wananchiwalidai kuwa ndugu zao waliteswa kikatili kwa muda mrefuna bila kupatiwa huduma za lazima kama chakula, maji na matibabu (siku 1 -2) hadi mauti yalipowafika. Kwa mfano Ndugu Kipara Issa wa Wilaya ya Kaliua na Ndugu Emiliana Gasper Maro wa Gallapo, Wilaya ya Babati. Aidha, wananchi hao walidai kuwa mahojiano kwa watuhumiwa yaliambatana na mateso makali kwa muda mrefu kiasi cha kusababisha vifo.

Vilevile, watuhumiwa wengine waliodaiwa kupoteza maisha wakati wa Operesheni Tokomeza ni Ndugu Wegesa Kirigit wa Kijiji cha Remagwe na Ndugu Peter Masea wa Kijiji cha Mrito (Tarime), Ndugu Mohamed Buto (Masasi) na Gervas Nzoya (Kasulu).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uthibitisho wa picha zilizotolewa na wananchi kuhusu kuteswa hadi kufa kwa Bi. Emiliana Gasper Maro, Serikali kuitia Mkurugenzi wa Wanyamapori ilitoa Taarifa kwa Umma ikipinga Taarifa iliyorushwa na kituo cha luninga cha *ITV* tarehe 19 Oktoba, 2013 kuhusu mauaji ya kutisha yaliyofanywa na Askari wa kupambana na ujangili.

Taarifa hiyo ya Serikali inapinga kuwa Askari wa Operesheni Tokomeza hawahusiki na kifo cha mtajwa. Taarifa hiyo imeonekana kukosa umakini kutokana na kujichanganya juu ya watu inaowazungumzia. Taarifa hiyo inazungumzia majina mawili tofauti (Evelyn Gasper na Mariana Gaspar Mallo wa eneo la Olongadiola) wakati mwathirika halisi ni Bi. Emilliana Gasper Maro, wa Kijiji cha Orngadida, Gallapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukatili dhidi ya Wanyama. Kuhusu vitendo vyatukatili kwa wanyama ilidaiwa kwamba ng'ombe walipigwa risasi, na ndama walikufa kwa kukosa maziwa kutokana na mama zao kukamatwa na kuzuiwa kwenye mazizi yaliyopo maeneo ya hifadhi kwa muda mrefu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Naibu Spika, Rushwa kwenye Mapori ya Akiba. Wananchi walidai kukithiri kwa vitendo vya rushwa kwa watumishi wanaosimamia mapori ya akiba ya Maswa, Kigosi Moyowosi, Burigi, Kimisi na Mkungunero kwa kutaja majina ya baadhi ya watumishi wanaowatuhumu.

Mfano ni Ndugu Kileo mtumishi wa Pori la Maswa, alidaiwa kuwa na tabia ya kutoza wananchi faini bila stakabadhi au kutoa stakabadhi kinyume na faini iliyotolewa au kutoa stakabadhi bandia. Aidha, katika pori la Kigosi-moyowosi, watumishi wafuataao walidaiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa; Ndugu Msocha, Alfred, Kobelo na Odhiambo.

Aidha, ilidaiwa kuwa katika mapori ya Kigosi Moyowosi na Kimisi zaldi ya wafugaji 100 wenyewe ng'ombe wanaokadirwa kuwa 50,000 wanalipia kuchungia ng'ombe wao kwenye mapori hayo ya hifadhi tangu mwaka 2000 kwa malipo maalum na hata Operesheni Tokomeza haikuwagusa.

Aidha, ilidaiwa kuwa Ndugu Msocha (Meneja wa Pori la Akiba la Kigosi Muyowosi), alituhumiwa na baadhi ya wananchi kuwa amekuwa akiwakodisha wafugaji hao kwa vipindi vya miezi mitatu, na wafugaji huruhusiwa kulipa tena muda unapoisha. Aidha, Mfugaji ambaye hulipa kiasi kidogo hulazimishwa kulipa huku akipigwa na mifugo yake kuuawa kwa kupigwa risasi.

Ilielezwa kuwa, Wafugaji na Askari Wanyamaporu huwasiliana kwa simu ilil kutekeleza makubaliano ya malipo kwa malisho yao. Namba za simu zinazodaiwa kuwa za Askari Wanyamaporu zimeorodheshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahusiano kati ya wananchi na Askari wa mapori ya Akiba. Wananchi wanaoishi kwenye Mapori ya Akiba yanayo wazunguka walidai kuwa katika mahusiano mabaya na Askari wa mapori hayo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mfano; wananchi wa kijiji cha Kimotorok, Wilaya ya Simanjiro na Askari wa pori la akiba la Mkungunero kiasi cha kuflikia hatua ya kutishiana maisha. Vitendo hivyo pia vipo kwa jamii zinazopakana na mapori ya Gurumeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama na Magereza kuzidiwa uwezo. Kutokana na Operesheni Tokomeza ilidaiwa kuwa vyombo Mahakama na Magereza katika maeneo husika vilizidiwa uwezo kutokana na wingi wa kesi na idadi ya Mahabusu.

Mfano ni Gereza la Wilaya ya Bunda lenye uwezo wa kuchukua jumla ya wafungwa na mahabusu 217 lililazimika kuchukua hadi watu 411. Baadhi ya watuhumiwa walikamatwa wanalazimika kusafiri umbali mrefu kuhudhuria kesi zao. Mfano ni katika wilaya ya Serengeti baadhi ya watuhumiwa walifunguliwa kesi Wilaya za Tarime, Bunda na Bariadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi wa Umma kuhusishwa na Ujangili. Ilidaiwa kuwa baadhi ya Watumishi wa Serikali na vyombo vya dola (Polisi) wanajihusisha na ujangili. Mfano ni Dereva wa *OCD*, Wilaya ya Ngorongoro aliyetuhumiwa kujihusisha na ujangili wa Meno ya Tembo. Askari huyo alihojiwa na viongozi wa Operesheni Tokomeza katika kituo chake cha kazi.

Vilevile, Ndugu Mohamed Ismail, Afisa Wanyamapori (W) Meatu anatuhumiwa kukutwa na nyara za Serikali. Aidha, Askari Polisi wawili (2) *Cpl. Isaack* na *PC Sixbert* wa Mugumu, Wilayani Serengeti walikamatwa wakiwa na meno ya Tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ilidaiwa kuwa baadhi ya Maofisa wa Serikali wamekuwa wakitumia magari ya Umma ama kusafirisha au kusindikiza watoroshaji wa nyara za Serikali. Mfano ni gari la Serikali liliokamatwa likifaulisha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]  
meno ya Tembo kutoka kwenye gari jingine huko Mkuranga  
kwa lengo la kuyasafirisha kwenda Dar es Salaam.

Sambamba na hilo baadhi viongozi wa jeshi la Polisi  
wametuhumiwa kusaidia watuhumiwa wa vitendo vy  
kijangili kutoroka na kuepuka mkono wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Migogoro kuhusu mipaka  
ya Maeneo ya Hifadhi. Wananchi walidai kuwa baadhi ya  
Mapori ya Akiba na Hifadhi yamekuwa yakipanua mipaka  
yake bila kushirikisha wananchi wa maeneo  
yanayowazunguka. Mfano; wananchi wa Wilaya ya Bunda  
wanaopakana na Pori la Akiba la Gurumeti.

Pia, wananchi wa vijiji vy  
a Kegonga na Masanga,  
katika Kata ya Nyanungu, Wilayani Tarime wako katika  
mgogoro wa mpaka na TANAPA wakidai kuwa bonde la  
Nyanungu limemezw  
na eneo la Hifadhi kutokana na  
TANAPA kuongeza mipaka yake bila kushirikisha wananchi  
wa maeneo hayo. Aidha, katika Wilaya ya Ulanga kuna  
mgogoro katika kata za Iputi na Lupiro dhidiHifadhi ya *Selous*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara za Wanyamapor  
katika Halmashauri kukosa vitendea kazi. Kutokana na silaha  
za Idara ya Wanyamapor  
katika baadhi ya Halmashauri  
kuchukuliwa wakati wa Operesheni Tokomeza kwa ajili ya  
uchunguzi, wananchi wamedai kupata shida kutokana na  
wanyama hasa Tembokuvamia mashamba na kuharibu  
mazao pamoja na kujeruhi au kuua watu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, Wanasiasa kushawishi wananchi  
kuishi kwenye maeneo ya Hifadhi. Wakati wa kutekeleza  
Operesheni Tokomeza ilidaiwa kuwa nyumba na maboma  
ndani ya mapori ya akiba zilichomwa moto. Mfano ni Wilaya  
ya Sumbawanga kijiji cha Msila Kata ya Mfinga na kijiji cha  
Kabage Wilaya ya Mpanda.

Hata hivyo baadhi ya wananchi wameanza  
kurejeakatika baadhi ya maeneo ya hifadhi kutokana na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

ushawishi wa wanaasiwa. Mfano ni katika Pori la Hifadhi ya Jamii Ubende Wilaya ya Mpanda walichangishwa shilingi laki moja (100,000/=) kwa kila kaya kwa ajili ya kupatiwa huduma za kisheria iwapo mamlaka husika zitajaribu kuwaondoa ndani ya hifadhi.

Aidha, Kamati ilipata taarifa kuwa, baadhi ya viongozi wa Vyama vya Siasa wamekuwa wakigawa kadi za vyama vyao kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya hifadhi na kwa ahadi kwamba, vyama walivyojunga nga navyo vitawatetea wasiondoke katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Tatizo la Vibali vya Wakulima wa Muda. Kamati ilielezwa lipo tatizo la raia wa nchi jirani kuingia nchini na kupewa vibali vyakuendesha shughuli za kilimo (*Peasant Permit*) kwa muda, ambavyo hutolewa bilakubandika picha ya mhusika/mwombaji hasa maeneo ya Karagwe.

Raia hao wanadaiwa kutumia nakala za vibali hivyo kuingiza nchini wahamiaji haramu ambao baadhi yao huingiza makundi makubwa ya mifugo hasa ng'ombe na wengine kutumia mwanya huo kuingiza silaha na kujihusisha na vitendo vya ujangili katika baadhi ya mapori ya akiba. Mfano ni Pori la Akiba la Ibanda Rumanyika.

Vilevile kuna tatizo la majangili kutumia vivuli vya wafugaji kuingia kwenye hifadhi huku wakiwa wameficha silaha, na hivyo kuwepo mazingira ya kushindwa kutofautisha kati ya majangili na wafugaji hususan katika maeneo ya hifadhi ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro katika eneo la Ushoroba (*Buffer Zone*) katika Kata za Lupiro, Mbugana Iputi Wilaya ya Ulanga, maeneo ambayo jamii imejenga miundombinu kwa miaka mingi ikiwa ni pamoja na shule, nyumba, mashamba, misikiti na makanisa huku Serikali ikiwa kimya kwa muda mrefu. Hata hivyo, wakati wa Operesheni Tokomeza wananchi hao walilazimishwa kuhama bila kuelekezwa waende wapi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Mheshimiwa Spika, Michango ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu Operesheni. Kamati ilibaini kuwa baadhi ya michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia Hoja ya Mheshimiwa Saidi Nkumba, haikuwa imefanyiwa utafiti wa kutosha kwani baadhi ya madai waliyoyatoa hayakuwa na uhusiano na Oparesheni Tokomeza.

Kwa mfano ni kweli kwamba ng'ombe 51 walitumbukia katika mto Rubana Wilayani Bunda na kufa, hata hivyo tukio hilo lilitokea mwezi Aprili, 2013 ikiwa ni miezi 6 kabla ya Operesheni. Aidha, ni kweli kuwa Wakazi wa Vijiji vya Kabage Wilayani Mpanda na Luchima Wilayani Mulele walihamishwa kutoka katika maeneo ya hifadhi na nyumba zao kuchomwa moto katika utaratibu uliofanywa na Halmashauri hizo mwezi Septemba, 2013 kwa lengo la kuwapeleka kwenye maeneo rasmi ya makazi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa kamati kuhusu tathmini ya utekelezaji wa operesheni tokomeza. Baada ya Kamati kuchambua nyaraka husika kuhusiana na utekelezaji wa Operesheni Tokomeza, kuwahoji viongozi mbalimbali wa Wizara na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kufanya ziara mikoani kwa lengo la kuhakiki yaliyojiri kutokana na Operesheni Tokomeza, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kwa kuwa, lengo la Operesheni Tokomeza lilikuwa kunusuru raslimali za nchi hususan Wanyamapori na hasa Tembo na Misitu, na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wameiunga mkono mbali na matatizo ya kiutendaji yaliyojiteza, Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba Serikali irekebishe haraka kasoro zilizojiteza katika utekelezaji wa Operesheni Tokomeza ili kuendeleza na kukamilisha awamu zote za operesheni kama zilivyo kwenye mpango na kunusuru raslimali za Taifa hasa wanyamapori na misitu ambayo inatishiwa kutoweka kutokana na vitendo vya ujangili.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Kwa kuwa, Kamati imejiridhishakwamba matatizo na upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa Operesheni Tokomeza yamechangiwa na maandalizi mabaya ya Mpango kazi ambao Waziri Mwenye dhamana hakuuidhinisha, na kwa kuwa, imedhihirika kuwepo hali ya sintofahamu (kwa mujibu wa hansard) iliyosababishwa na watendaji wakuu wa Wizara kwa makusudi kuamua kutomshirikisha kikamilifu Waziri katika hatua za mwisho za maandalizi ya Mpango kazi, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali iwachukulie hatua stahiki za kinidhamu Wasaidizi Wakuu wote wa Waziri walioshiriki katika Mpango kazi huo.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba pale Jeshi la Wananchi (JWTZ) linaposhirikishwa katika Operesheni ufanisi mkubwa hupatikana na kwa kuwa, bado iko haja ya kuendeleza Operesheni Tokomeza kwa maslahi ya Taifa na kwa kuwa, ushahidi wa mazingira *Circumstantial evidence* unaonesha kuwa Jeshi lilichukua uongozi wa Operesheni baada ya kugundua kuwa washiriki kutoka vikosi vingine (Polisi, KDU, TANAPA, TSF na NCAA) kwa kushirikiana na wafugaji wenyewe ushawishi wa kifedha pamoja na wanasiwa walihujumu operesheni hiyo.

Waliihujumu kwa kutoa taarifa kwenye mtandao mkubwa wa kijangili ambao umejengeka kuanzia Wizarani hadi kwenye maeneo ya Hifadhi na kusaidia ‘majangili papa’ wasikamatwe. Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba:-

Serikali kuchukua hatua za makusudi kuuvunja mtandao huo na pia kuandaa operesheni nyingine ambayo itapangwa na kutekelezwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Idara ya Usalama wa Taifa.

Kwa kuwa, kumekuwepo na operesheni kadhaa kabla ya Operesheni Tokomeza ambazo zililenga kupambana na ujangili, na kwa kuwa, Operesheni Tokomeza imeshindwa kupata mafanikio yaliyotarajiwu, na kwa kuwa, ushahidi wa mazingira unaonesha wazi kwamba, Kikosi Dhidi ya Ujangili (KDU) kimeshindwa kutimiza wajibu wake, hivyo basi Bunge linaazimia kwamba:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Serikali iimarishe kikosi hicho kwa kukifanyia tathmini na kukiunda upya ikiwa ni pamoja na kukiwezesha kwa raslimali (watu, fedha, magari, silaha za kisasa na vifaa vya mawasiliano kama redio na simu).

Serikali iunde chombo ambacho kitakuwa na jukumu la kusimamia na kutathmini utendaji kazi wa KDU. Iwapo utaratibu huo utazingatiwa ni wazi vitendo vya ujangili vitadhibitiwa bila kutumia operesheni kubwa kama Uhai na Tokomeza.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa vitendo vya utesaji na ukatili wa hali ya juu, ukiukwaji wa haki za binadamu na uzembe mionganini mwa Askari wa Operesheni Tokomeza (ushahidi wa wahusika upo), hali ambayo imesababisha baadhi ya Wananchi kupoteza maisha, kupata ulemau wa kudumu pamoja na kupoteza mali zao. Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba:-

Serikali iwabaini wote waliohusika na vitendo vya kinyama, mateso na udhalilishaji dhidi ya watuhumiwa, iwachukulie hatua stahiki na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa agizo hili katika Mkutano ujao wa Bunge. Ifanye tathmini ya kina kwa kuititia Wakuu wa Mikoa na Wilaya ili kujua kwa athari za Operesheni hii na kutafuta njia ya kutoa kifuta machozi kwa waathirika, ili kurejesha imani ya Wananchi kwa Serikali yao.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa Operesheni Tokomeza ilikuwa haikutengewa fedha katika Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 na kwa kuwa kiasi cha fedha *Tshs. 3,968,168,667/=* kilichopatikana kutoka Idara na Mashirika Tanzu ya Wizara haikutosheleza mahitaji ya fedha ya Operesheni Tokomeza kutokana na ukubwa wa eneo la Opereshene. Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba:-

Serikali kutenga Bajeti Maalum ya kutosheleza mahitaji ya Operesheni Tokomeza.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Serikali kutenga Bajeti kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uhifadhi katika maeneo ya Hifadhi ikiwa ni pamoja na kuweka raslimalil watu ya kutosha na miundombinu mingine muhimu.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa Taarifa kwa Umma iliyotolewa kwa Vyombo vya Habari na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori tarehe 23 Oktoba, 2013, haikuwa sahihi na pia ililenga kuudanganya Umma kwa kuficha mazingira na sababu za kifo cha Bi. Emilliana Gasper Maro. Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba:-

Serikali kuchukua hatua za kumuwajibisha Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kwa kuudanganya umma kwa kujaribu kuficha ukweli.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa kumekuwapo mchezo mchafu unaofanywa na baadhi ya Maafisa Wanyamapori, Maafisa misitu katika mapori ya akiba, Misitu ya Serikali na katika baadhi ya Hifadhi za Taifa wa ku pokea rushwa, kutesa wananchi, kuwabambika kesi na kujihusisha na ujangili, na kwa kuwa Kamati inayo majina na vielelezo vya wahusika.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye tathmini nchi nzima kwa lengo la kutambua kiwango cha vitendo vya rushwa miongoni mwa watumishi hao, na kuwachukulia hatua stahiki za kinidhamu wale watakaobainika kuhusika ikiwa pamoja na kuwawajibisha na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa baadhi ya viongozi wa kisiasa na Serikali waliingilia utekelezaji wa Operesheni Tokomeza kwa manufaa yao binafsi, kwa mfano, agizo la kuwataka wahusika wa Operesheni Tokomeza kutowagusa Viongozi wa Kisiasa wa ngazi zote, kauli ambayo ilitafsiriwa kuathiri utekelezaji wa Operesheni Tokomeza kwa kubagua Watanzania katika makundi ya Viongozi na Wananchi wa kawaida. Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Serikali kuhakikisha kuna uwajibikaji wa pamoja pale inapoamua kutekeleza jambo la Kitaifa kama Operesheni Tokomeza.

Kwa kuwa, Kamati imethibitisha kuwa, baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakiwadanganya wananchi waliothibitika kufanya shughuli za uchumi kwenye maeneo ya hifadhi, na kuwaahidi kuwatetea pindi Serikali inapochukua hatua za kuwaondoa katika sehemu hizo, ikiwa ni pamoja na kuwapa kadi za vyama vyao vya siasa.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kuhakikisha kwamba, wananchi hawaendeshi shughuli za kiuchumi kwenye maeneo ya hifadhi na kuwaonya wanasiasa waache kuwalaghai wananchi kwa maslahi yao binafsi.

Kwa kuwa,Kamati imebaini kwamba katika baadhi ya maeneo ya mipakani mfano Karagwe, Idara ya Uhamiaji hutoa vibali kwa raia wa nchi jirani vya kuishi na kulima hapa nchini, vibali ambavyo havina udhibiti wala tija kwa nchi, na kusababisha migogoro ya Mara kwa Mara kati ya wakulima na wafugaji lakini pia uharibifu wa mazingira kwa kuingiza mifugo hifadhini, Hivyo basiBunge linaazimia kwamba:-

Serikali isitishe mara moja zoezi la kutoa vibali hivyo, na kufuta viliwyopo na kuwataka raia hao wakigeni wenye vibali kuondoka nchini mara moja.

Kwa kuwa,Kamati imebaini kwamba zaidi ya asilimia 25 ya eneo la Nchi ni hifadhi,namipaka ya maeneo mengi yaliyohifadhiwa haijaainishwa, na kwakuwa Serikali haina uwezo wa (raslimali watu na fedha) wa kusimamia na kulinda mipaka ya maeneo haya kikamilifu. Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba Serikali kufanya yafuatayo:-

Kuridhia Idara ya Wanyamapor na Wakala wa Huduma ya Misitu kuajiri idadi ya watumishi wanaotakiwa kama Serikali bado inaendelea kuyahifadhi maeno hayo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Kuainisha mipaka ya mapori yote ya akiba, hifadhi za taifa na Misitu ya Serikali kwa alama maalumu na za kudumu ili kuepusha Wananchi kuingia katika maeneo hayo kwa kutojua mipaka. Kuyaachia mapori ya Serikali ambayo yamekosa sifa, ili yatumike kwa kilimo na ufugaji kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Kwa kuwa, yapo maeneo ya mapori na Hifadhi ambayo yana migogoro ya muda mrefu ambapo wananchi wameishi katika maeneo hayo kwa muda mrefu. Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba:-

Serikali irekebishe mipaka husika au iwahamishie Wananchi hao kwenye maeneo mengine yenye miundombinu. Serikali iwaagize Mawaziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maliasili na Utalii na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kutembelea maeneo yote yenye migogoro nchini na kuitafutia ufumbuzi ili wananchi waweze kuelewa hatma yao katika maeneo hayo kwani wamekuwa katika hali ya sintofahamu kwa muda mrefu.

Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwapo kwa migogoro baina ya Wananchi, Wawekezaji na hifadhi katika maeneo ya Meatu, Tarime, Bunda na ile ya Loliondo na Kimotorok ambayo inashughulikiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati inalishauri Bunge kuiagiza Serikali. Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba:-

Serikali kumaliza (kama ilivyoahidi) migogoro iliyopo Loliondo na Kimotorok na maeneo mengine mapema iwezekanavyo.

Kurekebisha haraka kasoro zote za kisheria zilizokiuwa kwa makusudi na Idara ya Wanyamapori kiasi cha kusababisha mgogoro baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Meatu na mwekezaji katika Pori la Hifadhi ya Jamii la Makao pamoja na kuawajibisha Watendaji wa Idara ya Wanyamapori waliosababisha mgogoro huo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Kwa kuwa, Kamati imebaini kwamba migogoro wanayokumbana nayo wafugaji ni kutokana na kuingiza mifugokwenye maeneo ya hifadhi pamoja na kero nyingine ni kutokana na kukosekana kwa miundombinu sahihi na endelevu kwa ajili ya ustawi wa mifugo na kwa kuwa, Mheshimiwa Rais aliunda Wizara mahsusisi kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini, akitambua umuhimu wa Sekta hiyo kwa uchumi wa Taifa, na kwa kuwa, Tanzania ni ya pili (2) kwa wingi wa mifugo Barani Afrika. Ni wazi kwamba adha wanazokumbana nazo wafugaji ni matokeo ya kutokuwepo sera na mipango madhubuti ya muda mfupi na mrefu.

Hivyo basi, Bunge linaishauri Serikali kumtaka Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kujipima na kuona iwapo bado anastahili kuendelea kuhodhi wadhifa alionao.

Kwa kuwa Kamati imebaini kuwa baadhi ya madai yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge Bungeni wakati wakichangia Hoja ya Mheshimiwa Saidi Nkumbailikuwa ni ya kweli.

Na kwa kuwa yaliyoelezwa katika madai hayo hayana uhusiano na operesi Tokomeza kwani yalitokea kabla ya oparesheni hiyo. Hivyo basi Bunge linaazimia kwamba Waheshimiwa Wabunge kuwa makini zaidi na kufanya utafiti kwa lengo kuhakikisha michango yao inakuwa sahihi na inalenga hoja mahsusisi iliyo mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, jukumu uliloikabidhi Kamati hii lilikuwa zito na lilihitaji umakini mkubwa na muda wa kutosha katika kulitekeleza. Kutokana na ufinyu wa muda na mazingira magumu wakati wa kutekeleza jukumu hilo, Kamati inakiri kwamba haikuweza kutembelea maeneo yote yaliyoathirika na zipo lawama kutoka kwa baadhi ya wananchi kwamba, Kamati haikuweza kupita katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuwahakikishia wananchi wote kuwa, kuitia taarifa mbalimbali za viongozi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]  
na wawakilishi wa waathirika mbele ya Kamati, malalamiko  
yao yamezingatiwa na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza katika maelezo yetu ya utangulizi, Kamati inaamini na kote tulikopita wananchi wanakiri kuwa, lengo na azma ya Serikali kuanzisha Operesheni Tokomeza Ujangili lilikuwa jema kwani lililenga kunusuru maliasili zetu kwa ajili ya maendeleo endelevu na heshima ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini maelezo yote yaliyotolewa na wananchi pamoja na viongozi wao yalikuwa na dhamira njema. Aidha, mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yanalenga kuisaidia Serikali kuchukua hatua za makusudi na haraka kurekebisha kasoro zilizojiteze wakati wa utekelezaji wa Operesheni Tokomeza Ujangili, ili kuepuka kutokea kwa vitendo vinavyoashiria ukiukwaji wa misingi ya haki za binadamu na Utawala Bora nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa dhati kutokana na kuiamini Kamati yangu na kuikabidhi jukumu hili zito. Hii ni ishara tosha kwamba una imani na Wabunge wako na kwamba wanaweza kufanya kazi kwa niaba yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe shukrani za dhati kwa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi yake vizuri na kuikamilisha kwa wakati. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru makatibu walioihudumia Kamati hii wakiongozwa na Ndugu Theonest K. Ruhilabake, ambao ni Ndugu Gerald Magili, Ndugu Chacha Nyakega na Ndugu Stanslaus Kagisa.

Aidha, ninapenda kuwashukuru viongozi wa Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji ambao walionyesha ushirikiano mkubwa Kamati ilipotembelea maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu Kamati inawashukuru watumishi wafuatao:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI]

Ndugu Silva Chindandi, Ndugu Ndigwako Mwaigaga, Ndugu Victoria Mizengo, Ndugu Germina Magohe na watumishi wengine ambao kwa namna moja au nyingine walishiriki katika kuihudumia Kamati hii hadi inakamilisha taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. ANNA ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa James Lembeli, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasiasili na Mazingira kwa kuwasilisha taarifa ya Kamati yako kwa niaba ya Wajumbe wako wa Kamati, tunakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge walioomba kuchangia hapa wako 70 lakini kwa hakika wengine ni wale ambao wana nia ya kuchangia kwenye ile Kamati ya Kilimo Mifugo na Maji nitajitahidi kuona wale ambao hasa lengo lao lilikuwa ni kuchangia kwanye Kamati ya Maliasili na Mazingira nadhani sasa tunaenda moja kwa moja katika uchangiaji.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimwa Naibu Spika, nina masuala mawili ambayo nahitaji mwongozo wako. Kwanza kabisa Mheshimiwa Naibu Spika taarifa ambayo imesomwa mbele ya Bunge lako Tukufu sio taarifa ambayo iko kwenye *Order Paper* na utaratibu wa Kanuni zetu unasema wazi kabisa kwamba jambo ambalo halipo kwenye *Order Paper* haliwezi likaingia kwenye mjadala wa Bungeni.

Hii taarifa ambayo imesomwa sio ile ambayo imetajwa katika *Order Paper*. Lakini kibaya zaidi Mheshimiwa Naibu Spika ni kwamba hii taarifa ambayo imesomwa mbele ya Bunge lako Tukufu ina mambo makubwa sana, inazungumza vitu vingi sana, hakuna Mbunge ambaye amepata nakala. Tunaingiaje kwenye

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

mjadala, tunaingiajaje kwenye mjadala kwa kitu ambacho taarifa yake hatuna, tutajadili nini zaidi ya kupiga blaa blaa hapa. (*Makof!*)

Kwa hiyo, tafadhali Mheshimiwa Naibu Spika naomba kama inawezekana mjadala wa hii taarifa ambayo imesomwa uahirishwe kwa muda tupatiwe nakala za taarifa ili tuweze kuchangia kwa kitu ambacho tunakisoma tusiingizwe katika mtego ambao tutakuwa tunajadili kitu ambacho hatutaweza kufanya nukuu, hatutaweza kusema taarifa ya Kamati imesema nini. Itakuwa sio sawa sawa hili Bunge lisipunguzwe hadhi kiasi kwamba tujadili kitu ambacho kanuni zinasema kinatakiwa itolewe nakala kwa Wabunge, lakini nakala hazijatolewa, nashukuru sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Waingereza wanasema *there come the time*. Ziko nyakati ambazo kama Kiongozi lazima ukubali kufanya kazi katika mazingira fulani. Nianze na la kwanza, mtakumbuka Bunge liliopita palikuwa na mambo mawili makubwa. Moja ni hili la masuala ya ujangili na jingine ni masuala ya matatizo yaliyopo kati ya wafugaji na wakulima nchini. Bunge hili likaazimia kwamba kwa masuala ya wakulima na wafugaji Nchini iundwe Tume ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Profesa Msolla na Tume hiyo inafanya kazi Tume ya Bunge wakati muafaka itakapokuwa imemaliza ripoti yake tutaipata.

Kwa hili la Operesheni Tokomeza, Bunge hili likaazimia kwamba Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ipewe jukumu la kufuatilia kama sehemu ya kazi yake ya kawaida, Kamti ile ikaunda Kamati ndogo ya watu 9 ambayo ndio wamefanya kazi hiyo, kwa hiyo leo wakati wanawasilisha kazi zao za mwaka mzima hii ni *appendix* mojawapo ya kazi zao za kawaida za mwaka mzima.

Kwa hiyo, kwa ripoti yao ya kazi zao za kawaida wameileta na wote tunayo nakala. Kwa sehemu ya hii ya *appendix* ambayo ni kazi maalum, ambayo walipewa kama Kamati, ndiyo hii ambayo Mwenyekiti ameisoma kama sehemu ya kazi yao ya mwaka mzima. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU SPIKA]

Kazi hii wameifanya kwa *pressure* kubwa sana katika muda mfupi sana, wamefanya kazi hawa watu mpaka leo saa 7 usiku walikuwa bado wanafanya kazi ya kuiweka vizuri hii ripoti yao. Kwa hiyo imeenda kwenye machapisho kwenye saa 3 asubuhi hii wakati tunaingia hapa, kuingia kuchapwa kule *Hansard* na kuna picha kuna kuna nini na kadhalika.

Kwa kuwa ratiba yetu ya Bunge mnaifahamu hapa tulipofikia na hali yake na haiwezi kuahirishwa jambo hili ndio maana tukaona ni vizuri isomwe bila kuichelewesha na bila kuahirisha ili Waheshimiwa Wabunge muweze kusikia na nawahakikishia katika muda si mrefu sana mtaanza kupata nakala za vitabu vyenyewe vya hotuba ambayo imesomwa hapa mbele yetu.

Kwa hiyo, sisi wenyewe ni Viongozi mazingira yetu ni hayo hakuna alieyepanga kwamba jambo hili liwe hivi au lisiwe hivi ni maamuzi yetu sisi wenyewe endapo kweli kwa taarifa nzito kama hii kwa mapendekezo ya Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba tuahirishe na mnafahamu ratiba yetu ilivyo. Kwa maana hiyo itakuwa jambo lenyewe ndio hivyo tena au tuweze kusonga mbele. (*Makofi*)

La pili lilihusu nafikiri nimemaliza yote mawili, nimeeleza yote mawili mnaonaje kwa muda kwa sababu muda wetu ni mdogo sana na wachangiaji wetu ni wengi kweli kweli basi tuwachukue hayo. Ni hili hili au kuna linguine. Haya haya.

Haya Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Zitto Kabwe, na Mheshimiwa Moses Machali. Haya wanen hao kule mwisho Mheshimiwa Mfutamba nani mwingine. Nawaombeni mseme kwa kifupi sana, halafu tuweze kuendelea. Mheshimimwa Kangi Lugola uanze wewe.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. KANGI N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika leo tulikuwa tunapokea taarifa tatu, ikiwemo hii ambayo ilikuwa ni ya Kiuchunguzi. Sasa Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa jambo hili ambalo limetoka kutolewa taarifa muda mfupi uliopita. Mimi hainiingii akilini Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tuna dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba tunajadili taarifa hii muhimu kwa Watanzania, kuhakikisha kwamba haya yote yaliyosemwa Wabunge waingie kwa undani kuyachangia na kutoa ushauri ili mambo haya Mheshimiwa Naibu Spika yasije yakajirudia tena, yasije yakatokea tena.

Sasa kwangu mimi nachelea kusema kwamba ratiba hii imepangwa namna hii ili kutunyima fursa Waheshimiwa Wabunge, iwe ni kupidisha pitisha tu mambo hapa haraka haraka na ndio mtindo wa kulindana, kulindana kunaanza hapo.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mwongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusitenge muda wa kutosha wa kujadili taarifa hii na mimi niko tayari kufanya kazi hii bure bila hata posho, kama kisingizio itakuwa ni hela. Niko tayari ili tuhakikishe kwamba taarifa hili tunaitendea haki. Kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Nianze na hili nisilibakize wala kulichelewesha Mheshimiwa Kangi Lugola amesema hana hakika kama kuna dhamira ya dhati na anahisi kuna hali ya kulindana mimi naomba sisi kama Wabunge na watu wazima tuaminiane katika baadhi ya haya mambo, siku zote za ripoti za Kamati mmeona tunaleta Kamati mbili kwa wakati mmoja. Tunaleta Kamati mbili kwa wakati mmoja. Kwa umuhimu wa jambo hili tumeleta Kamati hii kwanza tuipe umuhimu wa kutosha.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU SPIKA]*

Kamati mbili kwa wakati mmoja. Tunaleta Kamati mbili kwa wakati mmoja. Kwa umuhimu wa jambo hili, tumeleta Kamati hii kwanza, tipe umuhimu wote unaowezekana, tuweke muda wetu katika jambo hilo. Je, huko ni kukosa kuwa na dhamira? Je, ni kutaka kulindana na kadhalika? (*Makofii*)

Nafikiri tuwe na nia njema Ndugu zangu. Tunapoletewa mambo mazito *tusi-panic* tukaanza kuhisiana na kufanya hivi; badala ya kushughulika na kilichoko mbele yetu, tunaanaa kutuhumiana na kuhisiana na kadhalika.

Tumejitalidi kuhakikisha kwamba jambo hili linapewa kipaumbele hiki kikubwa, na baadaye hapa Mheshimiwa Waziri wa Nchi atatoa ombi tuongeze saa moja twende hadi saa 8.00. Jioni tutaendelea na hili suala mpaka tufike mahali fulani pa kuridhika. Mambo mengine sasa inabidi niseme ingawa ilikuwa aje aseme Mheshimiwa Spika; ni kwamba Kamati ya Uongozi imeamua shughuli zetu zimalizike kesho. Maana yake ni kwamba bado tunaweza kurekebisha muda wetu vizuri na hili jambo likapata nafasi nzuri tu kama ambavyo tulikuwa tumedhamiria. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli kwa maana ya uongozi na Kamati ya Uongozi, na sisi wote tumejitalidi sana kuhakikisha kwamba jambo hili linapata fursa nzuri ili muweze kulitendea haki.

Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wangu ulikuwa ni huo huo. Nakushukuru wewe kwa kukubali kwamba mmeona uzito wa tatizo, na Kamati ya Uongozi mtakaa ili mwone kama mnawezaje kuongeza muda.

Kikubwa ni kwamba tunesikia mauji ya wananchi wetu, tunesikia mifugo ilivyouawa, tunesikia ukatili mkubwa uliofanywa kwa wananchi wetu; sasa tunataka muda wa kutosha kwa ajili ya kushughulikia suala hili, na kwamba mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati, Wabunge

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. L. J. MPINA]

tunataka tupate fursa nzuri. Mapendekezo yapo, na tunayakubali moja kwa moja. Lakini yapo mapendekezo ambayo lazima tuyafanyie mabadiliko ili kuweza kutoa adhabu kali kwa watu ambazo wamehusika na suala hili. (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Lekule Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu tu kuongea kwa busara kwa sababu jambo hili limeniuma sana.

Kwa miaka 20 niliyokaa Bungeni, sijapata kusikia matatizo au hoja inayochoma kama hii. Kwa vile Kanuni zetu siyo Amri Kumi za Mungu, tunaweza tukavunja, tunaweza tukabadiilisha; na jambo hili tulijadili kwa kina. Bado ni machache yaliyosemwa. Wale wananchi walioko hapo ni wale ambao wamenyanyaswa, taarifa zao haziko hapa, hazijatajwa kabisa! Naomba hili jambo tulijadili kwa kina zaidi, hata kama linaenda siku mbili. Nakubaliana na Ndugu yangu Mheshimiwa Lugola kwamba hata tusipolipwa chochote, tuko tayari kukaa siku mbili kujadili hili jambo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina taarifa nyingine, hatujaitendea haki kujadili hii, na hatutajadili jambo lingine lolote ndani ya Bunge hili mpaka tupate muafaka wa taarifa hii ili yosomwa hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Viongozi waliokwenda kwenye *operation* wametudhalilisha, sasa hakuna mtu anayetaka kuitwa ni kiongozi wa Tanzania. Ni aibu! Hii inauma! Hata Wakoloni waliotutawala hawajatutesa hivi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika na Kamati ya Uongozi, naomba mljadili hili jambo kwa makini. Msipolijadili, tunaweza tukatoka ndani ya hili Bunge kama hamjatupa majawabu ya kuridhisha. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Laizer, nakushukuru sana. Nikuhakishie kwamba Wenyevit wanasikia, Mheshimiwa Spika anasikia, na hili jambo litapewa nafasi yake. Mheshimiwa Machali, una lingine au linajirudia ili tukoe muda?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nipo hapo hapo, ila nitajielekeza kwenye Kanuni ya 68 (7) isomwe sambamba na Kanuni ya 47 (1).

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya tumekuwa tunajadili hapa Bungeni kwa muda mrefu sana. Tunazungumza, lakini wakati mwingine huwa hatujitendei haki sisi wenyewe kama Wabunge, lakini pia na wananchi wetu ambao wametupa nafasi ya kuwawakilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati ya Uongozi ni muhimu na ni busara tu kwa kutumia busara ya kawaida, inapaswa kufanya kazi kwa kusikiliza Wabunge tunasema nini. Kama ambavyo amechangia Mheshimiwa Laizer, Mheshimiwa Kangi Lugola na Mheshimiwa Mpina, naomba tukubaliane kwamba hata pasipo kulipwa posho, tuijadili ikiwezekana hata siku tatu, tutakuwa tumeitendea haki. Kwa sababu hiyo, naomba nitumie Kanuni ya 47 (1) kutoa hoja kwamba tuahirishe mijadala mingine, na jambo hili tulijadili kwa siku ambazo hazipungui mbili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012 Uingereza, Waandishi wa Habari walim-tape binti mmoja tu akafariki dunia. Waziri Mkuu wa Uingereza alikuwa *holiday*. Aliitisha *special session* ya Bunge kujadili jambo hilo. Mtu mmoja tu!

Leo hii tumpata Ripoti ya Kamati ya Bunge ambayo inazungumzia *abuses* za hali ya juu za wananchi wetu! Za hali ya juu kama jinsi ambavyo zimeelezwa hapa, halafu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. K. Z. ZITTO]

tuone kama hii ni hoja kama hoja nyingine yoyote! Hapana! Lazima sasa tujigeuze kama *session* maalum ya Bunge kujadili taarifa hii. Kwa sababu hata hii Taarifa ya Kazi ya Kamati ya Mwaka haijawasilishwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu-*schedule* Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Maliasili, tu-*schedule* Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kilimo. Tujadili jambo hili kama *special session*. Vinginevyo tutakuwa hatutendi haki kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia *trace* hata ya mapendekezo. Angalia *abuses* zilizofanyika na *traces* za mapendekezo. *To be frank, to be honest*, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati una Askari wameua, una Jeshi limeua, una Wizara ya Maliasili ambayo imeshindwa kufuata taratibu zinazotakiwa katika kazi; halafu Waziri unayesema ajipime, ni Waziri wa Mifugo tu.

**MBUNGE FULANI:** Na Maliasili!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Kama siyo kumwonea ni nini? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Ni kumwonea! (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tusipojadili hili, tutakuwa hatutendi haki! Jambo hili linahitaji *full government responsibility*. Ahirisha kwa muda, Wabunge wapate taarifa; turudi hapa baada ya kama saa moja au nusu saa kujadili. Huwezi kusema kwamba Kamati imemaliza kazi saa 7.00 usiku, halafu toka saa tatu mpaka sasa saa 6.07 eti taarifa haijachapishwa. Bunge gani hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahirisha kikao, taarifa Wabunge wagawiwe, tufanye *special session* ya Bunge kwa muda wowote ambao tutakaokaa tujadiliane tumalize hili jambo, ndiyo mambo mengine yaendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuhusu jambo hilo. (*Makofi/Kicheko*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MBUNGE FULANI:** Sawa kabisa!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwashukuru sana wale wote ambao wamezungumza asubuhi ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Mheshimiwa Mfutakamba alikuwa wa mwisho. Samahani sana Mheshimiwa Mfutakamba.

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kufuatana na Kanuni ya 68 (7), nami nina suala la kuleta mbele yako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mfutakamba, siyo ilikuwa tumalize hili kwanza? Basi malizia.

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Ndiyo ndiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema jana Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi alizungumzia suala linalohusu ujenzi wa gati 13 na 14; Naye Mheshimiwa Waziri alikuwa ameeleza tatizo la ujenzi wa hili gati na kwamba Kampuni iliyopewa hilo jukumu, ilionekana...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mfutakamba!

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilinde.

**NAIBU SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Mfutakamba. Wanachosema Wabunge, soma nyakati tu. Tuliweke baadaye jambo hilo. Baadaye kidogo! Nakushukuru sana kwa kunielewa.

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU SPIKA]

Waheshimiwa Wabunge, napenda kupokea maoni yaliyotolewa na Wabunge wenzetu hapa kuhusiana na tunafanya vipi kuhusu jambo liliilo mbele yetu. Niwahakikishieni kwamba Kamati hii imefanya kazi yake kwa usiri mkubwa kama inavyopasa kuwa. Taarifa hii iliyopokelewa na kusomwa hapa, hata mimi mwenyewe ndiyo nasikia kwa mara ya kwanza haya mambo. Ndiyo maana nasema, ile hoja ya kusema kwamba kuna njama, kuna nini; hakuna njama za namna hiyo.

Kwanza napenda kuwaondoa wasiwasi huo kwamba kuna jambo hilo, na Kamati ya Uongozi ambao ndio Washauri wetu Wakuu na ni Wajumbe wako hapa, hata wao hawajui undani wa taarifa hii kwamba kulikuwa na jambo gani. Kwa hiyo, ilikuwa ni vigumu kuweza kujua namna ya kuweza kuendana nalo. Lakini kwa yaliyojiri hapa ambayo sote sasa tumeyaona na kuyasikia yaliyofanyika hapa, nadhani ni busara sana kwamba Kamati ya Uongozi ikutane mara moja. Nadhani tukiwapa muda wa nusu saa, unaweza ukawatosha. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba nisitishe Shughuli za Bunge kwa muda wa nusu saa kuwaruhusu Kamati ya Uongozi kwenda kuungana na Mheshimiwa Spika pale kwenye Ukumbi wa Spika haraka sana ili kuweza kutupatia mwongozo wa namna gani ya kushughulika na jambo hili.

Naomba kusitisha shughuli za Bunge. (*Makofi*)

(*Saa 6.58 Bunge lilsitishwa kwa muda*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyokumbuka, muda mchache uliopita mlitoa mapendekezo hapa kwamba Kamati ya Uongozi ikutane kwa dharura, kwa haraka na niwataarifuni kwamba Kamati ya Uongozi imekutana na imejadili na kuzingatia ushauri ambao mmeutoa, kwa hiyo Kamati ya Uongozi imeelekeza kwamba mjadala huu uendelee asubuhi hii hadi saa 8.00 mchana, tutaahirisha na jioni tuanze saa 10.00 na tuendelee hadi saa 3.00 usiku. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU SPIKA]

Baadaye kidogo tutamwomba Waziri wa Nchi hapo mbele ya safari afanye ule utaratibu wetu wa kawaida ili tuweze kuzingatia mabadiliko hayo ya muda na muweze kuyaafiki ili tuweze kufanya hivyo. Sasa bila kupoteza muda, naomba tuendelee na wachangiaji kwa ridhaa yenu. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Said Nkumba na mchangiaji wa pili atakuwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Zitto ajiandae.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia.

Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wake kwa kazi nzuri waliyofanya kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii vilevile kuwapa pole Watanzania wote walioathirika na operesheni hii Tokomeza kama ambavyo taarifa ya Kamati ilivyojieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze tu kuchangia kwa kuona dosari zilizopo kwenye mfumo wetu wa kiserikali. Kwenye taarifa ambayo kwa kweli tumepewa na Mheshimiwa Mwenyekiti hapa, tumeambiwa kwamba imefika mahali Watendaji wa Serikali wakawa wanajifanyia mambo yaliyoleta athari kubwa kwa wananchi wetu, lakini baadhi ya Mawaziri wakawa hawaelewi kinachoendelea. Hili ni jambo bayaa na hili ni jambo ambalo kwenye mfumo wetu wa Serikali lazima lirekebishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme kwamba hapa ndani tunaweza tukawa tunaendelea kufukuzana tu na Mawaziri kila siku, leo tutafukuza huyu kesho tutafukuza huyu keshokutwa tutafukuza huyu. Lakini kama tusipoangalia tatizo liko wapi, tunaweza tukaendelea kuwa na Serikali kila wakati; katika kipindi cha miaka mitano Mheshimiwa Rais anapata kazi ya kuondoa Mawaziri na kuweka Mawaziri wengine.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. S. J. NKUMBAJ]

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa naomba, Serikali ni lazima iwave meno ya kutosha Mawaziri kutekeleza wajibu wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri hapa watakubaliana na mimi kwamba wanapambana na matatizo makubwa katika kutekeleza mambo yao. Baadhi ya Watendaji wa Serikali katika baadhi ya Wizara wana viburi ambavyo wanafika mahali hata Waheshimiwa Mawaziri sasa kutekeleza baadhi ya wajibu wao inakuwa ni ngumu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana jambo hili lipatiwe ufumbuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye athari zilizojitokeza. Nataka niseme mambo mawili tu. Hili la athari, ni fedheha kubwa, ni aibu kubwa kwa Watanzania wetu na mimi siungi mkono haya maelezo yaliyokuwa yanatolewa hapa ya Mwenyekiti wa Kamati kwamba Mheshimiwa mmoja tu, Mheshimiwa Mathayo ndio ajipime. Mimi nataka niseme, maana kwa Mheshimiwa Mathayo ni ng'ombe ndio waliokufa; lakini wapo watu waliokufa. Sasa kama unaweza kumwadhibu mtu kwa ng'ombe kufa, ukawaacha wale ambao kwa kweli kumetokea mauaji ya binadamu, tutakuwa hatujatenda haki. Kwa hiyo, nilikuwa nataka niombe, kila mmoja ajipime. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nawasilisha tarehe 30 niliwasilisha, lakini baadaye yakawepo maneno, hayo ni maneno ya wanasiasa. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba kazi nzuri iliyofanywa na Kamati imedhihirisha wazi kabisa kwamba Wabunge tunapoleta hoja zetu hapa tunazo hoja za msingi kwa maslahi ya Watanzania kwa maslahi ya wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba, bila ya kumpa kazi Mheshimiwa Rais, yaani unampa kazi Mheshimiwa Rais aliyekupa nafasi ya kukuteua, hebu kaa wewe mwenyewe, jipime wewe mwenyewe; mimi hapa nimekuwepo toka mwaka 2000. Baadhi ya Mawaziri hapa baada ya kupima upepo, walikuwa wanajiondoa mapema.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. S. J. NKUMBAJ]

Mnawapa kazi, tunabadilisha hapa na ratiba, na nini. Hivi watu wengine hapa wangeshatoa maamuzi yao mapema, tusingekuwa na kazi hizi tunazoendelea kurudiarudia hapa. Kuingia unaingia kwa shangwe, lakini lazima ukubali kwamba kuna siku nyininge watu wakisema ondoka, basi unajiandaa wewe mwenyewe mapema, usimsubiri Mheshimiwa Rais akufukuze.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watu waliosababisha mambo haya wanajitambua. Mimi sina sababu ya kuendelea kuwataja mmoja baada ya mwingine. Mimi nasema, bila ya kumpa tena kazi Mheshimiwa Rais ya kuanza kusema kwamba anabadilisha Baraza la Mawaziri, hawa watu kama walivyofanya watu wengine huko siku za nyuma, itakapokuwa inafika kesho wawe wameshatoa kauli yao na Bunge hili lilitidhie na Mheshimiwa Rais afanye kazi ya kufanya mabadiliko kama ambavyo amekuwa akifanya mabadiliko baada ya watu wengine kuondoka kwa ridhaa yao. Hili siyo jambo geni. Hakuna aliyechaguliwa Ubunge hapa kwa nafasi ya Uwaziri. Wote tumechaguliwa Ubunge na nafasi ya Uwaziri kila mmoja hapa kwa nafasi yake anaweza akapewa na Mheshimiwa Rais katika kuendelea kumsaidia kuendesha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naiomba Serikali kwa wale wote ambao kwa kweli imedhihirika wameumiza wananchi wetu, wameua wananchi wetu, wametokomeza mifugo na kuwaacha wananchi wetu katika hali ya umasikini Serikali ichukue hatua kubwa sana ya kuhakikisha kwamba hawa wanapata adhabu yao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wameachwa kwenye hali mbaya sana. Katika maeneo mengi wananchi wengine wameachwa vilema, wananchi wengine wameachwa masikini baada ya mifugo yao kufa. Jambo hili haliwezi kuvumiliwa kwa sababu siyo Sera za Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Hawa ni watu wachache, wamefanya haya mambo kwa maamuzi yao, watu wengine wamekula rushwa katika baadhi ya maeneo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. J. NKUMBAJ]

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali ichukue hatua za dhati kabisa kuhakikisha kwamba watu hao wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Baada ya maneno haya naendelea kuwaomba tena radhi Watanzania na ninaendelea kuwaomba kabisa msamaha Watanzania wote kwa haya yaliyotokea. Lakini nasisitiza kwamba lazima sheria ichukue mkondo wake.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Nkumba kwa kutuanzishia mjadala. Nilisahau tu kuwaambieni kwamba ile Taarifa ya Kilimo, Maji na Mifugo yenye we haitajadiliwa leo wala katika Mkutano huu, yenye we itakuja katika Mkutano mwingine utakaofuata hapo mbele ya safari. Kwa hiyo, tujikite katika jambo ambalo liko mbele yetu.

Mheshimiwa Abdulkarim Shah nilishakutaja na Mheshimiwa Zitto Kabwe utafuata.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Bismilah Rahman Rahim!

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote na jamii ya wananchi wa Tanzania, naongea nikiwa na masikitiko makubwa sana kwa sababu nimeyaona yale yaliyotokea huko vijijini katika baadhi ya maeneo niliyokwenda.

Kwanza naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni mmoja ya watu tuliokuwa katika Tume kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na nilongoza upande wa Kagera, Mara, Manyara na Arusha kama Kamati ndogo iliyokwenda huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonisikitisha zaidi, pale Mheshimiwa Rais anapoamua kuteua mtu kwa mapenzi na akajua kwamba huyu atanisaidia, kumbe masikini ya Mungu baadaye anakuja kuwa tatizo katika nchi hii. Mwisho wake

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. A. E. H. SHAH]

ni kukidhalilisha Chama chetu, Serikali yetu, lakini kumdhalilisha hata yule aliyejikuwa amemteua. Kwa sababu maneno yanayoandikwa kwenye hizi *Blogs* ni machafu sana yanayokashifu viongozi wetu. Sasa linapofikia jambo hilli, lazima tukubali kwamba unapokabidhiwa dhamana fanya kazi uliyokabidhiwa, siyo ufanye ya kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyotendeka huko kama tulivyotoa kwenye taarifa yetu ni mambo makubwa sana. Ule Umma uliouona pale juu, wale ni punje tu ya Wawakilishi katika nchi hii. Naamini kwamba kuna baadhi ya maeneo wengine hawakuweza kufika kutokana na umasikini walioupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, unateuliwa na Mheshimiwa Rais kusimamia eneo fulani, wewe linatokea jambo operesheni hii imetesa watu maeneo kwa mfano; ukienda kule Nyanungu, Mwamtemi, Matombo, Sakasaka, Itilima, Mbogo, Bukore, Kimotolo lakini ukifika Galapo lazima ulie! Lazima ulie! Nililia wakati wa kuhoji wale wananchi kwa yale yaliyofika pale. Halafu wewe kiongozi unakwenda kutoa taarifa kwa Umma kwenye gazeti, unasema mauaji yale yaliyotokea eti ni *blood pressure*. *Blood pressure* sijui Kiswahili chake nini? Shinikizo la damu. Mheshimiwa naomba nikuoneshe picha hii. Hili ni tangazo lillilotolewa.

Angalia picha hii! Yule mwanamke pale ni mtu aliyejuka kwa *blood pressure*? Angalia pale, kuna chuma kimemtoboa kwenye jicho. Peleka mbele picha uangalie alivyoburuzwa mgongoni! Ni Mtanzania yule, mwanamke! Watu wanalia wa Kijiji cha Galapo. Sio huyo, watu wengi wamepoteza maisha! Tunasema hili hatukubali. Angalia mgongo, yule mtu wa *BP* yule? Yule kafa kwa *BP*? Wataalamu, kuna Madaktari humu, angalieni. Ule ni mgongo na katikati kuna majani, labda ile haionekani vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hapa ni *blood pressure*? Unakwenda kuongopa! Mtanzania mwenzako; hukuzaliwa? Hukutoka kwenye mifupa ya wanawake wa Kitanzania? Wewe unakwenda kutesa!

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. A. E. H. SHAH]

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tusikubaliane nalo na ninawashawishi Waheshimiwa Wabunge hakuna kukubali. Watu wameteswa, watu wameuana! Binadamu, wewe mtoto umetoka kwenye mifupa ya Watanzania, unamwambia Mtanzania mwenzako atembee na mnyama aliyekufa! Eeh! Unamwambia Mtanzania amwingilie swala aliyekufa? Jeshi gani hilo? Polisi gani huyo? *KDU* gani huyo? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli tutaendelea kutoa wahanga kila siku hapa Mawaziri lakini Watendaji wetu ni wabaya sana. Naomba nirudie kunukuu maelezo aliyyoyatoa Mheshimiwa Lusinde kwamba maadui zetu sisi wa Serikali hii sio hawa Wapinzani. Maadui zetu ni Watendaji wetu, wameshindwa kusimamia. Wewe unakwenda kuambiwa katafute; ni jangili gani waliyemkamata?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda Vituo vyta Polisi vyote! Nenda Minjingu ukaangalie, *OCCID* anavyotesa watu! Kamuua *OCCID* na mtu mmoja anaitwa sijui Shironga, Sharango sijui Shirungani sijui jina lipo; ndio waliomuua. Tena wanakwenda kumwambia kabisa mtoto wake wa kiume, tunakwenda kumuua mama yako; na kweli asubuhi walipigwa simu njooni mchukue maiti yenu. Unyama gani huu? Nenda Bukore, lakini nachosema, maneno mengine yatasemwa na wengine.

Ninachosema, nchi hii kama hawa Waheshimiwa Mawaziri wakiendelea kukaa kwenye maofisi tu, nchi hii watu wataendelea kuuana kila siku. Nasema lazima Waziri wa Ardhi na timu yake, Waziri wa TAMISEMI na Ma-GN yake anayoyaandika pamoja na Waziri wa Maliasili lazima wakapige kambi kule maporini vijijini, hata kama wao hawawezi kutafunwa na mbung'o lakini wajue kuna Watanzania wanaoathirika, wakategue mtego huu wa kuweka mipaka iliyokuwa wazi. Bila hivyo, wale kila siku watakuwa ndio uchumi wa Watumishi wa Maliasili katika mtando mzima wa biashara. Wala hakukuwa na Operesheni Tokomeza Ujangili, ilikuwa ni Operesheni Tokomeza Mifugo. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. E. H. SHAH]

Mheshimiwa Naibu Spika, unasikia! Hilo limesemwa! Tunaambiwa nyinyi viongozi mna laana? Unawaambia tupunguze mifugo; mifugo inapunguzwa kwa kutoswa kwenye maji? Mifugo inapunguzwa kwa kupigwa risasi? Halafu Waziri yule pale eti leo anashangilia kutajwa kwamba anaonewa; hukuokolewa! Wewe ulikuwa wapi? Waziri wa Mifugo, wale wanateseka, umesema nini? Umetumaliza kwenye uvuvi wewe! Kiko wapi leo nchi hii katika uvuvi? Wapi kwenye uvuvi na aseme mtu. Serikali upande wa uvuvi inachangia asilimia ngapi pato la Taifa kutokana na uvuvi? Keshatumaliza tikitiki! Tumekwisha tikitiki! Yaani katusaga kabisa! Sasa anakwenda upande wa mifugo mniamalizwa. Tuliyyasema haya lazima wakubali kwamba hawa wote waliokuwa hawako kamili katika kushughulikia yale waliyopewa na Mheshimiwa Rais, wao wanakwenda kushughulika na biashara zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Rais anaona hili ni zito, basi tunaomba Idara ya Uvuvi irudishwe Maliasili. Kule wamechemsha! Wao wanaangalia mifugo tu. Au waweke mtu ambaye anaelewa masuala ya uvuvi. Sasa katumaliza uvuvi, anawaingilia mifugo na watu wa mifugo ili na wao wapate kupungua pale kazi zisiwe nyingi, basi bora ng'ombe wale wapigwe risasi. Ndiyo wanavyoona!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachosema, haya mambo watu wawajibike. Wale viongozi watatu katika Mpango kazi ule uliotolewa, waliokabidhiwa dhamana siyo wafukuzwe kazi, washitakiwe kwa makosa ya kuua kwa makusudi na timu yao yote waliokwenda. Nendeni Andajega huko, leo kunaitwa Gwantanamo. Tanzania ikafananishwe na Gwantanamo, eeh! Tanzania ikafananishwe na sehemu mbalimbali mbaya! Mpaka watu walisema labda Serikali ilichukua majeshi kutoka nje kuja kutuua. Wao labda walikuwa wanaona haya. Unaona! Hebu tuangalie, tumekwenda maporini; tumeambiwa hapa pana meno ya Tembo karibu sijui tani ngapi. Mbona hatujaona hata mizoga kumi ya Tembo? Pengine ni ujinga tu, wanachukua pale pale *Ivory Room* wanauzuwanajifanya kuzungushazungusha tu, halafu wanakwenda. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. E. H. SHAH]

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifanye DNA kwa pembe zote zile zilizokamatwa na zile zilizokuwepo tuone kama hakuna pembe feki mle. Labda wahamishe sasa hivi. (*Makof*)

Kwa hiyo, tunavyosema, haya jamani yaliyotokea ni mabaya sana. Watu wamedhalilishwa, watu wamebakwa, watu wamevurugwa chini; mwanimke wa Kitanzania unamwambia jangili, halafu unamlazimisha; sema wewe! Lete bunduki ya mumeo! Hana bunduki; anayo! Watu wamedhalilishwa mbele ya watoto wao, unaambiwa mfanye mwanao! Kwanini mnafanya vitendo hivi? Unafanywa mbele ya wakwe zako! Hebu angalia, mama yule, aah!

Mheshimiwa Naibu Spika, yalikuwa hayo tu. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda wetu ndiyo huo, namwomba sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atupitishe kwenye ongezeko la muda ili tuweze kuendelea hadi saa 8.00 leo mchana kwamba tuweze kuanza saa 10.00 jioni na kuendelea hadi saa 3.00 usiku.

### **HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013.

KWA KUWA, Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge wa kushughulikia Taarifa za Mwaka za Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na Shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa, zimepangwa kumalizika tarehe 20 Desemba, 2013;

NA KWA KUWA, ratiba ya Shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu wa Kumi na Nne imepangwa kwa kuzingatia kalenda ya Mikutano ya Bunge;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU(SERA, URATIBU NA BUNGE)]

NA KWA KUWA, ratiba hii inaonesha kwamba majadiliano ya Taarifa za Kamati za Bunge za Ardhi, Maliasili na Mazingira pamoja na Kilimo, Mifugo na Maji yamepangwa kufanyika leo tarehe 20 Desemba, 2013;

NA KWA KUWA, Kamati ya Uongozi ya Bunge katika Kikao chake kilichofanyika leo tarehe 20 Desemba, 2013 katika Ukumbi wa Spika, iliamua kuwa Taarifa za Kamati hizo ziwasilishwe na kujadiliwa moja moja kwa lengo la kutoa fursa pana kwa Wabunge kujadili kwa kina kila Taarifa;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) Bunge linakutana hadi Saa 7.00 mchana na kuahirishwa mpaka saa 11.00 jioni ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake zilizopangwa kikamilifu, na wakati huo huo kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge wengi kupata fursa ya kujadili Taarifa ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, inabidi Bunge litengue Kanuni 28(2);

NA KWA KUWA katika Kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika leo tarehe 20 Desemba, 2013 Wenyevitit wote wa Kamati za Kudumu za Bunge waliohudhuria wamekubaliana na umuhimu wa kutengua Kanuni husika;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa Shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Nne Kanuni 28(2) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(2) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge linakutana hadi saa 7.00 mchana ambapo Spika ataahirisha Shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa 11.00 jioni itenguliwe na badala yake Bunge liendelee mpaka saa 8.00 mchana ambapo Spika ataahirisha Shughuli za Bunge na lirejee saa 10.00 jioni na liendelee mpaka saa 3.00 usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoka hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nashukuru hoja imetolewa na kwa kweli imeungwa mkono. Wote kabisa wameafiki, nawashukuruni sana. Tunaendelea kwa ratiba hiyo ambayo imetajwa.

Sasa namwita Mheshimiwa Zitto Kabwe, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kwa majonzi makubwa sana kwanza kutoa pole kwa Watanzania wote ambao kwa namna moja ama nyiningine wameathirika na Operesheni Tokomeza. Kwa wale ambao wamepoteza maisha, Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Kwa wale ambao wameteswa na kubakwa, lazima tuweze kuona wakiwa hai kwamba wametendewa haki na Baraza hili la Wawakilishi kwa wananchi, Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba kumekuwa na vitendo vya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Ujisoma taarifa hii ukurasa wa 23, ukurasa wa 31, ukurasa wa 32 na ukurasa wa 36 zote zinaonyesha kwa ushahidi namna ambavyo Watanzania wameteswa. Hawajateswa na wagoni, wameteswa na Askari wao ambao ni wajibu wao kuwalinda. Wanatoa kodi zao kwa ajili ya kuwavisha, kuwalisha, kuwalishwa viatu, kuwanunulia silaha, lakini vitu hivyo ndivyo vimetumika kwenda kuwaresa, kuwanyanyasa na kuwaua wananchi.

Katika ukurasa 23 Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi anakiri, anaiaambia Kamati kwamba kulikuwa na upungufu, kwa mfano, ukatili dhidi ya mifugo na vitendo vya unyanyasaji wa wananchi kwa kuwaresa kiasi cha kuwasababishia ulemavu wa kudumu au vifo.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. K. Z. ZITTO]

Mheshimiwa Naibub Spika, ukienda ukurasa wa 36 Kamati kinagaubaga imetaja na watu waliokufa. Wamemtaja Kipara Issa wa Kaliua, Emiliana Gasper Maro wa Babati, Wegesa Kirigitu wa Remagwe na Ndugu Peter Masea wa Kijiji cha Mrito Wilaya ya Tarime vyote hivi viwili; Ndugu Mohamed Buto wa Masasi na Gervas Nzoya wa Kasulu. Hawa ni Watanzania ambao wameuawa katika katika Operesheni ambayo inaendeshwa kwa amri ya Serikali. Hatuwezi kuvumilia vitendo kama hivi hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa imeonesha watu ambao wameteswa. Kwa mfano, ukurasa wa 32, Diwani wa Kata ya Sakasaka Wilaya ya Meatu, Ndugu Peter Samwel ambaye alining'inizwa miguu juu kichwa chini na Askari; Diwani ambaye amechaguliwa na wananchi, kiongozi; na humu kwenye Taarifa hii tumeambiwa kwamba kulikuwa na maelezo kwamba wanasiasa wasiguswe. Lakini huyu ni Diwani, amechaguliwa na wananchi, ameteswa katika operesheni hii; ambapo tungetegemea ingekuwa ni operesheni kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, kupambana na ujangili na kuweza kuhakikisha kwamba wanyama wetu katika Hifadhi za Taifa tembo wetu wanadumu. Lakini matokeo yake operesheni hii ikaenda kuwashughulikia wananchi pamoja na mali zao kwa maana ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa inasema, wanasiasa walihujumu operesheni hii. Ukurasa wa 19 na ukurasa wa 21 wa taarifa. Lakini Taarifa haituambii ni wanasiasa gani hao! Haisemi wanasiasa hawa kwa majina yao ni akina nani? Kwa sababu mambo haya ni lazima yajadiliwe kwenye Baraza hili la Wananchi. Hili ndilo Baraza la Taifa. Hakuna sababu ya Kamati kutumia maneno kama baadhi ya Mawaziri. Baadhi ya wanasiasa. Kwa sababu kazi ya kiuchunguzi ya Kamati inapaswa ituletee taarifa ambazo ni kamili kabisa.

Kwa hiyo, tungependa Kamati ije kufafanua hawa wanasiasa ni akinanani? Kwa sababu ni dhahiri zoezi hili liliifanyiwa hujuma. Ni dhahiri! Ni dhahiri zoezi hili ambalo lilikuwa na lengo la kuhakikisha kwamba tunaokoa tembo wetu, limefanyiwa hujuma. Ni kwa makusudi au kwa bahati

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. K. Z. ZITTO]

mbaya, sisi hatujui, lakini lazima hujuma zilikuwemo na ni lazima hatua ziweze kuchukuliwa kwa watu ambao wanahuksika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza asubuhi kwamba operesheni hii iliendeshwa na Wizara tatu, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Maliasili na Utalii. Haiwezekani kamwe pasiwe na uwajibikaji katika Wizara hizi, haiwezekani! *Whether Mawaziri wamefanya makosa au hawakufanya makosa, kwa sababu ndivyo tunavyotaka kuweka misingi ya uwajibikaji katika nchi yetu. Kamati inapendekeza Waziri wa Mifugo ajipime. Waziri wa Mifugo ng'ombe wake ndiyo wameuawa. Mifugo yake ndiyo imeuawa; ajipime. Mawaziri ambao wananchi wamekufa, wasijipime.* (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo, hili jambo ni kubwa sana na ndiyo maana wewe mwenyewe na Kamati yako ya Uongozi mmeamua tuwe na Kikao hiki Maalum siku nzima leo mpaka saa 3.00 usiku, hajawahi kutokea katika historia ya Bunge letu. Kwa sababu ni kikao muhimu sana, kinawahuksika kinawahuksika wananchi wetu. Watu wamekufa! Hakuna namna yoyote ambayo tunaweza kuwaonesha wananchi kwamba tumekasirishwa na kitendo hiki, tumekasirishwa na kuteswa kwao, tumekasirishwa na kuuawa kwao, tumekasirishwa na akinamama zetu kunyanyaswa na kubakwa! Hakuna namna zaidi ya Serikali nzima kuwajibika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposema Serikali nzima kuwajibika, nina maana ya Waziri Mkuu kuchukua *political responsibility*, ndiyo njia pekee ya kuweza kuonesha kwamba tumekerwa na jambo hili. Tumeumizwa na jambo hili! Ndiyo njia pekee ya kuhakikisha kwamba Serikali nyingine zitakapoundwa zijue, hata akifa Mtanzania mmoja, akiteswa Mtanzania mmoja, akibakwa mwanamke mmoja wa Kitanzania kwa kazi ya halali au ya haramu, ni lazima wanasiasa tuwajibike. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. K. Z. ZITTO]

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba, kwa heshima na taadhima kabisa Waziri Mkuu achukue *political responsibility*. Sisi kama Bunge hatuna nguvu ya kumtoa Mheshimiwa Kagasheki, hatuna nguvu ya kumtoa Mheshimiwa Nahodha, hatuna nguvu ya kumtoa Mheshimiwa Nchimbi, hatuna nguvu ya kumtoa Waziri wa Mifugo ambaye mifugo yake imeuawa na anatakiwa kujipima; lakini sisi kama Bunge tuna nguvu ya kumtoa Waziri Mkuu. Siyo kwa makosa aliyoafanya; Mzee Mwinyi alipojiuzulu, hakufanya makosa. Walikufa watu Shinyanga huko, yeye alikuwa Dar es Salaam, alichukua *political responsibility* na historia ikamwonesha baadaye akaja kuwa Rais wa Jamhuri ya Tanzania. (*Makof*)

Kwa hiyo, haina maana kwamba kuchukua *political responsibility* ni kuwa umefanya makosa. Kuchukua *political responsibility* ni kuonesha kuchukizwa na yaliyotokea. Kuchukizwa na raia wako kuumizwa, kuchukizwa na akinamama wa Kitanzania kubakwa na kuchukizwa na Watanzania kuteswa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo hoja ambayo nilikuwa naomba niitoe kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuchukua *political responsibility* juu ya jambo hilo. Kama hachukui, Bunge linaweza kuchukua taratibu zinazopaswa kwa mujibu wa Kanuni kuweza kumwondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia atafuatiwa na Mheshimiwa Lulida.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa nitoe pole na masikitiko makubwa kwa Watanzania waliopoteza uhai wao kwenye operesheni hii, uhai wa mwanadamu ambao ukishatoweka huwezi ukaurudisha tena; lakini uhai ambao wenzenetu Watanzania wamepoteza maisha ni fedheha kubwa siyo kwa Tanzania tu, kwa dunia nzima kwa sababu taarifa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. J. F. MBATIA]*

iliyotolewa hapa ipo duniani kote sasa kwamba Tanzania ndivyo tulivyo. Kwa hiyo, ni aibu na fedheha kwa Taifa zima la Tanzania. Yaani Taifa letu tumefikia hatua ya namna hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya, utafiti wa kina walioufanya na kuweka mambo yote kwa uwazi. Hapa kuna Askari sita wamepoteza maisha, raia wa Tanzania 13 wamepoteza maisha; tunatakiwa kutafakari kwa kina kwa nini tufikie hatua hiyo? Kwa nini, kwa nini, kwa nini tumefikia hatua hii? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu tatizo hili ni kubwa sana. Halikuanza jana wala juzi; hili ni tatizo la kimfumo na limelelewa kwa zaidi ya miaka ishirini na kitu. Nakumbuka tangu Baba wa Taifa akiwa hai alilalamika kuhusu mambo ya Loliondo mwishoni mwa miaka ya 1980, mwanzoni mwa miaka ya 1990; wanyama wakiwa wanauzwa mwanzoni mwa miaka ya 1990, hali ikiwa ni tete na ndiyo maana leo hii mnaona kwamba ripoti imetaja baadhi ya Wabunge. Ingekuwa ni vyema majina ya Wabunge wote yakatajwa kwa majina waliohusika kwenye mchakato huu wote ili kuweka mambo wazi. Huwezi ukasema tu baadhi ya Wabunge, tuwataje tu tujue kwamba Wabunge moja, mbili, tatu wanahuksika kwenye mambo haya. Wametajwa baadhi ya wanasiasa; na wanasiasa watajwe vilevile wawekwe wazi majina yao tujue ni nani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini isitoshe, ninaposema ni tatizo kubwa la kimfumo, hapa vinatajwa hata Vyama vya Siasa; navyo vitajwe vilevile Vyama vya Siasa hivi na hivi vimehusika katika mambo haya. Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Jeshi linahuksika, Polisi wanahuksika, Askari wa Wanyamapor wa wanahuksika. Kwa hiyo, hata wale waliopewa dhamana ya Ulinzi wa Usalama wa Taifa letu nao wamehusika katika mauaji haya ya kikatili na ya kinyama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalendo wa Taifa upo hatiani, upo katika mashaka. Sasa kama wote wamehusika, Bunge limehusika, Serikali imehusika, Vyombo vya Ulinzi na

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. J. F. MBATIA]

Usalama vimehusika, ni jambo la kutafakari na kuwa na utulivu wa ndani sana. Je, Tanzania tutafika? Tuko wapi? Taifa letu leo hii lipo wapi? (Makof)

Tunaomba kwa nia njema tu, wale ambao wamehusika isionekane kwamba; hawa Watendaji inaonekana wamekuwa Miungu watu dhidi ya viongozi. Lakini hata Waziri, kwanza Mheshimiwa Maige ndio aliondolewa kwenye Wizara hii kwanza, kwenye vurugu vurugu tu. Sasa leo hii imeangukia tena Wizara hii hii: Je, najiuliza, kama siyo mfumo, Waziri atafanya kazi kwa *route match*, yaani awe ni kiongozi kwenye Wilaya, awe kiongozi kwenye Mkoa, awe kiongozi kwenye Hifadhi awe ndiyo Waziri, ndio Mtendaji, awe nani, kwa hivi ni tatizo kubwa la kimfumo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba lazima tu *itemize* yaani kuwe na moja, mbili, tatu, nne na tuweze kuona ni namna gani iliyo bora kuhakikisha *mitigation measures* zinachukuliwa ili kuondokana na tatizo hili. Kwa sababu tatizo limejikita na ni mfumo wa kifisadi uliokolea, ni mfumo uliokomaa ambapo hakuna wa kumfunga paka kengele, kila mmoja anamwogopa mwingine, ni hatari kubwa kweli kweli! Ni hatari kubwa kweli kweli! Kama magari ya Polisi yanahusika, yanafanya Operesheni, lakini tujue tatizo hili katika Bara la Afrika kila baada ya dakika 15 Tembo moja anauawa. (Makof)

Tukiangalia Zimbabwe ndiyo inayoongoza sasa hivi. Kwa hiyo, mtando unavuka hata nje ya mipaka ya Tanzania na kama huo mtando ni mkubwa kiasi hicho: Je, sisi kama Taifa, sisi kama Tanzania na Bunge hili ambalo kazi yake ni kuisimamia Serikali, hili Bunge liweze likaisimamia vizuri Serikali lazima Bunge kwanza lijitakase; wale Wabunge waliohusika wawajibishwe na wajiwajibishe wenyewe tu waziwazi, ndiyo tutakuwa na ile *moral authority, moral integrity*, tuwe na uadilifu wa dhati wa kuinyoshe Serikali kidole. Sasa katika ripoti nitamwomba Mheshimiwa James Lembeli tuwataje hao Wabunge. Tuwataje hao Wabunge ili angalau Bunge hili Tukufu lijitakase kwanza, halafu tuwe na nguvu ya pamoja ya kuiwjibisha Serikali. (Makof)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. J. F. MBATIA]

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nani amfunge paka kengele kama mchezo ndiyo huo? Je, Vyombo vyta Ulinzi na Usalama vinavyotwaja hapa; halafu sasa inaonekana Operesheni ilianzwa vizuri na Wizara, Jeshi likachukua mamlaka, Jeshi limetajwa katika ripoti hii. Sasa Jeshi inawajibishwaje. Je, sisi ni kazi yetu kuwajibisha Jeshi? Je, sisi ni kazi yetu kumwajibisha Waziri wa Ulinzi kuchukua hatua hizo? Hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kwa unyenyekevu kabisa kwamba kwanza wakati tunasema tunawapa pole wale waliopatwa na matatizo haya, wajibu mkubwa wa kuhakikisha fidia inatolewa, lakini tukijuliza, licha ya kuwapa fidia na kifuta machozi, hatuwezi tukarudisha uhai wa binadamu hawa: Je, tuishie hapa hapa? Je, kwa nini mauaji yanatokea zaidi hata yaliyoandikwa hapa Mkoani Morogoro kila kukicha? Kwa nini mgogoro mkubwa katika ya Wafugaji na Wakulima unatokea kila kukicha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna kilomita za mraba 945,203 lakini tumeshindwa kugawa ardhi tu ardhi ya Tanzania vizuri! Wizara ya Ardhi inahitaji Shilingi bilioni 16 kugawa ardhi yote ya Tanzania vizuri hata na nje ya mipaka ya Tanzania, tuweke kituo hapa. Tumeshindwaje kuigawa ardhi ya Tanzania na kuweka utaratibu ulio mzuri mfugaji ajue yupo wapi, mkulima yupo wapi? Leo watu wanauana tu kila siku!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mkoani Morogoro mwaka 2012 mwezi Desemba hali imekuwa tete kwa wafugaji hakuna wa kuwatetea. Mheshimiwa Andrew Chenge - Mbunge wa Bariadi Magharibi na Mheshimiwa John Momose Cheyo – Mbunge wa Bariadi Mashariki tulishirikiana kwa pamoja mpaka tukaweka na Wanasheria waende Mkoani Morogoro. Lakini ukiangalia Mkuu wa Mkoa wa Morogoro alivyosimamia ile Operesheni ilivyokuwa chafu, mpaka na ukatili wa kinyama uliotokea Mkoani Morogoro, wafugaji walivyonyanyaswa! (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. J. F. MBATIA]

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Mkoani Kigoma maeneo ya Rungwempya kwenye mapori ya Kagera Nkanda, Makere, Rushingo, Ngugwe kote huko matatizo yaliyotokea, nani aliwajibika? Ndiyo maana nasema huu mtando ni mkubwa na wa kutisha. Minjingu pale kuna kijana mmoja alitolewa Mbonda Arusha Mjini akapelekwa Minjingu pale, aliteswa kweli kweli na haya yote yalifahamika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tena kwamba bila kutafakari kwa makini, kuwa na utulivu, kwa kuwa huu ni mfumo ambao umesukwa, ni mtando ambao uliosukwa na mtando huu umesukwa kwa misingi ya walionacho, ndiyo maana hata ripoti inaonekana kwamba wale walionacho na wanasiwa walio na uwezo mkubwa wasiguswe isipokuwa labda Madiwani hao ndio wanaonekana wako hoi. Lakini hawa wengine wote wamenyanyasika kwa misingi hii, lakini labda niseme haya ni matawi, bado shina lenyewe halijaguswa. Ndiyo maana inabidi turudi hata kwenye mfumo wetu wa kifisadi, unaibuka na wanasiwa wakitafuta fedha lukuki za kuingia kwenye mambo ya uchaguzi.

Kwa hiyo, unaweza kuona ni mfumo ambao ni mpana na mtando mpana; tujitazame kama Taifa, tujirudi kama Taifa, tunavuna aibu hiyo, tumevunja Katiba, tumevunja haki za kibinadamu, mambo mengi yamevunjwa ndani ya mfumo tulionao sasa hivi; Taifa tunanuka, tumefedheheka, Taifa limedhalilishwa, tumefikia mahali pa kuona basi karibu kila mahali panaoza, pananuka; ni aibu tumeibeba ni fedheha kama Taifa inabidi sote kwa pamoja kwa nia njema tu Serikali; na hili ni suala la Amri Jeshi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Katiba Waziri Mkuu ndio Msimamizi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Iakini Mkuu wa Shughuli za Serikali na Mkuu wa nchi ni Amri Jeshi Mkuu ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, atumie mamlaka yake aliyopewa na Watanzania kuhakikisha tutamkumbuka kwa kupambana na mtando huu uliopo kwa sasa hivi. Vinginevyo itakuwa ni hali mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Riziki Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuwaombea Wabunge wenzangu wote humu ndani tuwe na subira na atujalie kuwa na maamuzi yenyehekima, uadilifu na kuleta tija kwa wananchi wetu wanaotusikiliza sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe pole za dhati kwa waathirika waliofariki, wananchi. Askari wetu, sio wote waliokuwa katika ukosefu, kuna Sskari waadilifu ambao wamekutwa na vifo kama hivi na wao vilevile tuwape pole, maana nao wamekuwa kama binadamu. Vilevile wafugaji ambao wameathirika na zoezi hill, lazima tuwape pole. La nne, wanyamapor ambao nao wanaathirika katika zoezi hili na wao vilevile wamekuwa kama hawana watetezi, nasi tuwatetee na tuwape pole. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwa uadilifu na hekima na Mwenyezi Mungu anijalie nitoe busara angalau nchi yangu niitendee mema. Sasa hivi ninachokiona hapa ni njama za kuua utalii Tanzania, na ni njama za kuhakikisha uchumi wa Tanzania unaanguka. Lakini unaanguka vipi? Umetumia mtandao mkubwa sana. Sasa hapa tunagombanishwa na tutagombana sana, tutauana sana, lakini mwisho wa yote, wale wenye mtandao wao watapita katika mgogoro huu na watacaa pembedi wanacheka; "tumewamaliza Watanzania sasa hivi." (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nazungumza hivi? Tulikuwa na bandari yetu, ilipigwa vita mpaka sasa hivi wamehakikisha bandari yetu itakuwa haitumiki na uchumi wa Tanzania utateremka. Hii haina mjadala! Zilipangwa mbinu za kuhakikisha Bandari ya Tanzania Dar es Salaam haifanyi kazi tena. Ili bandari za wenzetu zifanye kazi uchumi uweze kuendelea katika maeneo ya wenzetu, Tanzania iangamie. Huu ni mtandao rasmi wa kuhakikisha Tanzania

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. R. S. LULIDA]

inadhoofika kibiashara, kiuchumi na kila kitu na kuongeza umaskini Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii wa Tanzania unachukua ajira kubwa kwa Watanzania. Wananchi wanaajiriwa *Ngorongoro Conservation*, Wamasai wanaokaa ndani ya *Ngorongoro Conservation* wanategemea utalii wa wanyamapor. Ukiachilia utalii, kuna na *Air lines*, zinaletwa ndege kila siku *KLM* kuleta watalii kwa ajili ya kuangalia wanyamapor. Lakini wale wawindaji haramu, majangili wana azma nzuri ya kuhakikisha Tanzania ujangili unatokomeza wanyama wetu na tutawagombanisha hawa kwa kutumia njia mbalimbali mojawapo ikiwa kutumia wafugaji na wananchi kwa ujumla. Wanatuchezea shere kwa vile wenzetu wametuzidi akili mbele sisi tuko nyuma. Katika kufanya hivi, watahakikisha wanalidhoofisha hili zoezi ili wao waweze kupenya wafanye shughuli zao za ujangili na utalii wa Tanzania utakwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanaathirika kwa kuonewa na wale walioonewa Serikali ifanye kazi ya kuwasimamia na kuhakikisha walifanya mambo yale wanapelekwa Mahakamani. Vilevile kwa upande wa pili, leo unamkuta mfugaji ana silaha kali ya kijeshi anaingia ndani ya hifadhi, lakini pembeni kuna ng'ombe na yule Askari anakwenda kule kupambana na mtu ambaye ana silaha ya kijeshi; unategemea patatokea nini hapa? Ng'ombe watakufa, Askari vilevile na yeye atakufa kama walivyouawa baadhi ya Askari na pengine na yule jangili atauawa kwa kutumia nafasi yake kwamba nimeingia ndani ya pori lile nikiwa na silaha. Lakini wanatumiwa hawa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa na Kamati yangu tulikwenda Katavi, Mlele, Kibaoni, Nkasi na *Selous*, wanasesma mama sisi tunasema nini? Tunataka *action!* Watu wanakamatwa; wakikamatwa vinapelekwa vi-memo; muachieni huyu. Huyo mtu mmekamata ana ugonjwa wa kisukari, akikaa jela atafungwa. Sasa maana yake ni nini? Unamwachia, yule ndio mwenye mtandao ameshika na anatumia njia nyingi; anatumia siasa, anatumia Askari,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. R. S. LULIDA]

anatumia Askari wa Wanyamapori, anatumia wafugaji ili kudhoofisha suala letu la utalii lisiende. Je, uchumi mkubwa wa asilimia 21 ukifa Tanzania tutakwenda wapi? Uchumi wa bandari, uchukuzi utakufa; uchumi wa utalii utakufa; tutakwenda wapi Watanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kuishauri Serikali, waungalie mtandao huu. Ni mtandao wa watu wanye pesa na wanajulikana. Sasa Serikali kama kweli inataka kuwa *serious* ifuatilie huo mtandao na mtajua wako wapi. Hawa ng'ombe wanaokamatwa Bukoba, Kigoma mpaka Katavi wanatoka katika nchi za jirani. Wanasema kabisa; tuliambiwa na Madiwani kule kwamba ng'ombe 15 kwa pembe moja na kilo moja ya pembe sasa hivi imepanda bei imekuwa Dola 4,500. Huu ni uhujumu uchumi. Kama hatuijangalii, nchi itahangamia na utalii utakufa, uchukuzi utakufa, lakini maana yake, tunapimana kibashara kati ya nchi na nchi. Tufike mahali tujiulize, tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutagombana humu ndani, lakini kwa baadhi ya wengine wana maslahi binafsi na ndiyo maana wanajikuta wanatetea kitu ambacho siyo kizuri. Kama Wabunge mnahuksika na hiki kitu, naomba mwache. Mnaidhalilisha nchi yetu. Katiba yetu imesema sisi tumejuja hapa kuja kuitetea Serikali na maslahi ya wananchi, siyo maslahi ya wafanyabiashara. Wafanyabiashara wamekaa pembedi wanaangalia sisi tunafanya nini humu ndani, wanacheza na sisi na katika kucheza na sisi tunaiangamiza nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati yangu nilikuwa na akina Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Mabumba, Mheshimiwa Mfutakamba, Mheshimiwa Kigwangalla na Mheshimiwa Rita, kwa kweli usiku tunasindikwa na Askari. Askari hawa wanatuambia hapa kuna moja, mbili, tatu na hii hali inatusikitisha hata sisi Askari. Je, tupoteze maisha yetu hivi na hatuna watu wa kututetea? Hivyo na hao Askari vilevile wanakutana na watu wana silaha, wanaingia ndani ya mbuga. Kwa mfano, sasa hivi kipindi cha masika unaingiaje katika mbuga ya wanyamapori na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. R. S. LULIDA]

unaingia na silaha ya kijeshi? *Footsteps* zako ni sambamba na Tembo, halafu pili ukianza vita wakifa ng'ombe unalalamika. Kuna malalamiko ambayo ni ya haki, lakini kuna vitu vingine kama kweli umejiingiza katika ufugaji wako kuwa ni jangili, acha! Serikali ifuate sheria, haki na uadilifu. Sheria za nchi zikisimamiwa, hakuna mambo kama hayo ya kusema mimi nitaingia katika mbuga au nitaingia nitafanya mambo fulani; ni watu kuvunja sheria!

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona leo mwanamke anaingia benki na silaha kwenda kuiba. Lakini atakuambia mwanamke anaingia kwenye mbuga kukata kuni, anakwendaje kukata kuni ndani ya mbuga? Kuna simba, tembo, nyati, chui, kweli huyu mwanamke anakwenda kukata kuni mle? Hakati kuni mwanamke huyu! Anakwenda kufanya ujangili kama alivyofanya mwanamke huyu kuingia ndani ya benki kuiba. Kuna baadhi, sio wote, lakini wanawake wengine wanataka kutumiwa katika hilo zoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Kangi Lugola na atafuatiwa na Waziri Kivuli, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niliomba mwongozo wakati ule nikatumia maneno kwamba muda hautoshi na kuna dalili kwamba tunataka kujenga tabia ya kuwalinda wale ambao wametufikisha katika mazingira haya. Pengine kulindana, nianze na kunukuu ukurasa 43 wa Taarifa ya Kamati. (*Makofi*)

"Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia hoja ya Mheshimiwa Said Nkumba, haikuwa imefanyiwa utafiti wa kutosha, kwani baadhi ya madai (naomba nirudie) Kwani baadhi ya madai waliyoyatoa, hayakuwa na uhusiano na Operesheni Tokomeza." Kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. K. N. LUGOLA]

mfano, ni kweli ng'ombe 51 walitumbukia katika Mto Rubana Wilayani Bunda na kufa pamoja na Mlehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama huku siyo kulindana ni nini? Mimi Askari ninayepewa kazi ya kupeleleza mtu aliye na magunia mawili ya bangi, lakini nilipoenda kufanya upekuzi nikakuta nina magunia 20, lakini nikaamua nichukue mawili tu kwa sababu ndiyo niliyoambiwa. Magunia 18 nikayaacha, nikasema hayana uhusiano na idadi niliyoambiwa. Tunakwenda wapi? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo hivi vimefanywa na Serikali hii hii na vimefanywa kwenye hifadhi hii hii chini ya Waziri huyu huyu, halafu mnasema haya ni ya nyuma, hayana uhusiano na hatuko makini. Nina wasiwasi! Hata haya, mimi na Mheshimiwa Said Nkumba tusingeleta hoja, yakatokea baada ya miaka mitano na yenyewe yangedaiwa hayana uhusiano kwa sababu yalifanyika zamani. Tunakwenda wapi na tabia hii ya kulindana?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimevaa nguo nyeusi hizi siyo kwa bahati mbaya, ni kwa sababu ya kuwakumbuka wafugaji waliouawa kikatili na wengine kupata vilema, kubakwa na nyumba kuchomwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mungu anipe nguvu niendelee kuongea. Mwili wangu umekuwa dhaifu, natetemeka!

Waheshimiwa Wabunge, kama mlimsikiliza vizuri Mheshimiwa Shah wakati anatoa zile picha na akasema yeye ambaye alifika kwenye matukio, alilia. Kilio hiki tutakuwa wageni wa nani endapo tutafunika kombe mwanaharamu apite? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Operesheni Tokomeza Ujangili, nilisema hapa Bungeni kwamba iligeuzwa ikawa Operesheni Tokomeza Wafugaji. Taarifa ya Mheshimiwa Lembeli imesheheni matukio kwamba kweli wafugaji walitokomezwa; imeonyeshwa mifugo ilitokomezwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. K. N. LUGOLA]

Waheshimiwa Wabunge, akinamama mlionizaa kutoka tumboni mwenu, ninajaribu kujiuliza, nyinyi kama akinamama wale akinamama waliokuwa wanabakwa na mwanamume zaidi ya mmoja, walikuwa katika hali gani wanabakwa akinamama hawa? Nyinyi akinamama ndio mnajua uchungu, walikuwa katika hali gani? Wanaingiliwa na watu, watu hao pengine wameathirika! Tunataka kufunika kombe mwanaharamu apite! Bunge hili litahukumiwa! Wanaume wenzangu Waheshimiwa Wabunge, taarifa inasema, mwanamume mwenzetu alilazimishwa kufanya mapenzi na mti. Sisi kama wanaume, tangu lini mwanamume akafanya mapenzi na mti? Lazima tutende haki, lazima tuseme ukweli! Sasa nataka kusema ukweli, naomba mnisikilize vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hainiingii akilini, kitendo cha kupeleka Operesheni ya Kijeshi (*Military operation*) kwa civilian kwa watu ambao hawana silaha, hawana hata rungu tukawapelekea majeshi yamesheheni bunduki na mabomu, hapo ndipo ambapo tulianza kufanya makosa. Hainiingii akilini kuambiwa kwamba waliokuwa wanahuksika na operesheni ni Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania ndio lilikuwa lina-command. Hainiingii akilini, ana-command katika nchi ya namna gani? Ana-command katika utawala wa namna gani? Nchi yetu utawala kuanzia Rais, tuna Waziri Mkuu ambaye anaangalia shughuli za kila siku za Serikali yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati operesheni hii inafanyika, hata siku moja hukufika kwenye maeneo. Ulikuwa wapi Mheshimiwa Waziri Mkuu wangu? Ulikuwa wapi? Watu wanabakwa wanakuwa, ulikuwa wapi Mheshimiwa Waziri Mkuu? Kwa utaratibu wa nchi yetu, tumekupa kila aina ya usafiri kuanzia ndege, helikopta, ving'ora kila wakati fyee, fyee, vinalia; ulikuwa wapi Mheshimiwa Waziri Mkuu mambo haya yanatokea? Halafu leo mjiondoe katika jambo hili, haitawezekana! (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri wakati ule nikichangia nilisema mtaponea wapi? Naomba

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. K. N. LUGOLA]

niwakumbushe tena. Mambo yaliyosemwa hapa yakiwahusu Mawaziri, Ulinzi, Wanajeshi ndio waliobaka, ndio walioua, ndio waliojeruhi, ndio waliofiga mifugo, Waziri wa Ulinzi narudia tena utaponea wapi? Ninahakikisha utakapopona katika Bunge hili kama halitatenda haki, mbele ya Mwenyezi Mungu hautapona! Waziri wa Mambo ya Ndani, Askari Polisi kwenye Operesheni wameua, wamebaka watu, wamewapa watu vilema, wamefiga mifugo, utaponea wapi? Kama Bunge hili halitatenda haki, nakwambia mbele ya Mwenyezi Mungu hautapona! Kwa sababu damu hizi zitakuwa juu yenu! (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii. Taarifa hii hapa inasema, ulikwenda, unasema mimi sihusiki, walihinyang'anya kazi zote. Waziri unanyang'anya kazi na wewe bado unafanya kazi; ni Waziri wa namna gani wewe? Unalipwa mshahara, Operesheni kubwa namna hili, hawa waliokuwa wanaenda kufanya Operesheni, walikuwa wanajuaje hapa siyo , haturuhusiwi; walikuwa wanajuaje *beacon* za hifadhi na mapori zinaishia hapa? Kwa nini wasingeenda hata kwenye Vijiji vyote au kwenye Miji wakati wewe ndio ulikuwa na dhamana? Utaponea wapi Mheshimiwa Kagasheki? Wewe unahuksika moja kwa moja! (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Mifugo wakati ule nilisema ataponea wapi? Lakini katika Taarifa wameisoma mpaka mwisho nimegundua hakuna mahali alipohusika. Anataka kutolewa kafara, Mifugo yake imeuawa; hausiki na sera, ipo kwenye ardh; yeye anahuksika na wafugaji waliouwa pamoja na mifugo. Lakini ana suala la uzembe! Wafugaji na mifugo inauwawa na wewe ukiwa wapi Mheshimiwa Mathayo? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema hapa, huu mtindo wa kusema kwamba viongozi wajipime, wajipime nini? Naendelea kumshauri Mheshimiwa Rais, kama tuanitakia mema nchi yetu, na kama tunataka Chama cha Mapinduzi kiendelee kuaminiwa na Watanzania, amfukuze Waziri Mkuu wa nchi hii mara moja. Namshauri kwamba, Mawaziri wote

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. K. N. LUGOLA]

hawa hawawezi wakakwepa; watu wachukue *responsibility*! Huyu Mheshimiwa Maige mliyemfukuza, ye ye ndiye aliyekwenda porini kuchukua twiga? (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, kama mnataka kujenga heshima ya Bunge, lazima tuwe na Bunge lenye viwango. Bunge ambalo lisilo na *double standards*. Mheshimiwa Maige aliondoka, na ninyi, Mwalimu Nyerere alisema, wote *manziganyanja!* Lazima watu ambao wameua kwenye Wizara zenu, wametesa watu, nanyilazima mwondoke, ndipo tutakapojenga heshima ya nchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliopoteza mifugo yao; mtu alikuwa na mifugo, anaamka asubuhi ni maskini. Lazima kuwe na utaratibu wa kuwafidia watu hawa. Lazima watu hawa wafidiwe, wameonewa, mifugo yao imechukuliwa, imeuawa, lazima wafidiwe. Watu waliopataa vilema; sisi kila wakati ukikohoa hapa, unapelekwa India; wale wote waliobainika wana makovu, lazima Serikali ichukue *responsibility*, watu hawa wakachunguzwe vizuri, wapatiwe matibabu ya kutosha, kama ni India wapelekwe, kama tunavyopelekwa watu wengine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naenda kukaa, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ambayo wananchi wanaiamini, lakini kuna baadhi wanataka kuifanya Serikali yetu ichukiwe, mimi nitakuwa mtu wa kwanza na katika hili kwa kweli sitakubaliana na Mheshimiwa Rais endapo atakaa kimya na kutowafukuza watu hawa.

Mimi nitakuwa wa kwanza kuleta Bungeni hapa, nitakuja na hoja ya kumfukiza Waziri Mkuu ambaye tunamlaka naye. Huwezi ukakaa Ofisini, Watanzania wanakufa, wanafilisika, halafu mnakuja hapa mnasema: "ni wale walioko kule." Mbona na nyinyi mko Ofisini kule, hizi kazi hamzifanyi? Maana yake nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu nimeyaongea haya kwa uchungu, laiti nyinyi mngekuwa katika maeneo haya...

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. K. N. LUGOLA]

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa Mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana. Kuanzia Waziri Mkuu na hao wengine, namshauri Mheshimiwa Rais awafukuze kazi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa atafuatiwa na Mheshimiwa Lekule Laizer.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliopta kuwapa pole Watanzania wote waliopata na maswahiba haya. Ni jambo linalohuzunisha hasa ukizingatia kwamba Serikali yoyote duniani kipaumbele chake cha kwanza ni kulinda raia wake, lakini kwa bahati mbaya haya yametukuta katika Taifa letu.

Niwakumbushe Watanzania na Wabunge kwa ujumla *you can hate the government still you can love the country*. Unaweza ukaichukia Serikali, lakini bado ukawa mزالendo. Kwa bahati mbaya sana, wakati mwingine tunapoishambulia Serikali watu wengine wanaona kwamba sisi sio wazalendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ambayo yanaudhi, yanakera, yaleta shida kwa Taifa letu. Toka Bunge hili limeanza kwa ujumla wetu wote, tumejitahidi kwa kadri ya tunavyoweza; ukiangalia pamoja na timu yetu yote ya Mawaziri vivuli na Kambi ya Upinzani na Wapinzani wote kwa ujumla, tumetumia *resources* zetu zote ambazo ni *limited*, hatuna usafiri, ma-researchers, lakini tumefanya kwa bidii kwasababu ya uzalendo kujaribu kuishauri Serikali hii ili nchi yetu iwe ni mahali salama ambapo kila mtu anaweza akaishi. Serikali huwa zinakuja na kuondoka na nchi inabaki pale pale. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MCH. P. S. MSIGWAJ]

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena, kuichukia Serikali siyo kwamba wewe siyo mzalendo. Unaweza ukaipenda Serikali, ukawa siyo mzalendo. Ndugu zangu, haya matatizo yaliyotokea katika Taifa letu, Mawaziri mtakwepea wapi kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Kangi Lugola? Maliasili ya nchi yetu imegeuka imekuwa ni balaa kwa Watanzania. Pesa za watu wengi walizonazo katika mifuko yao ni *blood* kwasababu hakuna haki inayotendeka kwa ajili ya kupata hizo pesa. (*Makofi*)

Ni kweli tunataka ku-*conserve nature, at whose expense?* Tunataka tulinde mazingira yetu, kwa gharama ya nani? Mimi mwenyewe napenda kutunza mazingira, lakini tunatunza mazingira kwa gharama ya nani? Nimesema *priority* ya kwanza ya Serikali yoyote ni ku-*preserve* uhai wa mwanadamu, lakini ni kinyume cha Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nibanane na Waziri mwenzangu, haya mambo tumeyazungumza nami nimesema kwa ujumla wetu wote kwa pamoja. Kwa miaka mitatu ambayo tumekuwa hapa Bungeni, tumetoa ushauri. Lakini kwa bahati mbaya wote kwa ujumla wetu tuwe wakweli hapa, tumebezana, tumeitwa majina ya kila aina tunapozungumza mambo ya uzalendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme bila kumung'unya maneno, Serikali yako Mheshimiwa Waziri Mkuu mna mazoea ya kupuuza mambo ya msingi ambayo yana tija kwa Taifa hili. Hili Taifa ni letu wote! Tumezungumza humu ndani katika Sekta mbalimbali, tumetaja watu wengine kwa majina, wafanyabiashara ambao wanahusika na ujangili. Tumewataja humu, wakati mwingine tumekosea *spelling*, imekuwa *issue* kutaka kupata *political popularity*. Wakati mwingine tukizungumza mambo ya msingi ya kuokoa Taifa hili, inageuka inakuwa *personal attack* wakati lengo letu ni kuliokoa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yamezungumzwa, tumejenga siasa, lakini mtumbwi wetu unazidi kwenda chini. Kama hatutashirikiana wote kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. P. S. MSIGWA]

pamoja ili wananchi walio tuita huko nje walio tuchagua waone kweli tunaisimamia Serikali na tunaipenda Tanzania, tutakuwa tunawadanganya. Mambo ambayo ni *trivia/ndiyo* yana nafasi kubwa katika Bunge hili. Lakini mambo ya msingi yanayoliangaliza Taifa yanaleta chuki na hatuyatendei haki. Katika ripoti, pamoja na kwamba Kamati imefanya kazi nzuri, nami niungane na wenzangu wote kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hatuna chuki na wewe binafsi, *we love you*, wengine ni baba yetu, ni mzazi wetu, lakini hili lazima uwajibike ili tuoneshe tuna-value uhai wa Watanzania na tuoneshe tunajali akinamama waliobakwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwa Mheshimiwa Waziri Kagasheki, nimezungumza kama miaka mitatu! *For three solid years* tunazungumza mambo ya majangili. Leo kwenye ripoti hii, inasema, eti Watendaji wako wewe hukushirikishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Kagasheki, umetoa *statement* nydingi ambazo ni *irresponsible* wakati wa Operesheni hiyo. Kuna wakati mwingine umesikika ukisema kwamba, ikiwezekana wamalizane huko huko porini. Hii ni nchi ya utawala wa sheria! Kwa mujibu wa nchi yetu, ni Mahakama pekee inayoweza kutoa adhabu kwa mtu. Hizi ni kauli zimetoka kwa kiongozi mwenye dhamana. (*Makof*)

Vilevile umesikika na wewe mwenyewe unasema, "mtandao huu ni mkubwa sana. Nikijaribu kufanya kazi, nashindwa." *What are you doing in the office?* Kama ungekuwa muungwana, ungesema hii kazi nashindwa kuifanya Mheshimiwa Rais, kwa sababu vitendea kazi vyako vinanizuia, kazi hii hapa. Tungekuheshimu, ungejiuzulu kwa heshima kubwa nzuri. Lakini wewe umekuwa kwenye vyombo vya habari na unapiga kelele kama mimi kivuli ambaye sina kitendea kazi. Sasa unafanya nini Ofisini? Kwanini tunakulipa? (*Makof*)

Kamati inasema kwamba sisi hatumjui Katibu Mkuu, *Director*, sisi tunakujua wewe ndio unayewajibika. Tulitegemea uje na ripoti hapa kwamba baada ya wale watu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. P. S. MSIGWAJ]

kushindwa kufanya kazi, mimi nimechukua hatua moja, mbili, tatu, nne, tano. Sisi hatuwajui Watendaji wa huko, wewe ndio *political representer*, tunakutafuta wewe. Sasa ukija hapa useme kwamba sijui hukupewa ripoti, hikufanya nini, lakini umetoa matamko mengi ambayo hatuwezi kukubaliana nayo kama ni muungwana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasema Bunge hili kama tunatenda haki, kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Lugola, tumwombe radhi Mheshimiwa Maige, na tumwombe radhi Mheshimiwa Ngeleja. Kwa sababu kama tunasema ni mfumo, sasa tumewatoa wa kazi gani? Mheshimiwa Maige hakwenda msituni kubeba wale Twiga wala Mheshimiwa Ngeleja haendi Mtera au Kihansi kwenye masuala ya umeme, tuliwasulubu hapa, tukapiga makofi. Kama hatutendi haki, maana yake lile Bunge linaendeshwa kwa rushwa, hatutendi haki. Kama tuliwatoa Mawaziri wallikuwepo, sasa kama tunajua ni mfumo, kwanini tuliwatoa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zilipita *rumours* hapa kwamba lazima waondoke, wamelilettea Taifa hasara, leo tunazungumzia Twiga? *Those are animals!* Wakabebwa uwanja wa *KIA* pale. Lakini *we are talking about peoples lives*, halafu tuzungumze mambo ya mfumo hapa, kwani hatuuji? Tunazungumzia damu za watu, watu wamebakwa, wamekufa, hakuna cha mfumo hapa! *You guys must go!* Kama mnatuheshimu, ni vizuri Waziri Mkuu ungekuwa unatayarisha makaratsi saa hizi, unaandika barua ya kujiuzulu, tukufanyie *farewell party* nzuri kwamba ulifanya kazi kiungwana na ukaondoka halafu wa chini yake na nyinyi mwanze kufuata msururu. Akina Nchimbi msipofanya haya mambo, damu itawalilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nahodha na wewe bahati mbaya una rekodi mbaya kutoka kule Zanzibar. Naona hii dhambi inakufuata, inakulilia damu ya watu ipo mikononi. Tumepewa dhamana na wananchi, hatuwezi kukaa kimya. Kama kweli *we are serious about this*, hatuwezi kukaa kimya. Mumuunge mkono, mshauriane. Tunasema kwa nia nzuri! Uzuri wake, bado ni Serikali yenu, hatusemi CHADEMA au *CUF* tutaingia,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. MCH. P. S. MSIGWA]*

hapana. Atakaa Mheshimiwa Rais, atamchagua Waziri Mkuu mwagine, tena wa CCM hao hao! Hatusemi hata tunaomba Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ni Serikali yenu. Wapo Mawaziri ambao ni *sincere* na hata ninyi hatusemi mmekuwa *involved directly* lakini tunazungumza uhai wa watu. Kwa heshima na taadhima, andikeni barua na tunapozungumza hapa, inakuja mambo ya uchama, tunazungumzia Taifa sasa, hatuzungumzii Serikali.

Tunazungumzia Utaifa ambao wamekufa Watanzania. Watanzania waliokufa ni wa Vyama vyote, tunazungumzia Utaifa kwa heshima ili tuweke *landmark*, tuweke historia kwamba tunataka tuwe na Taifa zuri la kuwajibika. Tunaomba mtakapoanza, mfanye vizuri, tuwaage vizuri, kwamba mmeweka *landmark* kwamba tutajifunza hata kutoka kwenu na sisi wadogo wadogo tunaojifunza siasa mtakuwa mmetusaidia. (*Makof!*)

Niwaombe, hizi damu zitawalilia! Hivi vyeo ni dhamana, hatutaki baadaye tutakapochukua nchi tuwapeleke *The Hegue*, kwasababu hamtapona! Haiwezi kumwagika damu kirahisi, tunaona watu wanapigwa, wanaonewa, halafu mtapita hivi hivi. Itapita miaka kumi, tutawafuata tu. Ninawaomba mwajibike. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi wamezungumza masuala haya. Nawaomba viongozi ambao tumepewa dhamana, kauli tunazozitoa ambazo ni *irresponsible*, zinaleta shida, zina-cause matatizo. Haya tujifunze liwe funzo maana yake hatuwezi tukawa tunarudia yaleyale.

## **TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu ya muda naomba iwe fupi sana. Mheshimiwa endelea, taarifa iwe fupi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MBUNGE FULANI:** Naibu Spika, ahsante sana. Nataka kumpa taarifa tu mchangiaji, kwamba Mheshimiwa Shamsi Nahodha hana rekodi mbaya Zanzibar. Kaondoka uongozi ule kama taratibu zetu za CCM zinavyokwenda kwamba hakuna utawala wa kifalme. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mchungaji, unayepokea Taarifa?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani umesahau, siyo historia mbaya, umesahau watu waliuawa Pemba? Maoni yako kaweke kwenye *pegin hole* nitayachukua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu, hili suala siyo la utani, na ndiyo mambo kama haya, tunazungumza mabo *serious* halafu watu wanaleta utani hapa. Hatuko hapa kulindana. Tunazungumza mambo *serious* yanayohusiana na uhai wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu niwe muungwana tu, mimi nirudie tena ndugu zangu, *you can hate the government and love your country and sometimes through to love your government is hating your country*. Kwa hiyo, usichukulie mara zote kuishabikia Serikali yako kwamba wewe ni mzalendo; na isichukuliwe mara zote kwamba kuichukia Serikali yako kwamba wewe sio mzalendo. Naomba Wabunge wote hili suala tushirikiane wote kwa pamoja kwamba Waziri Mkuu kwa heshima na taadhima *a-step down* na Mawaziri hao watatu; Mheshimiwa Nchimbi, Mheshimiwa Kagasheki na Mheshimiwa Nahodha mtakuwa mmejenga heshima hata kwa vizazi vinavyokuja nyuma kwa ajili ya kulijenga Taifa letu tunavyokwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**MBUNGE FULANI:** Hatoki mtu hapa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lekule Laizer, mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana wa leo.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii. Lakini naomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, hili suala la Taarifa, Taarifa kuwapinga wenzenu Taarifa wakismama kuongea jambo hili, naomba likome. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili kwamza nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati, nakupongeza sana kwa taarifa, pamoja na Wajumbe wenzako waliokuwa kwenye Kamati. Naomba tusichukulie jambo hili kisiasa ndugu zangu. Waliokufa sio wanachama wa Chama cha Mapinduzi, wala CHADEMA wala nani, ni Watanzania wenzetu. Wagonjwa mpaka sasa ni Watanzania wenzetu.

Jambo hili ni kubwa mno! Katika nchi ambayo inasemekana ina amani, amani sasa iko wapi kama ni sisi wenyewe ndio tunauana, tunaibiana mifugo, tunanyang'anyana? Hebu niulize tu, meno yaliyokamatwa Zanzibar shehena kubwa, ni nani kauawa pale? Iliyokamatwa Dar es Salaam, kauawa nani? Kati ya hawa wafugaji waliouawa ni yupi alikamatwa ana meno ya Tembo? Hivi wafugaji sio Watanzania? Hivi wamekuja Tanzania bahati mbaya mpaka mmegeuza mnawaita sasa wafugaji haramu? Uharamu wa kutoka wapi? Uharamu wa wafugaji ni nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili, ikikosekana mtu wa kuwajibika, Bunge hili livujwe, kwasababu hatuna maana ya kuwa Wabunge wa watu wanaouawa kila siku na kupigwa risasi halafu tunajiita Wabunge; Wabunge wa kufanya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mama huyu wa Galapo alikuwa na nyara gani ya Serikali? Masikini hata bunduki hawezi kushika, anauawa kwa ajili gani? Halafu bahati mbaya, inatolewa taarifa kabla hajauawa kwamba leo tutamuua; kwa ajili gani? Mzee wa miaka 70 kupigwa risasi tatu, alikuwa ana nini? Hivi Maaskari hawa walilotumwa na Serikali ilipata taarifa hii kwamba kuna watu waliouawa wamechukua hatua gani? Mifugo inapigwa risasi,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. M. L. LAIZER]

mmechukua hatua gani? Mlikuwa mnasubiri taarifa iletwe ndani ya Bunge? Sisi Wabunge ndio tutazunguka kutafuta? Kama Wabunge hawakuagiza hii Tume iundwe, Serikali mngeyamaza mpaka lini? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni baadhi tu! Hii ni taarifa ya wafugaji waliokaa hapo juu. Kuna mauaji makubwa. Mwenyekiti nakupa hii taarifa; uchanganye Taarifa hii, mauaji yaliyopo hapa, unyang'anyi uliopo hapa na Taarifa yako. Unawaona wale wafugaji? Wote wamevaa nguo nyeusi kwa ajili ya kuomboleza. Nami nimevaa nguo nyeusi kwa ajili ya kuomboleza. Wale wapo kule juu. Taarifa uliyosoma ni ndogo, kwasababu ni kweli hukuweza kufika maeneo yote. Hapa kuna mauaji mengine ya maeneo ambayo wewe hukufika. Kuna unyang'anyi mkubwa wa ng'ombe walioyang'anywa wafugaji. Mheshimiwa Mbunge Kasulundumbayi ng'ombe zake 725 zimechukuliwa mpaka sasa. Huyo ni Mbunge yupo hapa, nadhani atachangia, atasema! (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Wafugaji leo tunahitaji tuambiwe uharamu wetu wafugaji. Hivi ni mfugaji yupi alikamatwa na nyaraka za Serikali? Ni nani? Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, napenda kutaniana na kuleta mambo ya siasa hapa, jambo hili siyo la siasa wala la Chama, ni letu sote. Hatusimami hapa kwa ajili ya kupata kura za mwaka 2015 hapana, tunasimama kutetea Watanzania walotuchagua. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii imechaguliwa na wananchi. Sisi hapa tumechaguliwa na wananchi. Wananchi hao ndio wanakufa, halafu tunyamaze! Ubunge wetu hauna maana kuliko uhai wa Watanzania. (Makof)

Kwa hiyo, naomba jambo hili Serikali ilichukulie kwa nguvusana. Ikishindikana, kama mnang'ang'ania madaraka, vunjeni hili Bunge. Tuvunje hili Bunge, ichaguliwe Serikali nyingine. Kwa sababu tukivunja, hakutakuwa na Baraza ya Mawaziri. Hata Mawaziri ni Wabunge. Litachaguliwa Baraza lingine la Mawaziri, watakuja wengine. Wananchi hao hao

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. P. S. MSIGWA]

walioumia watafanya uchaguzi, watachagua Wabunge wengine na Mawaziri wengine watapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lekule Laizer kwa ushauri wako.

Waheshimiwa Wabunge, niwahakikishie kwamba wale ambao mmejiorodhesha kwenye orodha, mtapata nafasi ama wote ama karibu wote kwa ule muda ambao tuishukuru Kamati ya Uongozi kutuongozea. (*Makofi*)

Niwakumbushe kwamba tutarudi hapa saa 10.00 jioni, ni vizuri kuwahi, mjadala huu ni mzito. Kwa hiyo, wale hasa ambao wamejiandikisha majina ni vizuri ukawepo kwasababu ukirukwa kama utakuwa haupo ni vigumu tena kupata nafasi.

Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa Machali.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

(*Saa 8.00 mchana Bunge lilitishwa hadi saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Spika (Mheshimiwa Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kufuatana na orodha tuliyonayo. Msemaji wa kwanza mchana huu atakuwa Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Paresso ajiandae.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nipongeze sana hotuba ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, pamoja Kamati kutoweza kufika katika Jimbo la Tunduru.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tunduru ina Majimbo mawili na bahati nzuri Mbunge anayezungumza sasa hivi ndio Mbunge wa kwanza kulalamika na kuleta kilio cha wananchi kudhulumiwa, kudhalilishwa, kuuawa na niliwhi hata kutoa majina ya watu waliouawa na mahali walipouliwa, lakini kwa bahati mbaya halikupewa uzito. Jambo hili kwa kweli sisi wananchi wa Tunduru halikutufurahisha hata kidogo. Katika hili lazima niwe mkweli.

Mheshimiwa Spika, nilisema katika Bunge liliopita kwamba laiti kama yale ambayo niliyaeleza humu Bungeni juu ya kilio kile yangeweza kufuatiliwa na kuchukuliwa maanani, leo tusingefika hapa tulipo. Lakini kwa bahati mbaya na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, aliamua kwamba tutaionyesha dunia na tutaionyesha Tanzania kwamba yale aliyozungumza Mbunge Mtutura ni ya ukweli.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza yale, kwa bahati mbaya zaidi, siku ya tatu baada ya mimi kuzungumza Bungeni, nikatokea kwenye Magazeti kwamba mimi ni jangili, zikawekwa picha tatu pale kwamba mimi ni jangili na bunduki zangu; bunduki ambazo sina na bunduki ambazo hata namba hakuna. Lakini hiyo yote ilikuwa ni kufifisha jitihada za kuwatetea wanyonge wanaodhulumiwa katika nchi hii.

Leo karibu Wabunge wote wanazungumza lugha moja, lugha ile ile ambayo mimi Mtutura nilizungumza. Sasa sijui kesho vile vile Wabunge hawa wote waliozungumza watatokea kwenye Magazeti kwamba nao ni majangili kama nilivyotokea mimi!

Mheshimiwa Spika, nilizungumza hapa kwamba kuna watu wameuawa, watu wamepatiwa ulemavu, kuna watu wamenyang'anywa mali zao, lakini halikuchukuliwa uzito wowote. Sasa leo madhali uzito umeshachukuliwa, kwa kweli

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. M. A. MTUTURA]*

namshukuru Mwenyezi Mungu, ni katika kuthibitisha kwamba yale niliyozungumza ni ya kweli.

Mheshimiwa Spika, nashangaa katika hotuba hii ya Mwenyekiti jambo moja; wanasema kwamba Mheshimiwa Waziri hakushirikishwa, hakuhusika katika operesheni hii. Kauli hii naishangaa, kwa sababu akiwa Arusha Waziri wa Maliasili alionekana kwenye televisheni ya Taifa na televisheni ya *ITV* akiwa anaota matamko matatu tena mazito. Tamko la kwanza nanukuu. Alisema kwamba: "Kuna operesheni kubwa inakuja, Watanzania mjiandae." Tamko la pili, alisema: "Operesheni hii itakuwa ya aina yake." Lakini tamko lingine zito, alinukuliwa akisema kwamba, anawaomba Maaskari masuala ya majangili wayamalize huko huko.

Mheshimiwa Spika, hii ni kusema kwamba hata yale maamuzi yallyiyofanywa na hao Askari, Waziri wa Maliasili alikuwa anayajua na ilikuwa ni baraka zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo hapa ripoti inasema kwamba ye ye hakushirikishwa, taarifa hii ilikuwa imeandalisha na watu wengine; siyo kweli! Ni namna ya kutaka kukwepa wajibu na majukumu ambayo yalikuwaepo mbele yake.

Mheshimiwa Spika, juzi tumempoteza kiongozi mkubwa sana, Mheshimiwa Nelson Mandela. Mheshimiwa Nelson Mandela amepata heshima katika nchi yake, Bara la Afrika na dunia nzima kwa sababu alithamini uhai wa watu na alithamini zaidi uhai wa wanyonge. Yeye mwenyewe alikuwa katika nafasi nzuri tu, angeweza kuendelea kuishi. Lakini akasema maisha yake mazuri siyo kitu, isipokuwa ni lazima ahakikishe kwamba anatetea wanyonge walio wengi. Leo tunamuenzi, tunamheshimu kwa sababu ametetea uhai wa watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika imani ambayo ninayo mimi ambayo kwa bahati nzuri Waziri wa Maliasili, kaka yangu Mheshimiwa Bwana Kagasheki anayo vile vile, wote sisi ni Waisilamu; Mwenyezi Mungu anatuambia kwamba endapo mwili wa mwanadamu utaoza juu ya ardhi, basi nyumba 60

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. A. MTUTURAJ]

zilizouzunguka mwili huo, watapata adhabu kubwa sana mbele ya *umri kiamu*. Anazungumziwa mwanadamu, hii yote ni kuonyesha utukufu wa mwandamu. Leo watu wanauawa mbugani, wanaliwa na fisi, leo watu wanauawa wengine hawajulikani wako wapi. Ni adhabu kubwa kiasi gani hawa tulio wapa mamlaka juu ya kutetea uhai wa watu, juu ya kutetea uhai wa wanyama, watayapata mbele ya Mwenyezi Mungu. (*Makofii*)

Ndugu zangu, nafasi hizi tulizopipata ni za muda, ni za kupita. Lakini ubinadamu wetu, kulinda uhai wa wananchi wetu, ni lazima uheshimiwe kupita vitu vingine vyo vyote. Leo msimamishe Mbunge ye yote hapa atakayeunga mkono suala la ujangili, hakuna! Nami naridhia kabisa kwamba wale majangili ambao wapo ndani ya Bunge hili watajwe na uthibitisho ukipatikana wafikishwe mbele ya vyombo vya Sheria. Lakini siyo kutumla tu magazeti kuchafua watu, eti tu kwa sababu amebainisha uchafu fulani uliopo ndani ya Wizara yako. Hii si sahihi. Majangili wote watajwe na wanahusika kiasi gani, na ikibidi wafikishwe katika vyombo vya Sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nisingefurahi kabisa nipigiwe kengele ya pili, naunga mkono hoja zote isipokuwa iambatane na marekebisho kadhaa ambayo nimeweza kuyataja katika mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Moses Machali, nimemwona hapo, na Mheshimiwa Mpina yupo. Mheshimiwa Moses.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hoja iliyowasilishwa na Kamati ya Maliasili, Ardhi na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kusema kwamba naunga mkono hoja ambayo imewasilishwa na Kamati hii na nitoe pole kwa wote ambao wameathirika na operesheni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. M. J. MACHALI]*

ambayo ilikuwa ikifanywa ndani ya nchi yetu. Kwa sababu ukiangalia ni vitendo vya kikatili, ni vitendo visivyokuwa na ubihadamu kwa namna yoyote ile, kwa binadamu ye yeyote yule mwenye akili nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme, yote haya yanatokea kwa sababu kama Taifa tumepoteza uadilifu. Laiti tungekuwa waadilifu ni wazi kila mmoja angekuwa *responsible*, kuwa *accountable* kuhakikisha kwamba majukumu aliyopewa basi anayafanya vile ambavyo ilitarajiwa. Lakini hali imekuwa ni tofauti.

Kwa nyakati tofauti, Wabunge na hata wananchi na wanaharakati mbalimbali wamejaribu sana kuonesha vitendo viovu ambavyo vinafanywa na baadhi ya viongozi wa Serikali na wengine amba o ni Watendaji wa Serikali amba o walipewa dhamana ya kuhakikisha kwamba haki inatendeka. Lakini imekuwa ni dhaifu sana, imekuwa na kigugumizi cha kuweza kufanya maamuzi ya kuwashughulikia wale wote amba o wameonesha utovu wa nidhamu na matokeo yake tunasubiri mpaka tuone pengine kumekuwa kuna madhara makubwa sana ndiyo tunakuja kuchukua hatua. Haitusaidii, zaidi ni kuzidi kujenga chuki mi ongoni mwa watu na watu kamwe hawawezi wakawa na imani na Serikali yao kama watu hawawezi wakashughulikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia taarifa, imeainisha jinsi gani watu ambavyo wameuawa, imeainisha jinsi gani mwanaume analazimishwa kufanya mapenzi na mti. Wapi na wapi? Vitu gani hivi? Serikali gani hii? Kuna haja ya kuweza kuangalia kwamba pengine hivi hawa watu ambalo wamepewa dhamana ya kuweza kuongoza nchi yetu, wana dhamira njema? Kuna dhamira njema hapa?

Mheshimiwa Spika, Bunge kwa mujibu wa ibara ile ya 63 tuna wajibu wa kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali. Sasa mimi naomba nianze kuishauri Serikali kwamba Waziri Mkuu anapoteza uhalali wa kuendelea kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu yeye ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. M. J. MACHALI]

na sasa kama Wabunge tuko *serious* na sio watu wa maneno maneno, huyu ndiye ambaye tumepewa kwa mujibu wa Kanuni zetu na kwa mujibu wa Katiba, tuna mamlaka ya kumwajibisha Waziri Mkuu. Kwa hiyo, Wabunge tusiishie kwenye kusema, tusiishie kwenye kupiga kelele na kulalamika, tumepewa meno na Katiba, tumepewa meno na utaratibu kwenye Kanuni zetu za Kudumu za Bunge kwamba tunaweza tukapiga kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu na *Cabinet* yote itaondoka na hata wale Mawaziri wengine ambao pengine wamekuwa wanapigiwa kelele kwamba ni tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa sana, kwa sababu hata wakazi wa Mkoani kwangu, Wilayani kwangu, Jimboni kwangu nao ni wahanga, wameathirika kwa muda mrefu sana, maeneo haya ambayo tumekuwa tunayaeleza ya Kagera Nkanda, tunesikia kwamba huko Babati watu wamefanyiwa vitendo vya kikatili. Nilikuwa naangalia picha, kule Tarime kuna watu wamefanyiwa vitendo vya kikatili; watu wameuawa. Ukiangalia picha inasikitisha sana!

Mheshimiwa Spika, nisingependa sana kuchelea, nimelazimika kuandaa fomu mchana huu, nitaomba Waheshimiwa Wabunge tusiishie kusema, akina Mheshimiwa Kangi wamezungumza sana; naomba Mbunge yejote ambaye anaona kwamba ni mzalendo na anaipenda nchi yake na anachukuzwa na vitendo vya kikatili, vitendo vya kinyama, basi tusaini kwenye fomu hizi ambazo nimeziandaa za kupiga kura ya kutokuwa na imani na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa sababu ni wazi Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshindwa kuwasimamia Mawaziri wake.

Sasa hatuwezi tukaanzA na Mheshimiwa Kagasheki au Mheshimiwa Mathayo na wengine wote ambao wanatajwa. Tuanze na Waziri Mkuu. Waziri Mkuu ni tatizo, Mheshimiwa Mzee Pinda.

Mheshimiwa Lema naomba nikupe fomu, mimi nimeshasaini, nimeanza. Mheshimiwa Lema kama wewe ni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. J. MACHALI]

mzalendo naomba uanze kukusanya sahihi hizo. Mheshimiwa Mkosamali, tunaanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali, huo utaratibu wa wapi? Sokoni? Nawe Mheshimiwa Lema pia unachukua utaratibu wa Sokoni? Ala! (*Kicheko*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, ukisoma utaratibu kwa mujibu wa Kanuni umesema kwamba tukusanye sahihi na haijaaelezwu kwamba sahihi zinakusanywa wapi?

**SPIKA:** Haya, naomba ukae kwanza chini. Tunao ustaarabu wa kufanya mambo. Sasa wewe maliza kusema maneno yako, halafu utaendelea baadaye. Sasa unamwambia chukua hii fomu, chukua na mimi nimekaa hapa nakuangalia; haiwezekani Mheshimiwa Machali! (*Kicheko*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nitaomba pia na sahihi yako. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunasema na leo ninapozungumza mahali hapa, kumetokea mapigano kati ya wafugaji na wakulima katika Wilaya yangu na mtu mmoja amepoteza maisha. Lakini chimbuko la migogoro yote ni Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kasulu inayoongozwa na Mkuu wa Wilaya, Bwana Danhi Makanga. Haiwezekani tumezungumza hapa, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani - Mheshimiwa Pereira Silima, alifanya ziara tarehe 23 Julai, 2013, ameshuhudia watu wamejitokeza wana POP, wamekuja kwenye Mkutano wa Hadhara wanamweleza kuna tatizo na chanzo cha matatizo ni Mkuu wa Wilaya Bwana Danhi Makanga.

Mpaka leo Waziri Mkuu tumemweleza toka mwaka 2011, tumemweleza Waziri Mkuu, amekuwa anajinyonganyonga na maelezo yake. "Aaa, ngoja tuliangalie hili jambo limekaaje." Mwaka 2011 kwa *specific issue* moja mpaka leo! Kuna Waziri Mkuu hapa?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. J. MACHALI]

Mheshimiwa Spika, haiwezekani tukavumilia kuona damu za Watanzania zinamwagika, rasilimali za wananchi zinaharibowi, halafu kuna watu wamekaa Ofisiini, wanalipwa pesa zinazotokana na kodi za Watanzania halafu tunakuja hapa inakuwa kila wakati sisi ni kulalamika. Jambo hili halikubaliki. Ndiyo maana nimelazimika kuandaa hizi fomu. Kwa kweli hapa sasa itakuwa ni kipimo cha uwajibikaji na uzalendo wa Wabunge kwa nchi yao, kama mtaacha kusaini, basi wananchi naomba muelewe kwamba tatizo la kwanza la msingi ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wala siyo wengine na ndiyo maana wana haki ya kuweza kutuwajibisha Mbunge mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika hili Chama cha Mapinduzi mnawajibika kuwa mfano. Nimesikitika hata pale baada ya kuwa tumeahirisha Bunge kwa muda wa nusu saa. Unapita unamsikia Mbunge anazungumza anasema; ooh, Taarifa hili ni kama inakialbisha Chama chetu cha Mapinduzi; Taarifa hii inaivua nguo Serikali yetu. Kwa hiyo, hii Kamati ni watovu wa nidhamu tuwashughulikie. Badala ya kusema tumpongeze Mheshimiwa Lembeli na Wajumbe wote kwa kuweza kuibua na kufichua uozo, ujisadi wa kila namna ambaao umedhihirisha ukatili uliofanywa na watu wachache na kwa maslahi ya watu wachache, mambo yasiyokuwa na tija, watu wengine wanafikiria waende kuwajibisha Mheshimiwa Lembeli pamoja na Wajumbe wengine. Huu ni utovu wa nidhamu! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, nyinyi ndio ambaao mko wengi hapa. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi nimewasikia halafu nimewa-quote. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi mnaipeleka nchi yetu mahali pabaya, hasa wale ambaao mmekuwa na mitazamo ambayo wakati mwingine haisaidii nchi yetu. Sio wote lakini angalieni, *majority* kwa kweli kuna shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, sahihi hizi nitazikusanya baadaye. Wabunge ambaao hamtasaini, basi mtakuwa mmetusaidia sisi twende tukawaambie wananchi malalamiko yote ambayo yanatolewa hapa, tatizo ni Wabunge wale ambaao

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. M. J. MACHALI]*

watakuwa wamekataa kusaini hizi fomu na tutazianika uwe ni Mpinzani, uwe ni CCM, wananchi watatuhukumu kwa matendo yetu.

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuliangalia tatizo hili, Kamati ilichokifanya, imetuonesha tu, na hiyo ni sehemu tu ya matatizo ambayo yanajitokeza. Tumekuwa tunaeleza baadhi ya Watendaji wamekuwa wanachukua rushwa huko kwenye maeneo.

Sasa kule kwetu imetajwa hilo eneo ambalo ni Kigosi Myowosi; baadhi wamekuwa wanachukua fedha kutoka kwa wafugaji halafu wanaruhusu kwenda kuchunga mifugo yao kule. Tumeeleza mara kadhaa, tunasema Kamati za Ulinzi na Usalama katika Wilaya zetu ni tatizo la msingi, na ni wachochezi wakubwa wa migogoro mbalimbali ambayo inajitokeza. Hatua hamchukui! Mnataka tuwaambieje? Au mpaka pengine labda yakamatwe marungu mje mpigwe vichwani ndiyo labda pengine mtasikia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tufanye nini? Basi mpishe tuje tukae na wengine tuone, tutaonyesha *standards* pengine za kuipeleka nchi yetu namna gani. Maana yake ni wazi sasa kwamba mmeshindwa kazi. Kama inafika mahali Mheshimiwa Mzee Kagasheki kama ambavyo Kamati ambavyo kwa kweli imeeleza kwamba Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa Wanyamapori wamefanya vitu vya ajabu, mpaka inafika mahali wanamdharaau Waziri!

Nafikiri Mzee wangu, rafiki yangu Mheshimiwa Kagasheki, ingekuwa ni uungwana upishe pengine; amua tu kuwajibika ili kusudi kuweza ku-set precedence kwamba hawa Watendaji, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wamekuzidi nguvu, usisubiri mpaka wakati mwingine rungu la Mheshimiwa Rais. Utakuwa umeonesha uungwana wa hali ya juu na utakuwa kweli umetengeneza kitu ambacho Waziri Mkuu huyu anasema kwamba, Mimi Mheshimiwa Rais akiniondoa ndiyo nitashukuru nitaona kwamba ni jambo jema. Unasubiri mpaka uondolewe! Unasubiri uondolewe kwa nini? (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. J. MACHALI]

Mheshimiwa Spika, tusipoangalia, Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaitumbukiza nchi yetu katika machafuko kwa sababu ya mambo kama haya. Haya mambo, oneni tu kwamba, sasa hivi tunasema hatuna amani ila tuna utulivu ambao umeamba...

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Waziri Mkuu awajibike.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Paresso.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kabla sijasema sana, nianzie na upande wa mapendekezo ukurasa wa 47.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 47, Kamati inapendekeza pale kwenye Kipengele kile cha pili, "Serikali ifanye tathmini ya kina kwa kupitia Wakuu wa Mikoa/Wilaya kujua athari ya *operation* hii na kutafuta njia ya kutoa kifuta machozi kwa waathirika."

Mheshimiwa Spika, naomba pale kwenye "Kifuta Machozi" ionekane ni "kifuta machozi na fidia kwa waathirika".

**SPIKA:** Hebu sema vizuri, ni ngapi?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 47.

**SPIKA:** Mh!

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Kwenye kipengele cha pale juu, "Serikali ifanye tathmini ya kina..."

Mheshimiwa Spika, nina tatizo la muda.

**SPIKA:** Ahaa, ni *bullet* ya pili.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, eeh *bullet* ya pili; "*ifanye njia ya kutoa kifuta machozi kwa waathirika*", badala yake ioneckane "*kifuta machozi na fidia kwa waathirika*". (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hapo ndipo kwenye marekebisho na nianzie hapo hapo kwamba, tumeshuhudia matatizo makubwa haya ya wananchi wetu wameharibiwa mali zao, ng'ombe wao wamepigwa risasi, ng'ombe wao wameuwawa, ukatili mkubwa wamefanyiwa, wameharibiwa rasilimali zao nyingi sana na Serikali, na watendaji waliokwenda kufanya hivyo ni Watumishi wa Serikali. Kwa hiyo, hatuwezi kuzungumza suala la kifuta machozi, hapa tunazungumza suala la fidia katika mali.

Mheshimiwa Spika, tutapeleka kifuta machozi katika zile familia ambazo ndugu zao, jamaa zao wamefariki kwa sababu, hakuna malipo ya uhai wa mtu, lakini katika rasilimali Serikali ilipe fidia. Tathmini ifanyike Serikali ilipe fidia kwa wananchi hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo napata faraja kwamba mambo haya yameingia hapa Bungeni. Wale wananchi tunaoishi, mmesikia hapa Meatu imetajwa kutoka mwanzo wa ripoti karibu mpaka mwisho. Matatizo haya yanafanyika kila siku! Sasa sisi tume-*experience* haya matatizo yanatajwa kila siku na tunalalamika kila siku, hakuna asiyejua, kuanzia kwenye ngazi ya Wilaya Watendaji wote wa Wilaya wanajua, Mkoa wanajua, Taifa linajua, Wizara zote zinajua; lakini matatizo haya yameendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, mimi na Mkuu wa Wilaya pamoja na Kamati nzima ya Ulinzi na Usalama, tulienda kushuhudia

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. L. J. MPINA]

mateso makubwa ya kundi la ng'ombe 3,000 walikuwa wamefungiwa kwa zaidi ya siku nne bila maji, na bila malisho. Walienda kutolewa kwa amri ya Mkuu wa Wilaya siku ile, Mheshimiwa Rosemary Kirigini. Lakini *imagine* kama sisi Viongozi siku ile tusingeenda, ingekuwaje?

Mheshimiwa Spika, Watendaji hawa wamefanya, Waziri wa Maliasili na Utalii, acha hili la Tokomeza linalozungumzwa, haya yote anayajua wala hakuna hatua yoyote ile inayochukuliwa. Sasa mpaka unajiuliza, hivi sasa uende ukaseme kwa nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu wamefanyiwa ukatili huo mkubwa ng'ombe wao kupigwa risasi, na hapa ninapozungumza, wananchi wangu wa Kata ya Tindaburigi, Sakasaka pamoja na Lingeka, ng'ombe wao 20 walipigwa risasi. Wizara ya Maliasili na Utalii wallkuja pale kutoa tamko kwamba watawalipa wananchi hawa. Leo miezi minane imepita, hakuna hata jawabu, wala hatujaelezwa imekuwaje. Ng'ombe wale wamepigwa risasi, wananchi wamefilisika, hawana hela hata ya kununua chakula, wananchi hao masikini lakini Serikali yao waliyoiweka madarakani inawafanyi ukatili wa namna hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna lile pendekezo namba 48, siwezi kulisoma; ambalo linazungumzia jinsi wananchi wanavyotozwa bila risiti. Katika Jimbo langu, tumefanya kila jitihada za kuhakikisha kwamba, wananchi hawa hawaonewi, lakini sikio la kufa halisikii dawa. Maaskari wa Game Reserve wameendelea kuwaonea hawa wananchi kila siku.

Mheshimiwa Spika, siku ile tunaenda sisi tukakuta kundi lingine, sisi tulipata kundi moja nikiwa mimi pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama. Tulivyoenda kwenye kundi la pili tukakuta wametozwa *fineya Shilingi* milioni 18 bila risiti. Baada ya kumkamata huyu Kileo aliyeandikwa hapa, baada ya kuitwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama alikuja kukiri kwamba amekusanya zile pesa bila risiti na kwamba atazirejesha fedha hizo kwa wananchi. Baada ya hapo, kesi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. L. J. MPINA]*

hiyo ikaingiliwa na Mkoa na Wizara, mpaka leo hatujui kinachoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wanatoza *fine* porini, wanawaonea wananchi, Serikali haipati fedha na hakuna kinachoendelea na huku wakiendelea kuwafilisi wananchi. Lakini haya yote yanafanyika siyo kwamba Wizara hii haina Waziri. Sasa yanazungumzwa haya, anasema *operation* hiyo mimi sikuijua. Je, na haya hayajui Waziri wa Maliasili na Utalii? Haya hayajui? (Tumelalamika, tunapiga simu za moja kwa moja, tunafanya mawasiliano na tunakutana naye ana kwa ana, hakuna hatua inayochukuliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaongea ukaishia *point* moja tu muda ukakuishia. Sasa hapa naomba pendekezo lifanyike. Liongezeke pendekezo kwenye Kamati ambalo mimi napendekeza tuweke kifungu kitakachosema: "Serikali ifute kipengele cha Kanuni ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapor Na. 5 ya mwaka 2009 inayoruhusu Maaskari kutoza *fine* ya mifugo porini." (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii imekuwa ni biashara. Wananchi wetu hakuna eneo ambalo wamenyanyaswa kama hili. Ng'ombe wao zinapigwa risasi kwa sababu wamekosa hela za kulipa. Wamenyanyaswa, wamefanyiwa maasi yote kwa sababu maaskari wale wanataka pesa siku hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 51 ile *bullet* ya tatu inayozungumzia mapori ya Serikali ambayo yamekosa sifa, ili yatumike kwa kilimo na ufugaji kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi. Ili yatumike kwa kilimo, siyo ufugaji; yatumike kwa kilimo na malisho ya mifugo na kiongezeke kipengele kitakachozungumzia suala la *buffer zone*.

Mheshimiwa Spika, ukienda Jimboni kwangu, Kisesa, mwambao wake wote ndiyo mpaka wa pori la Akiba la *Maswa Game Reserve*. Ule mpaka ni barabara tu imelimwa kama unavyoona njia hii, yaani huku Hifadhi na hapa watu wanaishi. Kwa hiyo, ni kazi ngumu kweli kweli kuweza kufanya yale mambo mawili kwamba upande huu ni ufugaji wakati

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. L. J. MPINA]

ni tutu tu limelimwa, upande huu ni ufugaji na upande huu watu wanaishi.

Mheshimiwa Spika, lakini yale yote yametokeaje? Kwa nini wananchi wamesogea mpaka imekuwa hivyo? Ni makosa ya Serikali yenyewe kuhakikisha kwamba, inalinda zile *buffer zone*. Sasa kwa sababu makosa yamefanyika ni lazima tutafute *buffer zone* sasa hivi. Serikali iliunda Tume ya kupitia suala hili; wananchi wametoa mawazo yao, leo ni mwaka mzima hatuajelezwa hata imekuwaje.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba katika maeneo yanayopakana na hifadhi ambayo hayana *buffer zone*, watakapopitia ile mipaka yao upya hizo *buffer zone* ziweze kutengwa ili kuwawezesha hawa wananchi kupunguza sana matatizo waliyonayo sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa sasa nimemaliza hayo mapendekezo muhimu ambayo nilitaka yakae sawasawa, hili suala lilipotokea la Tokomeza, wananchi walipiga simu kila mahali kuuliza Mheshimiwa Mbunge imekuwaje? Ndugu yetu kakamatwa hapa? Kwa sababu, wananchi walikamatwa kwa mbinu za kivita, saa 8.00 za usiku; sasa Mbunge unampigia Mkuu wa Wilaya, hana taarifa; Unampigia Mkuu wa MKoa, hana taarifa. Unapigia Taifa unaambiwa kwamba, hiyo ni *operation* ya Serikali na Wabunge msijihushe, sikilizeni kazi ambayo sisi tumepanga kuifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huyu Mheshimiwa Ndekeja ambaye amezungumzwa hapa wa Kata ya Sakasaka ni Diwani wa kwenye Jimbo langu. Ndiye yuko kule mpakanii kabisa mwa *Maswa Game Reserve*, aliteswa sana; licha ya kuning'inizwa, licha ya kupigwa, licha ya kulazimishwa kufanya mapenzi na mti, Diwani huyu walipomwuliza akasema yeye ni Diwani, wakamwambia kwamba chukua kiatu chako upige simu. Upige simu kwa kutumia kiatu chako na uwafundishe wananchi wako, uanze kuwahutubia wananchi wako namna ya kuishi kandokando ya hifadhi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. L. J. MPINA]*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wamefanyiwa hayo mambo makubwa sana na huyo ni Mheshimiwa Diwani. Wenyevit i wa Vijiji na Vitongoji imekuwa ni utaratibu tu wa kawaida kupigwa porini na kunyanyaswa sana.

Mheshimiwa Spika, mpaka hapa tunavyozungumza, mimi Jimboni kwangu kuanzia mwaka 2008 mpaka leo, wamekuwa wananchi zaidi ya nane kwenye pori lile. Siyo kwamba taarifa hizi hazijulikani Wizarani, na siyo kwamba taarifa hizi hazijulikani Serikalini, lakini hakuna mtu anayechukuliwa hatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa kama hakuna mtu anayechukuliwa hatua, wakati tunajua wapo watu wenye dhamana hii, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba anayetakiwa kuchukua hatua ndiye anayefanya mambo haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kabisa kwa dhati kwamba hata kama ingegharimu kiasi gani, wale Mawaziri waliohusika na mchakato huu, waondoke kwenye nafasi zao, kwa ajili ya kuwatendea haki Watanzania. Hatuna namna nyiningine ya kuizungumzia damu iliyomwagika, hatuna namna nyiningine ya kuwazungumzia kama yule mzee bубу, sikumbuki ametajwa kwenye ripoti ni bубу, ambaye alipigwa risasi mpaka sehemu zake za siri zote zikaharibika! Bубу, alijaribu kuwaeleza maaskari kwa sababu alikuwa anashangaa jinsi ambavyo wanamtesa baba yao, akajaribu kuwaeleza kwa hisia ya mkono, akapigwa risasi tatu sehemu zake za siri, ipo kwenye ripoti hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania tumewafanyia hayo! Tumewakosea sana! Tumewadhulumu sana na ni lazima sisi tuwajibike katika dhuluma hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Nilikuwa naeleza kama kuna watu wanataka kufanya *amendment* kwenye mapebdekezo haya, bado wanayo nafasi ya kuandika. Kwa sababu, ukisema namna hii kama alivyosema Mheshimiwa Mpina, haitoshi.

Atusaidie kuandika, halafu yawasilishwe kwa utaratibu unaohusika. Kwa sababu, tukifika mahali tutafika tukakapopitia maazimio haya kama kuna *amendment* zinatolewa. Sasa tukifanya tu hivi jumla kama unavyosema, siyo rahisi.

Nadhani umeelewa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Sawa Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Haya, namwita Mheshimiwa Cecilia Paresso atafuatia Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kama yupo na Mheshimiwa Shekifu ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika ripoti hii ya Kamati. Awali ya yote, napenda kutoa pole kwa wote walioathirika na *operation* hii ambayo najua kwa namna moja au nyngine imewaletea usumbufu mkubwa sana katika maisha yao ya kila siku. Lakini pia niipongeze Kamati kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuibua jinsi ambavyo haki za binadamu zimekiukwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mujibu wa taarifa hii ya Kamati, washiriki wa *operation* hii ni wanajeshi, ni Askari mbalimbali, ni Askari wa *KDU*, Askari wa *TANAPA*, Askari wa Wakala wa Huduma, Askari wa *NCSA*, waendesha mashitaka na Mahakimu 100. Tafsiri ni nini kama washiriki wa *operation* hii ambao ni wanajeshi wetu na maaskari wetu, lakini wamefanya vitendo hivi vya udhalilishaji, wamefanya vitendo hivi vya ubakaji, wamefanya vitendo vya kuuwa, hii ni tafsiri ya jinsi ambavyo Jeshi letu na Askari wetu walivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini ni lazima tutafakari pia ni namna gani hawa wamepatikana? Kwa sababu, kama

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. C. D. PARESSO]

wanajua misingi yao ya utendaji kazi, kama wanajua kweli kuna Utawala wa Sheria, wasingeefikia huko. Lakini hii inatupa tafsiri kwamba kuna tatizo katika upatikanaji wa wanajeshi wa nchi hii, Askari wa nchi hii wa vikosi vyote kama ni *KDU*, *TANAPA*, ni Wakala wa Huduma, ni Askari *NCSA* na wengine. Kwa sababu, kama wangkuwa wanajua kazi zao haya yote yasingetokea, wasingedhalilisha watu, wasingegebaka watu, wasingegekuwa haki za binadamu kwa kiasi kikubwa kiasi hicho.

Kwa hiyo, lazima kuna tatizo pia katika upatikanaji wa hawa wanajeshi, katika upatikanaji wa hawa maaskari. Hakuna utawala wa sheria. Utawala wa sheria uko wapi? Kama tunajua taratibu za kisheria, ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, wasingeapaswa kuuwa watu hata kama mtu ana kosa au hana kosa. Kuna taraibu za kufuatwa kwa mujibu wa sheria. Lakini wamefikia hatua wanauwa watu. Kwa hiyo, tunaona kuna tatizo pia katika suala zima la jinsi washiriki hawa walivyofanya suala hilo zima la *operation*. Lakini tunaambiwa *operation* hii ni ya kijeshi. Sasa sielewi, tupate tafsiri hata ya kijeshi ndiyo hii? Tafsiri ya *operation* ya kijeshi ni ubakaji? Tafsiri ya *operation* ya kijeshi ni udhalilishaji? Tafsiri ya *operation* ya kijeshi ni udhalilishaji? Ni ukiukaji wa haki za binadamu? Haya ni masuala ya kutafakari, ni masuala ya kulaaniwa kabisa kwa yote yaliyotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini niongelee kidogo kuhusu Wilaya ya Karatu ambapo natoka. Hadi leo tunapoongea, kuna kijana anaitwa Ezekiel Matai amekamatwa na Askari wa *TANAPA* na Maaskari wengine kama ndio hawa hawa wanaoendelea na *operation*, amekamatwa tarehe 30/11/2013 mpaka leo yuko rumande. Ameteswa, hayupo rumande, hajulikani alipo, familia hawajui alipo, anashikiliwa kwa sababu gani? Hatujui!

Mheshimiwa Spika, sasa tunaambiwa *operation* imesimamishwa, lakini mbona bado wanaendelea kukamatwa? Mbona wanawekwa ndani hawafikishwi Mahakamani wako rumande mpaka leo? Halafu mnasema kuna uatwala wa sheria? Taratibu zinataka ndani ya saa 24

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. C. D. PARESSO]

mtu awe ameshafikishwa Mahakamani, lakini mpaka leo hajafikishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kijana mwingine anaitwa George Nina, alitoka kuchota maji, amekamatwa na Askari wa *TANAPA*, hii ni Karatu. Anakamatwa, akafikishwa kituoni, akapewa pembe ya Tembo, halafu wanamfungulia mashitaka. Lakini wakati anakamatwa hana hiyo pembe. Amefika Polisi huko Kituoni ambapo wana vituo vyao hawa Maaskari anapewa, anakabidhiwa hiki kitu halafu anaandikiwa mashitaka.

Mheshimiwa Spika, hii inahuzunisha sana! Halafu Kamati za Ulinzi na Usalama Wilayani zipo, lakini hao ma-*DC* kazi yao ni siasa tu. Kazi yao kila siku ni kuchunga *CHADEMA* wanafanya nini. Wameshindwa kazi zao! Wameshindwa kuangalia haki za wananchi, wameshindwa kusimamia haki za msingi za binadamu za wananchi wanaowaongoza katika maeneo yao, hakuna wanachofanya. Matokeo yake Wabunge tunalalamikiwa, tunaletewa malalamiko, tukijaribu kufuutilia na kuuliza tunaambiwa tunaingilia suala hili. Hatutaweza kunya maza kama tunaona wananchi wananyanyasika, wananyanyaswa na kudhalilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nielezee suala la matatizo ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji. Mambo haya tumeyasema sana na wakati tunachangia bajeti ya Wizara ya Maliasili mwaka 2012, Waziri alituambia wameunda Tume ya kuangalia matatizo yote ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji vilivyo jirani. Lakini mpaka leo hatujaiona hiyo ripoti.

Mheshimiwa Spika, hatujui ripoti inasema nini, lakini mahusiano yanaendelea kuvurugika. Mfano mzuri ni Mamlaka ya Ngorongoro na Wilaya ya Karatu; wananchi walioko jirani na pale wananyanyaswa. Tumeshaoingea huku Bungeni, tunapiga kelele, hakuna kinachofanyika; halafu leo mnasema kwamba, Waziri mwenye dhamana hahusiki? Kikombe hiki hutaweza kukiepuka, utakibeba tu. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. C. D. PARESSO]

Mheshimiwa Spika, nielezee suala la mahusiano. Pamoja na kwamba, kuna mahusiano mabaya, lakini kuna mahusiano mabaya kati ya wananchi na Askari wa Wanayamapor. Haya yote kama hatuimarishi uhusiano, kama ni uhusiano mbaya, wananchi hawataacha kudhalilishwa? Wataacha kunyanyaswa? Ni lazima watanyanyaswa. Watanyanyasika, lakini kama Wabunge watetezi wao na kama kweli kuna utawala wa sheria tunaomba na tunaitaka Serikali ifuate taratibu hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitoe mapendekezo. Hapa ni lazima kuwepo na uwajibikaji wa pamoja. *Collective responsibility* ni lazima iwepo. Suala hili kama lingekuwa limetokea kwa nchi zilizoendelea, kama ingetokea ni Marekani, Uingereza au ni wapi, nchi ambazo zina demokrasia ya kweli, Mawaziri leo wasingekuwepo hapa, wangeshajiuzulu siku nydingi hata kabla ya hii ripoti, wangeshaachia nafasi zao. Lakini kwa sababu utamaduni wa baadhi ya Watanzania na baadhi ya Viongozi hatujali uwajibikaji, ndiyo maana mpaka leo wapo. Ni lazima kuwepo na uwajibikaji wa pamoja, tena siyo kusukumwa, mlipaswa siku nydingi sana mwachie hizi nafasi. Nimesema kikombe hiki hakitaweza kuwaepuka, damu za Watanzania zilizopotea, waliouawa, waliojeruhiwa hazitawaepuka. Kikombe hiki mtakibeba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu lingine, ni lazima kuwepo na fidia kwa watu wote walioathirika. Fidia ya watu wote, mazao, wanyama walioathirika, ng'ombe, watu, fidia lazima ipatikane na siyo kifuta jasho. Kwa sababu, mnajificha kwenye jambo la kifuta jasho, kifuta jasho haina maana yoyote, tunataka fidia halisi ilipwe kulingana na uharibifu uliotokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kidogo kwa kuelezea suala la mgogoro wa Hifadhi ya Ngorongoro na Wilaya ya Karatu. Mara nydingi tumemwomba Waziri aje, na Karatu ndiyo njia kuu ya watalii kwenda Ngorongoro; kama tutaendelea kupiga kelele tukiwaambia mje mrekebishe mipaka kati ya vijiji vyaa jirani na Hifadhi ya Ngorongolo na hamtakuja, itabidi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. C. D. PARESSO]

Peoples power itumike. Itabidi tuwazuie hawa wageni wanaopita pale Ngorongoro, tutawazuia wageni ambao wanaingizia pato ya Taifa hili. Kwa hiyo, tunaomba jambo hili lazima mje mkae na watu wa Karatu, mkae na vijiji vya karibu pale tuongee tumalize matatizo haya ya mipaka tuondoe unyanyasaji uliopo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Paresto. Sasa namwita Mheshimiwa Lediana Mg'ong'o, hayupo; Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Azza Hamad; hawa ninaowaita sirudi tena nyuma. Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa nashukuru, mimi ni mmojawapo wa Wajumbe katika Kamati ya Uchunguzi ya Tokomeza ambayo Mheshimiwa Spika uliridhia ikafanye kazi. Mimi nashukuru sana, nilikuwa nasema lakini nimekwenda kushuhudia. Nililia field! Nililia! Huwezi amini kama tuko Tanzania! Huwezi kuamini, yule mama picha imeoneshwa sehemu ya uso, sehemu ya mgongo, huko kwenye kifuko cha uzaji kimefumuliwa kimetoka nje; sehemu ya mbele na sehemu ya nyumba yote imechanwa. Mama mwenye watoto, watoto wake wanashuhudia. Wale watoto leo utawaambia nini kuhusu Serikali ya Chama cha Mapinduzi? Utawaambia nini? Huwezi kuwaambia kitu! Tunalipeka wapi Taifa?

Mimi nimeshuhudia, Wasukuma watani zangu, yaani mtu anakuja anasema mimi nina wake wane, nina watoto 11; nilikuwa na n'gombe 200, haki ya Mungu wamefilisi hajabaki hata mmoja. Wamekwenda wemepiga mnada, waliniomba Sh. 180,000/= kwa kila ng'ombe lakini wamepiga mnada kwa Sh. 60,000/= na mimi nimezuia kwenda kuwagombea kule n'gombe lakini sijapewa senti tano.

Mheshimiwa Spika, hali inatisha huko chini. Hali ni mbaya! Watu wamefilisiwa, familia zinateseka, watu wanaishi kama wakimbizi katika Nchi yao. Lakini bora ya wakimbizi. Katika maeneo ya wakimbizi, wanatengenezewa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. S. L. A. KIWANGA]*

miundombinu, wanapewa maji, wanapewa mahema. Lakini leo Watanzania wamechomewa nyumba, wamefilisiwa ng'ombe, wako chini ya miti wanakaa, mvua, juu mali yao na watoto.

Mheshimiwa Spika, hali ni mbaya. Sasa chanzo ni nini? Kuanzia chini kwenye ngazi ya Kitongoji ni rushwa, ngazi ya Kijiji ni rushwa, ngazi ya Kata ni rushwa, ngazi ya Wilaya ni rushwa niliyoshuhudia. Lakini rushwa hizo inaonekana zinakwenda mpaka juu. Sasa akina nani wanapokea hizo rushwa, ni lazima tuijulize. Hali ni mbaya kuliko maelezo.

Nchi hii itakuja kuingia kwenye machafuko makubwa. Ndiyo maana unasikia kule Mwanza watu wameua, siyo kama wamependa na mimi sifurahii, kushinda kwa leo, juzi Malinyi Igawa, watu wameua. Polisi wameua na wananchi wameua. Magari yamechomwa moto, Kituo kimechomwa moto. Ukiangalia vurugu hii ni ya nini? Wafugaji, mipaka, wakulima, hifadhi, wanyamapori.

Sasa ni lazima kama nchi tuone tumekosea wapi, tujipange upya, lakini tunajipangaje upya wakati mfumo mzima, yaani Serikali nzima kuanzia ngazi ya Kitongoji mpaka Kijiji kote kumeoza, tutaanzia wapi? Huo mtindo ni wa nchi nzima. Mimi nilidhani Morogoro tu. Sasa bahati nzuri, nimekwenda Bukombe, Biharamuro, Karagwe, Kaliua, Kasulu, Mpanda na Sumbawanga kote baba mmoja, mama mmoja. Lazima tuchuke hatua! Hii nchi tunaipeleka wapi?

Mheshimiwa Spika, hali mbaya. Mimi ingekuwa ni amri yangu, tuanze upya. Ingekuwa ni amri yangu, Serikali nzima ibomoke tuanze upya. Hali ni mbaya kupita maelezo. Wakulima wanalia, wafugaji wanalia, watu wa kawaida wanalia, Mawaziri wanalia, Rais analia, Wakuu wa Wilaya wanali, Wabunge tunalia, Taifa la kulialia! Tunaenda wapi ndani ya nchi hii? Hali ni mbaya kuliko maelezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi niko kwenye Kamati na tumejadili, tumekubaliana, tumeleta hapa ili kama mnaona kwamba kuna nyama za kujazia, ndiyo wakati wenu sasa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. S. L. A. KWANGA]

Wabunge mjazio nyama ili sote twende kwa pamoja tuliokoe Taifa hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, huko Iputi kwa muda tuliopewa, yaani hatukufanya kazi ile, hatukufikia maeneo mengi. Kwa hiyo, hii taarifa tumeiweka lakini kuna watu wengi sana wameathirika ambao hatukuwafikia, kuna maeneo mengi sana yameathirika hatukuyafikia kama taarifa hii inasema labda wamezulumiwa n'gombe 5,000 ukute labda huku tulikoacha kuna ng'ombe zaidi ya 100,000. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna mchezo mbaya. Maafisa wanakaa kabisa, Tokomeza imekwenda pembeni, Maafisa wa Wanyamapor wamewapeleka wale watu wao wafugaji katikati ya pori, hata Tokomeza hawakuwaelekeza waende huko. Waliokuwa wanaonewa kufilisiwa ni wale wananchi wallioko pembezoni mwa hifadhi ndani kabisa ya mapori wananchi wapo, wana ng'ombe wao, wanalipa kila baada ya miezi mitatu na watu wanachukua hela bila risiti na mtando unajulikana kuanzia chini mpaka juu. Hiyo ndiyo hali halisi! Kama kuna takwimu za mifugo zinaletwa ndani za nchi yetu, hizo takwimu ni feki. Kwasababu gani? Je, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo ulishawahidi kwenda kuhesabu mifugo katikati ya mapori? Kwanza huwezi kujua, wamejificha kule. Kwa hiyo, ni lazima tuanze upya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwanini linatokea tatizo hili? Hakuna majosho, hakuna miundombinu, wafugaji wanahangaika na mifugo yao, wanagombanishwa na wakulima, Wizara ya Mifugo ipo. Ipo ipo tu! Wewe unashughulikia mifugo, unajua nchi hii mifugo iko wapi na inafanya nini na kuna marambo mangapi, na hao ng'ombe wanasaidiwaje? Sasa sisi kama Kamati tumeleta hapa ili tusaidiane twende kwa pamoja. Hapa hamna kutafuta mchawi, lakini tunataka nchi yetu iwe na amani na utulivu. Lakini kwa sasa hakuna amani wala utulivu, watu wanashindwa kulima, wanashindwa kufuga. Watu binafsi wanajinufaisha kwa mifuko yao. Misitu inateketezwa, Wenyeviti wa vijiji wapo, Watendaji wa vijiji wapo, hali ni mbaya kuliko maelezo. (*Makofî*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

/MHE. S. L. A. KIWANGA/

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mjumbe, siwezi kusema sana. Niliyolia kule *field* yananitosha na leo sitaki kulia tena. Watu wamebakwa, watu wamedhalilishwa, tena wamebakwa mande wanasema, tena mbele na nyuma, hali ni mabaya! Akina mama wako tayari kutoa ushahidi *live*, maana wengine wameona ajabu! Wazee watu wazima wamebakwa, mtu amepigwa risasi mbele ya watoto wake ng'ombe karibu elfu moja na kitu wamefilisiwa hawakubakiwa hata unyoya, mtu amekufa.

Mheshimiwa Spika, ahsante, hali ni mbaya! (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante, sasa namwita Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE: ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninayo shukurani mbele za Mungu na mbele za Bunge lako Tukufu kwa uchungu na kwa moyo wa kuumia kuwapa pole ndugu zetu wote waliopatwa na mambo haya, na tunaamini kabisa Mungu ni mwaminifu, atawatia nguvu na tunaamini kabisa na hili litapita na tutavuka tutaendelea Mungu atatusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo nataka nichangie, mimi nimeumizwa na jambo moja. Jambo ambalo tangu limetokea na muda ambao tunao leo kuwa ni kimya, sijasikia watu waliofungwa, hatujasikia watu walioamatwa kuwa Gerezani, hatujasikia lolote ambalo limefanyika kuhusina na jambo hili, ni ngumu sana kueleza vizuri na watu wakaelewa. Kwa hiyo mimi niseme tu, niwaombe raadhi sana ndugu zetu. Lakini hebu turudi kwenye akili ya kawaida, hivi ni nani ambaye ni kiongozi wa nchi atume Jeshi lake kwenda kutotomeza, halafu atokomeze watu wake?

Mimi nahisi jamani, tukubaliane Watanzania wote hili jambo tulipime, ndani yake lina kitu gani? Hivi kweli mtu ambaye anaipenda Serikali hii iwepo madarakani, halafu umepewa kazi ya kuifanya uende kule uchinje watu halafu useme ni Serikali inayofanya mambo haya. Jamani, hebu turudi kwenye akili zetu; uzembe upo ni kweli; lakini kweli yaani

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. N. MSHAMA]

Mheshimiwa Rais atume watu waende waeue watu halafu warudi ionekane kwamba Serikali haifai? Jamani kama kuna uchochezi wowote...

**SPIKA:** Acheni watu waongee!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Kama kuna jambo lolote linafanyika ambalo linawezekana kabisa kwa ajili ya kuangusha Serikali hii linafanyika Mungu awasaidie sana wanaofanya mambo haya. Siyo sawa! Hata kama unataka kutoa Serikali, unataka kuingia wewe, utaingia wapi kwenye hali kama hii? Utachukua nchi gani iliyoharibika namna hii? Wewe watakuaminije kwamba ukija una Roho Mtakatifu ambaye huwezi kufanya mambo hayo? Kwa hiyo, ninahisi na ninaomba tusilikizane.

**SPIKA:** Ana dakika zake, mwachseni amalize nanyi mtapata nafasi.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, sijamsapoti Waziri yejote, lakini ninawaza jambo moja, yule anaekwenda kufanya jambo hilo, ametumwa na Serikali iliyopo?

Kwa hiyo, mimi ninachojua, hizo njama siku moja zitawarudia wale wanaofanya. Inawezekana hata hapa mpo ili kusudi tuabike Watanzania. Mnataka Rais wetu Kikwete aibike aonekane hafai. Lakini najua Mungu kama aishivyo, ukweli utajulikana na ubaya utaonekana.

Mheshimiwa Spika, ni sawa Mawaziri wamekosea. Ni kweli, hata Waziri wa Mifugo nilimfuata kuhusu kule ng'ombe zetu, kuhusu wanawake kule walivyofanyiwa, anasema mambo yanaendelea, uchunguzi unafanyika. Haiwezekani ukafanya uchunguzi zaidi ya miezi mitatu, haiwezekani. Lakini: Je, yule anayefanya vile, aliyekwenda kuchoma mwanamke ametumwa na Chama cha Mapinduzi?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo! Hapana!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Watanzania hata wao wanajua kwamba inawezekana wale wenyewe uroho na usongo wa nchi yetu, mnataka kuchukua madaraka kwa kutupaka matope, mkawa nyie mnayafanya ili kusudi watu wawaone ni watakatifu. Hata kama mtakataa, ukweli utabaki kuwa ule ule. Nataka kusema, bado nakataa na siwapongezi Mawaziri, siwakubalii, wana nafasi yao walitakiwa kuifanya, lakini na wewe unayepita nyuma ukahakikisha unavuruga nchi hii, Mungu kama aishivyo, na wewe utakapokuwa unafikiria utachukua nchi hii halafu ubaki kuitawala kwa kuua watu, haitawezekana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mbona mnaingilia hotuba ya mwenzenu?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Inawauma! Wanaji-*suspect!* Ndio wachochezi wakubwa! Mimi nasema hata hao mliowapa pesa waweze kufanya hivyo, hata kama wamef...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mshama na wewe jadili hoja! (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Eeeeh! (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Sasa na nyie mnazomea kwa nini? Mheshimiwa Mshama, jadili hoja na nyie acheni kuzomea.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, hoja ndiyo hiyo. Nami nataka kuongelea yale yaliopotiwa mahali hapa, na wala siwapongezi. Narudia tena, uzembe unaweza ukawepo, lakini na wewe uliyetumika kufanya hivyo, mbele za Mungu utahukumiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachotaka niseme, tangu hiyo hali imetokea, ilitakiwa Mawaziri hawa tungeshasikia watu kama 10 au 15 wako ndani, inawezekana kabisa. Lakini hatuwezi kuangalia shilingi kwa upande mmoja, kwamba Serikali Serikali tu; ndiyo mmsonda Serikali, lakini niombe, operation inapokuwepo, wale waliopewa majukumu ya kwenda mbele si wapo? Mbona hatujasikia wamewekwa ndani? Wale waliopewa magari kwenda kufanya hiyo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. N. MSHAMA]

operation si wapo? Mbona hatujasikia wapo ndani? Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu na niwaombe hata Mawaziri, sina hata haja ya kusema. Kusema kweli ukiona pitcha tulivoona pale, ukaona mtu bado hajasema chochote kama Waziri utakuwa umekosea. Mimi nathani ilitakiwa sasa hivi muwe mmeseka chochote kwa sababu, mmeshindwa kutekeleza majukumu yenu, lakini na wale walio nyuma yenu wanaofanya hivyo bado watahukumiwa.

Kwa hiyo, naomba tu niwape pole watu wangu wa Nkenge ambao mmepata matatizo lakini ninaamini kabisa baada ya hili tutakwenda kusimama sawa na kuangalia ukweli uko wapi na wale waliokuwa kwenye *operation* tuombe Serikali iwawajibishe ili tuweze kuwa na imani na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, wakati wowote, kunapotokea jambo usiangalie shilingi upande mmoja, uigeuze na nyuma. Msukumo wa watu kufanya hivyo unatoka wapi? Msukumo wa kufanya hivyo nyuma yake kuna nini? Kwa hiyo, inawezekana kuna watu hapa au nchini mwetu hawaitakii mema Serikali iliyopo na ndiyo maana wamefanya hayo yote. Kwa hiyo, mimi niseme nakubaliana na waliochunguza, lakini bado nasema watu wanaofanya hayo wakijulikana wasiachiliwe, wawekwe ndani na ikiwezekana wafungwe maisha kwa sababu wamepoteza maisha ya wenzao.

Mheshimiwa Spika, katika haya machache, naomba Mungu awabariki. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kaika Telele, atafuatiwa na Mheshimiwa Jackson Mwanjale.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kusema kidogo kuhusiana na Operesheni Tokomeza Ujangili.

Mheshimiwa Spika, mimi ni kati ya Kamati Ndogo ya Kudumu ya Bunge na Ardhi Maliasili na Mazingira; Kamati ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. K. S. TELELE]*

watu tisa, ambayo ilikwenda katika Mikoa ya Pwani, kule Rufiji, Morogoro, Iringa, Songea, Mtwara, kwa maana ya Masasi na Tunduru, tuliwaita watu wa Tunduru, ndugu yangu Abdalah Mtutura watu wako tuliwazungumza, tulikutana nao na tulizungumza nao na hayo ambayo ulisema tangu mwaka 2012, ni kweli tulithibitisha, lakini usiwe na hofu kwa sababu watu wa Tunduru tumewatendea haki, kama Serikali itachukua hatua ambazo Kamati imependekeza.

Mheshimiwa Spika, jambo hili lilikuwa ni kubwa. Operesheni hii, wananchi walituambia, hao wanajeshi ambao wameletwa kusimamia Operesheni hii wametolewa wapi? Haiwezekwa ikawa imesimamiwa na Jeshi la wananchi wa Tanzania JWTZ, wanajeshi ambao kwa muda mrefu wameshiriki katika *operations* mbalimbali na wakaleta mafanikio, leo inakuaje ghafla hali ikaharibika kiasi hiki! Wallituambia bila shaka hawa watu mmewatoa kule *Darfur*, ni watu waliopigana kule *Darfur* au Kongo *DRC* wakaletwa moja kwa moja bila kupewa maelekezo bila kupewa chochote wakaenda kwa wananchi. Jambo hili kwa kweli hata sisi tunesikitika sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kama ultutuma kuitia Kamati hii Ndogo, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati amefanya kazi kubwa, tumezunguka, tumefanya kazi na tukaleta haya ambayo tunazungumza mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, jambo hili hakukuwa na ushirikishwaji kabisa, na wanadai kuna taarifa za intelijensia ambazo ndizo walikuwa wanafuata. Lakini taarifa zenyewe kama hizo, wanawenza wakatumbukiza mambo ya kisiasa huko ikawa ni fitina wala siyo taarifa ambazo zitasaidia nchi, ni kutafuta nani mchawi, na kukomoana kisiasa na vitu vya namna hiyo. Ndiyo maana watu kwa kweli wameathirika kiasi hicho. Lakini wanajeshi wenyewe wanasema, haiwezekani kabisa, hata kama tumeshirikisha vyombo vingine, lakini hatuwezi sisi wanajeshi kuongozwa na raia. Nafikiri hapo ndiyo wamekosea kwasababu majeshi haya yakitoka kwenye *barracks*, kwenye makambi yao kwenda uraiani, ni eneo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. K. S. TELELE]

lingine tofauti kabisa hili. Ilipaswa eneo lile liwekewe miongozo na utaratibu na usimamiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile operesheni hii pia ilitawaliwa na usiri mkubwa. Usiri ukishavuka kiwango, basi mtakuwa mnajifanyia wenyewe mnavyoona kwa sababu hamtaki kuwashirikisha watu wengine. Kuna mfumo mzima wa Serikali, ngazi za vijiji, ngazi za Wilaya, ngazi za Mkoa, lakini kote huko hakuna walioripoti huko; hawajaripoti kabisa katika mfumo wa Serikali. Sasa mambo yakiharibika huko, nani atakwenda kumlilia nani au kumwelezea shida yake? Imekuwa ni tatizo kubwa, imetawaliwa na usiri. Nakubali operesheni yoyote inakuwa na siri lakini usiri nao wa kupitiliza hauwezi kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, hakukuwa na maeleo ya nani afanye nini, wapi, wakati gani na kwa namna gani? Ili mradi operesheni hii inasimamiwa na Jeshi, basi watu wengine wakakaa pembedi. Sasa majeshi siku zote wana tabia ya ku-over do, kufanya zaidi kuliko ambavyo waliekelezwa. Kwa sababu hakukuwa na *checks and balances*, hakuna mtu ambaye angeweza kuzungumza na wanajeshi, hawaelewi lugha yoyote, wao ni kupiga tu, wanakwambia wewe tumepata taarifa una silaha, unasema hapana! Unanyukwa mpaka unakiri kusema uwongo. Sasa hili ndilo limewapata wananchi wengi. Hata wale ambao wanamiliki silaha kihalali, wana vitabu vyao, wamechukua silaha lakini vitabu vile vyakumiliki silaha wameviacha. Sasa kwa kweli hii imetutisha hata sisi.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaposema operesheni hii imesitishwa ili kujaribu kurekebisha kasoro na upungufu uotokea, sijui kama itawezekana kwa sura hii tunayokwenda nayo. Kilio ni kikubwa sana, wananchi wamefanyiwa visivyo, kuna ukiukwaji mkubwa sana wa haki za raia na haki za binadamu na utawala wa sheria haupo kabisa katika utekelezaji wa jambo hili. Watu wamepigwa, wamenyang'anywa fedha na mali nyingine, mifugo ndiyo hiyo imepigwa risasi, wamekamatwa watu wakiwa wako

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. K. S. TELELE]*

katika shughuli zao tu za kawaida, wanakamatwa wanapelekwa kwenye vituo wanavyovijua wao.

Mheshimiwa Spika, kilimo pamoja na shughuli nyiningine za kusaidia wananchi katika harakati za kiuchumi na kujisaidia kupata chakula, kila kitu kimesimama kwa sababu ya hofu hiyo operesheni. Hajatokea hiyo operesheni ikawapendeza watu hata kidogo. Watu wamekwenda mafichoni kule porini kabisa, wanapanda miti huko wanasilizia nini kinaendelea. Operesheni kweli imesimamishwa au hapana? Lakini nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili mmepega kelele, tumetia *pressure* mpaka hiyo operesheni ikasimama japo kwa muda na ndio maana nasi tumetumwa kwenda kuchunguza madhila ambayo yamewafika wananchi hawa. Naomba tena katika jambo hili lazima Wabunge tuungane pamoja, tuwe kitu kimoja kusimamia na kuona kwamba haki za raia amba ni wananchi wetu zinasimamiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niwape mfano, kule Ngorongoro alikuwa ameteuliwa mhifadhi mmoja kwenda kuwa mhifadhi wa Ngorongoro, lakini bahati mbaya huyo mhifadhi wale Wamasai wanapigiana simu lomoni zao zile, siyo hizi simu za nini, kuna simu ambazo wanapigiana wenyewe zinakwenda kwa kasi hata kuliko simu hizi. Sasa wakajua sehemu za Loliondo kuna ng'ombe karibu 6,000 waliwekwa Mahabusu na Maaskari wa Serengeti. Sasa waliposikia huyu mhifadhi ambaye ndiye aliidhinisha hiyo pia anakuja Ngorongoro, walimkataa moja kwa moja na wakamwambia Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara, ondoka na mtu wako, hatuna haja naye, ameweka ng'ombe zetu Mahabusu na huyo mtu kwa kweli hajaendelea na huo wadhifa wakuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Kwa hiyo, ameondoka. Kwa hiyo, hakuna litakaloshida Bunge hili tukiamua kwamba jambo hili sasa liwe namna gani, sisi ndio tuna maneno ya mwisho katika kusimamia haki za wananchi waliotuleta katika Bunge hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi napenda niishie hapo, niseme kwa kweli ifanyike utafiti wa ndani kabisa kuwabaini

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. K. S. TELELE]

wote waliopata matatizo, waliopoteza mali zao, walipoteza ndugu zao najua roho ya mtu huwezi kufidia, lakini angalau ifanyike jambo kubwa fedha zitafutwe fidia ifanyike kwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa nafasi hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Nilimwita Mchungaji Mwanjale, atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuongea kwa jioni hii hasa kwa hoja hii ambayo iko mbele yetu. Hii hoja ni nzito, kwa sababu kule kwangu mimi iliokea na hata mtu mmoja nakumbuka alikufa kwa sababu ya matatizo haya ya mifugo lakini ilikuwa ameuawa pale na wananchi. Lakini shida ambayo naipata hapa ni mfumo uliopo katika nchi yetu. Sijajua kwa nini mambo yanatendeka, yanafanyika mambo makubwa na mabaya sana lakini habari hazipatikani kwa wahusika. Nakumbuka zamani hizo nchi yetu ilikuwa kati ya nchi ambazo zilisifiwa kwamba hapa unaweza ukaingia, lakini kutoka siyo rahisi, utakamatwa tu. Kama Israel, kama Marekani na wapi ilikuwa haitokei hivi, ilikuwa katika historia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi mambo yanatokea mazito, makubwa, lakini hakuna wala haijulikani, watu wanauawa hakuna mtu anayejua. Lakini sisi kama Wabunge tuko hapa nafkiri tunawakilisha wananchi mpaka ifike hapa tuanje kujadili, wakati mwingine ni vigumu sana ndugu zangu. Lakini nilikuwa nauliza tu, mfumo wetu ukoje? Kuna mambo mengi yanafanyika siyo haya tu ambayo leo tunayazungumzia, yanatokea, lakini hakuna habari. Kuko kimya utafikiri hakuna usalama, hakuna nini, tutafika wapi? (*Makofii*)

Mwisho nikiangalia pale Dar es Salaam naona kuna mobu ya watu wengi sana kutoka maeneo mbalimbali. Wako watu wengi, naona Wasomali pale wamejaa, hata hujui

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. L. N. MWANJALE]

kama hawa kweli wanaingia kwenye mipaka na sijui kama nao wanajulikana na kwa sababu rushwa imekuwa ndio tatizo kubwa. Nirahisi mtu mmoja akahongwa akasababisha watu wengi wakafa kwa sababu ya rushwa tu. Anaweza akaruhusu watu wakapita halafu wakaja kufanya madhara makubwa, kuja kukumbuka ni baadaye. Nilikuwa naomba *system* ya nchi ambayo tulizoea kuifahamu tangu zamani, enzi ya Mwalimu Nyerere iko wapi? Irudi hiyo! (*Makofii*)

Tukienda kwa namna hii, siku nyingine tutajikuta jamani tunapigwa, tunauawa kama wenzetu Kenya walivyouawa kwa sababu hatujui ni vipi tunaishije. Ndiyo maana watu wakati mwengine wanasesma kwamba nchi hii inaishi kwa mashaka kuliko nchi nyingine zote zinazotuzunguka. Maana yake ukiishi Kenya, unaona kama ujambazi uko mwingi, lakini sisi bado tunaambiwa kwamba ni wa kwanza kwamba tunaishi kwa mashaka. Kwa hiyo, ina maana kuna kasoro mahali fulani. Nilikuwa naomba hiyo tuiangalie.

Mheshimiwa Spika, nimeona hata hizi hela ambazo tunasema wanawachaji wakulima, wafugaji kule kwangu nilikusanya *receipt* nyingi sana nikapeleka mpaka kwa Mheshimiwa Waziri wakati huo. *Receipt* mtu anachajiwaa Shilingi milioni mbili, Shilingi milioni tatu, ana ng'ombe sijui wangapi! Jamani tunatenda haki nchi hii? Naomba tujaribu kuangalia hayo. Bado naendelea kuomba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vita hivi vyta ujangili nalinganisha na vita vyta madawa ya kulevyaa. Inaelekea kwamba kuna watu wazito sana ambaa wanafanya kazi hii. Kwa sababu kama ingekuwa ni watu wadogo hivi vita vyta ujangili vingekuwa vimekwisha, lakini sasa kwa sababu inagusa pengine na watu wazito kwa hiyo wanajaribu kuzuia haiendi. Tunahangaika na madawa ya kulevyaa, wapi! Kila siku watu wanakamatwa, lakini wanaachiliwa, hakuna watu ambaa kweli wanataka kutumikia Watanzania. Nilikuwa naomba jamani tuanze upya sasa.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. MCH. L. N. MWANJALE]*

Kwa hiyo, vita hivi ni vikali sana. Inawezekanaje majangili wanafanya miaka na miaka, tunazungumza ndani ya Bunge, tunaongea, lakini hakuna hata jangili mmoja anakamatwa? Tunasema nini? (*Makof*)

Kwa hiyo, ina maana kuna kasoro mahali fulani, na lazima tuijulize hapo. Kuna kasoro katika mfumo wetu, kuna kasoro katika usalama wetu, kuna kasoro nyngi sana ambazo zinafanya kwa kweli mambo yasiende jinsi ambavyo tunataka yaende. Haiwezekani kabisa kwamba mambo yanatokea na Serikali isijue na tusichukue hatua yoyote ile, haiwezekani. Nilikuwa naomba kwa haya ambayo yametokea, mimi naunga mkono kwa Kamati jinsi ilivyochambua, ilivyotembea, ilivyofanya ziara naunga mkono kwamba kwa kweli maoni ya Kamati ni muhimu kabisa yazingatiwe. (*Makof*)

Kwa sababu lazima tuanzie hapa, maana yake nikihukumiwa mimi leo siyo mwisho wa maisha yangu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tuyazingatie maoni ya Kamati, tuje kwamba Kamati imefanya kazi yake vizuri, maana tuliwatuma wenyewe. Imefanya kazi nzuri na kazi hii lazima ithaminiwe na ninaomba kwa wale walioathirika na mimi nitangulie kusema nawapa pole sana wale amba wameathirika. Hata kule kwangu waliathirika; wamechajiwa ng'ombe, mtu mmoja amelipa Shilingi milioni kumi. Hebu fikiria, mkulima anachajiwa Shilingi milioni kumi, mfugaji, Shilingi milioni kumi, unatoa kwa mara moja. Ni sawa na kwenda kununua ng'ombe wengine huko, lakini unaambiwa lazima ulipe.

Kwa hiyo, ina maana kwa kweli kuna watu amba wameumia nchi hii na labda sasa kuanzia hapa tutaanza kujifunza na kwenda jinsi ambavyo kwa kweli inatakiwa twende. Nafikiri kuna kitu tunajifunza hapa. Makosa yanatokea, tunajifunza kitu hapa na Mungu amefanya mambo haya yawe wazi bila wasiwasi kwa sababu anataka tujifunze kitu nchi yetu tuanzie hapa sasa kwenda inavyotakiwa.

Mhesimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru kwa uchambuzi wa Kamati hii, wamechambua vizuri na vizuri

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. L. N. MWANJALE]

tuangalie maamuzi yao na Bunge liazimie vile inavyotakiwa, kwa sababu tukienda kwa kubembelezana, tutajikuta nchi hii siku moja tunakamatwa wote tunapigwa hapa wala hatujui. Kuna usemi watu wengi wanasesma, inawezekana hii *force ni external*, imetoka nje lakini sisi tuko wapi? Mbona tumepewa majukumu ya kuweza kutekeleza? Si tungefanya sehemu yetu? Hata kama kuna mtu anatoka nje, anataka kutulazimisha lakini sisi upto, ndiyo tunatakiwa tuwajibike tufanye kazi hiyo. Akija mtu wa nje hawezi kushindana na mtu wa ndani maana sisi tutakuwa tayari tumeshajizatiti. Kwa hiyo, naomba kwamba kwa yale ambayo yapo na yale ambayo yamezungumzwa tuyazingatie.

Mheshimiwa Spika, nami naomba nimalizie kwa kusema hayo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Meshack Opulukwa.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza naomba madihegi, kama kanuni zako zinaweza kuniruhusu, basi uniachie mimi na Bunge zima tuweze kulia japo dakika mbili. (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**SPIKA:** Hujaungwa mkono! (*Kicheko*)

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nasema hayo kutokana na yaliyotokea, na yanayoendelea kutokea. Katiba hii ibara ya 14, 15, 16 na 17 inaelezea haki ya kuishi na pahali gani mtu anaweza akachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, naunga mkono taarifa ya Kamati hii kwa asilimia 1000, siyo 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kipindi cha nyuma, wakati Waziri Mkuu akijibu maswali hapa Bungeni, Mheshimiwa Khatib Said Haji akanyanyuka kumwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu; Mheshimiwa Waziri Mkuu kauli

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. K. K. KOMBO]

ulyotoa ya "piga" twakuomba uifute. Lakini Waziri Mkuu akarejea kauli ile akasema: "piga tu, piga tu, piga tu." (Makof)

**SPIKA:** Maneno hayo yako Mahakamani. Mheshimiwa Kombo endelea kuzungumza, usiwasikilize hao wanakutia balaa.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Ishaalah! Meseji ishafika Mheshimiwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niseme kwamba matokeo haya yanayotokea Tanganyika leo, ni historia ya matokeo yaliyotokea Zanzibar Unguja na Pemba. Wakati yalipokuwa yakitokea kule, waliokuwa wakitekeleza haya ni vyombo vyatya ulinzi na usalama vyatya nchi yetu. Leo vyombo vilevile vyatya ulinzi na usalama vyatya nchi yetu na vlongoz i wale wale wanatekeleza yale ambayo yalikuwa yakitekelezwa Zanzibar. (Makof)

Sasa basi, kwa usalama wa nchi hii na kwa sababu Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali ni Waziri Mkuu, nasema kwamba Mheshimiwa Pinda, amepinda, na sasa ili anyooke, basi awajibike na walio nyuma wamfuate. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nchi hii imefika pabaya. Leo yanayozungumzwa ndani ya Bunge hili kwamba watu wamefikia hatua ya kuzinishwa na wakwe wao au watoto wao, yamefanyika ndani ya Kisiwa cha Pemba, lakini ukimwoteza mwenzio kidole kimoja, ujue kama vitatu vinakuelekea wewe. Lakini vilevile unapomwapiza Mama wa Kambo kama afe, basi mara nyingi atakufa mama yako mzazi. (Makof)

Sasa nasema kwamba wakati umefika na wala hii siyo fitina ya siasa, tusitie maneno ya siasa hapa. Walioleta ripoti hii ni Kamati na Kamati hii ina Wabunge wa kutoka pande zote. Hapana siasa! Tusikae hapa tukizungumzia siasa. Mambo mengine ni ya ukweli na huu ni ukweli mtupu! Umefika wakati sasa tutafakari nchi inakwenda pabaya, nchi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. K. K. KOMBO]

inakwenda pabaya! Kwa hiyo, nasema, tena narudia kwamba kila aliyejusika na hili basi awajibike. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, huyu Danhi Makanga kila siku nasikia anatajwa; hivi jamani Serikali ipo, mtu huyu anatajwa kila siku, Mkuu wa Wilaya, anaadhibu watu, ana makanga gani huyu? Ni Makanga wa aina gani? (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, nafika mahali najiuliza, hivyo kweli Watanzania tumejitawala? Kweli Watanzania tumejitawala? Kama tumejitawala, ni aibu kusema kwamba tunajitawala wakati wananchi wanaadhibiwa, wao na mali zao. Tujilize, ni Mkoloni gani aliyemchukua mtanganyika akamweka hadharani uchi kumzinisha na mwanaye? Yuko? Au akamfanyisha mapenzi na mti, yuko? Leo sisi Watanzania wenyewe kwa wenyewe? Nakwambieni ndugu zangu mlifiokwa na maafa haya, maafa haya siyo yenu ni yetu sote ni ya Watanzania wote. Kama tunataka kuwahakikishia kama maafa haya ni yetu sote, basi lazima haki itendeke. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kingine kinachoshangaza na kunisikitisha ni kuona kwamba Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama tunayapeleka nchi nyingine kwenda kulinda haki na amani ya nchi zile. Lakini ndani ya nchi yetu, kwa Jeshi hilo hilo leo tunakosa amani. Tunakwenda wapi? Hivi ndugu zetu wamesibiwa na nini? Kama Serikali haiwalipi, iwalipe. Tusitie siasa! Kama Serikali haiwalipi Wanajeshi au Polisi, iwalipwe inavyopaswa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba dhuluma iliyofanywa kama haikuchukuliwa hatua, basi sisi wote ni *masuul*, na tutakwenda kuulizwa kesho mbele ya Mwenyezi Mungu. Kama waliohusika na makosa haya hawakuchukuliwa hatua zinazopasa na tukasema kwamba labda wasimamishwe tu, wasiadhibiwe, basi kesho tutakwenda kujibu mbele ya Mwenyezi Mungu. Ni lazima sheria ichukue mkondo wake. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. K. K. KOMBO]

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba. Wale waliokuwa na kauli ya kusema kwamba, labda wengine ni wasafi; walio toka Zanzibar, ni wasafi kweli kwa nguo walizovaa, lakini makovu wanayo. Kwa sababu, walianzia huko na hapa leo ya endelezwa. Jembe ni lile lile, uliobadilika ni mpini, basi! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache na mimi nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kombo. Sasa namwita Mheshimiwa Meshack Opulukwa na Mheshimiwa Anne Kilango.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kusema japo kwa uchache kuhusiana na taarifa hii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wachangiaji wengi wamesema, wananchi wameteseka sana, wananchi wameumizwa sana, wananchi hawa hawa wamepata mahangaiko ambayo hayajawahi kutokea tangu kuweko kwa misingi ya Ulimwengu.

Mheshimiwa Spika, naona kulikuwa na lawama ambayo imetoka kwenye Kamati kwamba inasema Waziri mwenye dhamana ya Mifugo ajitadhmini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sioni sehemu yoyote katika taarifa hii ambayo imeletwa na Kamati ambayo inamu-*implicate* kwa njia yoyote ile Waziri wa Mifugo. Kwanza ni Wizara ambayo tulitengea fedha kidogo sana katika Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii iliomba Shilingi bilioni 193 kwenye Bajeti ambayo tunaendelea nayo. Lakini kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ilikuwa ni Shilingi bilioni 48 tu. Lakini baada ya kulialia na kupiga kelele kwamba fedha ni kidogo, na kwa unyeti wa mifugo ambayo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. M. J. OPULUKWAJ]*

wananchi wanayo, Bunge hili Tukufu likaridhia kwamba tuongeze Shilingi bilioni 20, kwa hiyo, Bajeti ya Wizara ikawa ni Shilingi bilioni 68. Katika Bajeti hii, fedha ya maendeleo tulyoidhinisha katika Bunge hili ilikuwa ni Shilingi bilioni 28, lakini fedha ambayo imeshatoka mpaka leo tunapoongea katika Bunge hili Tukufu ni Shilingi bilioni tatu tu. Leo hii tunataka kumsulubu Mheshimiwa Waziri wa Mifugo eti kwamba hafanyi kazi. Kazi gani ambayo atafanya bila kuwa na fedha ya kuweza kufanya kazi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilitegemea, wakati ambapo Kiti chako kinatoa maelekezo kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwenda kufanya uchunguzi, ingelikuwa ni sambamba na Wizara yenyeye dhamana ambayo ni Wizara ya Mifugo, ili nao waweze kujiridhisha kwa sababu walioumizwa na mifugo iliyokufa iko chini ya Wizara ambayo ni ya mifugo. Lakini Wizara hii tukaicha. Leo hii Kamati inakuja na kusema kwamba eti Wizara hii imeonekana kwamba ilikuwa haifanyi kazi na hivyo iweze kujitathmini. Hakuna cha kujitathmini hapa! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hili kuna watuhumiwa watatu wakubwa. Mimi sitaki kufika kwa Waziri Mkuu. Mtuhumiwa wa kwanza ni Wizara ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Kama kuna mahali katika nchi hii ambapo wananchi wameteseka sana, na hasa wafugaji, na mateso haya yamesababishwa ama yameletwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wanahangaishwa na faini ambazo zinatozwa kwenye maeneo ambayo wanasesma wameingia katika maeneo ya hifadhi; wananchi hawa wamekuwa wakikamatwa na kubambikiziwa kesi ambazo nyingi hazina msingi. Nimekwenda kwenye Gereza la Maswa, ambapo nimekuta kulikuwa kuna wafungwa kama 210 hivi. Katika hao wafungwa zaidi ya asilimia 90 ya wafungwa hawa, ni wale ambao eti wana makosa yanayotokana na kukutwa aidha kwenye hifadhi, ama kubambikiziwa nyara, na kesi za

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. J. OPULUKWA]

kusingiziwa. Hii ni kwa sababu ya Wizara ya Maliasili na Utalii.  
(*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna faini nyingi sana ambazo haziko hata katika Sheria ya Wanyamapor, ambazo zinatozwa na Wizara hii. Kwa mfano, nilikuwa najaribu kunukuu baadhi tu ya faini ambazo zimekuwa zikitozwa na Wizara ambayo iko chini ya Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki. Kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, kuna bwana mmoja anaitwa Kidwida Kwiyela, ambaye eti alilingiza ng'ombe kwenye hifadhi na akatozwa Sh.13,500,000/=, ambayo haipo kabisa hata kwenye sheria zetu za Wanyamapor. Tukio hili lilitokea tarehe 27 Oktoba, 2013. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiacha hilo, naambiwa kwenye Halmashauri ya Same, kuna mtu anaitwa John Msofe, eti alilingiza mifugo ndani ya Msitu wa Vumari, akatozwa faini ya Sh. 6,850,000/= tarehe 24 Julai, 2013. Najaribu kutoa mifano au picha kidogo ili angalau uweze kuona jinsi gani Wizarsa hii ilivyoza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mfano mwengine wa tatu ambaao ni wa mwisho kwa uchache, kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, kuna bwana ambaye ni mfugaji anayeitwa Ndula Mihambo; tarehe 9 Oktoba, 2013 alitozwa faini ya Sh. 5,500,000/= eti kwa kuingiza mifugo ndani ya hifadhi. Tunawapeleka wapi Watanzania hawa?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwa sababu kuna watuhumiwa, nambari moja Wizara ya Maliasili na Utalii; Namba mbili, ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na nambari tatu, ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hizi ndizo Wizara ambazo kwa kweli zimesababisha maafa yote haya ambayo yamekuwa yakiendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi, katika kitabu hiki ambacho ni Taarifa ya Kamati, tnaambiwa kati ya yale makundi ambayo yaliyohusika ni pamoja na Mahakimu, kwamba kulikuwa na Mahakimu 100 ambaao walikuwa nao

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. M. J. OPULUKWAJ]*

ni miongoni mwa hawa watu waliokuwa wanaendesha zoezi hili. Mimi nataka kufahamu; hivi hawa Mahakimu 100, maana yake ni kwamba alikuwa anakamatwa mfugaji, anapelekwa kwa Hakimu; Hakimu anaambiwa sasa wewe kwa sababu ndiyo kazi ya Mahakimu hii, kutoa hukumu; anatoa hukumu kwamba wewe nadhani adhabu yako itakuwa ni kutembea na mnyama aliyekufa; wewe ni kutembea na huu mti mkavu; na wewe lazima ubakwe mbele ya watoto wako wakikuangalia. Hii ndiyo kazi ya Mahakimu? Mimi nadhani labda ilikuwa ni kazi hiyo, kwa sababu sioni mahali popote ambapo Mahakimu hao wangeliweza kuingia kwenye *operation* hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa utaratibu wa kisheria, kama kuna mtu ana kosa, kama kuna mtuhumiwa, atapelekwa Mahakamani; Mahakama ile itakaa; mashahidi watapelekwa, kesi itasikillizwa, mwisho wa siku hukumu itatolewa. Lakini sasa kulikuwa na Mahakama za porini; Mahakama za chini ya miembe; Makama za msituni; wanakamatwa watu; Jeshi linakamata watu, na kuwapeleka pale, Hakimu anahukumu, watu wanashughulikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo yanaudhi na yanakera sana yanayofanywa na Serikali yetu. Sitaki kusema kwamba ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi; ni Serikali yetu kwa sababu ndiyo wenye dhamana ambayo tumewapatia wawze katuongoza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na *operation* hii kuzuiliwa, kwamba sasa tumevida *stop* ili uchunguzi uweze kufanyika; lakini kuna *operation* ambayo ninaiita ni *min-operation* iliyoanza kufanyika tena kwenye Wilaya ya Meatu mwanzoni mwa mwezi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Simiyu iliagiza *operation* ifanyike kwenye Wilaya ya Meatu, kwenye kijiji cha Lukale, pamoja na Bukundi. *Operation* hii imefanyika watu wamekamatwa, na watu wamefunguliwa kesi. Lakini kibaya zaidi, mtoto mmoja wa miaka saba na miaka minane, walifunguliwa kesi na kuwekwa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. M. J. OPULKWA]

*lock-up* zaidi ya siku tatu, eti kwamba mpaka baba zao waje, au wazazi wao waje ili wale wafungwa waweze kubadilishana. Kwamba mtoto atolewe ili baba yake aingizwe ndani. Kesi hii ni nambari 932 ya mwaka 2013. Watoto hawa mmoja anaitwa Gida Juli wa miaka minane, pamoja na Makumbi Gida Hasi wa miaka saba.

Mheshimiwa Spika, nitapenda angalau uweze kupata picha hii kwenye meza yako ili angalau uweze kuona jinsi gani Serikali hii inatufikisha mahali ambapo siyo pazuri.

*(Hapa picha husika ilioneshwa Bungeni  
na Mzungumzaji)*

**MHE. MESHACK J. OPULKWA:** Mheshimiwa Spika, alikamatwa katika *operation* hii hii Mzee wetu tunayemheshimu sana, Mheshimiwa Jeremiah Mbulyambate aliyekuwa Mbunge katika Bunge hili Tukufu kwa kipindi kilichopita. Mzee huyu aliyofanyiwa ni mambo mabaya sana. Kwanza alipelekwa kusikojulikana kwa muda upatao siku tatu. Watoto wake walimtafuta, wakilia baba yetu amekwenda wapi? Lakini haya ambayo Mzee Jeremiah Mulyambate yaliyo mpata...

*(Hapa Kengele illilia Kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ni kengele ya pili.

**MHE. MESHACK J. OPULKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Anne Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Muhammad Chomboh.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni kiongozi mwanamke, Mbunge wa Jimbo mwanamke. Nina uhakika viongozi wote wanawake waliomo humu ndani leo wanapata uchungu sana. Kwa sababu sisi akinamama tunazaa. Yaliyowapata hawa wananchi wetu ambao wametupigia kura sisi, tumewazaa sisi.

Kwa hiyo, tunapata uchungu. Nawaomba Watanzania waelewe, kwamba hili jambo limetuumiza Wabunge wote. Hakuna Mbunge hata mmoja humu ndani, bila ya kujali itikadi yake, ambaye hili jambo limemfurahisha. Asije akatokea mtu akadhania yeye labda ndiye aliyeumia zaidi, ni Wabunge wote tumeumia roho zetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hapa ndani ya Bunge kuna Wabunge na kuna Serikali. Wote tuko humu ndani. Naomba Waheshimiwa Wabunge kwanza, niwaombe radhi Watanzania wote ambao wameumia, ambao hata wamepoteza maisha yao, ni kweli hawawezi kunisikia. Niwaombe radhi, kwamba matendo haya yamefanywa na Watendaji wa Serikali yangu mimi. Siwezi kusema vinginevyo. Ni Watendaji. (*Makofî*)

Naomba nikubali kweli, nilisimama siku 70, nikaomba kura, Chama changu kikashinda, lakini haya yametokea; lakini Mwenyezi Mungu anajua kwa nini yametokea. Naomba nianze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu mlioko hapa ndani, wote sisi ni viongozi. Wote sisi hapa ndani ni Viongozi. Naomba kwa ruhusa yako nimnukuu, Marehemu Baba wa Afrika, Mheshimiwa Nelson Mandela alisema nini wakati wa uhawake. Lakini ninazungumza kwa ajili ya wenzangu wote. Sisi ni viongozi, hili limetokea. Alisema hivi, ninaolmba nimnukuu:

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. A. K. MALECEL]

"Kinachohesabika siyo tu ukweli kwamba tulishi. Bali ni ile tofauti tulioileta kwa maisha ya wengine, ndiyo inayoleta maana ya maisha tulioishi." Naomba kurudia. Marehemu Nelson Mandela alisema: "Kinachohesabika siyo tu ukweli kwamba tulishi, bali ni ile tofauti tulioileta kwa maisha ya wengine ndiyo inayoleta maana ya maisha tulioishi." (Makof)

Mheshimiwa Spika, viongozi wote tuliko hapa ndani, tuna makosa katika hili. Ndiyo! Wabunge tunayo makosa yetu, kwa sababu kuna Wabunge wametajwa hapa! Itabidi Kamati tunawasihi sana...

**WABUNGE:** Aaah!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muwe mnasikiliza kwanza. Kama hauna kosa si usikilize?

**MHE. ANNE K. MALECEL:** Tunawasihi Kamati, wale wenzenetu Wabunge mliowasema, kwamba kuna Wabunge waliohusika na Madiwani wamehusika, watajwe kwa majina. Ndiyo maana nasema kuna Wabunge wamehusika. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kitu kimoja. Tangu tumepata uhuru, hili jambo ni baya tukubali. Hili jambo ni baya sana!

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliohusika, ni lazima na sisi tuje kwamba tutachukuliwa hatua. Hatuachwi hivi! Ni lazima tuchukuliwe hatua! (Makof)

Mheshimiwa Spika, hili jambo linatia taabu. Linaumiza roho! Wananchi wetu wameteswa, wameumizwa,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. K. MALECELA]

wameuwawa, mifugo imeuawa, mpaka sasa hivi kichwani kuna kitu kinanisumbua; hili jambo limetokea wapi? Ina maana kuna mahali hatukuwa makini. Kuna mahali hatukuwa makini sisi wote. Ndiyo! Kuna mahali hatukuwa makini! Kuna siku nilisimama hapa Bungeni nikasema, Waheshimiwa Wabunge tunafanya kazi? Niliuliza hapa, tunafanya kazi?

Mheshimiwa Spika, kule Jimboni kwangu kuna wafugaji na wakulima. Lakini mimi sisemi uwongo na wala sijisifu; migogoro ya wakulima na wafugaji huwa nakwenda nikiwa kama Mbunge. Nakwenda huko kwenye matukio nakaa na wafugaji, nakaa na wakulima, naangalia ule mgogoro umetokea wapi, najaribu kuongea na wakulima na wafugaji wangu.

Kwa hiyo, hata sisi, hili la kukaa na kuangalia kule wananchi wetu walipo ni *responsibility* yetu. Ni *responsibility* yetu na sisi kwenda kuangalia hii migogoro tukiwa kama viongozi. Kama viongozi, Serikali inafanya, lakini na sisi Wabunge, mbona na mimi nafanya mara nydingi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninalo eneo la Nadururu. Eneo la Nadururu ni la wafugaji watupu, lakini wapo pamoja na wakulima, kila siku migogoro nakwenda. Lakini tuseme ukweli, Serikali yangu ni lazima sasa tuone kwamba matatizo ni makubwa kuliko tulivyokuwa tunayasikia. Sasa ni wazi matatizo ni makubwa kuliko tulivyokuwa tunayasikia! Serikali inabidi ichukuliwe hatua kubwa sana kuanzia leo, siyo kuanzia kesho. Serikali inabidi ichukuliwe hatua kubwa sana ili turudishe matumaini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, lazima turudishe matumaini kwa wananchi wetu. Hatua gani itachukuliwa? Hiyo hatua itabidi ichukuliwe leo. Ichukuliwe leo! Tunafanyaje? Hatua gani inachukuliwa? Ichukuliwe leo! (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ANNE K. MALECELÀ]

Mheshimiwa Spika, kitu kinaanza kidogokidogo, hili jambo lilianza kidogokidogo sana, hakuna kitu kizuri kama kuchukua tahadhali. Sisi akina mama tunaambiwa ni waoga lakini siyo waoga, akina mama wanajua kuchukua tahadhali sana. Mama ukiona kitu kidogo unastuka unachukua tahadhali, ndivyo tunavyoishi sisi, ndivyo Viongozi Wanawake tunavyoishi. Nawasihi Serikali, mmechelewa kuchukua tahadhali. Ilipoanza kidogo mkaona ni kitu kidogo, siku zote kidogo ndiyo kinachozaa kikubwa. Leo tupo na kitu kikubwa humu lakini kilianza kidogokidogo. Sasa Serikali ni lazima leo hii kabla ya kesho muwaoneshe Wananchi kwamba, mmechukua hatua, mmerekebisha leo hii. (*Makof!*)

Naipongeza sana Kamati na ninaiunga mkono Taarifa yenu yote, lakini itabidi muwataje na hao Wabunge. Lazima muwataje na hao Wabunge humu ndani ili isiwe kila wakati sisi Wabunge tunainyooshea kidole Serikali. Naomba hao Wabunge watajwe hapa ili nao tuwasulubu. Ndiyo maana ninasema japo mnakataa kwamba hapana, no, wote humu ndani hatukufanya kazi iliyostahili. Tulipaswa kuona haya matatizo na kuwachukulia hatua wote kwa pamoja. Wabunge pamoja na Madiwani wote hawa ambaao ni Wanasiasa wenzetu, ambaao wameingia kwenye hii shughuli, nao watajwe humu ndani, maana sasa hivi tunaongelea Wizara tu na Wabunge tunataka kuwajua. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Ripoti ya Kamati, mmefanya kazi kwa muda mfupi sana, mmegundua mengi lakini nina uhakika kama wenzangu wanavyosema, mlikwenda kasehemu kadogo kwa sababu muda ulikuwa mdogo. Ina maana mngekwenda nchi nzima, tunegundua mambo makubwa sana. (*Makof!*)

Kwa haya tuliyoyagundua, Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwa unyenyekevu sana, kesho tuone kuna mabadiliko. Mjirekebise mahali na Watanzania waone Serikali imejirekebisha, imerekebisha haya mambo, maana wale waliokaa kule juu ni wafugaji, kilichowaleta ni kutaka

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. ANNE K. MALECELÀ]

kujua tunafanya nini. Kwa nini wamekaa pale juu?  
Wanatusikiliza sisi Wawakilishi wao hili jambo tumelichukuliaje.

Naomba niwahakikishie Watanzania wote huko mliko kwamba, Wabunge wote humu ndani tumeumia sana tena tunaona aibu. Tumeumia, tunaona aibu, lakini tunaomba tuwahakikishie kwamba, hii *situation tutai-handle* haraka iwezekanavyo na tutarekebisha yote ambayo hatukuyafurahia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru na naunga mkono Ripoti ya Kamati na marekebisho tutaleta ili tusaidie tufike mahali tuwe na Azimio moja kama Wabunge na hakuna mambo ya kusema chama hapa; katika hili ni Wabunge wote tumeumia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Kamati. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Muhammad Chomboh, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kamani!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi hii jioni ya leo.

Ningeanza ku-declare *interest* kwamba, mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati ya watu tisa waliotembelea mikoa mbalimbali kwenda kubaini kilichotokea katika Operesheni Tokomeza. Mimi nilipangipa Mkoa wa Pwani, Morogoro, Iringa, Ruvuma na Mtwara. Kati ya yaliyotajwa ndani ya Taarifa yetu ya leo, mengine ni mimi mwenyewe nimeyashuhudia kwa macho yangu, kwa maana ya kuwahoji na kuwasikiliza wahanga wa kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, nimejifunza mengi katika ziara yangu hiyo, lakini pia nimeona mambo mengi sana. Kwanza, nilicho jifunza ni kwamba, Operesheni Tokomeza, Watanzania wote katika sehemu niliyopitia wanaiafiki kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH]

masilahi ya kulinda rasilimali za nchi yetu, lakini wanailaani sana kwa namna ilivyotekelawa.

Katika kupata mawazo mengi na kujifunza mengi kwa Wananchi, kuna jambo moja nililoligundua kwamba, Operesheni Tokomeza pamoja na mipango yote iliyopangwa, haikuwa imetayarishwa au wametayarishwa watekelezaji, kwanza, kisaikolojia, lakini pia kimafunzo kwamba, wanatakiwa wakafanye nini. Walikurupushwa wakakurupuka kila mmoja ana lake na kila mmoja ana mategemeo yake katika hili. Hicho ndicho kilichosababisha yatokee haya, kwa sababu katika sehemu zote tulizofika, kila mmoja anayetuambia hivi, anayetueleza na hasa wale Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama, tukiwaliza mmeshirikishwaje katika Operesheni hii, wanasema hawajashirikishwa wala hawana habari. (*Makofi*)

Walisema kwa mujibu wa walivyokuwa wanasikia kutoka kwa wale waliotheswa ni kwamba, hakukuwa na weledi wa Kiaskari hasa kama Polisi amba ni mahususi kwa *interrogation* au kwa usaili wa kukamatwa au namna ya kusachi ilikuwa ni vurugu tu. Sasa hakukuwa na matayarisho au maandalizi maalumu katika Operesheni hii na hicho ndicho kilichosababisha uvunjifu wa haki za binadamu, watu kuteswa na kuadhibiwa mpaka ikafikia hatua ya watu kupoteza maisha yao.

Naiomba Serikali kwanza cha muhimu kabisa pamoja na yote haya, baada ya kutegemea Operesheni Tokomeza irudi mara moja, lakini kwa njia ambayo wale washiriki au watekelezaji lazima wapate mafunzo na maelekezo thabiti wakafanye nini. Hapo tunaweza tukafanikiwa; kwa sababu hivi tunavyoongea na wakati ule tupo katika *field*, bado ndovu walikuwa wanaendelea kuuawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuja jambo lingine sasa, wanasema kwenye msafara wa mamba na kenge wamo. Kuna mambo mengine yalijitokeza kwa hujuma za kisiasa na kibashara, hayo yote tuliyabaini. Kuna watu

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH]*

walichomeana, fulani anahusika kwa sababu ya wivu wa kibiasara na wengine kwa wivu wa kiuchumi au kisiasa, tumeyabaini! Kwelli, wapo majangili na wapo wanaohusika, lakini walijitokeza na watu wengine. Inabidi kabla hajachukuliwa hatua ya kurudia tena Operesheni Tokomeza, kuwe na habari za kiintelijensia ambazo zina uhakika, waondoke watu wa kwenda kufanya kitu fulani, mahali fulani na kumshika mtu fulani, tutafanikiwa. (*Makof*)

Tumezungumza sana na Waheshimiwa Wabunge, wamezungumza sana namna mifugo ilivyozungumzwa. Tulyapata pia si ya mifugo tu hasa katika Mkoa wa Morogoro, Wakulima pia. Haikuwa kazi yetu sisi kutafuta matatizo ya wakulima na wafugaji, lakini Wizara yetu pia ilikuwa inahusika na mambo ya ardhi na maliasili.

Kuna matatizo baina ya wafugaji na wakulima, nafikiri wenzangu walioko kwenye Kamati Teule watakuja kutoa maelezo. Wakulima na wao sijaona kama kuna mtu anawasemea, lakini wanateseka sana na wafugaji. Mkulima analima kwa msimu mwaka mpaka mwaka, lakini mfugaji anaweza akaingiza ng'ombe zake 1,000 au 2,000, kucha moja tu asubuhi hakuna kitu, matokeo yake wanapigana wanauana. Yametokea na mtayasikia Kamati itakapokuja kuwasilisha. (*Makof*)

Mimi nimeyakuta Morogoro, nimeona na hili niliseme na wakulima nao sijaona chama cha wakulima hapa kuja lakini na wakulima pia. Mimi siyo mfugaji ni mkulima, nawazungumzia wakulima wenzangu maana wafugaji wamewazungumzia wafugaji wenzao hapa, nalo ni lazima tulitafakari, Kamati itakuja kutoa Ripoti yake.

Cha msingi zaidi, mateso yaliyotokea na vitendo vilivyotokea, havikuwa vya kiungwana kabisa. Mfumo wa Serikali kwa kiasi kikubwa sana tutawasulubu Mawaziri, watakuja hawa na wengine, lakini kama Serikali hajabadilisha mfumo wake wa Mawaziri kuwapa kilemba cha ukoka, kule kwetu tunaita kilemba cha ukoka na kilemba cha ukoka kazi yake ni kubebba mzigo wa kuni,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH]

siyo cha kuhukumu mambo. Tunawapa hapa kilemba cha kubeba mzigo wa kuni tu wewe Waziri lakini mambo yote yanaamuliwa na Watendaji na wanaamua bila kumshauri Waziri. Wanathhubutu kusema, wewe aliyekuchagua Rais na mimi nimeteuliwa na Rais; tena nini? Ndiyo hapa tulipofikia!

Ndugu zangu, tukae tukatafakari, watakaoondoka wataondoka na watakaobaki watabaki, lakini tujue Serikali ina wajibu wa kufumua mfumo mzima wa utekelezaji. Tunapiga kelele, haya yametokea kwa sababu kuna mauaji, lakini ubadhirifu, wizi na kila kitu, ni mambo ambayo yanatekelezwa na Watendaji siyo Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamani, atafuatiwa na ...

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika kuhusu nini?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, hii hoja ni muhimu sana na wakati inaendelea, Mawaziri wote ambaao ni *concerned* hayupo hata mmoja hapa, hii inaashiria kama ni dharau kubwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Dkt. Kamani!

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami ya kuchangia katika mada iliyopo hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapa pole Watanzania wote waliofikwa na mawaha yaliyotokea wiki chache zilizopita. Pia naungana na waliovaa nguo nyeusi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]*

na mimi nimevaa nguo nyeusi, nikiwa pamoja nao, mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, lakini nataka kuonesha kwamba na Chama changu kimeguswa kwa haya yaliyotokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vilevile kuwapa pole watu wangu wa Jimbo la Busega, Mzee Nanai na wenzake, ambao walilazwa kwenye matope kwa sababu ya kutafuta ukweli juu ya mambo yanayotokea. Hii ni kwa sababu watu hawakuwa na taarifa za kutosha, lakini na watu wa Mkoa wa Simiyu kwa ujumla.

Nitaomba nipate ufanuzi wakati Watendaji wa Serikali au Mwenyekiti wa Kamati anapo jumuisha, Serikali ilipotoa tamko kwamba, Operesheni imesitishwa, mbona ng'ombe bado wameendelea kushikiliwa kwenye maeneo ya hifadhi mpaka sasa hivi? Ilimaanisha nini hiyo kusitisha Operesheni? Nataka kupata ufanuzi juu ya hilo. (*Makofii*)

Vilevile ninapenda Bunge lako na Watanzania kwa ujumla, wafahamu kwamba, hili tunalozungumzia ni jambo moja baya limetokea, lakini haimaanishi kwamba, Serikali inafanya mambo yote mabaya. Jana na juzi tulikuwa tunazungumza na kusifia mambo mazuri ya kuweka umeme, ya Miradi mbalimbali ya Ujenzi wa Barabara na kadhalika. Hili ni baya limechafua, lakini bado kuna mambo mengine mazuri na ninaomba hili lishughulikiwe kwa sifa yake kama lilivyojiteza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo nisingependa kulalamika sana kama nilivyolalamika siku ya kwanza tulipochangia suala hili lilipotokea, kwa sababu lilikuwa linaleta uchungu mkubwa sana. Leo ninapenda nitoe ushauri kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yake, kwa jinsi walivyofanya utafiti na kutuletea Taarifa ambayo tunajidili hapa. Jambo moja kama halikuwekwa kwenye mapendekezo na Serikali ikalichukua, tatizo hili litaendelea kujitoneza. Jibu la uhakika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]

Ia kupunguza migogoro kati ya wafugaji na maeneo ya hifadhi na wakulima ni kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyetu na maeneo yetu ya makazi. Sijalionia hili likijitokeza barabara kwenye mapendekezo ya Kamati, kwa sababu tutatoa suluhisho la sasa hivi tu lakini litajirudia. (*Makofi*)

Wanyamapori wana maeneo yao yaliyobainishwa, kuna Hifadhi za Taifa, kuna Mapori ya Akiba, yanatambulika kisheria, lakini hakuna maeneo yanayotambulika kisheria ya wafugaji. Sasa hawa wanaingiliwa na wakulima; wao wanakwenda wapi? Ndiyo maana migogoro hii inatokea. Kwa hiyo, ninapenda kushauri kwamba, mifugo iwekewe maeneo na iwe katika mpango wa matumizi bora ya ardhi ili maeneo ya kilimo yabainike, ya mifugo yaeleweke, ya makazi, ya hifadhi na kadhalika. Mkishaweka mpango bora wa matumizi bora ya ardhi, *automatic* watu wataangalla uwezo wa eneo lile kubeba mifugo kiasi gani, kwa sababu huwezi kuzidisha zaidi ya uwezo wa eneo lililopo; vinginevyo, utaenda kuharibu, tutakuwa tunahamahama. (*Makofi*)

Wizara ya Mifugo haijapata rasilimali za kutosha au Sekta ya Mifugo haijapata rasilimali za kutosha kushughulikia matatizo ya wafugaji. Sasa tunazima moto, lakini bila kujielekeza kwenye hoja za msingi za mahitaji ya mifugo, za malisho, za mabwawa, za majosho na huduma za ugani, tatizo hili litaendelea kujitokeza, kwa sababu wafugaji watakuwa wanatafuta majibu wao wenywewe na majibu ya malisho ni kwenda ndani ya hifadhi, kwa sababu Serikali haijawawekea mazingira sahihi. Kwa hiyo, hili nilitaka kutoa ushauri kwa Serikali yetu ili iangalie njia ya muda mrefu ya kumaliza tatizo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, nchi yetu na shughuli za uhifadhi haziwezi kuwa zinaendeshwa kwa Operesheni kwa sababu kazi ya kuhifadhi wanyamapori ni ya kudumu; inakuwaje tunalazimika tufikie kwenye Operesheni? Hii ina maana tumeachia udhaifu umeendelea kujengeka kwa muda mrefu mpaka inafikia sasa hauvezekani tena tunaitisha Operesheni. Hii siyo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]*

namna nzuri ya uendeshaji wa shughuli za Serikali na namna nzuri ya kuendesha shughuli za uhifadhi. (*Makofii*)

Wakati ule akiwa Waziri Mheshimiwa Maige, alisema Serikali imekubali kutoa ajira mpya za askari wa wanyama pori 2,000, kwa sababu Wizara ilikuwa inalalamika haina watumishi na haina maaskari. Leo sijui ni miaka miwili au mitatu, sijaona askari hawa wanaajiriwa; tunategemeaje kuyalinda hayo maeneo ya hifadhi? Kwa nini hakuna Watumishi wa kutosha na sisi tunaangalia maeneo hayawezi yakajilinda? Kwa nini hawana magari, kwa nini hawana vionambali vyta kuweza kubaini majangili mapema? Hili nafikiri ni tatizo ambalo limeachwa limeendelea kukua na hatimaye tumefika kwenye mgogoro mkubwa kama huu.

Kwenye Mapendeleko ya Kamati wamesema Kikosi Dhidi ya Ujangili ni dhaifu kinahitaji kuundwa upya. Kwa nini kimeachiwa mpaka kikafikia hatua hiyo? Haya ni mambo ambayo lazima yaangaliwe.

Kuna wakati Wizara walisema wanataka kutengeneza *agency*, taasisi maalum kwa ajili ya kusimamia Mapori ya Akiba. Juzi nimesikia Mheshimiwa Rais, ameshasitisha tena kuanzisha hizi *agency*. Kwa nini imechelewa muda wote kama kuhifadhi haya maeneo ni muhimu kwa kiasi hiki?

Ningependa nishauri kwamba, kama hii shughuli inabaki ndani ya Idara, iwezeshwe Idara hiyo kusimamia vizuri.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, mwelekeo wa Wananchi sasa hivi ni kujenga chuki dhidi ya wanyama pori na wanyama pori ni rasilimali muhimu sana kwa Taifa letu kwa sababu ya utalii na kwa sababu ya wajibu mwininge tu, Mungu aliumba binadamu waishi pamoja na wanyama, hakuumba dunia hii ya binadamu peke yake. Mwelekeo na huduma zinazoelekezwa kwa nguvu zaidi kulinda wanyama pori, inafanya Wananchi wajenge hasira kwamba

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]

kwa nini wanyama pori wanapewa umuhimu wa pekee kuliko watu. Sasa hii siyo picha nzuri. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mimi ninapendekeza kama ilivyopendekezwa na wazungumzaji wengine, Wananchi walioathirika wapewe fidia au kifuta machozi ili watu warejeshe miyo kwamba, Serikali inawasikiliza. Hivi sasa kuna tatizo kubwa la wanyamapori kuingia maeneo ya Wananchi kuharibu mazao. Jimboni kwangu sasa ni lugha ya kilaa siku ndovu kuingia na kuharibu mashamba ya Wananchi, lakini nguvu inayotoka upande wa Serikali kuwasaidia na kuwalinda hawa watu siyo ya uzito ule ule kama ambayyo wanyamapori wakiathiriwa na watu. Hii ndiyo inayojenga chuki, siyo vizuri, wote wapewe uwiano sawa; ni muhimu sana kuwa na wanyamapori kwa sababu ni wa muhimu katika Uchumi wa Taifa letu, tunapata watalii, lakini inatupa heshima kwamba tunawajibika katika kulinda rasilimali za Dunia; lakini wanadamu wasiwe wahanga wa kuumia kwa sababu wanalinda wanyamaporii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, imeelezwa kwamba, kwenye Operesheni hii kulikuwa na Mahakama. Nimeshangaanamna gani wafugaji walikuwa wanakamatwa pale pale na wanahukumiwa pale pale, wakati siku zingine, nyakati zingine, watu wa hifadhi wanakamata majangili, wanakamata watu wenye nyara, wakipelekwa Mahakamani kesi zinakaa miaka saba, miaka mingapi hazijaisha. Hii Mahakama Kuu inaona wafugaji tu, hii Mahakama huwa haioni watu wanaohujumu nyara za Taifa; meno ya tembo yanakamatwa kesi haina mwisho?

Mapolisi wamekamatwa wanasindikiza hata sijasikia kama wamefutwa kazi! Sasa hii Mahakama uhuru wake umekuwa haiguswi? Mahakama hii imekuwa ni Serikali yake? Hili ni eneo ambalo sijui kwa sababu sisi ni Bunge, huu uhuru wa Mahakama mbona unaangalia eneo moja tu, wafugaji wanapigwa faini mara moja, lakini wezi wa Nyara za Taifa, askari wanafanya kazi nzuri ya kulinda lakini hata wakikamata kesi inazungushwa hatimaye hati

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. DKT. TITUS M. KAMANI]*

inapotea bila mwelekeo. Sasa nilifikiri kwamba, hiki chombo lazima kiangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lote hili limegusa Watanzania wengi sana, limeibua hisia nydingi sana za Uchumi na ni Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ndio iliyosimamia Operesheni hii. Serikali ni ya Chama cha Siasa, nilifikiri ni vizuri sana kuangalia kwa sababu tunaendesha Siasa, tuangalie Chama cha Mapinduzi kijangalie katika mazingira haya tunaifanyaje siasa ili tuendelee kuwa na uhalali? Tunaweza tukapakapaka mafuta, lakini lazima tuangalie tutaingia kwenye Uchaguzi, lazima tujiangalie sifa yetu tunasimama imara namna gani, tunawalinda namna gani Watanzania wetu na tunawajali kiasi gani. Lazima tuwafariji tuonekane tuko pamoja nao. Nami nashukuru kwamba, hapa Wabunge wote wamezungumza vizuri kwa sababu tunataka tuwafariji Watanzania.

Kingine, nashukuru Mamlaka hizi za Hifadhi kuna wakati mwininge zinachukua juhudzi za makusudi kupunguza migogoro. Eneo langu karibu mwambao mkubwa sana ninapakana na maeneo ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Tunapozungumza miundombinu ya mifugo, tunapata tabu kupata msaada hata kutoka Wizara inayowaka na mifugo, lakini watu hawa wa Wanyamapori wanasaadilia ili kupunguza migogoro. Kulikuwa na migogoro kwangu lakini haikuwa mikubwa kama katika maeneo mengine. Kwa hili ningependa *spirit* hii iendelezwe kwa maeneo yote katika nchi hii ili Taifa liendelee kuwa na amani.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, atafuatiwa na Mheshimiwa Murji!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa nami kuchangia hoja hii. Naomba nianze kwa kusema kwamba, kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu, mtumishi anapofanya makosa, makosa hayo yanahesabika kuwa ni makosa ya mtumishi na makosa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

ya mwajiri wake. Kwa hiyo, Watumishi wa Serikali; Askari Polisi, Magereza, Wanyamapori na Askari Jeshi, wanapotumwa kwenda kufanya kazi wakaenda kuua, kisheria wanahesabika kuwa wao kama watumishi wameua na mwajiri wao Serikali iliyowatuma imeua. (*Makofii*)

Ukitaka kushitaki ili ulipwe fidia unamshitaki huyo aliyebeba bunduki akapiga risasi, unamshitaki na mwajiri wake aliyemtuma akampa na hiyo bunduki. Kwa hiyo, tafadhalii sana, tusiingize hoja zisizokuwa na mashiko hapa kwamba, haya mambo hayajafanywa na Serikali. Serikali ndio hao Wanajeshi walioua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, si mara ya kwanza kwa nchi yetu kupata janga la aina hii. Miaka karibu 40 iliyopita, mwaka 1976, Jeshi la Polisi walitumwa kwenda kukamata watu waliokuwa wanashukuliwa kuwa wachawi Mkoo wa Shinyanga. Walienda Maaskari Polisi wakakamata Wanawake kwa Wanaume, Wazee, wakawatesa mateso mabaya kabisa, wengi wakauawa. Ilikuwa Serikali ya Chama kimoja wakati huo, Iakini taarifa zilipojulikana kwamba, Serikali na Vyombo vyake vimeua Watanzania, hatua zilichukuliwa, Waziri wa Mambo ya Ndani wakati huo Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Naibu wake Mheshimiwa Peter Siyovelwa na Mkuu wa Mkoo wa Shinyanga Mheshimiwa Peter Kisumu, waliwajibika. *Inspector General* wa Polisi, nafikiri Phillemon Mgaya, aliwajibika. Maaskari waliouwa walishaktiwa kwa mauaji. Ukiangalia Ripoti za Sheria za Tanzania kuna kesi maarufu sana inaitwa Jamhuri dhidi ya Elias Kigaja na wenzake, walishaktiwa kwa mauaji kwa kufanya kazi waliyotumwa na Serikali. (*Makofii*)

Tunapozungumza uwajibikaji, tuna maana hiyo. Wale wenye mamlaka kisiasa, Kiongozi wa Serikali humu ndani Bungeni, Waziri Mkuu, hayupo hapa awajibike; Waziri wa Ulinzi ambaye Jeshi lake limeua awajibike; Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye Mapolisi wake wameua awajibike; Mheshimiwa Kagasheki ambaye *Game Officers* wameua awajibike; Waziri anayehusika na Usalama wa Taifa, Mheshimiwa George Mkuchika asijifiche awajibike na

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

wale waliota amri na waliozitekeleza wawajike kijinai kama Elias Kigaja na wenzake walivyowajibika. (*Makofii*)

Huo ndiyo utaratibu wa nchi hii na rekodi ni ya karibu miaka 40. Haitakuwa halali, hatutaeleweka kama nchi, Bunge hili hili limemwajibisha Mheshimiwa Edward Lowassa na watu wake mwaka 2008, leo Watanzania wameuawa kwa amri ya Serikali, kwa bunduki za Serikali na Watumishi wa Serikali, Mheshimiwa Mizengo Pinda akaachwa aendelee kuwa Waziri Mkuu na Mawaziri waliohusika wakaachwa waendelee kuwa Mawaziri na wale waliotekeleza hizo amri wakaachwa kuendelea kutumikia kwenye Utumishi wa Umma; hatutaeleweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo tunahitaji bado Bunge lako Tukufu liyaangalie kwa makini. Taarifa ya Kamati inasema kwamba, Operesheni Tokomeza iliendeshwa Kijeshi, baada ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kutoa Amri Namba 001/13 juu ya utekelezaji wa Operesheni Tokomeza. Operesheni ya Kijeshi; tangu lini tuambiwe na kwa mujibu wa Sheria ipi Jeshi la Wananchi wa Tanzania linajihuisha na *law enforcement?* Tangu lini na kwa mujibu wa sheria ipi Wanajeshi waliofundishwa kupigana vita, ambao amri ya kwanza waliofundishwa ni ukilenga silaha lenga upige uee na kwa mujibu wa sheria ipi wameruhusiwa kwenda kufanya kazi za Kipolisi?

Mheshimiwa Spika, katiba yetu imeelekeza kwenye Ibara ya 32 na Ibara ya 44, mazingira ambayo Jeshi linaweza likaingia huku uraiani. Pale ambapo Rais ametangaza uwepo wa hali ya hatari (*state of emergency*), angalia Ibara ya 32(1) na (2); na pale ambapo Rais ametangaza uwepo wa hali ya vita. Hapo ndiyo unaweza ukaingiza Wanajeshi wa JWTZ. Kwenye Operesheni Tokomeza tuambiwe lini Rais alitangaza hali ya hatari; na lini alitangaza uwepo wa hali ya vita? Hilo hali ya hatari na hali ya vita ikitangazwa, ndani ya wiki mbili taarifa inaletwa Bungeni na Bunge lilitakiwa kuiridhia. Tuambiwe lini na kwa utaratibu gani Wanajeshi waliofundishwa kuua, waliofundishwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

kupigana vita, wameingia kwenye kazi ya law enforcement? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu, kwenye Ripoti hii inayosema kwamba, Operesheni iliendeshwa kivita, kulikuwa na amri ya Mkuu wa Majeshi. Hawa Wajumbe wa Kamati kwa nini hawakumhoji Mkuu wa Majeshi na kwa nini hawakumhoji Waziri wa Ulinzi nani aliyekuwa Kamanda wa Operesheni hii ya Kijeshi; kwa nini hamkumhoji na kwa nini hamumsemi?

Mheshimwa Spika, sote tulioko humu ndani tuliapa kuilinda, kuihifadhi na kuitetea Katiba hii. Katiba yetu inasema wazi katika Ibara ya 13(6)(a), ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha. Katiba hii inatamka kwenye Ibara ya 14, kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka katika jamii, hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria.

Ibara ya 15(2) inasema, itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo, isipokuwa tu kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria au katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na Mahakama. Ibara ya 16(1) inasema, kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake na pia kupata heshima ya hifadhi ya maskani yake.

Ibara ya 24(1) inasema, kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa Katiba. Ibara ya 24(2) inasema, ni marufuku kwa mtu ye yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au kwa madhumuni mengine yoyote bila idhini ya sheria ambayo itaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili. Matakwu yote haya ya Katiba yamekanyagwa kanyagwa na Serikali hii na Watumishi wa Serikali waliopewa amri ya kwenda kukamata majangili. (Makof)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. TUNDU A. M. LISSU]

Mheshimiwa Spika, kwa wanaonisikiliza, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo hapa, lakini Idara ya Mahakama, utaratibu gani wa kuwachukua Mahakimu kwenda kwenye Operesheni! Waziri wa Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mnapaswa kuwajibika au kuwajibishwa kwa hili. Haiwezekani Mahakama ikawa ni chombo cha kusaidia ukiukwaji wa Katiba wa aina hii. Tunahitaji uwajibikaji wa kisiasa Mawaziri na Mwanasheria Mkuu, tunahitaji hao Mahakimu waliokubali kukanyaga viapo vyao vya kutenda haki bila woga wala upendeleo, wafukuzwe kazi. (*Makofi*)

Namna pekee ya Serikali kurudisha heshima ni kufanya utakaso kwa kuwashughulikia wakosaji wote hawa niliowasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, hakuna kitu kinachoitwa kifuta machozi katika nchi hii katika sheria zetu. Mtu akikosewa, akiumizwa, akinyang'anywa mali, sheria zetu zinasema analipwa fidia inayostahili, ndivyo Katiba inavyosema. Habari ya watu kufutwa machozi, wanafutwa machozi kwa kulipwa fidia iliyotamkwa na sheria. Kwa hiyo, ndugu zangu tuachane na hii habari ya kifuta machozi, tudai watu wetu walioumizwa walipwe fidia.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nyigine kuna sheria inaitwa *posse comitatus*; ni marufuku kutumia Jeshi la Vita kwa *law enforcement*. Marufuku kutumia Majeshi yaliyofunzwa kuua watu vitani kwa shughuli za kiraia. Nimeona mapendekezo ya Kamati yanasesma Operesheni iendelee. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante, kengele ya pili. Leo umejitahidi kuongea kama Mwanasheria. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Agripina Buyogera!

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, mimi niliombia kuchangia Kilimo.

**SPIKA:** Ooh, basi wamechanganya majina na mwininge ameniambia hivyo hivyo. Mheshimiwa Buyogera!

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nikupongeze sana kwa ujasiri mkubwa ulioufanya wa kuunda Kamati na kuituma kazi ambayo inahalalisha na kuwaonesha Watanzania kazi na majukumu ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niseme, Waswahili wanasema, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, lakini ukweli unauma na ukweli ni wa Mungu. Kwa hiyo, leo ndugu zangu mnaoambiwa ukweli lazima uwaume, lakini ukweli ni wa Mungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini nasema haya? Tangu nimeingia Bungeni, kuanzia mwaka 2011 nimeanza kuzungumzia mambo mabaya na machafu yanayofanywa na watu wa Idara ya Maliasili katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, lakini hamkunisikiliza hata kidogo. Nimewahi kuzungumza humu nikasema ndugu zangu, nikiwa hapa Bungeni sitaki kufanya siasa, nipo kazini. Mimi ni mama, ninayoyaongea haya nyaongea kwa uchungu. Ameongea Mheshimiwa Mama Anne Kilango, haiwezekani mama unayejua uchungu wa kuzaa, ukashuhudia watu wanauawa katika Jimbo lako halafu ukakaa kimya. Serikali haikunisikiliza na haikunisaidia hata siku moja, lakini ukweli ni wa Mwenyezi Mungu leo mnaumbuka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kuwapa pole sana Watanzania wote waliopatwa na matatizo haya. Mimi nilidhani labda ni Jimboni kwangu tu, kumbe ni Watanzania walio wengi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA]

Nawapongeza sana Kamati, mmefanya kazi takatifu na yeote atakayewalaani, Mungu atawalipa. Malaika wa Mungu watawalinda wala msiogope, kwa sababu mmetenda haki. Ninayasema haya kwa sababu ninajua watu wetu jinsi tulivyo, binadamu tumezoea kusifiwa. Nadhani itakuwa ni Kamati ya Kwanza kuja kuanza kumwaga radhi hapa Bungeni kwa masilahi ya Watanzania. (Makof)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, wameyasema yaliyopatikana kule Kasulu. Ninarudia tena kuwapa pole wapiga kura wangu, nikianzia kule Kitanga alikouawa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji wa kupitia Chama cha Mapinduzi, ambaye ametajwa na Kamati. Pia Kamati hamkufika na wala hamkushirikisha Wananchi wa maeneo husika sijui ni kwa nini wakati Wajumbe walioenda Kasulu kule Kitanga wamepewa taarifa! Mheshimiwa Diwani kaambiya kuna Kamati inakuja huko, wakasubiri lakini baadaye wakapigwa simu kwamba, taarifa walizopipata kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama imewardhisha. Kwa hiyo, hilo lilinitia mashaka kidogo, naomba nishukuru kwamba, kwenye taarifa yenu mneyataja angalau yale machache yanatosha.

Mheshimiwa Spika, kitu kilichofanywa na Serikali hii ni kibaya sana. Kule Mvugo wameuawa Vijana, wakaona haitoshi watu wengine mpaka leo wanatafutwa wamepotea wanasema mama tulikuta majivu. Tunahisi wale watu baada ya kuona wameua watu wengi, wakaamua kupoteza ushahidi, wakakata miti na kuwachoma binadamu wenzetu. Kijiji cha Mvugo kule Jimboni kwangu. Kwa hiyo, nasema kwamba, wakati tunapopanga kulipa fidia, tuangalie sana hawa akina mama walobaki wajane huko vijijini baada ya waume zao kuuawa, watoto watasonaje. Serikali iwasomeshe. (Makof)

La pili, niungane na Mheshimiwa Kamani, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi; juzi tu baada ya Bunge kusitisha Operesheni hii, kule Kasulu chini ya usimamizi wa Mkuu wa Wilaya na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama, wameendesha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA]

Operesheni nydingine ambayo wameenda kufyeka mahindi ya wakulima zaidi ya ekari 80. Kwa hiyo, tunapojadili kwamba, Serikali ilipe fidia, hata hao wakulima nao muwaangalie; watasomeshaje watoto wakati mahindi yao yamefyekwa? (*Makof*)

Lingine, ninaomba Bunge lako Tukufu linisaidie, liagize Wizara ya Maliasili, wawasiliane na ndugu zao Mawakala wao kule Kasulu, zile baiskeli zote za walalahoi ambazo ndiyo shangingi za wapiga kura wangu, zilizofungiwa pale Idara ya Ujenzi, waruhusu walalahoi wakachukue baiskeli zao. Maana kama ni adhabu mmewapa, kipigo wamekipata, mahindi mmefyeka na baiskeli! Inauma sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wapo Wananchi kule Kasulu mpaka leo tunapozungumza wapo jela. Mkulima unamkamata eti amekwenda kulima kwenye hifadhi, unampeleka kwa Hakimu tena hata dhamana hakuna, anafika anawekwa miezi sita. Nikamwambia baba yangu Paulo wewe, Hakimu wa Wilaya ya Kasulu kwa nini usitumie hata hekima za kawaida; huyu mkulima hajawahi kuwa mwizi, hajawahi kuwa jambazi; leo unamkamata jela miezi sita; unamchanganya na majambazi unafundisha nini Taifa letu? Kwa hiyo, kuna vitu vya kuangalia kwa kina, lakini Serikali lazima ikae itulie na ijipange upya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumevida kelele hapa Mheshimiwa Danhi Makanga; Yesu wangu, Mheshimiwa Danhi Makanga alitoka Kibondo akalilia kuja Kasulu, kumbe alikuwa anajua Kasulu kuna dili. Leo amekuja kutuletea ukabila. Miaka yote tunaishi Kasulu hatujawahi kuwa na vita ya Wasukuma na Wakulima. Leo Mheshimiwa Danhi Makanga ametuchonganisha na wafugaji. Ninaongea wafugaji wako hapa wanansikiliza. (*Makof*)

Mimi ndiyo Mbunge wa Jimbo la Kasulu Vijiji na maeneo yote hayo yenyeye athari yako kwenye Jimbo langu. Nilikuwa naongea na Kiongozi wetu mmoja hapo, nikamwambia mmekosea, ninyi ndiyo mnasababisha hii vita. Wafugaji mnakuwa kundi la DC na Kamati ya Ulinzi na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA]

Usalama, Wakulima wanakuwa kundi la Mbunge; kuna utawala gani wa hivyo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ameongea ndugu yangu Mheshimiwa Anna Kilango, Mbunge wa Jimbo kama mimi. Niliwahi kumwomba Spika ruhusa mwaka 2012 tukiwa kwenye Kikao cha Bajeti, nikasema Bunge halikaliki, kule wakulima wangu wamezuiliwa kuvuna mazao. Nikaondoka hapa kwenda Jimboni, Mheshimiwa Mkuchika wewe ndiyo ulimpigia simu Mkuu wa Mkoa asitishe ile Operesheni. Sasa inakuwaje Wabunge tunaleta taarifa mnatupuuza!

Nimefika mahali nimeamua kukaa kimya, nikafikiri inawezekana Mheshimiwa Danhi Makanga amewekwa kule makusudi kwa kulinda ng'ombe wa Viongozi wa Kitaifa; au inawezekana biashara ile anayoifanya ya kuhakikisha Waha wetu na Wasukuma walioko kule wanaoishi Kasulu wananyanyasika, kulipishwa mafaini yasiyoeleweka; dili ni la Viongozi na ndiyo maana nikaamua kukaa kimya kwa sababu haiwezekani Mbunge ana dhamana kama Mbunge mwngine, unasemaje Serikali isikusikie? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba hayo yafanyike, baiskeli zirudishwe kwa Wananchi, Wakulima wangu wafikiriwe fidia. Wale waliohusika, Askari wa Wanyamapori, Askari Polisi walioshiriki katika mauaji, Askari wa Wanyamapori walioshirikiana na Mgambo kufyeka mahindi ya wakulima, nisikie ni wangapi wamekamatwa. Haiwezekani mazao ya Wananchi yanapotea, halafu hakuna mtu hata mmoja ambaye yuko chini ya uchunguzi kana kwamba haya mahindi yamejiangamiza yenye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiona migogoro inaendelea kuna uzembe. Tunakutegemea wewe uliongoze Bunge lako Tukufu ili tuweze kumsaidia Mheshimiwa Rais kuiokoa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Haya ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mbassa!

**MHE. JITU V. SONI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Naomba niungane na wenzangu wote, kwanza, kuwapa pole wote ambao wameathirika na wamepata tatizo kutokana na Operesheni Tokomeza. Kesho kutakuwa na Misa Maalum kwa ajili ya yule mama ambaye aliuawa kule Galapo, Bibi Emiliana Maro Gasper, anatoka katika Jimbo langu.

Mbali na hilo, naipongeza Kamati kwa kufika huko na kupata ukweli na kuja kuusema huo ukweli mbele ya Bunge hili na Watanzania wote waweze kujua nini kilichojiri. Ile Operesheni nia ya Serikali ilikuwa njema, lakini ilivyotekelizwa haikufuata utaratibu wowote ule wa kibinadamu wala sheria yoyote. Watu wallkamatwa hovyo tu kwa kuhisiwa. Inawezekana mimi Jitu kama nina visa na mtu nikikutaja unakamatwa. Yule alikuwa mama wa nyumbani, amechukuliwa nyumbani kwake na amechukuliwa baada ya kumfuatilia mume wake akiwa amepotea siku tatu hajulikani mahali alipo.

Mume wake alielezea kwamba, alipoona watu wengine wanateswa, ye ye alikubali kukiri yote kwamba anahusika na yote. Hivi kama alikubali kukiri alihusika na yote mbona baadaye aliachiwa tu kienyeji? Mtu anakubali kwamba ana silaha halafu unamwachia kienyeji baada ya mke wake kuuawa?

Mheshimiwa Spika, naomba mbali na hao wengine, labda Kamati pia haikujua kama kuna watu waliofanya *statements*, Wataalam wa Serikali, Madaktari waliofanya *post-mortem*. Mbona hiyo *post-mortem* ya kwanza ambayo inasema alikufa kwa *pressure* ni tofauti na *post-mortem* ya pili iliyo fanywa na Madaktari wengine wa ndugu wa marehemu na raia wengine waliochangia ili *post-mortem* ifanyike? Wao tunawafanya je? Wanatakiwa kuchukuliwa hatua kali kwa sababu wameshiriki moja kwa moja katika hayo mauaji kwa kupoteza ukweli na ushahidi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JITU V. SONI]

Mbali na hilo, Diwani wa Magugu alikamatwa na wafanyabiashara wa kawaida, walipelekwa huko Minjingu wakawa na hofu hiyo hiyo. Hatukulala usiku huo, ni baada ya kwenda kutoa pole kwa huyu mama siku ya pili. Watu walikuwa na wasiwasi kwamba na wengine yatawatokea hayo hayo, eti wanamiliki silaha. Tungeoneshwahata mfano wa silaha moja iliyokamatwa. Leo Wananchi wamekosa imani, hata wale ambaa walikuwa wanakubali kusaidia kwamba fulani huwa anafanya kazi hii au fulani huwa anauza nyama pori, hawapo tayari kwa sababu utaitwa jangili wakati wewe unaisaidia Serikali. Imani imepotea kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wote ambaa wamekamatwa, kuna mzee mwininge bado mpaka leo yuko ndani, wa kule kule Mamire, kazi yake ni kuuza mkaa, kisa amekosana na mtu. Polisi wamekuja, wanasachi nyumba, wakati wanasachi nyumba ndani yule wa nje anasema siyo huko njoo huku. Wakaenda kwenye Kihenge; mtu ambaye hajui hiyo nyumba, hajui mahali ilipo, anaenda kuonesha mahali eti pembe ya ndovu imefichwa; ni kweli?

Kwa hiyo, Wananchi wamekosa kabisa imani. Tunashukuru kwamba, ilisitishwa Operesheni Tokomeza. Mimi nisingependekeza kwamba iendelee kabisa mpaka hapo utaratibu mzima na mpangilio mzima utakapojulikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kwenda kusachi nyumba ya mtu, Viongozi husika, Serikali inaanza kwa Mwenyekiti wa Kitongoji. Haikuchukuliwa hatua yoyote. Huyu mama aliporudishwa baada ya kuteswa kutwa nzima, kijana wake ambaye anatembea na magongo naye aliteswa, amevunjika mguu, alipigwa, aliteswa. Majirani waliosogelea pale wote waliteswa, ili kubana watu wasijue ukweli. Hivi kosa lake ye ye angesema wapi kwamba hizo silaha walikuwa wanatafuta. Siku ya pili inatoka kwenye Vyombo vyaa Habari kwamba amekutwa na mkia wa twiga! Hivi utamaduni na mila za wanawake wa kwetu, wanaenda kuwinda kweli? Hata siku moja! Kama ni mwanaume, hata

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JITU V. SONI]

Wananchi wote wanasema wangembana yule mwanaume angesema kama ni kweli. Huyu mama alikosea nini? (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba wote, asiachwe mtu hata mmoja, hata yule aliyeshiriki kupotosha ukweli, wawajibishwe. Hiyo ndiyo itakuwa njia pekee ya kumtendea haki huyu mama. Watu walisema pale, inawezekana huyu ndiyo akawa amejitolea kafara kuokoa Watanzania wengi wasiendelee kuteseka. Kweli, baada ya muda kidogo Operesheini Tokomeza ikasimamishwa.

Tunaomba Serikali iangalie, kwanza, iwafikishe wote wale waliohusika na mauaji ya huyu mama, kwa sababu wanajulikana tena kwa majina. Hakuchukuliwa pale klenyeji, alichukuliwa na Maaskari wanaojulikana, sasa wao ndiyo watuambie walimpeleka wapi, walifanya nini mpaka hapo walipomrudisha akiwa marehemu. Wote wachukuliwe hatua, wafikishwe kwenye Vyombo vya Kisheria ili siku nyingine mwingine asije akarudia. Leo yamemtokea Emiliana, kesho inaweza kuwa mimi au wewe au mwingine yejote. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba, hapa hakuna cha siasa, hapa tunalenga haki na uhai wa Taifa letu. Tunataka tuboreshe ili kesho na keshokutwa yasitokee haya yaliyotokea. Kwa hiyo, ni muhimu waliohusika wote wafikishwe kwenye Vyombo vya Sheria. Mimi ningeomba kama ni Mahakamani, iwe ni *fast track* watu waone matokeo haraka, siyo kesi inachukua miaka mitano. Hao wengine ambao wamekamatwa bado wapo ndani, waachiwe mara moja kama hakuna ushahidi na pia Wananchi wajulishwe. Haki zao wanazijua, lakini labda hao Maskari na wale ambao wanafanya kazi hizi za kukamata watu na kupekua, ndiyo wafundishwe upya haki na sheria inasema nini; kwamba, ukitaka kwenda kukagua mtu, ukitaka kukamata mtu ufuate sheria ipi na wajibu wako ni nini. (Makof)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JITU V. SONI]

Mheshimiwa Spika, naomba hatua za haraka zichukuliwe, lakini pia wote waliohusika wawajibishwe. Tunasema mara nyingi labda ni Waziri huyu au yule, tati zo lipo kwa Watendaji wetu; ni uozo. Kwa sababu hii ni moja tu Operesheni Tokomeza, huko kwetu tuna mgogoro wa ardhi na TANAPA, kila siku mifugo inakamatwa, inatozwa faini. Mahakama imehamia huko. Hizo sheria za kufainisha mtu milioni moja, mbili, tano; inatoka wapi wakati Mahakama zipo? Mahakama zitafanya kazi gani? (Makof)

Mheshimiwa Spika, ningeomba Serikali iangalie namna ya kumaliza mgogoro wa mipaka baina ya Vijiji na Hifadhi zote ambazo hivi Vijiji vimezunguka. Serikali irudishe imani ya Wananchi, kwa sababu hakuna hata mmoja ambaye anahusika na ujangili au hata kuuza nyama pori, hakukamatwa na watu wanawajua. Wangeshirikiana na Wananchi wangewapata watu wote na Wananchi wangeunga mkono. Watu wasiokuwa na hatia ndiyo wamekamatwa na wale ambao wanafanya ile biashara bado wanaendelea nazo. Bado wanyama wanauawa, nyama zinazuwa kama kawaida. Mtapata ushirikiano na nani? Ni vizuri Viongozi wa hizi Hifadhi pia wapate mafunzo ya namna ya kuishi na raia. (Makof)

Hakuna Serikali mbili, Serikali ni moja. Hata wale ambao wapo kwenye Hifadhi, pamoja kuwa ni Askari, bado wanawajibika. Wanaishi katika nchi yetu ya Tanzania, Katiba yetu ni moja na sheria ni hiyo hiyo moja, hawapo katika nchi yao nyininge. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba, mbali na hiyo ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili. Mheshimiwa Dkt. Mbassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Lema!

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote, niungane na Watanzania wote, kuwapa pole wale waliodhurika katika Operesheni hii na nina imani Mungu atawasaidia.

Mheshimiwa Spika, suala hili tunaliongea leo hapa kwa uchungu, lakini niseme ni suala la muda mrefu sana. Waswahili wanasma usipoziba ufa utajenga ukuta. Sasa leo hii tunashuhudia huo ukuta.

Mheshimiwa Spika, tumemaliza uchaguzi tarehe 31 Oktoba, 2010. Swali langu la kwanza kuleta hapa Bungeni ilikuwa la Wafugaji na kero nzima iliokea pale Wilayani, Halmashauri walipoamua kupitisha Operesheni kwa ajili ya Mazingira. Suala hilo likasimamiwa na Daktari aliyejukwepo kipindi kile, Bwana Peter Yamanga. Wananchi walipata adha hili hii, ng'ombe wamekamatwa wametolewa kwenye maeneo stahiki ya Vijiji wamepelekwa kwenye Hifadhi. Faini zilizotozwa pale hazieleweki. Ninaiuliza Halmashauri ilikusanya shilingi ngapi kutokana na zoezi hili? Hakuna inasikitisha. Wanapewa stakabadhi ambazo nydingine ni za Ngarawa. Wamechomoa tu wameandika, mtu ametozwa milioni mbili inaanidikwa laki mbili. Watu wameweka pesa mifukoni.

Mheshimiwa Spika, kana kwamba haitoshi, siku moja tukamtaka Mkuu wa Kambi ya Wanyama Pori atuletee taarifa tu ya jinsi gani wamefanya kazi na jinsi gani wamekamata mifugo inayoingia kwenye hifadhi na faini walizotozwa, ilikuwa inasikitisha ile taarifa. Ndani ya kikao inaonesha wamekamata idadi kubwa ya ng'ombe, pesa ni kidogo. Sehemu ambako wamekamata ng'ombe kidogo pesa ni nyangi. Tukamwuliza uwiano wa faini hii ukoje? Mnatumia vigezo gani? Jibu halikutoka.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 ndani ya Halmashauri ya Biharamulo kulikuwa na Operesheni Okoa Mazingira, ambayo ilikuwa Operesheni ya Kimkoa. Operesheni hiyo iliendeshwa katika misingi ile ile ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA]*

kuwanyanya wa fuga ji na wakulima. Nikauliza swali hapa Bungeni tathmini ya Operesheni hii ni nini?

Nilipewa majibu hapa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba, ndani ya Wilaya nne; Biharamulo, Muleba, Ngara na Karagwe, wamekamatwa wa fuga ji haramu kutoka nchi za wenzetu kule wanen na wamekamatwa ng'ombe 466. Suala la kujuliza; pesa iliyotumika kugharamia Operesheni ile ilikuwa zaidi ya milioni 400; ni nini hapa kimefanyika na hii ni pesa ya walipa kodi wa Tanzania? Mheshimiwa Spika, inauma sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikusomee sehemu ya barua ya Wafugaji wa Jimbo langu la Biharamulo waliyomwandikia Mkuu wa Wilaya. Walimwandikia wakimweleza hali ya manyanyaso jinsi ilivyo na walimpa kopi Mkuu wa Mkoa, nami vilevile nikapata kopi. Nitasoma sehemu tu ya barua hii.

Wanasema; askari wa wanyamapori wanatumia mgambo wasio rasmi kutafuta ng'ombe porini na hata ng'ombe wengine kuwatoa kwenye maeneo yasiyo ya hifadhi na kuwapeleka ndani ya hifadhi ilimradi wapate pesa.

Mheshimiwa Spika, ng'ombe wanakamatwa na kuwekwa kwenye mazizi yaliyoko porini zaidi ya siku saba mpaka 14 na kwa kutozwa faini na Maafisa Uhifadhi kwa fedha zisizo na uhalali, kwani hazina Stakabadhi ya Serikali, pia viwango vinavyotozwa ni vikubwa mno. Mfugaji mmoja wa ng'ombe anapokamatwa hutozwa faini ya shilingi milioni tatu hadi milioni 15. Sheria hii imetoka wapi? Inasikitisha.

Wakaendelea zaidi, wanasema wao wanaowakamata hao kwamba hawapo peke yao na wakiwakamata wale wa fuga ji kule porini, wanawaambia wawaambie matajiri wao waende na pesa nyingi na hao wanapokwenda kule hakuna suala la *ku-burgain* lete ulichonacho, haitoshi, kalete nyingine.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA]

Mheshimiwa Spika, nitaleta hii barua kwako uione. Wanasema fedha zile siyo zao tu, kuna mtandao na wakasema kwamba, zinakwenda mpaka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili, wakataja na akaunti namba ipo hapa. (*Makofii*)

Maelezo hayo yametolewa na Maafisa wa Wanyama Pori ambaao walikuwa watano. Wa kwanza, Jonathan Msiba, wa pili Rogate Legwado, wa tatu Nesphory Kahinga, wa nne Frederick Kobelo na wa tano ametaja kwa jina moja tu la Angelius. Inasikitisha.

Mheshimiwa Spika, wameitaja hapa akaunti ya NMB Namba 2061100044, wanakoweka hizo pesa. Sasa leo hii ndugu zangu masuala haya tunayaona kana kwamba yamelipuka juzi, ni ya muda mrefu na watu wanaelewa. Leo hii inasikitisha sana tupo hapa tunajadili suala hilli, Jimboni kwangu huyu mmojawapo Frederick Kobelo, katika Kata ya Nyakahula, wamekamata ng'ombe wengine na ye ye ndiye anayeongoza hilo kundi. Benako Ngara kwa Mheshimiwa Ntukamazina, ng'ombe wamekamatwa. Ju zi Profesa Kahigi ananiambia hata kule Bukombe nako tatizo ni hilohilo; kuna nini watu wasitii sheria? Waziri Kagasheki amesema hapa wamesitisha, lakini zoezi linaendelea; kuna nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hilli haliwezi kuvumilika mbele ya Watanzania; haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Septemba, Mheshimiwa Kagasheki alifika Jimboni kwangu na mmojawapo ya kitu alichokuwa akiangalia ilikuwa ni athari za mazingira na uharibifu wa mazingira. Kikao kile mimi kama Mbunge sikuambiwa, lakini Mungu mwema nikabahatika kupata taarifa hizo, alinikuta kwenye mlango wa Halmashauri tukaingia ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Kagasheki akamwuliza Mkuu wa Wilaya, Bwana nipe taarifa yako ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya. Mkuu wa Wilaya, Bw. Richard Mbeho,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSAJ

akasema hana taarifa yoyote na kwa sababu alikuwa anashughulikia masuala ya sensa na mapokezi ya Mwenge kwa hiyo kulikuwa hakuna kitu. Mheshimiwa Kagasheki huyu, aauliza kuna taarifa ya ng'ombe waliopigwa risasi katika Pori la Kasindaga; *RPC unasemaje? RPC* akasema ni kweli ng'ombe walipigwa risasi, lakini tulimtuma Afisa Upelelezi wa Mkoa afuutilie. Eeh, mrejesho ukoje? Anasema ni baada ya Askari wa Wanyama Pori kupambana na majangili ambao walijificha kwenye kundi la ng'ombe, wakati waki-shoot wale ngombe ndiyo walikufa. Suala ambalo haliji akilini na halikubaliki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Kagasheki akasema suala hili mnawaeleza nini Watanzania? Hakuna jangili hata mmoja ambaye alikamatwa akapelekwa polisi hakuna! Kuna aliyejeruhiwa walau akapelekwa hospitali kutibiwa hakuna! Kuna aliyeureka walau maiti mkaiacha pale, hakuna! Walikwenda wapi? Vitendo vya rushwa hakuna kitu kingine.

Mheshimiwa Spika, nikaenda na Mheshimiwa Balozi kwenye Kata moja ya Ruziba kufanya mukutano wa hadhara. Wananchi wanaopakana na hifadhi wakamweleza maudhi yote wanayotendewa na hawa askari wa wanyama pori. Wakampa risiti za ngarawa ambazo zinaandikwa tu viwango feki vya faini wanazotozwa na Mheshimiwa aliahidi kurudi mpaka kesho hajakanyaga Jimboni kwangu; inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, jana asubuhi hapa wakati namwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali, ulinionya kwamba nisihutubie, lakini nilikuwa najenga msingi wa swali. Mwendelezo wa yale yale ya Operesheni Okoa Mazingira yanayofanya Wananchi waichukie Serikali hii. Operesheni Okoa Mazingira imefanyika ikiongozwa na Mshauri wa Mgambo wa Mkoa, Kanali Nyamwihula. Wameenda wamefyeka mazao ya Wananchi katika Kata yangu hii ya Lusahunga, Kijiji cha Nyakanazi. Wameenda Kata ya Kaniha, mazao yameharibiwa, nyumba zimechomwa moto, mpaka mzee mmoja wa miaka 80 anasema sasa Serikali imenilazimisha niishi maisha ya ubachela ambayo nilikuwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA]

siwezi kuyaishi miaka yote. Ng'ombe wake wamechukuliwa, nyumba imechomwa na leo hii wale watu wanaambibiwa wanaishi kwenye hifadhi; inasikitisha.

Suala hili nimeliongelea hapa mara nyingi, nikitoa mfano wa Profesa Kahigi kazaliwa katika kijiji kile, miaka nenda rudi wako pale. Leo hii *TFS* wameweka mabango Wananchi wahame kufika Januari. Sasa mimi inanisikitisha. Vijiji vile vimepata usajili na hati ya usajili imetolewa tarehe 1 Septemba, 2012 na Serikali hii hii. Leo hii Serikali hii hii inatoa maagizo Wananchi wale wahame wanaishi kwenye hifadhi; hivi tuna Serikali ngapi? (*Makofii*)

Migogoro ya ardhi kila leo nimeisema hapa, hakuna anayechukua jukumu la kuja kuangalia kuna nini huku. Haya yote tunayaeleza. Juzi, nashukuru Kamati imekwenda pale inailoji Kamati ya Ulinzi na Usalama, *DC* anasema ana likizo ya siku nne; sijui likizo ipi? Nashukuru sana Kamati wamewasikiliza wale Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, lakini wakaenda kujiridhisha kwa wale ambao wameathirika.

Mheshimiwa Spika, kuna picha hapa zinasikitisha sana; makundi ya ng'ombe waliokuwa wamekusanya, wamewekwa porini, magari yanavyoenda kupakia wale ng'ombe, sasa sijui wanapakiwa wanaenda kwa nani na wanapelekwa sehemu gani? Wizi mtupu, majanga. (*Makofii*)

Mimi nasema kitu kimoja, tusipowawajibisha hawa Watendaji hapa hakuna suluhu na Wananchi. Ninachokiona hapa, tutaendeleza yaleyale sasa hatuyabariki, lakini watu wataanza kujichukulia sheria mkononi. Itafika mahala Wananchi sasa wanasema sisi na mifugo yetu tunajilinda. Sasa askari uende pale una bunduki unamkuta Mwananchi naye kajilinda pale ana bunduki, kitakachotokea ni nini? Yatakuwa ni maafa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana. Leo hii Wananchi ambao wameharibiwa mazao yao kwamba wapo ndani ya hifadhi hawatajwi sehemu yoyote ile.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA]

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Kamati.  
(Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lema, atafuatiwa na Mheshimiwa Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o!

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana. Wakati taarifa hii inasomwa, nimetafakari sana lakini kuna saa nilijisahau nikafikiri nipo kwenye Bunge la Uingereza, kwa sababu sioni kitu kigeni sana kinachowashtua Waheshimiwa Wabunge. Naona ni *style* mpya ya mauaji imekuja katika Taifa letu, lakini mauaji yameanza muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, watu wa Spain wana msemo unasema; "Tabia huanza kama utando wa buibui lakini huishia kuwa kama reli." Kinachotokea sasa ni mazao ya mambo madogo madogo mengi ya uvunjaji wa haki za binadamu, ukatili, ambao pindi yalipotokea huko siku za nyuma, Serikali haikutilia maanani sana kuyadhibiti na leo kinachotokea ni mambo ya kutisha sana.

Mheshimiwa Spika, katika Ripoti hii kuna mtu alilazimishwa kuchora nyoka wa chatu kwenye paja lake kwa kutumia wembe. Nilikuwa najaribu *ku-assume* unachoraje chatu kwa kutumia wembe. Hili la kuchora chatu kwa kutumia wembe kwenye paja la mtu linaweza likawa limezalishwa na matendo *yaliyofanyika* Tarime, ambapo Polisi waliua binadamu na wakaiba maiti *mortuary* wakaenda kuitupa barabarani kwenye Kata ambazo wale maiti wanajulikana walikuwa wanaishi kule.

Mheshimiwa Spika, haikuchukuliwa kwa umakini sana. Hawa Polisi wanaotaka kushutumiwa leo, tabia ile imeshakuwa kama utando wa buibui.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Haki za Binadamu, baada ya tukio la Arusha la Januari 5, ilisema kwamba, Polisi walikosea wakaua watu na wakajeruhi watu. Ripoti

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GODBLESS J. LEMA]

hiyo haijawahi kuingia Bungeni na mambo hayo yameendelea kuwepo. Kwa hiyo, *confidence* ya Polisi kuendelea kuua, kutesa na kudhalilisha, inasababishwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kitu ninachokiona hapa ni kimoja, hata leo Waheshimiwa Mawaziri wakiwajibishwa, Mheshimiwa Mkuchika huyu ambaye alikuwa amesahaulika anatakiwa aingie mara moja kwenye ile *list* ya kuondoka. Huyu anatakiwa aondoke kabisa, kwa sababu yeye ndiyo anasimamia Wizara ya Usalama wa Taifa. (*Makof*)

Katika mambo yote haya yaliyokuwa yanafanyika ninajuliza; Usalama wa Taifa ulikuwa wapi? Leo Bunge linafanya kazi ya kutunga Sheria, Bunge linafanya kazi ya kutunga Sera na kuishauri Serikali halafu Bunge tena liwe *FB*/ya Serikali wakati nchi hii ina Usalama wa Taifa! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tungekuwa na Usalama wa Taifa ambaao unafanya kazi ya ku-*protect* Taifa hili, haya mambo yasingefika huku leo Mawaziri wetu hawa kuambiwa wajiuZulu. Badala yake hata haya mambo yalivyoibuka huku Bungeni, yameibuliwa na Wabunge, haukuwa mkakati wa Serikali mambo haya kujulikana. Mheshimiwa Kangi Lugola na Wabunge wengine, ndiyo walianzisha hoja hii. Kiti chako Mheshimiwa Spika kikaazimia kuunda Kamati kwa ajili ya uchunguzi. Leo Bunge limetumia fedha limekwenda kufanya *investigation*, Bunge linaleta Ripoti mbaya ya mauaji kama haya; Usalama wa Taifa hauna *document*, haujui na Serikali hajui. Mheshimiwa Mkuchika imefika sasa mahali na yeye aunganishwe kwenye lile kapu na yeye aondoke. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama Chama cha Mapinduzi kitatenda haki na leo nilichokiona humu ndani ya Bunge, Wabunge wote tumepatana katika msingi wa kweli, kama Chama cha Mapinduzi kitafanya kazi ya haki, kazi ya kweli, hata kama chama changu kitashindwa kushika madaraka, lakini Chama cha Mapinduzi kikaendelea kutawala,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. GODBLESS J. LEMA]

kutawala kwa haki, hiyo siyo tu baraka kwa binadamu ni baraka kwa Mwenyezi Mungu. (*Makofii*)

Nami niwaombe Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, Waheshimiwa Mawaziri hatuwachukii, tunapowa-*critisize* maana yake tuna ku-*critisize* kwa ajili ya maisha yetu, ninyi ndiyo mmepewa dhamana na mnatawala. Angalieni mambo yanavyokwenda sasa, angalieni watu wanavyoumizwa. Mwanamke anaingiziwa chupa kwenye sehemu za siri. Ukitosha haya mateso yalisehma humu kama ni nchi ambayo ipo *sensitive* wangesema kwamba tu siyo Waziri Mkuu tunataka mpaka Rais awajibike. (*Makofii*)

Unajiuliza wako wapi Polisi? Hawa Polisi wenye *attitude* ipi tunaotaka waende wakawe waadilifu?

Mheshimiwa Spika, Viongozi wasipomrudia Mwenyezi Mungu, Taifa hili linakwenda kuanguka. Kwa sababu ukatili unaouona humu utafikiri ni shetani alishuka, nikawa najiuliza hivi shetani huwa kuna saa anashuka? Nikajua tu kwamba, kumbe ni shetani alishuka akatumia miguu, mikono na mioyo ya watu.

Mheshimiwa Spika, hapa siyo habari ya kujiuzulu tu, kuna watu wamefanya haya mateso, hawa watu watafutwe wawajibishwe. Tumesikia huko Korea, Rais amemnyonga mjomba wake kwa tuhuma za kawaida, huku kwetu tunacheka na mateso makubwa. Hawa polisi ambao wamesemwa humu ambao Mheshimiwa Nchimbi anawasimamia, hawa ni polisi ambao baada ya tukio la bomu la Soweto wamekamata mtu, wanapiga mtu, wanamlazimisha anitaje mimi kwamba ndiyo nilinunua mabomu, nipige mabomu, nimepiga mabomu kanisani, nimepiga mabomu kujiua mimi mwenyewe na jana yule kijana baada ya kutoka hapa amekamatwa. Amekaa mpaka saa 7.30 usiku mpaka ikabidi tuingilie kwa Waziri na kwa *IGP*, yule kijana ndiyo akaachiwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GODBLESS J. LEMA]

Hili suala ni hatari sana, hata sifa ya Waziri wa Mambo ya Ndani, sifa mojawapo aliyochanguliwa nayo ilikuwa ni ubabe na ukatili. Hatuwezi kuwa na Viongozi wanaochaguliwa kwa sifa ya ubabe na ukatili na kwamba, amefanya mambo mengi sana mabaya akiwa UVCCM ambayo chama kina imani naye.

Mheshimiwa Spika, mkiacha mambo haya yakaendelea hivi, watu huko nje wanaona, maskini wanaona, watu wanasiakia na wanaona hili ndiyo Bunge la kuwatetea. Tukiacha mambo haya hivi hawa wanyonge ambao mnafikiri hawana uwezo, mnafikiri hawana nguvu, siku moja Mungu atawapa namna nyiningine ya kujitetea. Mzee Mandela alisema ukimpuza na kumnyanyasa mtu mnyonge, haumfundishi njia ya kuwa mwoga, unamfundisha njia ya kujitetea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hawa Mawaziri wawajibishwe, Idara ya Usalama wa Taifa nchi hii haifanyi kazi yoyote. Tungekuwa na Idara *proper* ya Usalama wa Taifa, haya mambo unayokumbana nayo leo kwenye dawati lako yasingekufikia hapa yangeishia kule. Taarifa zingeenda kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa na zoezi hili lingesitishwa na Rais, lingesitishwa na Serikali, kwa sababu tayari walikuwa na taarifa. Watu wanauawa, watu wanapigwa, Usalama wa Taifa unafanya nini? Watu wanateswa wanafanya nini? *Intelligentsia* ya Usalama wa Taifa ambayo inasimamiwa na Mheshimiwa Mkuchika kazi yake ni moja tu, inaweza ika-*trace* Maandamano ya CHADEMA na kuyazuia lakininashindwa kuzuia mauaji kama haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hizi picha nilitaka nikupe mwanzo nikasema nisikupe kwa sababu niliona zitaku-*disturb*. Hizi picha zimetoka Tarime na nitakupa mwisho baada ya kikao hiki. Ukiziangalia hizi picha, mtu ameingiziwa msumari wa nchi sita sikioni halafu inapigwa nyundo. Ukiangalia hizi picha, mwanaume anashikwa sehemu za siri, anaingiziwa bisibisi sehemu za siri, zinatisha. Nilitaka nikupe hizi picha ofisini kwako, nilikwambia nakuja ofisini kwako na

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. GODBLESS J. LEMA]

tumeshauriana hapa na Mheshimiwa Machali tukasema  
hapana zitam-*disturb* mama.

Mheshimiwa Spika, kuna ukatili wa hali ya juu sana.  
*Father Kagasheki, I respect you*, nakuheshimu Mheshimiwa  
Kagasheki, chukua jukumu la kujitoa, chukua jukumu la  
kujiondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mkuchika, wewe si tu kuondoka, una  
mambo mengi ya kujibu. Mheshimiwa Nchimbi anasema  
ye ye ni Mjumbe, ana nguvu ndani ya Chama cha  
Mapinduzi. Jifunzeni kwetu Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa  
Spika, kwa namna inavyoendelea, hali hii ikiachwa, tutaona  
demokrasia siyo msingi wa kutafuta haki katika nchi hii.  
Tutawashawishi watu ikiwezekana tufanye Mapinduzi, kwa  
sababu kuna saa haki inatafutwa kwa nguvu. (*Kicheko/  
Makofi*)

**SPIKA:** Uondoe maneno hayo sasa. Si Sheria tupo  
tunatunga.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika,  
nimeliondoa, lakini nashukuru Mungu ujumbe umefika.  
Waheshimiwa Viongozi, niwaombe sana kwamba kwa hali  
ilivyo hii Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wote waliotajwa hawa,  
wapo wengi wa kutisha, nimesikia hapa dada yangu  
anataja Mheshimiwa Danhi Makanga kwamba ameenda  
kuleta ukabila kwao.

Mheshimiwa Spika, mimi kule Arusha kuna Waziri  
kabisa anaitwa Mheshimiwa Ole-Medeye, yaani sasa hivi  
ukabila kwake ni *issue*. Mpaka tumembadilishia jina  
hatumwiti tena bomu, anaitwa kipindupindu kwa sababu  
ukabila unatambaa, unaua. Huyu naye pia aingie humu.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ...

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Aaah ngoja *no, no*, hapana!

**SPIKA:** Naomba ujielekeze kwenye hoja.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, simchukii.

**SPIKA:** Naomba ujadili hoja bwana aah!

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, mimi ninaishauri Serikali, watu wote hawa wawajibishwe bila kumsahau Mheshimiwa Mkuchika, sijui amefanya nini amesahaulika kwenye hii. Bila kumsahau Mheshimiwa Mkuchika sijui kafanya nini wakamsahau! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tena ukiangalia kwa undani kabisa Mheshimiwa David Mathayo ambaye ng'ombe wake ndiyo wamepigwa ...

**SPIKA:** Jamani, mbona wewe unazungumzia watu aah! Zungumzia *issues*.

**WABUNGE FULANI:** Endelea!

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo David Mathayo, ukisoma taarifa hii imeonesha kwamba, yeye ndiye mbaya. Ukiangalia kwa undani ni kama anataka kuonewa. Hapa mtu wa kwenda naye vizuri wa kwanza Mheshimiwa Mkuchika, wa pili Mheshimiwa Nchimbi, wa tatu Mheshimiwa Kagasheki, wa nne Mheshimiwa Nahodha, wa tano Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Chikawe yumo naambiwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ijulikane kwamba, Waheshimiwa Viongozi siyo kwa nia mbaya kwa sababu msipoondolewa ama msipoondoka, tunapeleka taswira mbaya kwenye *public*. Wananchi wanaweza kuamua kufanya *resistance* kwamba, Viongozi hawa wamesimamia

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. GODBLESS J. LEMA]

mauaji, wamesimamia ukatili, lakini bado Serikali imewalinda. Mimi ninawashauri hamwondoki ...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naona na ugonjwa na majina. Haya naomba sasa nimwite Mheshimiwa Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie hoja ambayo imewasilishwa na Kamati kuhusu Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Wabunge tumetoka kucheka sana kwa sababu ya majina yanayotajwa. Jambo hili kimsingi hatupaswi kucheka hata kidogo, kwa sababu ni jambo la simanzi, ni jambo la huzuni na ni jambo la kusitikisha ambalo limeikumba nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo baya sana ambalo wamefanyiwa Watanzania, ni baya kuliko. Nami ninapenda niipongeze Kamati kwa sababu imefanya kazi nzuri sana. Mimi kama Kiongozi wa Chama cha Mapinduzi, siamini kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imewatuma waliofanya mabaya hayo kuyafanya mabaya, siamini. Ninachoamini ni kwamba, kuna watu ambao wameshindwa kuwajibika na kazi hiyo ikafanywa vibaya sana ambayo leo taswira yake kwa jamii ni mbaya sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ili kukifanya Chama cha Mapinduzi kiendelee kung'ara kama ambavyo ndugu yetu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Kinana, kazi ambayo amejaribu kuifanya iendelee kuwa nzuri, ni Mawaziri wanaotajwa kuwajibika. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. GODFREY W. ZAMBI]*

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivi, siyo kwamba, kuna mtu anachukiwa, hapa tunazungumza masilahi mapana ya nchi, lakini pia masilahi mapana ya Chama chetu cha Mapinduzi na kwa sababu jambo hili likizungumzwa inayozungumza ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, ili kuisafisha Serikali ya Chama cha Mapinduzi na kwa maana ya *ku-manage politics*, ni vizuri na ni ushauri wa kawaida kwamba, Mawaziri hawa wangepaswa kujiezulu.

Mheshimiwa Spika, wao siyo wa kwanza kujiuzulu, walishatangulia na wengine makosa waliojiuzulu nayo hata hayakugusa vifo vyta watu wala vifo vyta mifugo ya Watanzania ambayo ndiyo maisha yao. Kwa mfano, nina mifano michache hapa; Mheshimiwa Idd Simba alijiuzulu kwa kuruhusu vibali vyta kuingiza sukari iingie nchini, lakini Bunge likamtaka ajliuzulu. Mheshimiwa Kitine, alijiuzulu kwa sababu mke wake inasemekana alitumia hela za matatibu isivyo huko nje ya nchi. Angalia akina Mheshimiwa Ngeleja makosa waliyojiuzulu, akina Mheshimiwa Maige makosa waliyojiuzulu mengine hayakuhusu hata vifo vyta watu. Leo tunazungumza jambo kubwa ambalo moja kwa moja Watanzania wamepoteza mali, lakini mifugo ya Watanzania hawa maskini imekufa kwa sababu ambazo hata hazielezeki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili jambo wala halikustahili hata lifike hapa. Mimi ningewashauri hata Viongozi wa Chama cha Mapinduzi ambao wapo hapa, tushike jambo hili kama Serikali inayotawala na kwa ujasiri kabisa tuwaambie hawa Mawaziri wajiuze, mwisho wa kujiuzulu kwao siyo mwisho wa maisha. Ninaamini wengi hawa wana maisha mazuri hata kabla ya kuwa Wabunge na Mawaziri walikuwa na maisha mazuri. Wakiondoka kwa kujiuzulu watajenga heshima zaidi kwao, lakini pia na kwa Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naomba sana hili jambo nadhani hata tungefika kesho, tungefika labda hata jioni ya leo, iwe imetolewa taarifa kwamba, Mawaziri

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. GODFREY W. ZAMBI]*

hawa wamejiuzulu, ingependeza na ingewajengea tabia nzuri, ingewajengea mwenendo mzuri kwa jamii na hata baadaye wangkuja kurudi kwenye nafasi hizi kwa sababu walitoka kwa hiari yao wenyewe. Unajua kuondolewa kwa nguvu na kujiuzulu wewe mwenyewe ipo staha kubwa sana ya kujiuzulu.

Mheshimiwa Spika, tuwaambie suala la kuwajibika (*accountability*), ni suala la kawaida katika nchi nyingi duniani. Ukiambiwa umeondolewa, umefukuzwa, inajenga sura mbaya sana kwa jamii, lakini hao wenzetu ni Wabunge na kwenye Majimbo yao ambako wanatoka, watajenga heshima kubwa wanaposema wamejiuzulu.

Mheshimiwa Spika, mimi siamini kama kuna Waziri ambaye alimtuma Askari kule akaue, hakuna Waziri wa namna hiyo. Siamini kama kuna Waziri mwininge yejote amewatumwa watu wakafungwe hapo hapo wametenda kosa wafungwe. Wanatakiwa wawajibike kwa sababu mambo hayo yamefanywa wao wakiwa Viongozi katika Wizara hizo. Kwa hiyo, suala la *accountability* ni suala la kawaida duniani kokote.

Mheshimiwa Spika, mimi najiuliza kama wenzangu walivyotoka kuzungumza hapa; naambiwa Operesheni Tokomeza ilianza tarehe 4 Oktoba, 2013 ikaisha tarehe 1 Novemba, 2013, karibu mwezi mzima. Sasa unajiuliza kama imefanya karibu mwezi mzima na vitendo hivyo viovu vilikuwa vinatokea, hivi taarifa ziliikuwa hazifiki kwa Viongozi mpaka mauaji yanatokea mwisho wa siku wanakuja Wabunge wanaleta taarifa hizi Serikali ilikuwa wapi? Serikali ilikuwa haina masikio? Hii ndiyo inayoleta shaka katika utendaji kazi wa Serikali yetu na ndiyo sababu tunataka hasa wa Chama cha Mapinduzi tuhakikishe Serikali hii na wale ambao wanatajwa moja kwa moja wanawajibika.

Watanzania wasije wakaamini kwamba, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanawatetea watu ambao hawakufanya kazi vizuri. Hakuna mtu ambaye anaweza kumtetea mtu ambaye Wizara yake imewajibika katika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. GODFREY W. ZAMBI]*

mauaji, Wizara imewajibika katika kuhakikisha mifugo ya watu inapotea. Sidhani kama kuna Mbunge yeoyote anayeweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala hili naomba tuliseme, siyo suala la Chama fulani na kama wenzangu walivyotangulia, tunazungumza masilahi mapana ya Wananchi wetu, masilahi mapana ya Utanzania wetu. Kwa hiyo, ni suala la ujumla wetu Wabunge ambao tupo ndani ya Bunge na wakati tunaposimama masuala kama haya kwa Wabunge wote maana yake wote tunaguswa. Lingekuwa suala ambalo tunaenda kwenye misingi ya Vyama inawezekana tungekuwa tumetofautiana hapa. Naona tuungane kwa sababu wote tunaguswa na kupotea kwa maisha ya Watanzania, wote tunaguswa kutokana na Watanzania wale maskini kupoteza mifugo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani tuangalie kuanzia kule chini, wapo *DCs* ambao kazi hizi zimefanyika katika maeneo yao, kama wapo nao wawajibike. Wapo *RCs* ambao mambo haya yamefanyika katika Mikoa yao nao wawajibike. Vipo Vyombo vy'a Usalama ambapo katika maeneo yao yametokea haya, wawajibike. Hali kadhalika, Mawaziri ambao wanasimamia wawajibike ili tujenge picha nzuri katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo, Serikali lakini zaidi Chama cha Mapinduzi, tutakuwa tunajenga sura nzuri sana kwa Watanzania. Yapo mambo tunaweza tukasema tuanze uchunguzi leo, sawa uchunguzi unaweza ukafanyika, lakini uchunguzi utakaofanyika unaweza ukachukua mwaka mzima, miaka mwili, ndio baadaye uje uwafunge watu. Tunataka tuli-manage hili suala kisiasa ili Watanzania wajue kwamba, Wabunge ambao ni wawakilishi wao wanaumia mambo mabaya yanapotokea katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, hili jambo kama nilivyosema ni kubwa sana. Panapotokea uzembe tuhakikishie hatua zinazostahili zinachukuliwa wakati huo huo. Zile hatua nyingine zinazotarajiwa kwenda Mahakamani ziende, lakini

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. GODFREY W. ZAMBI]*

hatua ambazo Wabunge tunaweza tukasukuma, Wabunge tunaweza tukasimamia, basi zichukuliwe mara moja. Mimi nina hakika hata kama Mheshimiwa Rais yupo nje ya nchi, naamini wanawasiliana naye, Mheshimiwa Waziri Mkuu, anawasiliana naye; ni jambo ambalo hatupaswi kusubiri, uamuzi unatakiwa ufanywe leo.

Mheshimiwa Spika, nataka nishauri, tusiondoke hapa kesho tunamaliza Bunge, Mawaziri wanaohusika na wengine wote wanaohusika wakiwa wapo madarakani, italeta picha mbaya sana katika nchi yetu na kwa Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kazi nzuri ya Kamati, lakini hili tuliwekee uzito sana kwamba wote wanaohusika lazima wawajibike mara moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Kamati. Ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Taarifa ya Kamati. Kwanza, naomba niipongeze Kamati kwa kazi nzuri waliyofanya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuungana na Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa wote waliopata matatizo makubwa wakiwemo Wananchi wa Mkoa wa Iringa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tatizo hili ni kubwa na limemgusa kila mtu. Watu wamenyanyaswa, wameondolewa utu wao, haki za binadamu zimekiukwa kwa kiwango cha hali ya juu. Tumepata madhara makubwa kiasi kwamba, haya madhara siyo kwa wale tu walionyanyasika, lakini pia na familia zao. Kwa sababu watu walikuwa wanachukuliwa hawajui familia zao ziliko, watu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O]*

wamenyanyaswa kiasi kwamba wameondoa na imani hata ya kuishi kwa sababu tu ya ukiukwaji wa taratibu. Mimi ninaelewa kabisa Serikali ilikuwa na nia nzuri kabisa ya Operesheni Tokomeza ili kupambana na ujangili na hayo yote. Nina uhakika kabisa kwamba, wale waliotumwa kwenda kufanya Operesheni ile hawakutumwa kufanya waliyoyafanya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tupo ndani ya Jengo hili Tukufu na kila siku tunasali, kama kuna mtu au Chama chochote kimeingia nyuma ya mgongo wa wale watu, kwa kweli Mungu atakuja siku moja kutuhukumu. Tusiseme yameenda hivi, lakini pia tuangalie kwa sababu wale waliokuwa wanafanya hizo hujuma walikuwa wanatoa na maneno, hebu tuchunguze na yale maneno waliyokuwa wanayasema. Maneno makubwa ya kuikashifu Serikali, maneno makubwa ya kuita majina ya watu, tuyaangalie nayo yachunguzwe. Wote tusizungumze hapa, mimi ninaelewa kabisa, amesema mwenzangu pale kwamba, kwenye msafara wa mamba na kenge wapo.

Mheshimiwa Spika, tusiwe wote tunazungumza hili kama tupo pamoja, lakini kweli tupo pamoja toka mwanzo, tuchunguze. Tuchunguze haya tusikubali tu tufanye ndiyo, lakini pia uchunguzi uendelee tujue ndiyo halali hivyo au kuna mtu yupo nyuma ya hii Kampeni ambaye amesisitiza haya yafanyike na wafanye vitendo vyahamna ile.

Mheshimiwa Spika, watu wamekamatwa wengine wakiwa maofisini, wanafuatwa ofisini kwenda kukamatwa. Hivi kweli ujirani mwema uliotengenezwa tunajua kabisa hifadhi zimekuwa zinafanya ujirani mwema, Wananchi wamekuwa wanafanya kazi vizuri, wanashirikiana vizuri; hivi kweli kuna Kiongozi ye yote au Wizara yoyote iwatume wale waende kusema maneno waliyokuwa wanayasema?

Mheshimiwa Spika, mimi sikubaliani wala hainitumi kabisa kuamini kwamba, eti Operesheni ile ndivyo walivyokuwa wameambiwa kwenda kusema na kwenda kutenda vitendo walivyovitenda. Sikubaliani kabisa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O]*

kwamba, vitendo walivyofanya ni halali. Nataka niseme kwamba, uchunguzi uendelee ili tujue ni kitu gani kilichokuwa ndani ya Operesheni hii.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kulizungumzia ni kile kitakachotolewa, tunasema kifuta machozi. Hapa hakuna kifuta machozi ni kulipwa fidia kulingana na ukubwa wa tatizo. Watu wamepata ulemavu wa kudumu, wengine sasa hivi wanauguza majeraha. Je, kama amepata maumivu kwa ndani ambayo hatutayajua au wamepata maumivu mengine ya kisaikolojia? Ufanyike uchunguzi kila mtu alipwe kulingana na ukubwa wa tatizo alilolipata.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze lingine, naomba niwaambie Watanzania wenzangu, Chama cha Mapinduzi kipo pamoja nanyi, haya yamefanywa na watu hao wenyewe siyo Chama cha Mapinduzi. Kama mtu anafikiri kwamba, anatengeneza chuki kwa Chama cha Mapinduzi, hiyo siyo sahihi, wote tunaungana kupinga vikali tabia zilizofanyika. Tunaungana kama Wanawake wa Tanzania, kulaani matendo waliyofanyiwa Wanawake na Watoto. Nina uhakika katika tatizo hilo kuna wengine wameambukizwa Virusi vya Ukimwi. Hilo nalo ni tatizo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba wote tuwe kitu kimoja, tunazungumza hapa tukijua kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imesimama imara haitaki Mtanzania apate shida wala anyanyasike. Tunazungumza tukiumia wengine tunataka kulia kwa sababu tunajua mateso makubwa waliyoyapata. Watu wananing'inizwa kama kuku, miguu juu kichwa chini; hivi kweli hata Askari waliokuwa wanafanya vitendo hivi hawana huruma? Utafikiri hawakuzaliwa na mama au na baba; kwa nini wafanye unyama wa namna hii?

Mheshimiwa Spika, hili tatizo ni kubwa na wote tusimame kama kitu kimoja, lakini kila mtu aguswe upande wake kama ameshiriki kwa namna moja au nyinye na Mungu kweli atasimama. (*Makofi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O]

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia uangaliwe utaratibu, wale wanaoumwa wapelekwe kwenye hospitali na gharama zigharamiwe na Serikali kuwatibu na kuwafanyia uchunguzi, wapewe matibabu hata kama ni kupelekwa nje ya nchi wafanyiwe uchunguzi wa hali ya juu. Mbona sisi tunatibiwa tunapelekwa nje, wapelekwe nje ya nchi wakachunguzwe na matibabu yao yaridhishe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninapenda nikushukuru sana na nawapa Watanzania wenzangu moyo. Ninapenda niwaambie kwamba, wanyama tuna haki ya kuwalinda, tembo wetu wanakwisha tuwalinde. Nawapa moyo kwamba zoezi liliolofanyika lisiwakatishe tamaa kulinda maliasili ya Tanzania inayoteketea. Ninawaomba muendelee kuwa na moyo na imani na Serikali yenu na ipo inawalinda na itawasimamia. Mmetutuma hapa kufanya kazi ya kuwatetea na tutalinda haki zenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru na nirudie kuwapa pole Wananchi wa Mkoa wa Iringa wote, waliopata shida na wale ambao wamepata shida kwa chuki za watu binafsi na chuki za kisiasa. Tunaomba tuache chuki za kisiasa na chuki binafsi kwenda kuziweka kwenye kazi za umma na kama ni Mwananchi yejote hata kama ana matatizo yake, asitumie mwanya ambao Serikali imeuweka kutatua matatizo ya Wananchi kwa kutumia mbinu zake chafu na ashindwe na alegee. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Shekifu!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Taarifa ya Mheshimiwa Lembeli, ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge wako, mmetufungua macho. Haya

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

yaliyoandikwa humu ndani ni mambo mazito, si ya kibinadamu hata kidogo, ni ya kinyama na yanatakiwa yalaaniwe kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wanaotajwa kwa kusimamia Wizara zao, sina tatizo nao hata kidogo, tatizo ni ule uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, mimi nilishawahi kuwajibishwa na Bunge lako nikiwa Mwenyekiti wa PAC wakati huo, sikufanya makosa lakini kwa sababu nilikuwa nasimamia ile Kamati nikawajibishwa na Bunge lako. Mimi siyo wa kwanza, kwenye Jengo la Msekwa Mheshimiwa Prof. Mbilinyi tulimwajibisha, Mheshimiwa Mporogomyi kwa sababu ya minofu ya samaki Mwanza tukamwajibisha, Mheshimiwa Dkt. Ngasongwa tulimwajibisha, Mheshimiwa Iddi Simba na Mheshimiwa Kitine na Mheshimiwa Kitine alikuwa ni wa Utawala Bora tulimwajibisha.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nikuombe sana na niwaombe wale wanaotajwa, hatupendi iwe hivyo, lakini kwa upopo uliopo sasa ndani ya Bunge na nje ya Bunge, nawasihi sana hebu tupishe waje watu wengine wafanye kazi hizo. Vinginevyo, kitu ambacho skipendi na kimesemwa sana humu ndani, haitapendeza kama wenzetu hawa wataendelea kung'ang'ania hapo, kwa sababu kitakachofuata maamuzi ya Waheshimiwa hawa wakiona huu mti matawi yake hayakatiki, kinachofuata ni kukata mti mzima. Kukata mti mzima maana yake ni kumwondoa Waziri Mkuu, kwa hiyo, ukiondoka Waziri Mkuu itabidi Rais avunje Baraza la Mawaziri. Kwa miaka kumi hii kwa Serikali ya Rais wetu mchapakazi itakuwa ni historia ambayo siyo nzuri ya kuwa na Mawaziri Wakuu Wastaafu watatu kwa miaka kumi; haipendezi hata kidogo. Sasa Waheshimiwa Mawaziri wale mnaotajwa, nimewataja hapa Mawaziri waliojiuzulu, wengine hawakuwa na makosa hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Dkt. Ngasongwa alitoka lakini baadaye akarudi akawa Waziri tena. Tulimwajibisha kule ndani, baadaye akarudi akawa Waziri. Tulimhukumu kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

sababu ndiyo alikuwa kinara kwenye Wizara ile. Kwa hiyo, naomba sana na sipendi kurudia yale maneno ambayo yamerudiwa. Nawasihi sana Waheshimiwa Mawaziri, kwa siha ya Bunge letu na kwa siha ya nchi yetu na manufaa ya nchi nzima, chukueni uamuzi. Uamuzi ni mgumu kwelikweli lakini hakuna namna, tusaidieni, andikeni barua za kujuzulu ili nchi yetu ibaki salama salmini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shekifu!

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru wewe mwenyewe kwa kuteua Kamati hii na mimi nikiwemo. Namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, tulipoanza shughuli hii tulionyana hapa tukasema tutasema kweli daima fitina kwetu ni mwiko. Tulisema hatutakubali kwa njia yoyote ile kununuliwa kwa kauli yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru na nawashukuru wenzangu Kamati nzima ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, lakini zaidi Kamati hii Ndogo ambayo mimi ni mmojawao katika watu wanane. Mimi niliongoza Kanda, nilikwenda na Kiongozi wangu katika Kanda ambayo imekuwa na malalamiko mengi na ni Kanda ya Kaskazini ambayo ndiyo iliyo na hifadhi nyingi na mbuga za wanyama kubwa. Tulianzia Mkoa wa Simiyu, tukaenda mpaka Bariadi, Bunda, Tarime, Mugumu, Babati mpaka Kiteto.

Mheshimiwa Spika, mambo tuliyoyaona ni kweli yote yametajwa. Kubwa ambalo limeshazungumzwa na watu wengi nisingependa kulirudia ni mateso ya Wananchi. Kwa bahati mbaya sana, mimi nimekuwa Kiongozi Mkoa wa Manyara, nilishituka sana hasa baada ya kuona vitendo vilivyotendeka ambavyo sijawahi kuviona. Nimekuwa Bungeni hapa kuanzia mwaka 1995, lililoonekana kule ni kwamba, haiwezekani katika nchi ya Utawala Bora kama hii yatokee yale na mengi yameandikwa humu ndani sitaki kuyarudia. Sasa niseme ni wapi tumeteleza?

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. HENRY D. SHEKIFU]

Pengine upungufu katika Operesheni, makubwa yamekwishatajwa humu. Mimi niongeze tu ambalo halijatajwa humu ndani, kuna Wabunge wengine wamezungumza cheche huanza kama cheche, lakini hugeuka kuwa moto mkubwa. Tuliloliona kubwa sana, mshikamano wa Serikali, Serikali haizungumzi pamoja. Huo ni ukweli. Waziri wa Mambo ya Ndani ana yake, Waziri wa Majeshi ana yake, Waziri wa Maliasili yuko vyake, matokeo yake Operesheni imeanza bila msimamizi. *It was unguided missile.* Lilipoangukia ndiyo huko kulitokea yote haya. (Makofi)

Mawaziri hawa walipaswa kukutana kila siku ku-review matatizo yaliyoko katika Operesheni, hakuna kikao kilichoitishwa. Sisi tulihoji Mawaziri hivi kweli mpaka Operesheni, maana mwishoni tulikuja kuambiwa na Rais mwenyewe ndiye aliyepiga simu mbona nasikia manung'unico, ndiyo wakaanza sasa majibu hayaeleweki yako wapi! Matokeo yale yanaonesha wazi kabisa kwamba, Serikali haizungumzi lugha moja na kama Serikali haizungumzi lugha moja ni hatari sana katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana makosa haya ambayo yametokea, tusiyashabikie kwa hali yoyote ile kichama. Mimi nasikitika sana ninapoona busara hazitumiki tunaanza kuoneshana vidole, sisi tumesimama kama kundi moja kudai haki na matendo mema kwa watu wetu, hivyo ndiyo siasa inavyotaka. Sisi tumepewa utawala na nawahakikishia inawezekana ukapata Kiongozi kutoka upande mwininge lakini Viongozi wazuri wapo CCM. Huu ni ukweli usiopingika kwa sababu wote walioko mahali popote walipo, baba yao ni hicho Chama. Huwezi ukaacha damu yako, mzazi lazima damu ya mtoto wako hata akikua vipi akuheshimu. Mimi nasema sitaki kujiingiza kisiasa wala sitaki kuchafua hali ya hewa, nashukuru sana kwamba wote tumeunganika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa hatua inayofuata, tumelaumu, tumesema na tunaagiza zichukuliwe hatua za uwajibikaji. Kinachotokea baada ya hapo ni nini? Sisi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. HENRY D. SHEKIFU]

tumefanya kazi nzuri na mmetusifu na tumejitoa muhanga, huo ni ukweli. Niombe sasa kwamba, ni vizuri baada ya hili kuongezwe azimio kwamba kiundwe chombo cha kisheria ambacho kitakwenda kufanya tathmini ya ndani, ijlukane madhara yaliyopo kwa watu, kwa mifugo na hatua za kawaida za kisheria zichukuliwe. Watu wote wale wanaoangukia kwa Amiri Jeshi Mkuu, wakachukuliwe hatua na Amiri Jeshi Mkuu. Wale wanaoangukia katika utawala wa kawaida, wachukuliwe hatua na watawala wanaohusika. Jambo hili kwa heshima ya Serikali yetu, lisichukue muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, moja ya tatizo linalotokea ni maamuzi kuchukua muda mrefu kutekelezwa. Hivi sasa tunazungumza mambo yatakwenda shmoni, hakuna utekelezaji unaofuatiliwa. Sasa tukifika katika hali hii ndiyo maana Serikali inatetereka. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuheshimu sana, ni mtendaji mzuri, nimefanya kazi na wewe miaka mitano ni mfuatiliaji mzuri. Ninasema umeingia ugonjwa sijui umetoka wapi, watu hawapokei maagizo wakayatekeleza kwa mujibu walivyoagizwa. Hakuna Jeshi linaloitwa Tanzania, umchukue binadamu mwenzako umwambie panda mti ufanye mapenzi na mti, haijawahi kutokea katika nchi hii ya Tanzania! Hizi ni adhabu za kijeshi.

Mtu anafikia anaambiwa wewe fanya mapenzi na swala. Anaulizwa sasa ulifanyaje? Anasema aah, mimi nilimwingiza kidole na ninyi mnasikia ni kosa kubwa sana, ni udhalilishaji mkubwa sana. Nasema hakuna mtu aliywatumwa hawa kwenda kufanya hivyo, ni watu binafsi wachukuliwe hatua. Wapo kwenye Majeshi, wapo Polisi ambayo ni sehemu ya Jeshi, wapo uraiani, wote wachukuliwe hatua. Bahati mbaya, moja ambalo ni baya, ile *intelligence* ya Operesheni hii iliegemea upande mmoja, matokeo yake kwa sababu iliegemea upande mmoja watu wengine wameonewa. (*Makof*)

Tunaomba sasa Operesheni itakapoanza kwa sababu kuna umuhimu iendelee, Operesheni hii tukiacha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. HENRY D. SHEKIFU]*

nayo tutaleta janga kwa Maliasili; iwepo lakini ikiwezekana kiundwe kitu ambacho kitasimamia Operesheni kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taasisi zote na ushirikishwaji uwepo na majina yatafutwe kabla ya kuingia kwenye Operesheni, siyo tunakwenda kwenye Operesheni unaoneshwa nyumba ya Mzee Shekifu pale, huyu anahuksika mnakwenda mnampiga. Mambo yaliyotokea kule ni mabaya sana, naogopa hata kuyasema. Sitaki kwenda zaidi, naomba na tunawashukuru sana wale wote mliotusifu kwa kazi tulioifanya. Tumefanya kwa niaba yenu, kwa nia njema na kwa uhakika wa kweli. Tuliyoyatoa katika taarifa yetu, mtu yejote akienda kuyapinga ushahidi tumeonesha.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Hajji Khatib Kai.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante nami kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kabla ya kuchangia, nianze ku-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, lakini pia ni mionganoni mwa Wajumbe tisa ambaao walifanya uchunguzi wa athari zilizojitokeza katika Operesheni Tokomeza Majangili.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo unasema; "Tembea Uone". Nimetembea lakini kubwa zaidi nimeona Wananchi waliodhulumiwa, walioathirika na waliofanyiwa ukatili mkubwa ambaao binadamu hastahili kufanyiwa. Operesheni Tokomeza Ujangili ilikuwa na nia njema kwa masilahi ya nchi yetu na kwa usalama wa maisha ya rasilimali zetu hasa tembo ambaao wapo hatarini kuuawa na iwapo Serikali haitakuwa tayari kuwanusuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Operesheni Tokomeza Ujangili, Watanzania walio wengi waliamini, kwa ushirikiano wa Vyombo vyetu Usalama, mitandao ya kijangili itadhibitiwa na kumalizika kabisa. Kwa bahati mbaya sana, mitandao hiyo haijatetereka na tembo wanaendelea

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. HAJI KHATIB KAI]*

kuuawa. Kwa nini mitandao ya kijangili haijatetereka ni baada ya Operesheni Tokomeza Ujangili kuacha sura yake pamoja na kupoteza lengo lake.

Mheshimiwa Spika, nimetembea nimeona na nimekutana na waathirika kwa macho nimewaona, lakini tumezungumza ana kwa ana. Baadhi ya tuliyoyaona pale Bukombe, tulikutana na mwalimu wa shule ana punda wake watatu, kati yao kuna punda wa jirani yake alikuwa akifuatana na punda wake. Punda hawa walikuwa na watoto wadogo ambao ndiyo walikuwa wakiwachunga, kwa bahati mbaya sana punda hawa walipigwa risasi. Siyo hilo tu, mwalimu huyo huyo alikuwa na punda wake ambaye alikuwa amebeba mzigo wa kuni, Askari wa Wanyama Pori pamoja na Misitu walipomwona punda huyu walimkata miguu ya nyuma, punda yule akalia mpaka kufa. Ni hatari kubwa, vitendo kama hivi vinavyofanywa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda Biharamulo tukakutana na Mwananchi mfugaji alishikiwa ng'ombe wake 30, Mwananchi huyu akatakiwa alipe faini ya ng'ombe wake shilingi 6,000,000. Mwananchi yule akasema hana shilingi 6,000,000. Akaulizwa ana shilingi ngapi? Akasema shilingi 1,000,000. Akaambiwa ziweke hapo. Baada ya kuziweka alitakiwa atembee kwa magoti aje mpaka kwa wale askari. Baada ya kufika pale, ng'ombe wako hapo kwenye zizi na kuna mti akaambiwa aukumbatie. Baada ya kukumbatia mti akapigwa pingu akaambiwa leo utatusaidia ulinzi wa fisi hapa. Alipigwa pingu akabakia pale usiku mzima na aliambiwa asaidie ulinzi wa fisi kwa sababu wanawasumbua na wanakula mizoga.

Mheshimiwa Spika, palipokucha asubuhi askari wakamfuata mtu yule wakamwambia lete pesa, akawaambia hana. Akaambiwa unatuchezea ngoja tukuoneshe kwa sababu yuko karibu na mifugo yake, walitafutwa wale ng'ombe ambao wamenenepa kwelikweli, akaambiwa acha tukuoneshe na wakaanza kuwa-shoot ng'ombe akiwa anaona.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. HAJI KHATIB KAI]

Baada ya hapo wakamwambia viyi utatoa pesa ama hutoi; akawaambia pesa nimewaambia sina. Sasa akaambiwa lakini wakati huo simu yake wakiwa wameichukua wakamwambia tupe namba ya watu wako wa nyumbani. Akaleta simu yake wakamwambia tafuta namba ya jamaa zako, akawekewa sikioni akaambiwa zungumza na jamaa zako walete pesa. Alichokifanya alizungumza na watu wake na akaambiwa atoe shilingi 5,000,000.

Alipigia simu aliongea na jamaa zake wakaleta milioni tano ndiyo akaachiwa akaenda na mifugo yake, lakini mingine imekufa. Tukaenda Kaliuwa ambako alifariki Ndugu Issa Kipara Issa, tulikutana na ndugu yake baada ya kukutana naye akatueleza. Kwa bahati nzuri kukawa na jamaa mwингine anayetwa Ndugu Hussein, huyu walishikwa pamoja basi Ndugu Issa Kipara Issa, akateswa akapigwa na kuna maneno ambayo alikuwa akiambiwa kwamba; tutahakikisha hapa huponi na kama utapona basi tutahakikisha huwezi kulala na mke wako nyumbani.

Mheshimiwa Spika, jamaa yule kateswa pamoja na adhabu kubwa ambayo aliipata, mateso ambayo siyo ya Kibinadamu, Ndugu Issa Kipara Issa alibanza makende yake mpaka yakapasuka na kutoka damu. Alikufa wakampeleka hospitali, watu wake wakasikia yupo *mortuary* wakaenda kumchukua.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, tulipofika Mpanda tulikutana na mtu mmoja ambaye naye alishikwa, huyu kwa bahati nzuri ni Diwani, kisa alichoshikiwa yeye ni kwenda kutetea watu wake. Alishikwa kwa bahati nzuri huyu jamaa mwili wake ulikuwa mzuri, alikuwa amejaza kiasi fulani, akaambiwa wewe una matako makubwa sana leo tutayapunguza.

Mheshimiwa Spika, nakuomba uwaambie wahusika waioneshe hiyo picha ili uweze kuona au Wabunge waone jinsi mtu huyo alivyofanyiwa unyama wa hali ya juu. Pomoja

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. HAJI KHATIB KAI]

na mguu wake anasema ulidungwa kitu ambacho hakukijua ni nini, huu mguu wote umeoza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na vitendo wanavyofanyiwa Wafugaji hasa Jamii ya Wasukuma, havikubaliki na havivumiliki. Katika ubaguzi mbaya ambao uliasisiwa na firauni, Kurani Tukufu, aya nne, *surah al qasas* inasema: "Hakika ya firauni aliyejituza na kuchupa mipaka hakika katika ardhi akawaongoza watu kwa ubaguzi na kuwadhoofisha na kuwafanya makundi mbalimbali, akadhoofisha kundi moja na lingine, akawaulia watoto wao wa kiume akawaacha hai watoto wa kike, hakika ye ye alikuwa ni miongoni mwa waharibifu wakubwa mno."

Mheshimiwa Spika, kutowatendea haki na usawa unaowaongoza ni dhuluma na uharibifu mkubwa mno na dhuluma hiyo husababisha majanga yaslyotegemewa kama yaliyomfika firauni mwisho wake alighariki.

Mheshimiwa Spika, uadilifu na ...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kafumu!

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilikuwa nimejipanga kuchangia hoja ya Kamati, lakini naomba niseme machache kwenye hoja hii ya uchunguzi.

**SPIKA:** Ulikuwa umejipanga kwenye hoja gani? Kamati ya Kilimo?

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kidogo.

**SPIKA:** Mimi nimekuita kama hutaki nitafurahi.  
*(Kicheko)*

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba niwape pole Wananchi wote na hasa Wafugaji ambao wamepata matatizo haya. Kama Wabunge wengine walivyosema, kwa kweli Wabunge wote tupo nyuma yao na tunapenda wajue kwenye suala hili hatuna ubaguzi wala mambo ya kivyama. Tupo kwa ajili ya Wananchi wetu ambao mmepata matatizo poleni sana.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema Wabunge wengine, tatizo hili limefanywa na Serikali na ni wajibu wake kulirekebisha. Taasisi pamoja na Majeshi yetu wameshiriki na kuna watu maalum waliofanya haya makosa. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ichukue hatua za msingi sasa. Hatua hizo ni pamoja na kuwawajibisha wale wote waliohusika kuanzia ngazi za Mawaziri mpaka chini kabisa tusiache mtu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hatua nyine ambayo tunatakiwa kuchukua ni ya baadaye, kwa sababu inaelekea sisi hatuna jeshi lilitayarishwa kwa ajili ya kufanya Operesheni na *rescue* kama nchi nyine. Nchi nyine zinakuwa na jeshi linakuwa ndani ya jeshi, ndani ya polisi, ndani ya magereza na ndani ya hospitali, watu waliotayarishwa kwa ajili ya *ku-rescue* na kusaidia watu wakati wa majanga. Linapotokea janga hili, jeshi liliopo ndani ni kama Usalama wa Taifa, kuna watu wapo kila mahali wanapotakiwa kufanya kazi wanafanya kazi.

Jeshi hili la kushiriki katika kutoa *rescue* kwa ajili ya mambo yoyote yale ambayo yanayotokea pamoja na majanga, inatakiwa tuwe nalo. Watu hao wanatayaishwa na wanafundishwa, wanaweza kuwa wanakaa ndani ya Jeshi la Polisi au ndani ya Jeshi la Wananchi, lakini inapotekea jambo la msingi kama hili, wanakusanya wanatengeneza *command post* na *hierarchy* yao, kiasi kwamba watu waliotayarishwa, waliofunzwa. Sasa ukitumia watu ambao hawakufunzwa wametoka kupigana Darfur, matokeo yake ndiyo haya.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU]*

Mheshimiwa Spika, siku za usoni naiomba Serikali, tengenezeni hili Jeshi la chini, la ndani kwa ndani, linakaa kwenye Majeshi na Taasisi. Wengine wapo hospitali manesi, madaktari, polisi na wanajeshi wanafundishwa, wanakuwa kama watu wa usalama, wanafanya kazi huko, lakini inapokuja shida wanakusanya na kufanya kazi hii vizuri. Vinginevyo, tutakuwa tunarudia mambo haya haya, linapotokea jambo hilo unapeleka watu wasio na uzoefu. Watu wasiojua kutunza haki za binadamu, kwa sababu mambo ya *rescue* na Operesheni yanahitaji uwe umefundishwa, unapomchukua mtu, unamchukua lakini unatunza haki zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba kuunga mkono hoja. Kamati ifanye kazi vizuri, Serikali tunaomba mtekeleze. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso!

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nawapongeza kwa dhati Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo imekuja kubainisha ukweli uliodhihirika, tofauti na kile kilichokwuwa kinaonekana kwamba Wabunge wanasema vitu ambavyo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, mateso ambayo wamefanyiwa Wananchi ni mabaya sana, kwetu sisi Mpanda kuna Operesheni mbili zimefanyika; moja, Opesheni iliyooongozwa na Wilaya ambayo kimsingi haikuwatendea haki Wananchi amba wapo katika maeneo wanayoishi kihalali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ihakikishe inawachukulia hatua Maafisa husika wanaoendesha Operesheni ambazo zinaitia Serikali katika mazingira mabaya yanayoonekana kuwatesa Wananchi. Afisa Maliasili wa Wilaya ni mionganoni mwa watu amba wanachangia kuhujumu Wananchi kwa kuwafanyia

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MOSHI S. KAKOSO]

vitendo ambavyo siyo sahihi. Naomba huyo achukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, Operesheni Tokomeza imefanywa Mpanda katika maeneo ya Wilaya ya Mlele, imewafanya watu wengine sasa hivi ni marehemu. Ndugu Madirisha na Ndugu Kitafura, waliuawa lakini yupo Ndugu Luchagula ambaye sasa hivi kapata kilema cha maisha baada ya kupigwa risasi na kujeruhija mguu wake.

Ninaombala Serikali hawa wote waliopata madhara mabaya, iwachukulie hatua wale wote waliohusika, lakini bado Wananchi wafidiwe fidia ambayo inaweza ikawasaidia waweze kuishi katika maisha ya kibinadamu.

Kuna matendo ambayo yamefanyika ya uporaji hasa kuwanyanya jamii za Wafugaji. Serikali naomba iwaangalie jamii hizi za Wafugaji ambao wameteswa na kunyang'anya mifugo katika maeneo mengi ya nchi hii. Nilikuwa na Chama cha Wafugaji, wameeleza vitu vingi sana ambavyo Serikali imewafanyia kiasi kwamba, hata ukiangalia picha ambazo wametuonesha, huwezi kuamini kwamba yale matendo yanaweza kufanywa na Serikali.

Kuna tukio ambalo liliifanyika Mpanda kwenye Operesheni iliyofanywa na Serikali ya Wilaya kwenye Kitongoji cha Mnyamasi, mama mmoja alibakwa anaitwa Sakina Juma, alibakwa na Kikosi cha Operesheni. Naomba wahusika wote wafuatiliwe na wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, tusipowachukulia hatua, tunaidhalilisha Serikali na kuwafanya Mawaziri waonekane hawafanyi kazi. Tatizo kubwa liliopo ni Watendaji wa chini wa Serikali ambao hawasikii kitu cha aina yoyote na kuona kila Mwanachi yeye hastahili kuishi katika nchi yake. Nchi hii ni ya kidemokrasia na tumekuwa tukiitwa kisiwa cha amani. Kwa sasa Taifa la Tanzania kwa Wananchi wanavyotuona ni kama eneo ambalo ni Darfur ya pili. Naomba Serikali iliangulari kwa kina na iwaonee huruma jamii

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MOSHI S. KAKOSO]

ya Wananchi ambao kimsingi wana stahili ya kuishi katika nchi yao kwa amani na usalama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie jinsi ya kuwafidia Wananchi hasa waliopata tatizo la kuibiwa mifugo yao waweze kufidiwa na Serikali. Vilevile Serikali ilipe fedha kuwafidia wale Wananchi waliopatwa na maafa na kuangalia zile familia ambazo zimeachwa bila kupata huduma waweze kusaidiwa. Tukifanya hivi tutakuwa tumeisaidia jamii na wao wataona wapo karibu na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri kuwa, kuna maeneo ambayo Serikali inaweza ikayafanyia kazi ni pamoja na kutenga maeneo ya shughuli za ufugaji ili kuepusha migogoro isiyokuwa na ulazima. Kuna maeneo mengi ambayo Serikali imekuwa ikimillki ardhi kwa kiwango kikubwa na wakati huo huo Wananchi wamezidi kuwa wengi kiasi kwamba, ardhi ambayo ipo ni ileile kwa kipindi kirefu. Ninaishauri Serikali itenye maeneo ambayo yatafanywa kwa ajili ya shughuli za kilimo na yatakayoshughulika na shughuli za ufugaji. Tukifanya hivi tutakuwa tumewasaidia jamii na kuondoa matatizo ambayo yatawasaidia Wananchi kufanya shughuli zao bila kuichukia Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 41 Kamati iliona kwamba, kuna baadhi ya wanasiasa katika Kijiji cha Kabage walikuwa wanawachangisha michango Wananchi. Ninaiomba Kamati watoe ni nani aliyeweza kwenda kuchangisha hiyo michango ya shilingi laki moja. Eneo hilo ni eneo la Jimbo langu, lakini sijui ni mhusika yupi aliyekwenda katika maeneo hayo na kuchangisha Wananchi kiasi kwamba alikusanya pesa nydingi na kuwafanya Wananchi kuibiwa. Naomba Kamati itakapokuwa inafanya majumuisho yake, iandae na tupate majibu ni nani ambaye alihusika.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali isisite kuwachukulia hatua wahusika wote. Wengine ni *DCs*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MOSHI S. KAKOSO]

ambao walihusika katika Operesheni hii, ni vyema wakachukuliwa hatua ili kuwasaidia Wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya, nakushukuru sana, naomba niipongeze sana Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya na niwatakie kila la heri, Mungu awasaidie. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ukiwa jungu kubwa huwezi kukosa ukoko na huwezi kufurahisha kila mtu. Ninachofurahi ni kwamba, mmechangia kwa wingi na mmechangia bila kujali maeneo mnayotoka kwa sababu jambo lenyewe limetokea kila mahali. Kila lenye ncha haliwezi kukosa mwisho, nimefika mahali namwomba AG asimame, dakika kumi na tano!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati na Wabunge wote waliochangia. Ninaomba mwanzoni hapa kusema ninaunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili linafungua milango ya kuchukua hatua za Kikatiba na Kisheria. Msingi wa hatua hini ni Taarifa ya Kamati. Jambo ambalo limesababisha haya lilikuwa limelenga kwenye jambo jema. Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema, jambo la kudhibiti na kutokomeza ujangili, jambo jema. Jambo la kuokoa ndovu wetu na faru wa Tanzania. Operesheni za aina hii zimeshawahi kufanyika na tulitumia pia Jeshi la Ulinzi. Jeshi la Ulinzi si Jeshi la Vita ni la Usalama na Ulinzi. Kwa Mujibu wa Ibara ya 147 na 148, Amiri Jeshi Mkuu anaweza kuamuru Jeshi hilo kutumika kusaidia Majeshi ya Kiraia. Kwa hiyo, kimsingi ilikuwa sawasawa.

Katika Operesheni hizi inawezekana tukafanya kitu ambacho ni cha pamoja kwa ajili ya kuharakisha na tunaweza kuwatumia Mahakimu na Waendesha Mashitaka kwa pamoja. Haina maana kwamba, ukishika peleka funga hapana, ni kufuata utaratibu wa kawaida na mtu ambaye

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

hakuridhika na uamuzi wa Hakimu anaweza bado kukata rufaa.

Sasa hivi ilivyokuwa kwa mujibu wa Taarifa hii ya Kamati, kuna mambo ya uhalifu. Mambo haya ya uhalifu kama utakavyoona Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, yako mengine ambayo yanahitaji uchunguzi wa kina, uchunguzi wa kimahakama. (*Makofii*)

Ninashauri na hili halihitaji Azimio la Bunge; nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wanaosema Serikali ichukue hatua. Ninashauri kwamba, wakati mwafaka ukifika, nishauri hadharani lakini Wabunge wajue kwamba, ipo sababu ya msingi ya kutumia Sheria yetu ya Uchunguzi wa Kimahakama, Sura ya 32 ya Sheria zetu, ambapo Mheshimiwa Rais atashauriwa aunde Tume ya Uchunguzi, ambayo itaongozwa kama atakavyoona yeye ama na Jaji wa Mahakama Kuu au na Jaji wa Mahakama ya Rufani na kuteua Makamishna ambao watapitia mambo haya pamoja na hayo yanayosemwa humu kwamba wapo na Waheshimiwa Wabunge pia wanahuksika. (*Makofii*)

Tufanye uchunguzi wa kina tujue hao waliofanya hivyo vitendo ni akina nani. Hili jambo linanikumbusha siku ya kwanza nilipoanza kusoma hukumu ya kifo. Ni jambo linasikitisha na sidhani kama kuna mtu mwenye akili timamu anaweza kusema Waheshimiwa Wabunge wa Kamati wametunga mambo haya.

Jambo la pili ni uchunguzi pamoja na hizi Hadidu za Tume, uchunguzi wa Mawaziri wanaohusika na Sekta hizi, Makatibu Wakuu, Watendaji wa Wizara hizi wa ngazi zote na mwenendo wa Vyombo vya Usalama vilivyohusika katika zoezi hili. Sheria ile inaeleza namna ya kufanya uchunguzi. Jambo la tatu ni *consciousness*, wewe unajisikaje kama jambo hili likitokea mikononi mwako. Hilo nisingeweza kulifanya kwenye hatua hii ambapo ninamhemko. Ni jambo linalohitaji tafakuri na nadhani Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika na wanaosemwa, watafanya uamuzi wao wakipenda, lakini kama

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]*

hawatapenda pengine Mheshimiwa Rais anaweza kufanya yeye. Haya ni mambo ambayo mimi simo wala sishauri juu yake, lakini kushauri mtu mmoja mmoja naweza kufanya.

Baada ya kusema hayo, nikubaliane kabisa na Mheshimiwa Tundu Lissu, juu ya umuhimu wa sisi kulinda Katiba yetu. Katiba hii ni ndogo lakini ndiyo imetufikisha hapa. Watendaji wanafanya vitu kama vile hakuna Sheria na hawa wapo wengi. Tunahitaji kurudi nyuma na kuangalia mfumo wetu wa elimu na nidhamu. (*Makofi*)

Tatizo hili la kufanya vitu kwa kudharau sheria limekomaa. Wakati fulani lazima niwe mkweli, hata unapomwambia Mheshimiwa usifanye hivyo, anakwambia mimi nitafanya nina mamlaka. Tuache, ni vizuri kuomba ushauri wa kisheria, *at least* utakuja kusema nilishauriwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, utajivua hapo. Ukifanya mambo yakatokea hayo yaliyotokea, kila mtu Iwake. (*Makofi*)

Baadhi ya kauli zetu kama Viongozi zinahitaji tafakuri. Mwaka 1985, Mheshimiwa Mrema alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu Waziri Mkuu, aliniambia mimi kwamba, amshauri Rais aniteue niwe Jaji halafu yeye akisema mimi nafunga. Akisema mimi nafunga. Nikamwambia itakuwa ni ukiukwaji wa Katiba. Kwa hiyo, hili jambo ni gumu sana na nafikiri Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapo, kama nakosea ataniwajibisha, Serikali lazima ichukue hatua. (*Makofi*)

Yale yanayonihusu nitachukua hatua. Kwa mfano hilo la kushauri juu ya Tume ya Kimahakama ni lazima tufanye. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja tena na nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Nampa nafasi Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi; yupo? Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani; hayupo. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nizungumze kidogo katika Bunge lako Tukufu. Kwanza, niseme kwamba, naunga mkono hoja iliyotolewa leo na nimeisikiliza kwa makini sana, Taarifa alioisoma Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Lembeli.

Niseme kwamba, kwa mara nyingine tena, natoa pole, rambirambi zangu kwa wale wote ambao waliathirika katika Operesheni hii Tokomeza, ambayo kama mlivyo sema Waheshimiwa Wabunge na wengi mmetamka kwamba, lengo lake ilikuwa jema, makusudio yake yalikuwa mazuri, kwa sababu ya kutazama hali tuliyokuwa nayo ikitabili wanyama pori wetu hususani ndovu wetu pamoja na faru.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mtu mzima, nimesikia hisia nyingi sana zilizotolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge na wengine wamesema mimi kama mimi lazima katika hili kuna kitu kinaitwa *ku-take political responsibility*. Sasa mimi nasema kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliponiteua katika wadhifa huu, kusema kweli ilikuwa ni kwa furaha yake, unaweza ukasema ni katika *pleasure* yake, *the pleasure of the President* na naamini kabisa aliamini ningeweza kufanya kazi hii kadiri ambavyo ningeweza.

Kutokana na Operesheni hii yametokea yaliyotokea na yamesemwa yaliyosemwa ndani ya Bunge hili, nina uhakika bado utaratibu utafanywa kuweza kujua hali halisia, ukweli ukoje, aliyehusika ni nani, yaliifanyika kwa nini na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hali ya wanyamapori huko siyo nzuri, kama tunavyozungumza katika hiyo Operesheni hali iliyotokea kwa ndugu zetu, kwa jamaa zetu, ni kitu ambacho hakikubaliki. Kwa maana hiyo, niseme kwamba, mimi mwenyewe nimewasikia kwa kauli mlizozisema na bado nitahitaji ushirikiano wenu katika kufanya kazi zangu ndani ya Taifa letu hili.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]

Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii ama fursa hii, kutamka wazi kwamba, ni nia yangu kabisa kuteremka ngazi hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, nina-resign kama wanavyosema kwa Kiingereza na nitafuata utaratibu unaostahiki kuitaarifu Mamlaka ambayo iliniweka katika nafasi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo!

### **WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, napenda kuwapongeza Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii na Waheshimiwa Wabunge wote ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajibu *accusation* ambayo imejitokeza kwenye Ripoti ili hata kama kuna hatua zitachukuliwa hapo mbeleni, lakini Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wajue ukweli.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Ripoti hii iliyosomwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Ripoti nzima sikuonekana ila nimeonekana kwenye mistari ya mwisho kwamba nijipime, lakini hakuna *accusation* zozote kwenye Ripoti ile.

La pili, sikuitwa kuhojiwa na Kamati hii. Sijawahi kuona Mahakama inaweza kumhukumu mtu bila kumwita kwenye utetezi ama kumwuliza tatizo lilikuwa ni ninii! Sijaitwa.

La tatu, Ripoti hii imesema kuzunguka zunguka kwa wafugaji mpaka wanaingia kwenye mbuga za wanyama mpaka kwenye Hifadhi za Taifa ni kwa sababu nitanukuu, inasema: "Tanzania ni nchi ya pili kwa wingi wa mifugo Barani Afrika. Ni wazi kwamba, adha wanazokumbana nazo wafugaji ni matokeo ya kutokuwepo kwa Sera na Mipango madhubuti ya muda mfupi na mrefu; hivyo basi, Bunge

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI]*

linashauri Serikali kumtaka Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvubi kujipima kuona iwapo anastahili kuendelea kuhodhi wadhifa alionao."

Mheshimiwa Spika, inasema Sera haipo, Mipango haipo na mikakati haipo. Napenda kusema kwamba, Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006 imepitishwa na Bunge hili na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati aliyesoma alikuwepo kwenye Bunge hili. Hii ndiyo Sera ya Taifa ya Mifugo, ipo na ni *document* ya Serikali na ndiyo tunaitumia katika kutekeleza mikakati na Sheria kwa kutumia Sera hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna Mikakati ya Mwaka 2010. Mikakati hii ni kwa ajili ya kutekeleza Sera; ni *document* ya Serikali ipo. Kwa hiyo, hiyo *accusation* ambayo imekuja kwenye *conclusion* siyo ya kweli.

Nyingine inasema kwamba, hatuna Mipango. Tuna Mipango ambayo tumei-*launch* mwaka 2011/2012, ambayo ni *document* ya Serikali na imeingizwa kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano mpaka 2015/2016.

Kwa hiyo, kwangu mimi haingii akilini kwamba eti sina Sera, sina Mipango ya Kati na ya Muda Mrefu. Wanasema Mpare huwa anaauza ng'ombe kwa kesi ya kuku. Kwa ujumla wanataka haki wala siyo kweli kwamba wanauza ng'ombe kwa kesi ya kuku, ni kwa sababu wanataka haki hawataki kuonewa.

Mheshimiwa Spika, nimeshaeleza hizo *document* zipo na masuala yaliyoko kwenye mkakati yapo sita. Tatizo ambalo lipo kwa Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvubi ni la mfumo tu wa kitaasisi. Katika suala hili la kupima ardhi, Wizara yangu haihusiki na kupima ardhi. Ardhi inapimwa na Wizara ya Ardhi. Ardhi ina Sheria mbili; Sheria ya Namba 6 ya Mwaka 2007 inayohusiana na matumizi bora ya ardhi; na Sheria Na. 5 ya Mwaka 1999 ya Vijiji. Hao ndiyo wanaopima ardhi na Halmashauri zinaomba kupimiwa ardhi Wizara ya Ardhi kutokana na mahitaji yao. Wizara ya Mifugo haihusiki kupima ardhi kwa ajili ya mifugo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI]*

Mheshimiwa Spika, miundombinu, majosho, malambo na visima virefu kwa ajili ya mifugo havifanywi na Wizara ya Mifugo, vinafanywa na Halmashauri zetu nchini, ndizo zenye majukumu hayo kupitia fedha zinazotengwa kwa ajili ya *DADPs* na *Agriculture*. Sihusiki, Wizara yangu haihusiki, yetu ni Sera. Sasa ninahusishwa vipi kwamba nimeshindwa kuwaweka wafugaji mahali wanapotakiwa waende kwa sababu wamekosa miundombinu na ardhi?

Mheshimiwa Spika, masuala mengi ya utibabu, kutibu, huduma za ugani, yote yanafanywa na Halmashauri. Sasa kwa kweli nimeshangaa. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, ambao wameona nilikuwa naonewa. Nawashukuruni sana, *Mwenyezi Mungu Subhana Wata'ala*, atawajalia. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimezungumza kuhusu Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo ni Programu ya miaka mitano na thamani yake ni shilingi trilioni 1.33 na ina vipengele saba kama ifuatavyo:-

Kipengele cha kwanza ni uendelezaji wa nyanda za malisho ambazo fedha hizi zinatakiwa zipelekwe Halmashauri. Hiyo mipango nimeiandaa mimi kama llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010 inavyosema. Niliandaa na thamani yake kwa maana ya kuandaa malisho, nyanda za malisho na maji ni bilioni 298. Uzalishaji bilioni 324. Tafiti, mafunzo, ugani na maabara bilioni 315. Mfumo wa kisheria bilioni 40. Udhibiti wa magonjwa bilioni 135. Masoko, utambuzi na usajili wa mifugo bilioni 205. Masuala mtambuka pamoja na masuala ya Ukimwi na mambo mengine ya kiutawala shilingi bilioni kumi.

Mheshimiwa Spika, tangu niingie Wizara hii, fedha zimekuwa zinapungua mwaka hadi mwaka. Mwaka 2009/2010 bilioni 67, lakini Wizara ilipata bilioni 55 tu. Mwaka 2010/2011 zilitengwa bilioni 58.5, zilizotolewa ni bilioni 45 pekee. Mwaka 2011/2012 bilioni 57, zilizotolewa ni bilioni 43 pekee

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI]*

na kinacholipwa *hundred per cent* lakini *Development* haiwezi ikafikia *hundred per cent* kwa kiasi hiki ambacho tunapata hizi fedha. Mwaka 2012/2013 billioni 54.6.

Sasa niwaelezeni kitu; katika mwaka 2011/2012 ambapo ndiyo mwaka wa kwanza wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo hapa nchini, Wizara ilitakiwa ipate billioni 345 kwa mwaka wa kwanza lakini ilipata billioni 43. Hivi nitaenda benki mimi Mathayo nikakope pesa *CRDB* kwa ajili ya kujenga malambo? *I can not do that* au niende wapi nikatafute fedha niweze kukidhi mahitaji ya mifugo?

Mwaka wa pili, mwaka 2012/2013, fedha zilizokuwa zinatakiwa kwa ajili ya huduma za mifugo Tanzania ili wafugaji wasihamehame billioni 330, lakini Wizara imepata billioni 42. Mwaka wa tatu fedha zilizokuwa zinatakiwa ni billioni 275, lakini Wizara ilitengewa billioni 48. Kamati ilivyoomba sana hapa ndiyo zikaongezwa 20 zikafikia 68, lakini mpaka sasa nimepeta billioni 14 tu. Sasa mimi David Mathayo nitafanyaje? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Yesu peke yake ndiyo alinyoosha mikono mikate ikajaa kwenye vikapu watu wakala. Mimi naweza kusali kukawa na malambo? Ninaweza nikasali kukawa na visima virefu? Ninaweza nikasali ardhi ya Tanzania ikaongezeka? Haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ninasema ndugu zangu Mwenyezi Mungu yupo, kama ni haki kwamba, nijiuzulu kwa sababu nimeshindwa, basi Mwenyezi Mungu ye ye mwenyewe atawashughulikia hao amba wanafikiri Mwenyezi Mungu anagawa haki. Usiku huu nilikuwa nasali Zaburi ya 72, kwa sababu naona kabisa ninaonewa maana nilisikia harufu. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, utatuzi wa migogoro. Migogoro hii ni lazima Serikali itenye fedha za kutosha kwenye Wizara ya Ardhi kusudi wafugaji wapimiwe maeneo yao. Hili linatakiwa lifanyike na sasa hivi hii ndiyo *opportunity* ya

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI]*

kufanya hivyo, watengewe maeneo ya kutosha. Kuna watu wana mashamba makubwa sana ambayo hawajayaendeleza, wanyang'anywe wafugaji na wakulima wapewe. Lazima tufanye uamuzi ambao utawasaidia wafugaji na wakulima, maana wote wanahitaji ardhi. Lazima tuharakishe ujenzi wa miundombinu, lazima fedha za kutosha zipelekwe Halmashauri tuwe na miundombinu ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuhakikishe kwamba, fedha zinatolewa za kutosha, tutoe elimu na tuimarishe *research*, ili Wataalamu wetu wafanye *research* tuweze kupeleka matunda ya *research* kwa wafugaji wetu na wakulima wetu ili tuweze kuzalisha vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima pia kupitia Sheria, pale panapowezekana, mifugo na pundamilia wale yale majani kwa sababu haiwezekani tukafungia ng'ombe wasiingie, lakini majani yapo na pundamilia hawapo. Ng'ombe hawa tukarekebisha Sheria, mifugo na wanyamaporai wanaweza wakala kwenye pori moja kusudi tuweze ku-serve watu, tuweze ku-serve mifugo. Tungekuwa tunaagiza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofii*)

**SPIKA:** Aah, muda hatuna jamani. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naambiwa wengine utawasemea wewe. Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango mizuri. Kwa namna ya pekee, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ambao ndiyo wamewasilisha tathmini ya matatizo yaliyojitokeza katika Operesheni Tokomeza. Kwa kweli tunawashukuru sana.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, naomba kwa haraka haraka baada ya kusikiliza ile Taarifa, kwa Mtanzania yeoyote ambaye ameisikiliza na wale tulipata nafasi ya kuona hata picha, huwezi ukasita kusikitika. Lazima tuwape pole sana wale Watanzania wote na kwa kweli tutoe rambirambi kwa wale wote ambao katika Operesheni hii wamefikiwa na matatizo makubwa kiasi hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka niishukuru Kamati kwa sababu, pamoja na kwamba, walipewa muda mfupi, lakini wamejitätahidi sana. Wamejitätahidi katika kipindi kifupi wameweza kuwasilisha Taarifa mbele ya Bunge, Taarifa ambayo imetusaidia kufika hapa tulipofika leo. Nawashukuru sana, lakini nawapa pole vilevile kwa sababu najua haikuwa kazi rahisi, nchi kubwa hii, lakini wamejitätahidi sana kuweza kuzunguka angalau kwa kiwango walichowenza, kuweza kufikia baadhi ya maeneo na kupata maelezo mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nimesimama kusema kweli, kwa sababu nataka niseme tu kwa niaba ya Serikali juu ya Taarifa hii na yale ambayo ninafikiri kama Serikali na kama nchi, lazima tukubali kwamba, tutayapa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Operesheni hii imesimamiwa na Wizara tatu, kwa maana ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, kama Wabunge wengi mlivyosema, hizi ni Wizara zinazosimamiwa moja kwa moja na Mawaziri na ndiyo waliokabidhiwa dhamana ya kusimamia Wizara hizo. Chini yao wanao Watendaji, wanao Makatibu Wakuu, wanao Wataalamu mbalimbali na wanavyo Vyombo vilevile. Katika mazingira ya jambo hili, tunalo Jeshi la Polisi, Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Wananchi. Upande wa Maliasili wanayo vilevile Idara ya Wanyamapori ambayo ina askari ambao ndiyo walipewa jukumu la kusimamia jambo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nimesikiliza kwa makini, vitendo vimeoneshwa kwa kuititia Taarifa hii, vitendo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI MKUU]*

ambavyo havikubaliki; mauaji, ubakaji tumeelezwa na unyanyasaji ambao hauwezi kukubalika hata kidogo. Ipo mifugo ambayo vilevile imeuawa, sehemu nyingine imejeruhiwa na yapo mambo mengine kadha wa kadha ambayo yameelezwa katika Taarifa hii; vitendo vyote hivyo kusema kweli havikubaliki hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naelewa nia nzuri ya Operesheni hii na kama Waheshimiwa Wabunge wengi mlivyosema, ilikuwa ni dhamira ya Serikali kujaribu kupambana na ujangili hapa nchini na kujaribu kuona tuwakamate wale wote wanaohusika ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Sasa nadhani kikwazo au tatizo kubwa limekuwa ni namna Operesheni hiyo ilivyotekelvezwa, lakini kubwa zaidi ilivyosimamiwa. Hapa ndipo Wizara mnapoziona sasa kama vyombo ambavyo vinalo jukumu la jumla na kwa hiyo, ni lazima waone hilli kwamba ni sehemu ya usimamizi au sehemu ya jukumu lao.

Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane kabisa na Wabunge wengi mliota rai ya kuwataka Mawaziri hawa waone uzito wa haya yaliyojiteza na wao wenyewe wabebe ile dhamana kwa hiyari yao wenyewe. Wakati huohuo nimejaribu kutazama sana maelezo yaliyotolewa na ninataka nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa muda uliokuwa umetolewa kwa Kamati hii na kazi waliyofanya, inawezekana kabisa pengine kazi hii siyo timilifu, pengine inahitaji kufanyika zaidi. Taarifa walizopata ambazo zimehusisha mambo fulani fulani inawezekana vilevile zinahitaji kuthibitishwa zaidi na zithibitishwe kwa utaratibu ambao utatupa uhakika kwamba, wale wote ambao wamehusika kwa namna moja au nyingine, washughulikiwe kwa mujibu wa taratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wake nadhani ni mzuri na mimi kwa niaba ya Serikali nimeupokea. Kwamba, pengine isiihie hapa, zitakuwepo hatua za kiutawala pale itakapoonekana inawezekana haraka haraka zikaweza kuchukuliwa. Nadhani la maana zaidi kwa sababu hapa unaona kuna dalili kubwa sana za uvunjifu wa Sheria na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

matendo mengine ya kikatili, hapa unahitaji kuwa na Tume kama hiyo aliyoipendekeza, inaweza kusimamiwa na watu ambaao wana *calibre* nzuri, wazamie kwenye mambo haya, tuweze kubaini kwa uhakika wahusika wote ambaao kwa namna moja au nytingine, wamejiingiza katika tatizo hili kwa utaratibu ambaao umeelezwa na hawa sasa waweze kufikishwa kama ni kwenye Vyombo vya Sheria, basi tuweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutajaribu kujitahidi endapo Kamati na Bunge mtaridhia jambo hili, basi tutajaribu kutumia muda mfupi kwa kadiri itakavyowezekana, pengine ndani ya mwezi mmoja hiyo kazi iwe imekamilika, wailete ile Taarifa. Kupitia Bunge hili tuileteli muweze kuona kilichojojiteza kwa mmoja mmoja ni nini na hatua ambazo zimependekezwa na zile ambazo tutakuwa tumekwishazichukua tayari.

Jambo ambalo lazima tulione kwamba ni letu na ni lazima tuhakishe linasimamiwa vizuri sana. Kwa hiyo, kwa upande huo nataka nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka niwashukuru vilevile kwa kuwa katika maelezo yenu angalau mmetusaidia kwa kutambua umuhimu wa kuendelea kulinda hifadhi zetu. Kwa kweli, kwa jambo hili ninashukuru sana, kwa sababu taarifa niliyokuwa nimeipata mara ya mwisho nilipoambwa kwamba, kwa mfano Selous tumefanya sensa ya mwisho juzi, inaaminika kwamba, hivi sasa tuna tembo 13,000 tu, sensa iliyoleta imetangulia walikuwa 55,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaweza kuona kwamba, kama jambo hili ni kweli, hili jambo ni *serious*, ni kubwa sana. Nataka niwashukuru kwa kuliona hilo na mimi ninaamini kabisa maadam ridhaa ile kwamba, pengine ni vizuri Operesheni iendelee, itafanywa vizuri zaidi kwa lengo la kujaribu kulinda na kuhakikisha hifadhi hizi zinalindwa vizuri.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Tutazidi kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, tutakapokuwa tunazungumza mambo ya bajeti hapa, basi kwenye eneo hili la uhifadhi mwone ni namna gani mnaweza mkaisaidia Serikali, kuweza kuwa na bajeti na mfumo mwingine ambao utatuwezesha tuweze kufanya kazi hii iwe nyepesi zaidi. Kwa hiyo, katika hilo utakapofika wakati mwafaka, tutaomba tushirikiane kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nimesikiliza maelezo yote yaliyotoka kwa Waheshimiwa Wabunge, nilichukua jukumu la kuzungumza na Mawaziri wote wanen; nimekaa nao mmoja mmoja na kujaribu kuwaeleza yaliyojitokeza ambayo na wao wameyasikia. Katika mazingira haya, nadhani Wabunge walichoshauri, wanachokiona, nafikiri kina msingi mkubwa. Pengine ni vizuri mkaliona hilo kwa sababu mnasimamia sekta na walitarajia na sisi tulitarajia kwamba na ninyi mtakuwa na uwezo wa kusimamia vyombo vyenu, ilimradi hili limefika hapa basi pengine ni busara muweze kuona jambo hili tukubali Wabunge na ushauri wake uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo yangu na Waheshimiwa hawa wote, kimsingi, Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Maliasili na Utalii, ambaye mmemsikia yeye mwenyewe, ameamua *courageously*kuweza kusimama na kutoa tamko lake, walikubali kwamba, jambo hili ni zito na linastahili kupewa uzito unaotakiwa kwa upande wa Serikali. Kilichowafanya walikubali ni kwa sababu moja kubwa, vyombo vilivyo husika ni vyombo ambavyo viro chini ya usimamizi wao. Hili limewapa uzito wa kuweza kusema katika mazingira haya unafanyaje.

Mheshimiwa Dkt. Mathayo, amejieleza lakini nadhani hata baadhi ya Wabunge hapa nimewasikia mki sema, kwa maana ya Operesheni Tokomeza ni kweli kwa maana hakukuwa na vyombo ambavyo vimesimamia moja kwa moja kuona na yeye ni sehemu ya haya maovu na vitu vingine vyote. Anaweza kuwa na eneo lake tofauti, lakini haliwezi kuwa kwa maana ya vitendo ambavyo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

vimejitokeza katika zoezi hili. Nadhani ndiyo maana na yeze aliona asimame aseme mawili, matatu, siyo kujitetea, lakini naamini alitaka tu Wabunge mwone kwamba, uhalisia wake pengine ndiyo huo na inawezekana pengine tukalionia kwa mtazamo huo na tuone katika mazingira kama haya kweli anapaswa kuwajibika kwa msingi huu wa Operesheni Tokomeza au hapana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sikuishia pale, nilliona nimtafute Mkuu wa Nchi, Mheshimiwa Rais mwenyewe; kwa hiyo, nikazungumza nae, nimempa picha yote na yeze ameungana na Wabunge kwa sehemu kubwa kabisa. Amesisitiza sana kwamba, angependa matokeo ya Tume hiyo mtakayokubali kuiunda yasichukue muda mrefu. Wale wote, Watendaji wote, bila kujali ni wa ngazi gani, ilimradi alijiingiza katika vitendo viovu, basi wawajibike kwa mujibu wa taratibu za kisheria bila kuogopa, bila kujali, ili haki itendeke. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikamshukuru sana tu. Nikamweleza vilevile kwa upande wa Dokta Mathayo kwamba, yeze kidogo baadhi ya Wabunge wanalionia hivi. Sasa inaonekana ni kweli pengine kwa maana ya zoezi lenyewe liliyokuwa, tunaweza tusimhusishe moja kwa moja na jambo hili. Labda ukilitazama kwa maana ya kwamba, wewe ndiyo unasmamia Sekta ya Mifugo, pengine umeshindwa kuisimamia hiyo mifugo huko, ndiyo maana wanakwenda kwenye hifadhi. Hilo linaweza likaangaliwa kwa sura hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimemweleza yote mpaka mwisho, akapata picha yote. Alichosema tu ni kwamba, hapana tusigombane hapa, jambo hili ni kubwa. Najua Waziri wa Mifugo anaweza kuwa moja kwa moja hahusiki, inawezekana kabisa likatazamwa hivyo, lakini ndiye mwenye kusimamia Sekta ya Mifugo. Kwa hiyo, katika jambo kama hili ambalo ni la kisiasa siyo vibaya na yeze akaliona kwa mtazamo huohuo. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikasema basi vizuri, tutaangalia sasa Bunge litakavyotuelekeza mwisho wa yote. Bado nikaona amesitisiza kwamba, hapana yeye amekubali kwamba Mawaziri wote wanne, mengine yatatazamwa mbele ya safari; kwanza, katika hatua hii amekubali kuchukua uamuzi wa kutengua uteuzi wao wote wanne, pamoja na Mheshimiwa Dokta Mathayo, atakuja kuliona hilo lingine ambalo limejitokeza kwa maana hiyo ya pengine katika sura tofauti kidogo, kwa sababu kutengua leo haina maana kwamba, hawezi kumpa nafasi nyingine ya Uwaziri. Kwa picha iliyojitokeza na namna liliwyotazamwa na jamii pengine suluhu katika jambo hili ingekuwa ni hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilimwahidi kwamba, basi nitafikisha ujumbe huu mbele ya Bunge kwa lengo zuri tu la kutaka Watanzania wajue kwamba, Rais ameliona na uzito aliuona nadhani ndiyo umemfikisha kuliona hivyo; na akasema jambo kubwa hapa Mawaziri hawa moja kwa moja hawakutenda kitu chochote kiovu. Hawakwenda huko pengine kujaribu kufanya jambo lolote, lakini ukweli unabaki palepale, niliwakabidhi sekta hiyo kwa kuamini kwamba, itasimamiwa nao vizuri. Sasa ilimradi tumefika hatua hiyo, basi suluhu ya kweli katika mazingira ya kisasa ni hiyo. Kwa hiyo, tumekubaliana naye, basi naomba nifikishe hilo kama ni taarifa ya kutoka kwake, akirudi zoezi lile atalikamilisha yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, katika jambo hili nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kushirikiana. Ushirikiano mliouonesha katika zoezi hili ni mzuri, taarifa hii mmeichangia vizuri sana, kwa hiyo, naamini kabisa kwamba, hata katika mambo mengine makubwa kama haya, tutakwenda vizuri kwa pamoja kwa masilahi ya nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, pili, niendelee kuwaomba kwamba, ilimradi tatizo kubwa kwenye maeneo mengi ni la kibajeti, basi utakapofika wakati mwafaka wote

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI MKUU]*

tusaidiane kuona ni namna gani tunaweza tukalitekeleza jukumu hili kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, tatu, nataka niwasihi sana Watanzania wote kwa ujumla; sisi Wabunge, Watanzania kwa ujumla na Viongozi wote na Watendaji wote ambao tumepewa dhamana mbalimbali, lazima kila mmoja atekeleze wajibu wake kwa kuzingatia Sheria. Mwananchi wa kawaida afuate Sheria na sisi Viongozi tufuate Sheria, kwa sababu ni jambo la msingi na lazima wote tulitazame kwa mtazamo mmoja.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nirejee kusema kwamba, katika michango na maoni mliyotupatia, mambo mengi ni yale ambayo yakizingatiwa, si kwa maana ya Operesheni hii, kwa maana ya utendaji Serikalini, yatasaidia sana tunapokuwa tuna jukumu ambalo tunatakiwa tulifanye kwa pamoja. Kwa hiyo, haya yote, michango yenu pamoja na Ushauri na Mapendekezo ya Kamati, yatawekwa pamoja kwa maana ya kutusaidia siku zijazo. Kubwa ni hatua zitakazochukuliwa mara tu baada ya kumaliza zoezi hili; za kiutawala na zile za Kisheria hasa baada ya Tume ile, kama mtaikubali, kuwa imekamilisha kazi yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, nami naomba niungane na ninyi nyote kwamba, jambo hili ni letu wote, limetusikitisha, si jambo zuri, lakini Serikali itaendelea kuhakikisha tunasimamia kazi zetu vizuri kwa masilahi ya Watanzania wote. Nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja; njoo ukae huku kuna meza kubwa!

**MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii, kukushukuru kwa niaba ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Kamati Ndogo ya Uchunguzi na kwa niaba yangu mimi mwenywewe,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBÉLI – MWENYEKITI WA KAMATI

YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRAJ]

nakushukuru kwa kuiamini Kamati yangu, kufanya kazi hii kubwa na nzito.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imefanya kazi yake katika mazingira magumu, wakati mwingine kusafiri masafa marefu usiku na kushinda bila kunywa maji wala chakula. Lengo lilikuwa ni kutekeleza wajibu ambao Bunge lako Tukufu limeipa Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati Ndogo, ambao wamefanya kazi hii kwa uadilifu mkubwa, kazi ambayo imezaa matunda haya. Kamati ambayo licha ya Wajumbe kutoka katika Vyama mbalimbali, lakini katika jambo hili la Kitaifa tuliungana pamoja na kuifanya kazi hii kwa moyo wa kizalendo. Yalishaanza kusemwa maneno kwamba Kamati imehongwa.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie kuwa, hakuna aliyekatiza mguu wake mbele ya Kamati hii kujaribu kuishawishi kwa lolote alilokuwa nalo na ndiyo maana siri ya Taarifa hii haikujulikana mpaka leo asubuhi. Kwa hiyo napenda kuwashukuruni wote kwa kazi ambayo tumeifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze wachangiaji waliochangia kwa kuzungumza humu ndani ya Bunge na pia waliochangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge ni 33, akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Peter Pinda; nyote nawashukuru kwa moyo wa dhati kabisa kwa niaba ya Kamati. Waliochangia kwa maandishi ni wanane na kwa sababu ya muda sitawatambua kwa majina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa Taarifa yetu na maoni ambayo tulilishauri Bunge, kimsingi, yote yamekubalika na hili naomba niwashukuru sana. Naomba nitoe maelezo kidogo kwa mambo mawili; kwanza, la Mheshimiwa Waziri Mathayo, kwa nini Kamati ilimhusisha kwenye suala hili la Operesheni Tokomeza. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI  
YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA]

Mheshimiwa Spika, Januari 18, 2006, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa maagizo kwa Wizara hii mahususi ya Mifugo. Naomba nisome maagizo machache, alitoa jumla ya maagizo tisa, mionganoni mwa maagizo hayo lipo suala la kushughulikia wafugaji wanaohamahama. Hili lilikuwa agizo mahususi kwa Wizara hii. Tunavyozungumza hivi leo ni 2013, mifugo bado inahamahama mtindo ule ule wa 2006. Kulikuwa na agizo Wizara hii ijitätahidi kubadilisha wafugaji kutoka kwenye uchungaji kwenda kwenye ufugaji wa kisasa. Agizo lingine lilikuwa ni kutafuta *missing link* inayosababisha Sekta ya Mifugo isiendelee na kupata masoko, ikiwa ni pamoja na masoko ya nje na kuuza mifugo na mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Bunge limetumia leo siku nzima kuzungumzia adha ya wafugaji, kudhulumiwa, kuteswa na kunyanyaswa, kwa sababu mifugo yao inarandaranda. Jambo la kujuliza Waheshimiwa Wabunge; hii mifugo kwa nini inatembea muda mrefu kufuata hifadhi? Ni kwa sababu Sera ya Uhifadhi inasimamiwa, inatekelezwa, mipango ya uhifadhi inasimamiwa, inatekelezwa na ndiyo maana kule mifugo inataka kwenda.

Agizo hili la Rais lilikuwa linataka Wizara walau ioneshe nia ya kuiwekea mifugo miundombinu waache kuhamahama. Katika misingi hii, tuliona huwezi kutibu tatizo la mifugo kwenda hifadhini bila kuihusisha Wizara inayohusika na Mifugo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiona mtu anatetewa kwa hoja ambazo hazina mashiko, kuna kitu. Mawaziri wengine wametetewa pia, lakini hatukuona munkari ambao Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi alisimama na kushangilia wakati Waheshimiwa Wabunge wakisema ameingizwa kinyemela kwenye sakata hili. Ukweli utabaki hapa hapa kwamba, mifugo inazubaa, inazunguka, kwa sababu Mipango na Sera, pamoja na kwamba Mipango ni mizuri, Sera ni nzuri, lakini usimamizi wake hakuna. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI  
YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRAJ]

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kufafanua ni kuhusu Operesheni Tokomeza. Bunge hili litawalazimisha Mawaziri kuondoka katika nafasi zao kila mara kama jambo moja halitafanyiwa kazi; mfumo wa Serikali. (*Makofii*)

Ukisoma Ripoti yetu chimbuko la matatizo siyo Mheshimiwa Kagasheki, chimbuko la matatizo ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, ndiye aliyesababisha Mpango Kazi ambao ultayarishwa na yeze na ofisi yake na wasaidizi wake wakubwa, usitekelezeke *on the ground*. Kwa makusudi, Waziri hakuwa anapewa taarifa za mara kwa mara, *final document* ya Mpango Kazi, Waziri hakupewa na wala hakuwa na nafasi. Yapo mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwenye ushauri wa Kamati yetu kwa Bunge kwa maana ya Azimio, tuongeze kipengele kinachosema; Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Mpango wa Operesheni Tokomeza hawa wawajibishwe leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mapori kuna matatizo, Serikali imeagiza mifugo irejeshwe kwa wenyewe mpaka leo kwenye *attachment* zetu tumeonesha hapa Mheshimiwa Waziri Kagasheki alivyojitahidi, kunusuru ile mifugo ambayo mpaka tarehe 1 ilikuwa haijauzwa mpaka leo na majibu ni kejeli kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, hali siyo nzuri, rushwa iliyoko ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii inatisha. Ripoti imetaja watu humu, wanakusanya pesa kwa simu, lete kwa M-Pesa, namba za simu zipo humu! Naomba Serikali leo leo ianze kuzifanya kazi namba za simu hizi. Hali siyo nzuri, bila ya Watendaji hawa kusimama leo rushwa itaendelea, ng'ombe wataendelea kukamatwa na Wananchi wataendelea kunyanyawsa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwenye ushauri wa Kamati kwa Bunge kwamba, Katibu Mkuu wa Wizara

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI  
YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRAJ]

hii ya Maliasili na Utalii, asimame kazi kwanza wakati taratibu zingine zinachukuliwa na Watendaji wake Wakuu. Tumeona hapa taarifa kwa umma inapotosha kabisa mmeona picha hapa, lakini taarifa kwa umma inadanganya. Watanzania wanaiona vipi Serikali yao?

Kwa hakika tangazo lile halikwenda kwenye vyombo vya habari bila kupita kwa Katibu Mkuu anayehusika. Hili tukitaka kuondosha tatizo la nyoka ambaye ndani ya nyumba kila siku anagonga vifaranga ni kumsaka nyoka alipo, ponda kichwa, mambo yatakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge walioleta mapendekezo yaingizwe kwenye Maazimio. Mmojawapo ni Mama Kilango, ambaye katika Kifungu cha 7 lakini hili tayari limeshatekelezwa anasema; Waziri wa Maliasili naye ajipime ili Serikali iheshimiwe na Watanzania watuelewe kwamba, tumepata uchungu kutokana na maovu haya. Hili ni pendekezo ambalo Mheshimiwa Mama Malecela, aliomba lionezwe kwenye Maazimio ya Bunge.

Mapendekezo mengine ya marekebisho yafanyike katika maeneo yafuatayo; huyo ni Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, anapendekeza yafanyike mabadiriko katika ukurasa wa 47, *bullet* ya pili, kuongeza maneno “na fidia”, katи ya maneno “machozi na kwa”.

Mheshimiwa Spika, pili, katika ukurasa wa 48 anapendekeza kuongeza kipengele kipy Cha 15 baada ya kipengele na 8, kurekebisha vipengele vingine na kuendelea, kipengele kipy Kisomeke ifuatavyo: “Serikali ifute kipengele cha Kanuni ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyama Pori Namba 5 ya Mwaka 2009 inayoruhusu Maaskari wa Game Reserves kutoza *fine* za mifugo porini na badala yake kesi hizi zishughulikiwe na Mahakama.”

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. JAMES D. LEMBELI – MWENYEKITI WA KAMATI  
YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRAJ]

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 51 kipengele cha (12), mara baada ya *bullet* namba 3, kuongeza *bullet* namba 4, inayosomeka: "Kupitia upya mipaka ya mapori yote ya akiba na kutenga *buffer zone* katika mipaka na mapori na maisha ya Wananchi. Pia *buffer zone* zile zitungiwe Sheria kuzilinda ili zitumike kwa ajili ya malisho ya mifugo." (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, nakushukuru wewe binafsi na kwa namna ya kipee, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuunga mkono Mapendekezo ya Maazimio ambayo Kamati imeyaleta mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo katika Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** kwanza kabisa nitatumia kifungu cha 28(5) kuongeza dakika kusudi tukamilishe vizuri hii. Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Lembeli, kwa kutoa Maazimio hayo. Tumeshampa taarifa kwamba, Serikali ilikuwa inapendekeza tuongeze pendekoz moja la kuundwa kwa Tume ya Uchunguzi wa Kimahakama, Serikali ifanye hiyo kazi. Kwa hiyo, tunaomba pendekoz hilo pia liingie kwenye Maazimio ya Bunge. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba muiamue hoja ya mtoha hoja na mapendekezo yaliyoletwa na Mwanasheria Mkuu.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira  
ililikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, angalau mmejitalidi kidogo sana kutoingiza siasa kwenye kujadili jambo linalohusu nchi yetu. Tunaomba Waheshimiwa Mawaziri, angalieni kila sehemu, msiache mahali pakalala mkawategemea watu wengine, mnapokuja kuungua vidole wao hawapo mnakuwepo ninyi; kwa hiyo na wengine mjitätahidi.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA,  
URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya kutengua Kanuni za Bunge, kwa kutumia Kifungu cha 153(1).

Kwa kuwa Mkutano wa Kumi Nne wa Bunge wa kushughulikia Taarifa za Mwaka za Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na shughuli zingine, ulipangwa kumalizika tarehe 20 Desemba, 2013;

Na kwa kuwa leo tarehe 20 Desemba, 2013 Kamati ya Uongozi ya Bunge ilikutana kwa dharura kwa ajili ya kuzingatia Hati ya Dharura kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa;

Na kwa kuwa katika kikao hicho Wajumbe wote waliohudhuria waliridhia Muswada huo kusomwa kwa hatua zake zote katika Bunge hili, jambo linalohitaji Bunge kuongezewa muda wa kufanya kazi hiyo;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]*

Na kwakuwa kwa Mujibu wa Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2013, Bunge haliwezi kukutana na kufanya kazi Siku ya Jumamosi, Jumapili au Siku za mapumziko;

Na kwa kuwa ili kuwezesha Bunge kukutana Siku ya Jumamosi tarehe 21 Desemba, 2013, lazima Bunge litengue Kanuni ya 28(15) kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1);

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora za shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Nne, Kanuni ya 28(15) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(15) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, Bunge halitakutana Siku ya Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko, itenguliwe na badala yake Bunge likutane Siku ya Jumamosi, tarehe 21 Desemba, 2013 kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa sita mchana, isipokuwa tu kwamba siku hiyo hakutakuwa na maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitawahoji muiamue.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja illamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni za Bunge illafikiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nyote mmeafiki. Kwa hiyo, kesho kutakuwa na kikao kuanzia saa tatu kujadili Muswada ambao umefanyiwa marekebisho kiasi fulani. Kusudio letu sisi kabla ya saa sita tuwe tumekamilisha na waliopanga safari waweze kwenda.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

Leo asubuhi mlitangaziwa kuhusu kusudio letu la tafrija kuipongeza Kamati yetu kwa ushindi wa Kikombe cha Wabunge kule, lakini saa hizi ni mbovu kweli kweli. Kwa hiyo, chakula kipo hapo Kantini, anayefikiria kabla hajaenda nyumbani apitie ale chakula anakaribishwa, tafrija kama tafrija haipo, chakula kipo, mnakaribishwa nyote kwenye chakula hicho.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru tena. Najua wengine wote mlitaka kuzungumza, lakini haiwezekani mkaongea wote, mambo ya muhimu mlishtayaongea, wale waliokwazwa kwa maana walikosa nafasi ndiyo inavyokuwa.

Naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.57 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi,  
Tarehe 21 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*